# MATUMIZI YA FALSAFA YA USIHIRI KATIKA RIWAYA TEULE ZA EUPHRASE KEZILAHABI

Na

Silima Faki Makame

Tasnifu Iliyowasilishwa kwa Ajili ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dodoma

Chuo Kikuu Cha Dodoma

Oktoba, 2016

## ITHIBATI

Aliyetia saini hapo chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii iitwayo "**MATUMIZI YA FALSAFA YA USIHIRI KATIKA RIWAYA TEULE ZA EUPHRASE KEZILAHABI**" na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya kukamilisha masharti ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

……………………………….

Dkt. Athumani S. Ponera

(Msimamizi)

Tarehe…………………..

## IKIRARINAHAKI MILIKI

Mimi, Silima Faki Makame, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kutunukiwa shahada inayofanana na hii au nyingine yoyote.

Saini……………………….

Hairuhusiwi kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, na kusambaza au kuiga sehemu yoyote ya tasnifu hii bila ya ruhusa ya mwandishi wa tasnifu au Chuo Kikuu cha Dodoma

## TABARUKU

Nimeitabaruku kazi hii kwa baba yangu mpenzi, Bw Faki M. Haji, mama yangu mpenzi, Miza F. Makame, kwa kunilea, kunivumilia na kunijali katika kipindi chote cha utoto wangu hadi kufikia leo. Licha ya shida kubwa waliyoipata. Ili kuonesha kuwa ninazithamini juhudi zenu, nakiri kuwa nawapenda wote kwa moyo wa dhati. Ninawakabidhi tasnifu hii muipokee kama zawadi ya upendo utushikamanishao kwa pamoja katika maisha yetu ya kila siku, Mungu awalipe kheri. Amin.

## SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa taasisi na watu mbalimbali waliotoa ushauri na michango yao ya hali na mali iliyowezesha kukamilisha kazi hii. Awali ya yote, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kumshukuru Mwenyezi-Mungu (sw) kwa kunijaalia afya njema katika kipindi chote cha masomo yangu. Afya ambayo iliniwezesha kuikamilisha tasnifu hii kwa muda mwafaka.

Kwanza, namshukuru msimamizi wangu, Dkt. Athumani S. Ponera, ambaye licha ya majukumu mengi mengine yaliyomkabili lakini alijitolea kuniongoza na kunishauri hatua kwa hatua hadi kuikamilisha kazi hii. Ahsante kwa msaada wako usioweza kulipika kwa kitu chochote cha thamani ila Mungu akulipe kheri kwa kukuingiza peponi. Amin.

Pili, nawashukuru wahadhiri wangu wote, hasa Dkt. A. S. Ponera na Dkt. R. Y. Sebonde, kwa mwongozo walionipa katika kipindi chote nilichokuwa darasani kwa masomo.

Tatu, nawashukuru wanafunzi wa shahada ya kwanza wanaosoma fasihi ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu vya Dodoma, Chuo cha Kumbukumbu ya Abdul-Rahmani Sumeiti na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, kwa ushirikiano na mchango mkubwa walionipa hadi kukamilika kwa tasnifu hii. Kwani bila ya ushiriki wao ukusanyaji wa data usingekuwa na ufanisi.

Nne, shukurani za pekee zimwendee mke wangu, Mossi M. Ame, pamoja na watoto wangu, Khairat, Fatma, Husna, Abdul-latwifu na Mudrik, kwa uvumilivu mkubwa waliouonesha katika kipindi chote cha masomo yangu. Nawapa hongera kwa utulivu, msaada na mchango mkubwa walionipa. Kwa hivyo, nakiri na kuuthamini mchango wa hali na mali wa kila aliyenisaidia hata kwa kiwango kidogo. Mungu atulipe na aturahisishiye kila lenye manufaa ya dunia na akhera. Amin.

## IKISIRI

Tasnifu hii inajadili matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya teule za Euphrase Kezilahabi ambazo ni *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007), *Kichwamaji* (1974) na *Rosa Mistika* (1971). Tatizo lililomsukuma mtafiti kufanya utafiti huu ni kujaza pengo la kiutafiti juu ya matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule. Hii ni kutokana na tafiti zilizopo maktabani kuzungumzia juu ya mazingaombwe, aina na uhalisia wake tu. Kwa kutumia nadharia ya Uhalisiajabu mtafiti alichunguza matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule.

Utafiti uliongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu, huku ukijiegemeza katika muhimili wa kuwaeleza wahusika wa ajabu ajabu, mandhari na matukio ya kifantasia au ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, hadi kuyafanya yaonekane ya kawaida katika jamii. Data zilikusanywa maktabani na uwandani kwa upande wa Zanzibar na Dodoma. Mbinu zilizotumika katika utafiti huu ni Udurusu wa Maktabani. Data zilichanganuliwa kwa kuzingatia maelezo ya utafiti pamoja na msingi wa nadharia ya Uhalisiajabu. Utafiti umegundua kuwapo kwa matumizi ya falsafa ya usihiri. Kwa hiyo, utafiti umetoa mchango mkubwa katika kipengele cha fasihi andishi ya Kiswahili kwa upande wa riwaya.

Mchango mpya ulioibuliwa kutokana na utafiti huuni kuwapo kwa aina mbalimbali za usihiri katika riwaya teule na katika jamii ya Watanzania. Nazo ni usihiri wa kufarakanisha, usihiri wa mapenzi, usihiri wa sauti, usihiri wa mazingaombwe na usihiri wa hirizi. Mwisho, nadharia ya Uhalisiajabu kwa kutumia msingi wake imekuwa faafu kwa kufanyia tafiti juu ya riwaya zenye matendo, matukio na wahusika wa ajabuajabu. Na usihiri umebainika kuwa na faida na hasara.

## YALIYOMO

ITHIBATI ..... i
IKIRARI NA HAKI MILIKI ..... ii
TABARUKU ..... iii
SHUKURANI ..... iv
IKISIRI ..... v
YALIYOMO ..... vi
ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA ..... x
SURA YA KWANZA ..... 1
UTANGULIZI ..... 1
1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti Huu ..... 1
1.1.1 Falsafa ..... 1
1.1.2 Falsafa ya Kiafrika ..... 1
1.1.3 Usihiri ..... 2
1.1.4 Uchawi ..... 5
1.1.5 Ushirikina ..... 6
1.1.6 Uhalisiajabu ..... 8
1.2 Historia Fupi ya Euphrase Kezilahabi ..... 10
1.3 Usuli wa Tatizo la Utafiti ..... 13
1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti ..... 22
1.5 Malengo ya Utafiti ..... 23
1.5.1 Lengo la Jumla ..... 23
1.5.2 Malengo Mahsusi ..... 23
1.6 Maswali ya Utafiti ..... 23
1.7 Manufaa ya Utafiti ..... 24
1.8 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ..... 24
SURA YA PILI ..... 25
KIUNZI CHA NADHARIA NA MAPITIO YA MAANDIKO ..... 25
2.1 Utangulizi ..... 25
2.2 Kiunzi cha Nadharia ya Utafiti ..... 25
2.3 Mapitio ya Maandiko ..... 32
2.3.1 Maandiko Kuhusu Falsafa na Fasihi kwa Jumla ..... 32
2.3.2 Maandiko Kuhusu Usihiri na Mazingaombwe Ndani ya Kazi za Fasihi ..... 37

2.3.3 Maandiko Kuhusu Usihiri Nje ya Kazi za Fasihi ....................................................40
2.3.4 Maandiko Kuhusu Riwaya za Eupharase Kezilahabi ..............................................43
2.4 Mapengo Yaliyojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko ...................................47
2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili ...........................................................................................47
SURA YA TATU ..............................................................................................................49
METHODOLOJIA YA UTAFITI....................................................................................49
3.1 Utangulizi ....................................................................................................................49
3.2 Mpango wa Utafiti ......................................................................................................49
3.3 Eneo la Utafiti ...........................................................................................................49
3.4 Walengwa wa Utafiti...................................................................................................50
3.4.1 Jamii ya Watafitiwa...................................................................................................50
3.4.2 Usampulishaji na Sampuli Iliyotumika ..................................................................51
3.5 Ukusanyaji wa Data za Utafiti....................................................................................52
3.5.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data............................................................................52
3.5.1.1 Udurusu wa Maktabani...........................................................................................52
3.5.1.2 Dodoso......................................................................................................................52
3.5.1.3 Mahojiano ...............................................................................................................53
3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data...........................................................................53
3.6 Uchanganuzi wa Data .................................................................................................54
3.7 Itikeli za Utafiti............................................................................................................54
3.8 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti ...........................................................54
3.9 Mipaka ya Utafiti .........................................................................................................55
3.10 Changamoto Zilizojitokeza na Utatuzi Wake..........................................................55
3.11 Muhtasari wa Sura ya Tatu........................................................................................56
SURA YA NNE..................................................................................................................57
UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI.................................57
4.1 Utangulizi .....................................................................................................................57
4.2.1 Historia ya Usihiri kwa Jumla ..................................................................................58
4.2.2 Vijenzi vya Usihiri ......................................................................................................59
4.2.2.1 Jini ............................................................................................................................59
4.2.2.2 Shetani ......................................................................................................................60
4.2.2.3 Nyota .........................................................................................................................62
4.2.2.4 Ramli .........................................................................................................................64

4.2.2.5 Mzimu......65
4.2.2.6 Mitishamba......66
4.2.3 Muhtasari wa Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi......67
4.2.3.1 Muhtasari wa Riwaya ya Rosa Mistika......67
4.2.3.2 Muhtasari wa Riwaya ya Kichwamaji......67
4.2.3.3 Muhtasari wa Riwaya ya Dunia Uwanja wa Fujo......68
4.2.5 Aina za Usihiri Zinazojitokeza katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi......71
4.2.5.1 Usihiri wa Kufarakanisha......71
4.2.5.3 Usihiri wa Mapenzi......81
4.2.5.4 Usihiri wa Mazingaombwe......85
4.2.5.5 Usihiri wa Hirizi......91
4.3.1 Miktadha ya Kifo......95
4.3.2 Miktadha ya Makazi......102
4.3.3 Miktadha ya Matibabu na Usafiri......105
4.3.4 Miktadha ya Uzazi na Mapenzi......109
4.4 Sababu Zichangiazo Kutokea kwa Falsafa ya Usihiri katika Riwaya za Mtunzi Teule 114
4.4.1 Shughuli za Kisiasa......114
4.4.2 Shughuli za Kiuchumi......116
4.4.3 Shughuli za Kiutamaduni......120
4.4.4 Sababu za Kitajiriba......123
4.5 Athari za Matumizi ya Falsafa ya Usihiri katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi kwa Jamii......126
4.5.1 Athari Chanya......126
4.5.1.1Kuimarisha Mapenzi......127
4.5.2Athari Hasi......132
4.5.2.1 Kuingiza Maradhi Mwilini......132
4.5.2.2 Kujenga Maadili Mabaya......135
4.5.2.3 Kuleta Ugomvi Ndani ya Jamii......139
4.6Muhtasari wa Sura ya Nne......141

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ................142**
5.1 Utangulizi ..........................................................................................142
5.2 Muhtasari wa Tasnifu..............................................................................142
5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika..................................................144
5.3.2 Mchango Mpya Uliopatikana Kutokana na Utafiti..................................145
5.3.3 Maoni ya Mtafiti juu ya Utafiti Uliofanyika ...........................................146
5.4 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ...............................................................147
**MAREJELEO.............................................................................................149**
**VIAMBATISHO..........................................................................................157**
A: Barua za Ithibati ya Kufanyia Utafiti.........................................................157
A.2 Barua Kutoka Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ....158
A.3 Barua Kutoka Afisi ya Makamu wa Pili wa Raisi wa Zanzibar ...............................159
C.1 Picha Mbalimbali Zinazohusiana na Utafiti ...........................................................165

## ORODHA YA VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA

*AD =Anno Domini* (Maana yake ni baada ya kifo cha Kristo)

AS =Alaihi Salamu (Amani za Mwenyezi-Mungu zimshukie juu yake; mtue)

BAKIZA =Baraza la Kiswahili Zanzibar

*BC =Before Crist* (Maana yake ni kabla ya Kristo)

Bw =Bwana

Dkt =Daktari

*FM = Frequency Modulation* (Maana yake ni mfumo unaotumiwa na radio kurushia matangazo)

H =Hijiria (Baada ya kuhama mtume Muhamad na waisilamu kutoka Maka kwenda Madina)

Ht =Haina tarehe

Kv =Kama vile

Khj =Keshatajwa hapo juu

*Pg =Page*

*PhD* =Falsafa ya Udaktari

RA=Radhiyallahu Anhu (Radhi za Menyezi-Mungu zimshukie juu yake; mtume)

SAW=Swalallahu Alaihi Wasalama (Sala na amani za Mwenyezi-Mungu ziwe juu yake; mtune)

SW =Subuhanahu Wataala (Maana Mwenyezi-Mungu aliyetukuka)

TUKI =Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

Uk =Ukurasa

*WWW =World Wide Web*

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti Huu

Istilahi zilizofafanuliwa ni falsafa, falsafa ya Kiafrika, usihiri, uchawi, ushirikinana uhalisiajabu.

### 1.1.1 Falsafa

Kwa mujibu wa (Chuachua, 2010:10) anafafanua kuwa, falsafa ni taaluma ya kutafuta ukweli kuhusu jambo fulani (maisha) kwa njia ya kutafakari. Mtaalamu huyu anaiona falsafa kuwa, hutumika "kujenga mihimili ya hoja ili kuleta mapinduzi."Kwa upande mwingine falsafa ni tawi la elimu linalohusu asili, maana na sababu za vitu au mambo. Pia, kwamujibu wa *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010:80) falsafa ni mtazamo wa mtu kuhusu jambo fulani. Nayo,Wizara ya Elimu na Utamaduni (1992:45) inafafanua kuwa, falsafa ni taaluma inayojishughulisha na kutafuta ukweli wa jambo kwa njia ya kutafakari. Maelezo hayo yanathibitisha kuwa, falsafa ni mtazamo alionao mwanadamu katika kufikiria mambo yanayotokea. Kwa hivyo, falsafa inaweza kufafanuliwa kuwani elimu ya kutafuta uhakikawa mambo fulani katika maisha kwa njia ya kutafakari, huku mwanafalsafa akiongozwa na taratibu za kuyapatia ufumbuzi mambo yatokeayo katika jamii kwa kutumiahekima ndani yake. Hivyo, falsafa hutumika kutafuta ukweli wa matukio mbalimbaliya usihiri na mengineyo katika jamii.

### 1.1.2 Falsafa ya Kiafrika

Chuachua, 2016:07) anaifasili falsafa ya Kiafrika kuwa, ni taaluma inayoisaka kweli kwa njia ya kuutafakari ulimwengu. Naye(Simchimba, 2012:18) anafafanua kuwa falsafa ya Kiafrika ni jumla ya mitazamo, mielekeo na misimamo waliyonayo Waafrika juu ya mambo yanayowazunguka na yanayowatofautisha kati yao na jamii nyingine. (Label,

2013:2) anashadidia kuwa, falsafa ya Kiafrika, ni jumla ya mawazo na matendo waliyonayo Waafrika na matumizi yake katika kukabiliana na mazingira yanayowakabili kupitia maisha yao ya kila siku. Falsafa hii hutumika kumsaida mwanadamu kuweza kuwatawala majini na mashetani pamoja na viumbe wingine. Aidha, hutumika kuvitiisha viumbe vyote kwakutumia nguvu ya akili aliyonayo mwanadamu na kupaa angani kama ni njia mojawapo ya kukitekeleza kipengele kimojawapo cha falsafa ya Kiafrika kupitia usihiri. Hivyo, maelezo ya wataalamu hao yanathibitisha kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika. Kwa jumla,falsafa ya Kiafrika inaweza kuelezewa kuwa ni jumla ya fikra, mienendo, ukweli, na matendo yanayohusu na yanayolipambanua bara la Afrika na jinginelo ambayo Waafrika wanayaamini, wanayafuata, wanayatumia na wanayafanikisha katika nyanja mbalimbali kupitia maisha yao.

### 1.1.3 Usihiri

Ni tabia ya kufanya matendo ya kuangamiza na kuchukiza, yanayofanywa na wasihiri kwa msaada wa majini na mashetani kwa lengo la kuwadhuru wasihiriwa katika hali ya kificho na kubadilika badilika kwa mtindo wa kuhadaa na kushangaza machoni mwa hadhira(Audhi, 2004:143). Naye(Baali,1417H:13) anashadidia kuwa, usihiri ni makubaliano baina ya mchawi, mashetani pamoja na majini katika kuvitekeleza vitendo vya haramu, baada ya msihiri kukubaliana pamoja na kuwatii viumbe hao kwa wayatakayo. Hii ni kutokana na msihiri kupewa masharti wayapendayo majini na mashetani katika kumtumikia. Kwa mfano,msihiri kushurutishwa kuwatoa watu kikoa; yaani, kuuliwa watu katika mazingara ya usihiri na kupelekwa giningi, lakini wakifika huko wanakuwa wako hai.Pia, kuchinja wanyama huku damu yao kunyweshwa majini na mashetani.

(Ali, 2014:20) anafafanua kuwa, usihiri ni kila jambo ambalo sababu yake imefichika na imesawiriwa kwa namna isiyo ya hakika, pamoja na uficho na hadaa ili kuleta athari kwa msihiriwa au katika mazingira lengwa.Pia, (Buhairi, 2011:21) anashadidia kuwa, mambo yanayoweza kuzingatiwa katika kuibua usihiri ni pamoja na;kwanza, kuibuka mandhari zenye hisia nzito na za kuogofya hadi kuwafadhaisha wahusika.Pia, kutokwa na akili au kuzurura bila ya kujitambua. Pili, kudhihiri na kutumika kwa mojawapo kati ya vijenzi vya usihiri, kama vile jini na shetani wanaotia wasiwasi, mawazo mabaya na fikira mchanganyiko kwa wahusika na kufanya matendo yasiyo ya kawaida yasiyo na mpangilio maalumu katika maisha yao.Tatu, kujitokeza kwa ndoto zisizo za kawaida mawazoni mwa wanajamii, kuwapo kwa zana maalumu za kukamilishia matukio na matendo ya kutisha na kuzivutia nafsi za wasihiriwa hadiwakafanya mambo bila ya kutarajia au kujifahamu. Hali hizo za kubadilika kwa mitindo hiyo ndiyo inayochochea kutokea kwa usihiri. Kwa jumla, maelezo ya wataalamu hao yametoa mwongozo wa jumla kuhusu dhana ya usihiri.

Hata hivyo, usihiri unaweza kuelezewa kuwa ni hali ya uchawi au uramali wa kimaneno na kimatendo yanayosawiriwa kwa kificho, kugeuka geuka na kuhadaa. Hukamilika kwa manuwizi ya kisihiri na kishirikina baada ya uambatanishwaji wa shetani kutoka kwa mchawi ili kuleta athari katika mwili, moyo au akili ya msihiriwa.

(Swabru, 2009:6) anabainishadalili za usihiri kwa msihiriwa kuwa, huumwa na kichwa mara kwa mara au kiungo chochote katika hali ya kudumu, presha isiyoshuka na kuvilia katika macho. Dalili nyingine nikuingiza gesi, kutokwa na damu ya hedhi kwa wanawake bila kusita au kutokauka kabisa mwilini mwa msihiriwa.Aidha, usihiri hutumika kwamtu kuoteshwa ndoto bila ya kutozifahamu wakati anapoamka. Pia, ndoto za vitisho, kufukuzwa na wanyama wakali usingizini na kulifanya jicho la upande wa kushoto kuwa dogo kuliko jingine. Aidha, usihiri hutumika ili mshiriwa kupata uchovu saa zote,kuhisi

usingizi, macho kupata kiza kinachomzuia kufanya kazi na ibada kwa wakati huo.Maumivu ya kushangaza ya mgongo, moyo, kiuno, miguu na msihiriwa kuota anapelekwa kwenye watu wengi anapokuwa amelala.

Usihiri ni taaluma inayojikita katika fani ya falsafa ambayo hufafanuliwa kwa kutumia nadharia ya Uhalisiajabu,na imehusishwa na bunilizi za waandishi mbalimbali hususani riwaya. Dhana ya usihiri katikabunilizi za riwaya imefafanuliwa na wataalamu kadhaa wakiwamo Safari (1993), Mung’ong’o (1977) na Abdahu (2011). (Mung’ong’o, 1977:12-20) anafafanua kuwa matumizi na ukamilishwaji wa matendo ya usihiri katika riwaya, hujumuisha mambo kama vile mapango, mizimu, tunguli, mikoba, waganga, elimu na maarifa katika kuufanikisha usihiri, pamoja na mazingara ya wachawi na vyombo maalumu vya kurukia na kusafiria.

Aidha, taaluma yausihiri inatawaliwa na kanuni, miiko pamoja na sheria.Ikiwamo sheria ya kutunza siri za taaluma yenyewe. Kwa hivyo, Matumizi ya usihiri katika kazi za fasihi ni matokeo na mabadiliko ya usanaji wa kazi husika ili kwenda sambamba na mahitaji ya wasomaji.Aidha, kuwaburudisha na kufikisha ujumbe, pamoja na kuwafahamisha kuwa sayansi ya usihiri nafasi yake imechukuliwa na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Kwa jumla, usihiri umetumika katika hali mbili. Mosi, kuleta ukombozi dhidi ya unyang’anyi na uvamizi wa haki za wengine, kama vile mashamba na mifugo ili warudishiwe wenye haki hiyo. Pili, kuweka bayana athari za matumizi mazuri na mabaya yanayotokana na usihiri. Kwa kusema kuwa matumizi mabaya ya kitu chema hayafanyi kitu hicho kuwa kibaya, na kinyume chake. Pia, (Safari,khj:60) anafafanua sifa tatu za usihiri kuwa: mosi, anayeingia katika usihiri yampasa kula kiapo cha kujiunga na fani husika ili kutunza siri zilizoko. Pili, wasihiri huishi chini ya ulinzi kuliko wanavyolindwa maraisi na viongozi wa nchi. Tatu, taaluma ya usihiri inatawaliwa na sura mbili; yaani, ya wema na ya uovu.

Watu walio wengi huiona sura ya uovu na kuibananga taaluma husika.Taaluma ya usihiri inaweza kutumika kwa kuleta maendeleo na hata katika ulinzi. Kwa mfano, wasihiri wanaweza kuruka na kusafiri mbali kwa muda mfupi tena bila ya kuonekana. Hivyo, usihiri unao faida.Kwa jumla, ili usihiri utokee lazima pawepo mazingira, wahusika na matukio ya ajabuajabu yanayosawiriwa na msihiri kwa kutumia msaada wa majini na mashetani.

### 1.1.4 Uchawi

Kwa mujibu wa (Chuachua, 2016:288-289) anaufasili uchawi kuwa, ni dhana ya kimetafizikia[1] na wakati mwingine kiontolojia[2] kutokana na kuwapo kwa kani zinazoweza kuleta athari kutoka kwa mchawi hadi kwa aliyekusudiwa akiwa umbali wowote ule. Wahenga ni sehemu muhimu katika kupambana na kani za uchawi. Pia, 'uchawi unatumiwa kama sifa ya utambuzi wa 'mtu kweli' na 'si mtu' kama kigezo cha Ontolojia ya Kibantu.'Nalo*Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010:413) linaelezea kuwa uchawi ni utumiaji wa vitu mbalimbali kiufundi kama vile maandishi au mitishamba ili kumdhuru mtu; urogi. Pia, uchawi ni kitu chochote kinachotumiwa na mganga wa kienyeji kuleta madhara kwa mtu mwengine. Pia,*Kamusi la Kiswahili Sanifu* (2001:412) linaelezea kuwa uchawi ni ufundi wa kutumia dawa, aghalabu mitishamba na vitabu maalumu vya uganga ili kuleta madhara kwa viumbe; yaani, usihiri. Pia, (Safari, 1993:155) anafafanua kuwa, uchawi ni ufundi; yaani, utaalamu wa kutumia sio dawa tu, bali mbinu nyingine mbalimbali pamoja na vitabu maalumu vya uganga na mitishamba ili kuleta madhara kwa viumbe. Taaluma ya ufundi huu (uitwao uchawi) aghalabu huaminika na hutumika

---

[1] Ni tawi la falsafa linalotumika kutafakari kuhusu mambo na matukio ya ulimwengu kwa jumla ili kuyabainisha na kuyatofautisha yale yaliyo halisi na yasiyo halisi.Pia, falsafa hujishughulisha na kutafakari nafasi ya mwanadamu katika ulimwengu wake (Chuachua, 2016:9).

[2] Ni taaluma ya falsafa inayoshughulikia asili ya kuwapo au kuishi. Pia, hushughulikia kategoria za kuwapo pamoja na mahusiano yake. Taaluma hii kwa miaka mingi imekuwa ikijulikana kama metafizikia. Ontolojia hujishughulisha kujibu maswali kama vile, vilivyokuwapo ni vipi au vinavyosemekana kuwapo ni vipi? Vilivyokuwapo vinaweza kuwekwa katika makundi huku vikihusianishwa kulingana na viwango vya kidarajia pamoja na kufanana ama kutofautiana kwao? (Chuachua, 2016:08).

kuhasiri viumbe. Hapa haina maana kuwa hauwezi kutumiwa kwa manufaa. Maelezo haya yanabainisha kuwa uchawi hutumika kuleta madhara zaidi katika jamii kuliko manufaa. Hii ni kutokana na tabia ya roho mbaya na husda walizonazo wachawikatika matendo ya usihiri.Aidha,uchawi hutumika kuwaangamiza walengwa, pamoja na kuingiza bughudha na chuki kwa wasihiriwa ndani ya jamii. Kwa hivyo, uchawi unaweza kuelezewa kuwa ni imani, dhana na matendo ya uhakika yanayofanywa na wasihirikwa kutumia msaada wa majini na mashetani ili kuleta madhara kwa wasihiriwa kwa manufaa ya wasihiri. Tofauti iliyopo kati ya uchawi na usihiri ni ya kiistilahi tu bali zinalingana kitabia, kimatendo, kimazingira na kimandhari zinapotekelezwa na wasihiri (wahusika) wa matendo ya usihiri.

### 1.1.5 Ushirikina

*Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010:440) linafafanua kuwa, ushirikina ni tabia ya kuamini kuwapo kwa kiumbe kinginekwa kumdhuru mtu badala ya Mwenyezi-Mungu mwenye uwezo huo. Kwa mnasaba huo, ushirikina hutumika kuingiza hofu nyoyoni mwa wanadamu wengine na kuleta madhara ya kimwili, kijamii na kiutamaduni.(Al-Fauzi, ht:9) anafafanua kuwa, ushirikina ni kumjaalia Mwenyezi-Mungu kuwa na mshirika katika uumbaji na nguvu zake katika maisha yakila siku. Hii ni kutokana na msihirikina kuchanganya maombi na matendo kwa kutaka msaada wa asiyekuwa Mwenyezi-Mungu;aukumfananisha na kitu miongoni mwa ibada[3] ambazo zinastahiki kufanyiwa Mola pekee. Mathalani, kufanya ibada ya kuchinja kwa ajili ya mashetani na majini, wanadamu kujibadilisha kutoka sura moja hadi nyingine, pamoja na kuogopa madhara yaletwayo na mizimu. Aidha, kuruka angani kwa msada wa jinipamoja na kuchinjwa

[3] Ni kila jambo analolifanya mwanadamu ambalo analiridhia Mwenyezi-Mungu kupitia mfumo wa maisha ya kila siku (Ashkara, 1953:11).

wanadamu ndani ya mizimu ili kutoa kafara. Kwa hivyo, matumizi mabaya ya ushirikina huiangamiza jamii na kukosa maendeleo.

Maelezo hayo yanabainisha kuwa, ushirikina hutokea na hutumika katikahali kadhaa, baadhi yazo ni; kwanza, panapowekwa usawa wa uwezo alionao Mungu na ule alionao kiumbe. Hali hii hudhihiri kwa wasihiri kuona nguvu alizonazo Mungu ziko sawa na za kiumbe kwa utendaji, maombi na kukitaka msaada kiumbe wa aina yoyote. Kwa mfano, uwezo wa Mwenyezi-Mungu ni kuumba ulimwengu na kila kitu kilichomo. Uwezo huo hupewa na huegemezewa majini na mashetani kwa kuombwa na kutakiwa waumbe au watengeneze viumbe wafananao na wa Mungu. Au kutakiwa kuwalinda wanadamu ili wasidhuriwe na wachawi pamoja na kuleta kitu chochote kilicho nje ya uwezo wake. Yatokeapo hayo panakuwa panafanywa ushirikina kwa kuuweka uwezo wa kiumbe pasipo mahala pake. Aidha,ushirikina hutumiwa na mwanadamu kufanyia maombi ya sala kwa kukiomba kiumbe badala ya Mwenyezi-Mungu.

Pili, ushirikina hutumika kufanyia matendo ya kuogofya,kuzungumza na majini na mashetani, kuabudia mizimu na mapango, kuruka, kujigeuza mbwa na kuchinja wanyama huku damu wakipewa majini. Yote hayo hupelekea kuviona vijenzi vya usihiri kama vile shetani, mizimu na mapangokuwa na uwezo sawa kama alionao Mwenyezi-Mungu. Ushirikina upo wa aina mbili. Mosi, ushirikina ulio wa daraja ya juu. Huu ni ule unaoambatana na matendo ya uuwaji kwa kupelekwa watu mizimuni na ukataji wa viungo vya watu walio hai kwa lengo la kupata utajiri. Viungo hivyo huchanganywa na dawa za mitishamba. Aidha, kufanya matambiko kwa ajili ya mizimu na kuiomba, kufuga majini na kuwatuma kama walivyo viumbe wengine, kuomba makaburini na kufukua wafu kwa ajili ya kuchukuwa viungo vyao. Kama vile mifupa na mafuvu ya vichwa. Pili, usihiri wa daraja ndogo.Huu ni ule ambao haumtoi mhusika katika imani ya dini lakini hupelekea

kufanya maasi mbele ya Mungu. Kwa mfano, kuamini kuwapa kwa asiyekuwa Mungu au kufananisha kuwa mtu fulani yuko sawa na Mungu kwa huruma pamoja na kuzitegemea talasimu na hirizi katika kuondoa madhara. Maelezo yaAl-Fauzi (khj) ni kielelezo tosha kinachoonesha matumizi ya ushirikina katika kuufanikisha usihiri.

Maelezo ya*Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010) na Al-Fauzi (ht) yanabainisha kuwa, ushirikina hutumika na kujitokeza katika nyanja tatu; mosi, kufanya matendo yasiyo ya kawaida ya kuogofya na kushangaza. Kwa mfano, kuchinja mbuzi na kondoo mwenye sifa na rangi maalumu, kisha damu yake kupelekwa mizimuni na kupewa mashetani. Pili, mtendaji wa ushirikina hushirikiana na kufuata maelekezo ya viumbe wa ajabu na kuwasiliana nao katika ufanikishaji wake. Tatu, msihiri hutawaliwa na lugha za majini na mashetani pamoja na kuzungumza nao katika sehemu maalumu kama vile katika mapango,kilingeni na mizimu. Kwa jumla, ushirikina unaweza kuelezewakuwa ni tabia ya mshirikina kuamini na kufanya vitendo au maneno juu ya uwezo mkubwa wa kiumbe kingine kuleta madhara badala ya ule wa Mwenyezi-Mungu kwa kutumia majini, mizimu, talasimu za kisihiri na hirizi katika kufanikisha jambo fulani.

### 1.1.6 Uhalisiajabu

Istilahi hii imejengeka kwa maneno mawili; uhalisi na ajabu. Uhalisi ni hali ya jambo lilivyo *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010:420).Hii ina maana kwamba, uhalisini kuelezewa jambo kama lilivyo bila ya kuongeza au kupunguza. Pia, *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010:04)linazidi kufafanua kuwa, ajabu ni jambo lisilo la kawaida linaloshangaza na kufurahisha. Au tamko linaloonesha kiwango cha kushangaza. Kwa hivyo, muunganiko wa maneno hayo unafanya kupatikana kwa neno uhalisiajabu. Uhalisiajabu ni istilahi inayotumika kuelezea mkondo wa uandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia; yaani, kwa kuyaelezea

kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida kutokea katika jamii (Wamitila,2002:60).Hivyo, kufanyakazi kwa Uhalisiajabu hutokea kwa namna ya ajabuajabu katika jamii.

Kulingana na madai hayo,nadharia ya Uhalisiajabu inatumika kuelezea matukio ya moja kwa moja ya usihiri kwa njia iliyozoeleka na kuonekana ya kawaida katika jamii. Katika kuzingatia utokeaji wa Uhalisiajabu kwa mujibu wa (Wamitila, khj:117) anashadidiakuwa,huhitajika kutokea kwa mambo matatu. Mosi, kazi zinazotungwa kwa kutumia mtindo wa Uhalisiajabu huchanganya sifa za kihalisia na za kiajabu kupitia matendo yasiyoaminika katika kutokea kwake. Pili, hutawaliwa na mazingira, mandhari na wahusika wa ajabuajabu kupitia maneno na matendo yao.Tatu, mpaka uliopo kati ya yanayowezekana (mambo ya halisia) na yasiyowezekana unafutwa.Maelezo ya wataalamu hao yanabainisha kuwa, uhalisiajabu hutumika kuyaeleza mambo na matukio yasiyo ya kawaida kutokea ndani ya jamii, bali kwa kutumia nadharia hiyo huelezewa kama ya kawaida.

(Alexander, 1990:127) anashadidia kuwa, Uhalisiajabu hutumika kuelezea kazi zinazozungumzia usasa leo unavyomlazimu mwanadamukufikiria upya juu ya riwaya za kimapokeo kuhusu riwaya za uhalisia za karne zilizopita. Naye(D’Haen, 2005:191) anasisitiza kuwa, Uhalisiajabu ni tawi mahsusi la usasabaadaye (*Postmodernism*) linalotumika kuelezea sifa za Uhalisiajabu kama vile; kujirejearejea, uziada uliopindukia, uanuwai, mseto wa vitu, mwingilianomatini, kuchezea na kuyumbisha uthabiti wa wahusika na usimulizi wao. Aidha, kumchanganya msomaji kwa makusudi, kufuta mipaka iliyopo kati ya ulimwengu halisi na wa kubuni pamoja na vitu au hali tofauti. Pia, hutumika kuelezea hali iliyopoya kushangaza na kuogofya, mambo ya kiajabuajabuhuelezwa kwa namna ya moja kwa moja na kuonekana kuwa ya kawaida

kutokea katika jamii.Maelezo hayo yanaweka wazi matumizi ya Uhalisiajabu katika kazi za fasihi. Kwa jumla, Uhalisiajabu unaweza kuelezewa kuwa, ni hali ya maajabu, usihiri, mazingaombwe, vituko na miujiza, isiyowekewa mipaka iliyomo kwenye uyakinifu na uhalisi wa mambo yawezekanayo au la katika utokeaji wake wa kila siku. Kwa jumla, istilahi hizi zimesaididia kujua, kutoa mwelekeo, mijengeko na hali tofauti za matumizi ya falsafa ya usihiri.

## 1.2 Historia Fupi ya Euphrase Kezilahabi

Euphrase Kezilahabi[4] alizaliwa tarehe 13 Aprili, 1944 kisiwani Ukerewe[5] katika kitongoji cha Kalibusere, katika kijiji na kata ya Namagondo, iliopo tarafa ya Mbuga, wilayani Ukerewe, katika mkoa wa Mwanza. Kwa mujibu wa Ponera (2014b) akimnukuu mzee Pantaleo anasema kuwa, jina la Euphrase Kezilahabi limechimbuka kutokana na majina ya kijadi ambalo kwa ukamilifu wake ni Euphrase Vicent Mfunzi Kezilahabi anasema:

> Jina la Kezilahabi ni la kijadi; maana yake ni 'aliyekuja wakati wa matatizo'. Matatizo yaliyoikumba familia yao kabla ya kuzaliwa kwake na kuwafanya wazazi wampe jina hilo ni vifo vya ndugu kadhaa waliomtangulia Kezilahabi kuzaliwa. Katika ukoo wao watoto walipewa majina kulingana na sababu au mazingira maalumu yaliyogubika kuzaliwa kwa watoto husika. Wote hasa wanaume, wana majina yenye maana ya kijadi. Kuna Pantaleo Nagane, Deonatus Mnalwa, Valentino Msilangwa, na Evarist Mkwaya (Valentino na Evarist ni mapacha). Kwa mfano, maana ya neno 'nagane' ni mtu 'mjinga-mjinga (Ponera, 2014b: 128).

Eupharase Kezilahabi ni mtoto wa nane kati ya watoto tisa aliowazaa mama yake Euphrase Kezilahabi aitwaye Tilibuzya Edina Bilenjo, na baba yake aitwaye Vicent Mfunzi Bagaza. Jumla ya watoto wa kiume ni watano na wa kike ni wanne. Hadi sasa Euphrase Kezilahabi ana mke na watoto watatu ambao ni Alfred, Neema na George.

[4]Ni mwandishi wa riwaya, mashairi, tamthiliya na insha zinazohakiki fasihi. Fununu zinazopatikana katika maandishi yake zinaonyesha kwamba pengine ama yu miongoni mwa wadhanaishi wasiokuwa na uhakika kwamba Mungu yupoau miongoni mwa wale wasiokuwa waumini kabisa (Wafula na Njogu 2007:75).

[5]Nimojawapo ya visiwa vilivyomo katika ziwa viktoria. Kisiwa hicho hukaliwa na makabila makubwa mawili; Wakerewe na Wakara. Wakara asili yao katika kisiwa kingine kidogo zaidi kiitwacho Ukara kilichopo katika ziwa hilo (Ponera, 2014b, 133).

Alianza kujiunga na elimu ya msingi mwaka 1952 hadi 1956 alipomaliza darasa la nne katika shule ya msingi Nakasahenge, kijiji cha Namagondo. Alichaguliwa kuendelea na masomo ya darasa la tano hadi la nane katika shule ya Seminari ya Mtakatifu Maria ilioko Nyegezi, katika mji wa Mwanza. Baada ya kufanya vizuri katika mitihani yake aliendelea na masomo ya kidato cha kwanza hadi cha sita shuleni hapo ambapo aliishi kwa muda wa miaka kumi takriban. Mara baada ya kumaliza elimu ya sekondari alijiunga na Chuo Kikuu cha Afrika Mashariki. Kwa hivi sasa kinajulikana kama Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam mnamo mwaka 1967. Alihitimu masomo ya shahada ya kwanza mwaka 1970. Aliendelea na masomo ya shahada ya umahiri na kumaliza mwaka 1976. Hatimaye, mwaka 1985 alihitimu masomo ya shahada ya uzamivu katika chuo kikuu cha Wisconsin-madson kilichoko Marekani.

Euphrase Kezilahabi ni mwenye tabia njema, mkimywa na mpole wa kuzungumza. Na anapenda kuchanganyika na kushirikiana na watu wa rika zote katika shughuli mbalimbali za maisha. Maelezo hayo yanashadidiwa na Ponera (2014b:131) akiwanuku Mwenda, Mbatiah, Kitula na King'ei waishio nchini Kenya wanaosema:

> Mtu huyu ana chembechembe nyingi za uanafalsafa. Na hiyo ni baadhi tu ya tabia za wanafalsafa wengi. Wao huwa wakali kwenye kalamu; ilhali huwa wanyamavu na wenye mawazo sana ukiwa nao ana kwa ana.

Dondoo hili linathibitisha kuwa, tabia ya mtunzi ni ya ukimya kama walivyo wanafalsafa wengine. Kwa upande mwingine umbile la mtunzi ni la wastani, mwenye urefu wa futi tano hadi sita, mchangamfu, ni mtu wa watu asiye na majivuno, ni mpigania haki asiyependa kuonewa. Hali hii inathibitika kupitia maandiko yake. Mtunzi alichipukia katika ubunifu wa maandishi ya kazi mbalimbali za fasihi mnamo miaka ya sitini na sabiini katika karne ya ishirini. Ponera (2014b:141) anashadidia kwa kusema:

> …utunzi wake ulianza wakati ambao jamii imo katika fikra za uandishi wa kidemokrasia. Eupharase Kezilahabi alianza uandishi wake miaka ya 1970

> wakati huo tayari fasihi ya Kiswahili ilikuwa imepiga hatua kubwa. Zaidi tayari kulishazuka namna fulani ya mabadiliko katika fasihi hiyo.

Andiko hili linathibitisha kuwa, bunilizi za mtunzi zilikumbwa na mabadiliko ya kifikra juu ya usanaji wa kazi za fasihi. Mabadiliko hayo yalisababishwa na majaribio ya usanaji wa kazi za fasihi katika kipindi hicho. Kazi iliyompatia umaarufu ni riwaya ya *Rosa Mistika* (1971). Mbali na riwaya hiyo mwandishi anazo kazi mbalimbali katika uga wa fazihi zikiwemo riwaya, tamthiliya, hadithi fupi na mashairi ambapo maandiko yake kwa jumla ni kama yafuatavyo:

**a) Riwaya:**

*i) Rosa Mistika (1971);*

*ii) Kichwamaji (1974);*

*iii) Dunia Uwanja wa Fujo (1975);*

*iv) Gamba la Nyoka (1978);*

*v) Nagona (1990), na;*

*vi) Mzingile (1990).*

**b) Diwani za Mashairi:**

*i) Kichomi (1974);*
*ii) Karibu Ndani (1988), na;*
*iii) Dhifa (2008)*

**c) Tamthiliya:**

Tamthiliya pekee aliyoitunga hadi sasa ni *Kaptula la Marx (1978)*

**d) Hadithi Fupi:**

*i) ‘Wasubiri Kifo’;*
*ii) ‘Mayai Waziri wa Maradhi’;*

iii) *'Chamnyonge Utakitapika Hadharani';*
iv) *'Utapiamlo';*
v) *'Magwanda Kubilya na Vyama Vingi';*
vi) *'Ulingo wa Uchanguzi'. na;*
vii) *'Balenzi'.*

Kazi ya uhadhiri ndio aifanyayo kwa muda mrefu katika maisha yake. Alianza kufundisha katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam mnamo miaka ya themanini. Alipanda ngazi mbalimbali kwa kuanzia na msaidizi mkufunzi, mhadhiri msaidizi, mhadhiri mwandamizi, profesa mshiriki, hadi kufikia ngazi ya profesa kamili. Aidha, alipata kufundisha katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kwa wakati huu profesa Euphrase Kezilahabi anakufunzi katika Chuo Kikuu cha Botswana.

Euphrase Kezilahabi katika maisha yake ya uandishi wa kazi za fasihi amewahi kupata tuzo kutokana na kazi hizo, miongoni mwazo ni; Tuzo ya Zeze ya mwaka 2005. Hii ilitolewa na Mfuko wa Utamaduni ambayo kila mwaka hutolewa ili kuzithamini juhudi na mchango wa wautunzao utamaduni wa Mtanzania. Nyingine ni Tunzo ya Shaaban Robert '*Memorial Prise'* aliyoipata mwaka (1995) iliyolewa na Baraza la Kiswahili kwa sababu ya uandishi bora wa kazi zake hapa Tanzania. Na tuzo ya Kiitaliano ya *Edwardo Sanguinett Memorial Prise* (Ponera, 2014b; Bitende, 2012; na Faustine, 2012).

**1.3Usuli wa Tatizo la Utafiti**

Mshiu na wenzake (2007) wanazungumzia juu ya dhana ya falsafa kuwa, inatokana na maneno mawili yenye asili ya Ki-Giriki; "*philos*" na "*sophia*" yakiwa na maana ya "*love*" upendo na "*wisdom*" busara na hekima. Maelezo hayo yanabainisha kuwa, falsafa inatumika katika kuchunguza na kutafakari kwa kina juu ya asili ya vitu, sababu na maana ya mambo yatokeayo na kuyapatia ufumbuzi kwa kutumia busara na hekima. Nayo, Wizara ya Elimu na Utamaduni (1992) ikishadidia kuhusu maana ya falsafa inasema

kuwa, “Tafsiri sisisi ya neno falsafa ni kutafuta busara au kupenda hekima” maelezo hayo yanawiana na yaliyotangulia kwasababu maana zote mbili zina lengo la kutafuta jambo kwa kutumia busara pamoja na hekima. Kwa jumla, maelezo hayo yanafafanua kuwa, mwanafalsafa yoyote afikiriapo jambo, fikira hizo lazima zitawaliwe na busara, hekima pamoja na kuupata ufumbuzi wa jambo fulani lililojichomoza ndani ya jamii.

Falsafa inayo historia ndefu kama alivyo mwanadamu mwenyewe. Mwanadamu alichelewa kuigundua falsafa hadi katika karne ya kumi na sita ingawa ilikuwapo tangu alipoanza kuishi. Hii ni kutokana na udhaifu wa binadamu uliochangiwa na asili pamoja na maumbile yake. Kwa mujibu wa Mshiu na wenzake (khj:106) wanasema kuwa:

> *…By its origin philosophy started in the sixteenth 16$^{th}$century in Asia and Europe. This can proves by many documents present in Europe and Asia and other parts of the world such as Africa.*
>
> Kwa asili yake falsafa ilianza katika karne ya 16 katika Asia na Ulaya. Hii inaweza kuthibitishwa kwa maandiko mengi yapatikanayo katika Ulaya na Asia na katika sehemu nyingine duniani kama vile Afrika (Tafsiri ya Mtafiti).

Maelezo ya wataalamu hawa yanathibitisha kuwa, falsafa ilianza hivi karibuni mnamo karne ya kumi na sita tu, lakini mwanadamu kabla ya hapo tayari yupo katika dunia. Hivyo, hali hii inabainisha kuwa, mwanadamu alichelewa kugundua kuwapo kwa falsafa kwani tangu alipoanza kuishi katika ulimwengu na falsafa ilikuwapo.

Kiusuli falsafa inatokana na tabia ya udadisi, upekuzi na uhojaji wa wanafalsafa juu ya masuala yamzungukayo mwanadamu. Hii ni kutokana na silika ya utumiaji wa vipawa walivyonavyo kutaka kujua chimbuko na sababu za kila jambo litokealo katika mazingira yake. Kama vile usihirina dhana ya maisha. Mshiu na wenzake (2007) wanasema:

> *…Is the rational critical thinking in a systematic kind about the general nature of the world or reality, the justification of belief the conduct life reasoning*(pg. 106*).*

> Ni utaratibu wa kufikiri wa hali ya juu kuhusu aina zote za maumbile katika dunia au ukweli, kuzithibitisha imani na mila zikubalikazo pamoja na kutoa jawabu sahihi katika maisha (Tafsiri ya Mtafiti).

Maelezo hayo yanabainisha kuwa, falsafa ni taaluma izungumziayo juu ya ukweli wa jambo kwa kuongozwa na busara na hekima pamoja na kuyapatia ufumbuzi mambo yajitokezayo katika maisha ya kila siku. Masuala hayo hayatopatiwa ufumbuzi pasi na kuwapo kwa falsafa isaidiayo katika ujenzi wa hoja za kufikirisha. Falsafa huitofautisha jamii moja na nyingine kupitia maisha ya mwanadamu na jamii nzima kwa lengo la kuzitofautisha jamii hizo. Wataalamu kadhaa kama vile Label (2013), Chuachua (2016) na Simchimba (2012) wanaendeleza mawazo ya kuwapo kwa falsafa kwa kugusia juu ya aina na matawi yake pamoja na makundi yake. Hali hii huifanya falsafa kuwa dira iwaongozayo katika kuupata ufumbuzi wa mambo.

Falsafa ya Kiafrika hujidhihirisha katika nyanja za kiutamaduni, kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa uwakilishwaji wa maneno na matendo yafanywayo katika mazingira halisi ya Kiafrika. Nao, (Wafula na Njogu, 2007:117) wanasisitiza madhumuni ya kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika kuwa,ni kumuonyesha Mwafrika kimaneno na kimatendo kuhusu ulimwengu kusheheni falsafa. Wataalamu hawa wanaelekeza jambo la msingi kwamba, kila falsafa hujumuisha malengo pamoja na njia za kuwapo na ufanikishwaji wake. Mambo hayo ndiyo yatofautishayo falsafa ya jamii moja na nyingine.(Ponera, 2014a:21-25) anabainisha kuwapo kwa falsafa ya Kiafika na chimbuko lake. Ametaja vipengele vijidhihirishavyo katika falsafa kuwa ni; dini ambayo ndiyo chimbuko la falsafa kadhaa ziendeshazo maisha ya Waswahili,pamoja na falsafa ya ujamaa na kujitegemea. Kwa ujumla, mtaalamu huyo anathibitisha kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika kupitia kipengele cha dini kama kijenzi kimoja wapo cha falsafa hiyo.Ufafanuzi wa wataalamu hao unaweka wazi kuwa Waafrika wanayo falsafa yao kama zilivyo jamii nyingine. Hii ni kwa

sababu wanayo mawazo, fikira, ubunifu pamoja na kuyapatia ufumbuzi masuala yawazungukayo.

Maelezo hayo yanashadidiwa na *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010:80) kwa kusema kuwa, falsafa ni mtazamo wa mtu kuhusu jambo fulani. Kwa msingi wa nukuu hii inaelekeza kuwa falsafa ya Kiafrika inaangaliwa katika mitazamo, mawazo na mambo yaakisiyo maisha ya Mwafrika. Pia, inathibitisha kuwapo kwa falsafa hiyo inayotawaliwa na vigezo na misingi iegemezwayo juu ya uhai na kifo, imani, matumizi na matendo mbalimbali. Kama vile kuamini Mungu na mizimu kupitia falsafa ya Kiafrika. Ni muhimu mihimili na vigezo hivi viangaliwe kwa undani ili kuyafahamu malengo ya kila falsafa. Kwa upande wa mgogoro juu ya kuwapo falsafa ya Kiafrika au kutokuwapo, kwa kiasi kikubwa umetatuliwa na wataalamu kadhaa, kama vile Chuachua (2010) na Kenyatta (2004) kwa ubainishaji wa sifa na nguzo-msingi kwayo. Mambo kama vile uvaaji wa hirizi na kuwapo kwa dhana ya giningi ni ishara ya kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika katika uga wa usihiri. Ipo tofauti kati ya falsafa ya Kiafrika na zile zisizo za Kiafrika. Hii ni kutokana na kutofautiana kimawazo na kimtazamo kwa Waafrika na wasio Waafrika. Kwa upande wa migawanyiko na aina zake zinabainishwa kwa uwazi kwa kuzihusisha na walengwa wake.

Usihiri ni miongoni mwa kipengele cha falsafa ya Mwafrika unaoweza kufanikishwa katika Kilinge (sehemu maalumu ya kuchezea ngoma ya mahepe ya Giningi) au hata nje yake. Mambo kama vile mizimu, ramli na shetani yanaaminiwa kuwa ndiyo yaujengao usihiri wenyewe(Audhi,2004:57-58). Jamii zinazoaminifani hii hujenga dhana ya kuwa, usihiri una uwezo na nguvu za kuwadhuru watu wa mbali au wa karibu. Imani hiyo imeota mizizi barani Afrika kwa kuwafanyia wengine madhara ya usihiri. Au mtu kujifanyia mwenyewe kwa kuwadhuru wamzungukao katika familia na jamii yake. Hii

hutokana na kiapo alichoweka wakati wa kujiunga na usihiri kuwa yoyote yule amuangamize.

Ahmad (2008) akifafanua asili ya neno sihiri[6] anasema kuwa, limekusanya herufi tatu kutokana na asili ya lugha ya Kiarabu. Nazo ni; "*siin*", "*hee*" na "*ree*". Lenye maana ya mwishoni mwa usiku na mwanzoni mwa alfajiri. Hii ni kutokana na dhana ya usiku kugawanywa katika sehemu mbili (ya mwanzo na ya mwisho wa usiku). Shaarawi (1990) anaendeleza mawazo yaliyotajwa juu ya Sehemu hizo kufasiriwa kwa maana ya sahara au sihiri kunakosababisha kudhihirika yanayofichikana. Maelezo hayo yanathibitisha kuwa sihiri hutokana na mambo yanayobadilika katika hali isiyo ya kawaida, wala hayana uhakika kutokea kwake; yaani hadaa. Waarabu wanasema: "*sahartu-swabiyya*"; yaani, nimemuhadaa na kumsihiri mtoto. Wanamaanisha kuwa, anayekivutia kitu na kukihadaa basi anakisihiri. Mtume Muhammad (saw) anabainisha kuwa, "katika mambo yaonekanayo machoni mwa waja umo usihiri na katika ya siri zimo hekima". Hii ni kwa sababu mambo yaonekanayo hudhihirisha udanganyifu, huficha uhakika na kubadili hali ya ukweli kuwa ya uwongo au usihiri. Na mambo ya siri panahitaji hekima ili mtu kugundua siri zilizofichikana usihiri ukiwemo. Nyingine ni kuhadaliwa jicho "*sihirul-uyuni*"; yaani, sihiri ya macho. Au kusihiriwa jicho lione mambo yasiyokuwapo na yasiyo ya kweli kutokana na kuvutiwa kwake. Jicho hudhihirikiwa na kuona kuwapo kwa vitu vishabihianavyo, livijuavyo na vya halisi; kumbe ni vitendo vya kiini macho vifanywavyo juu yake ili kudanganyika na mazingira ya kuroga na kusihiriwa kwavyo.

Maana (asili) hiyo inawiana na neno "*witchcraft"*. Hii ni nomino yenye maana ya uchawi, ulozi, usihiri, na uramali (Johnson,1939:627). Maelezo ya wataalamu hawa yanaonesha

[6]Istilahi ya neno (sihiri) ndio asili na halisi badala ya mnyumbuliko wa neno (usihiri) lililotoholewa kutoka lughaya Kiarabu hadi Kiswahili (Kur-ani, 2:102; Jauhari, 2009; Ahmad, 2008; Bakaani, 2001; Mung'ong'o, 1997). Kwa hivyo, (sihiri na usihiri)zimekuwa na maana sawa lakini utafiti huu umetumia istilahi ya usihiri ili kuweka mpaka na kwenda sanjari na maudhui ya utafiti.

kuwa, neno usihiri limetafsiriwa kutoka lugha chanzi ya Kiarabu hadi lugha lengwa ya Kiswahili. Kwa jumla, usihiri, sihiri na uchawi una maana sawa kitabia, kitafsiri, kimaono na kimatendo. Tofauti ipo katika asili ya maneno tu. Kwa hivyo, maneno haya, yalikusanya dhana na maana sawa katika utafiti huu. Ili kutomchanganya msomaji, uendaji sambamba kimaudhui na uwekaji mpaka wa utafiti, istilahi iliyotumika katika utafiti huu ni ya usihiri. Dhana hii ilishughulikiwa kwa kumaanisha hali ijengwayo kimaneno, kimatendo, ishara, michoro na mazingira yaliyosawiri mambo yasiyo ya kawaida ayatendayo mwanadamu katika utokeaji wake. Kwa hivyo, usihiri ni utokeaji wa uhakika wa mambo yasiyoweza kuonekana kiurahisi kwa macho. Hubainika, hudhihirika na hujulikana kwa vitisho, hadaa, na udanganyifu wa uhalisi wake katika macho ya kawaida ya wanadamu katika nyakati za usiku au mchana.

Ali (2014) anabainisha kuwa, dhana ya usihiri ina historia ndefu tangu kuumbwa kwa ulimwengu, na haikupingwa kuwapo kwake. Hii ni kwa sababu Kur-ani na Biblia vinalizungumzia suala hili kwa uwazi. Kuhusu uhakika, namna, mtazamo, utekelezaji wake, na matatizo kadhaa yasababishwayo na usihiri, pamoja na taaluma yenyewe kuleta faida au hasara kwa jamii yameweza kubainishwa. Abdahu (2011) akithibitisha kuwapo kwa usihiri kupitia historia za mitume anasema kuwa, ulidhihiri wakati wa nabii Idrisa[7] (as). Na wafuasi wa nabii Nuhu waliuendeleza kivitendo na kwa kujifunza. Ulipata nguvu wakati wa nabii Suleiman; na wasihiri zaidi waliongezeka katika kipindi cha nabii Mussa (as). Usihiri ulishika kasi watu walipoanza kufundishwa na mashetani. Wakiwafundisha yale waliyoteremshiwa na malaika wawili (Haaruta na Maaruta) bila ya kumkufuru Mwenyezi-Mungu (malaika hao). Watu walijifunza pasi na kumdhuru yoyote hapo kabla.

[7]Ni babu wa baba wa nabii Nuhu. Ni mtume wa mwanzo kutazamia nyota pamoja na kuzijua hesabu zake. Utumiaji huo wa nyota ulikuwa ni mojawapo ya miujiza aliyopewa na Mwenyezi-Mungu. Pia,mtume huyo ni wa mwanzo kuandikia kalamu, ushonaji wa nguo, uvaaji na utengenezaji wa nguo kwani hapo kabla watu walikuwa wakivaa ngozi. Aidha, walitengeneza mizani, vipimo na silaha za mapambano ya vita. (Abdahu, 2011: 35 akimnukuu Abuhayani, Juzuu 8:32 Baharil-Muhitwi).

Uongezekaji wa husda na choyo vilichochea usihiri kutumika vibaya hadi Mtume Muhammadi (saw) kusihiriwa na Labid bin A’sam. Pia, Wakati wa nabii Mussa (as) usihiri ulifananishwa na fani maalumu ya kiufundi mithili ya fani nyingine. Na wafuasi wake waliamini kuwa ndio jambo la kulitegemea na kusifikana kwalo. Mwenyezi-Mungu aliwafundisha mitume wote njia za kujikinga na kupambana na usihiri.

Dhana na matumizi ya usihiri hujitokeza katika midhihiriko mbalimbali ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kwa kuwasiliana na msaada wa mashetani, majini, waganga, wabashiri na wachawi katika ulimwengu usioonekana (giningi) na unaoonekana (katika mandhari ya kawaida). Aidha, ushadidiaji uliomo katika maandiko matakatifu na kuhanikizwa na mazungumzo ya wanajamii. Matumizi hayo yanaweza kutofautiana kwa namna moja au nyingine katika jamii. Hivyo, hayawezi kutenganishwa na kazi za fasihi. Hii ni kutokana na sababu kuu tatu: Mosi, jamii na matendo ya usihiri hutendwa na huambatana na wanajamii. Pili, fasihi huakisi uhalisi wa jamii, na kwa kiasi kikubwa hutumika kumulikia yaliyomo. Tatu, lengo la watunzi ni kufichua na kuondosha matendo hayo, pamoja na wasomaji kuyafahamu. Kwa hivyo, dhana na matumizi ya falsafa ya usihiri kuonekana mabaya au mazuri kwa kutafsiriwa na wanajamii wenyewe kwa mujibu wa matakwa ya mtu mmoja mmoja au kikundi na jamii nzima kutegemeana na matumizi lengwa.

Ponera (2014a) anathibitisha kuwa, kwa upande wa kazi za fasihi usihiri ni miongoni mwa mbinu bunilizi iliyojichomoza mnamo miaka ya sabiini katika karne ya ishirini. Na utumiaji wake ulichangiwa na mabadiliko ya fikra, majaribio, ulimbwende na usanaji wa kazi zenyewe. Madai hayo yanaungwa mkono na Abdahu (2011) kwa kubainisha kuwapo kwa taaluma ya sayansi kavu kama vile upigaji ramli, watu kugeuzwa vizuu, matamshi ya usihiri, urukaji wa kutumia ungo na utumiaji mashetani hutumika kupimia dhana,

uashiriaji na matumizi ya falsafa ya usihiri. Kwa kusaidiwa na maandiko matukufu na yale ya bunilizi pamoja na akili za wanadamu. Jamii za Kiafrika zinakabiliwa na matatizo ya usihiri na ushirikina yanayopelekea kuleta migogoro. Wataalamu kama vile Abdahu (2011) na Ismail (1968) wamechunguza na kukiri kuwapo kwa usihiri, kanuni na misingi yake kama zilivyo taaluma nyingine. Kwa mfano, kuwapo kwa mfunzaji na mfunzwaji wa usihiri. Aidha, ikirari ya kuwapo kwa hasara zitokanazo nao. Pia, Safari (1993) anabainisha kuwa, usihiri ni imani iliyoanza nchi za Ulaya katika karne zilizopita na kusambaa hadi Afrika. Imani hiyo, ilichangiwa na ugumu wa maisha na matatizo yaliyopo kama ni msingi mkuu wa chimbuko lake. Maelezo hayo yamethibitisha kuwa, kutokana na kukosekana kisingizio cha kuegemezewa matatizo yaliyomkabili mwanadamu palisingiziwa usihiri. Sayansi na teknolojia imesaidia kupunguza hofu, woga, masharti na taratibu za usihiri za kumdhuru msihiriwa ili kujinufaisha msihiri. Aidha, elimu yenyewe hufundishwa kwa misingi ya ubinafsi zaidi kuliko kuleta manufaa ya jamii nzima.

Kwa hivyo, kazi za wataalamu hao zinatoa mwelekeo wa kuliendea na kulichunguza suala la matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule. Kwa sababu wataalamu waliotajwa hawajaonekana hata mmoja anayelidodosa kwa kutumia mwelekeo wa kiutafiti. Kutokana na jamii kusumbuliwa na hali hiyo tangu kuumbwa kwa dunia hadi leo watunzi, wasomi na matabibu wamekuwa wakitafuta tiba ya kujikinga na kutunga kazi zizungumziazo usihiri. Kwani wasomaji wengi wamekumbana na kipengele hiki kwa upande wa maudhui. Hasa kazi za fasihi zilizosanwa miaka ya sabiini na thamanini katika karne ya ishirini. Ni vema watafiti, wahakiki na wanajamii kuchunguza dhana na matumizi ya falsafa ya usihiri ili kuielekeza jamii uzuri na ubaya wake.

Wamitila (2008) anabainisha kuwapo kwa uhusiano na mfungamano kati ya fasihi na falsafa, kutokana na kufikiri na kudadisi kwa uwakilishwaji wa maandishi katika riwaya,

tamthiliya, hadithi fupi na ushairi. Maelezo hayo yanasisitiza kuwa miingiliano na mifungamano hiyo hupatikana katika hali mbili. Mosi, maarifa yatumikayo kueleza hali na misingi ya maisha ya mwanadamu kwa kutumia akili aliyonayo. Huu ni mtazamo wa jumla udhihirishao dhana ya falsafa itokanayo na tabia ya kufikirisha. Pili, kuiangalia falsafa kwa uchunguzaji wa asili na maana zenye mwelekeo wa kimawazo ambapo hujumuisha mtazamo wa kuelimisha. Hali hii inaashiria kuwa, fasihi yoyote hujumuisha falsafa kwa upatikanaji wa maarifa na matendo yawakilishwayo kifalsafa. Vitambulishi kama vile usawiri wa wahusika na mitazamo yao humuelekeza msomaji kwenye kuijenga na kuiimarisha falsafa ndani ya fasihi na kwengineko.

Riwaya ni maandiko yawasilishwayo kwa urefu kinathari katika hali ya kubuni, yenye visa na hadithi zizungumziazo uhalisi katika jamii (Wamitila, 2008; Johnson, 1939). *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010) limeshadidia kuwa, riwaya hujumuisha tungo ndefu zibuniwazo zenye visa na hadithi changamano kwa uandishi wa kinathari katika kusawiri uhalisi wa jamii. Kwa hivyo, utafiti huu ulizichunguza kwa kina riwaya tatu za Euphrase Kezilahabi ambaye alisaidia kutoa mwelekeo wa matumizi ya falsafa ya usihiri kupitia riwaya hizo. Kazi zake zilichomoza zaidi mnamo miaka ya sabini na tisini katika karne ya ishirini na kuendelea kuvutia hadi leo. Zilitumika kutolea mwelekeo huo. Sababu za uchaguzi wa kazi hizo ni kwamba, usihiri upatikanao katika riwaya hizo unaakisi uhalisi, kusawiriwa katika hali ya ajabuajabu, kuogofya, kushangaza na kuwa kigezo cha kuigwa katika jamii. Kuvutiwa na ufafanuzi wa mtunzi juu ya mitindo na aina mbalimbali za usihiri. Aidha, takriban riwaya zake zote sita zililigusia suala la usihiri kwa namna moja au nyingine ingawa katika sehemu ndogo. Mbali na riwaya mtunzi ameandika ushairi, hadithi fupi na tamthiliya bali hazikutafitiwa. Utafiti ulizichunguza riwaya zake tatu tu na riwaya ya *Gamba la Nyoka* ilitumika kutolea mfano katika kipengele cha athari chanya za

usihiri. Pia, utafiti unaamini kuwa, matumizi ya falsafa ya usihiri yaliyomo yaliwakilisha kazi zilizobaki.

Ingawa juhudi kubwa imefanywa na wataalamu mbalimbali kushughulikia vipengele vya falsafa katika bunilizi mbalimbali za kifasihi. Na maandiko tofauti yazungumziayo usihiri yasiyo ya kifasihi. Miongoni mwao ni Safari (1993), Yusuf (1983), Middleton (1963), Haji (2011), Kasim (2005), Ali (2014), Swanaib (2014), Swabun (1976), Kabalani (2008), Twauha (1972)na Ibrahim (2005). Wataalamu hao wametoa mawazo mazuri kuhusiana na masuala ya usihiri na imekuwa dira kwa utafiti huu. Hata hivyo, pameonekana pengo la kutafitiwa kwa upande wa matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule. Hii ni kutokana na kutofanyiwa utafiti na kufafanuliwa kidogo tu kipengele hiki kwa upande wa riwaya. Hali ambayo husababisha jamii na wasomaji wengi kutozifahamu kazi zizungumziazo falsafa ya usihiri. Kudumaza fasihi ya Kiswahili na kuleta migogoro katika jimii. Matatizo yote hayo yalichangiwa na; ugumu wa fani yenyewe na wataalamu wachache walioichunguza. Kwa hivyo, utafiti huu ulichunguza matumizi ya falsafa ya usihiri katika kazi za Euphrase Kezilahabi.

## 1.4 Tamko la Tatizo la Utafiti

Dhana na matumizi ya falsafa ya usihiri yameshughulikiwa na kutafitiwa kwa kiasi kidogo kwa kuyahusisha na kazi za fasihi za mwandishi Euphrase Kezilahabi. Kwa muda mrefu usihiri umetajwa kwa ufupi ndaniya maandiko matakatifu na mazungumzo ya wanajamii. Wataalamu na watafiti kama vile Swanaib(2014), Kabalani(2008)na Ibrahim (2005) wamelichunguza kwa jumla suala hili pasi na kugusia kipengele cha matumizi ya falsafa ya usihiri katika hali ya pekee kiutafiti.Wanazuoni hao walijihusisha na dhana ya usihiri kwa jumla kwa kuchunguza baadhi tu ya vipengele vya usihiri vikiwemo mazingaombwe,tiba ya usihiri na mashetani.Huku wakiacha mwanya wa kutofafanua

mahusiano yaliyopobaina ya mazingaombwe na usihiri. Pia, kazi hizo hazikufafanua kwa uwazi juu ya aina za usihiri uliomo na jinsi ulivyoweza kutofautianana mazingaombwe. Hali ambayo husababisha kutotafitiwa vema kwa dhana hii na kufinya mawanda ya uga wa fasihi ya Kiswahili hususani riwaya. Kwa hivyo, hupelekea uelewa mdogo wa wanajamiikwa kutozifahamudhamira na falsafa za mwandishi kuhusu usihiri na matumizi yake. Hatimaye, kutofikiwa kwa upeo wa kuijua falsafa ya Kiafrika kwa upande wa usihiri kwa ujumla. Hivyo, utafiti huuulichunguza matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi.

## 1.5 Malengo ya Utafiti

### 1.5.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya teule za Eupharase Kezilahabi.

### 1.5.2 Malengo Mahsusi

a) Kuchunguza aina za usihiri zinazojitokeza katika riwaya teule za Euphrase Kezilahabi;

b) Kuchunguza miktadha ambayo usihiri huelekezwa katika riwaya za mtunzi teule;

c) Kuchunguza sababu zichangiazo kutokea kwa falsafa ya usihiri katika riwaya teule na;

d) Kutathmini athari za matumizi ya falsafa ya usihiri kwa jamii na wasomaji wa riwaya teule.

## 1.6Maswali ya Utafiti

a) Aina za usihiri zinazojitokeza katika riwaya teule za Euphrase Kezilahabi ni zipi?

b) Ni miktadha gani ambayo usihiri huelekezwa katika riwaya za mtunzi teule?

c) Ni sababu gani zichangiazo kutokea na kutumiwa falsafa ya usihiri katika riwaya teule?

d) Kwa namna gani matumizi ya usihiri unaotumiwa na mwandishi teule unawaathiri wasomaji wa riwaya na jamii?

## 1.7Manufaa ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yamekamilisha kuleta manufaa yafuatayo: Mosi, yamesaidia kueleza kitaalamu athari za matumizi ya falsafa ya usihiri katika jamii na wasomaji kupitia kazi za fasihi. Pili, yamechangia kuelewa sababu za kutokea na kutumiwa falsafa ya usihiri kwa mtunzi husika. Tatu, yamewasaidia wahakiki kuzisoma kazi zilizosanwa juu ya falsafa ya usihiri kama kionjo cha fasihi ya zama hizi. Nne, yameibua mbinu mpya za utafiti juu ya kazi za fasihi. Tano, yamesaidia kuzichambua na kujua miktadha ambayo usihiri huelekezwa zaidi katika riwaya na jamii. Sita, yamesaidia kujua aina za usihiri na tiba zake kwa wanajamii. Saba yamesaidia kuzihakiki na kuzichambua kazi za Euphrase Kezilahabi.

## 1.8Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii ilizungumzia juu ya utangulizi, ufafanuzi wa istilahi muhimu zilizotumika katika utafiti, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti, na historia ya Euphrase Kezilahabi.Hivyo, sehemu inayofuatia inazungumzia kiunzi cha nadharia na mapitio ya maandiko.

## SURA YA PILI

## KIUNZI CHA NADHARIA NA MAPITIO YA MAANDIKO

### 2.1Utangulizi

Sura hii inajadili kuhusu kiunzi cha nadharia ya utafiti,pamoja na mapitio ya maandiko mbalimbali yanayohusiana na utafiti huu. Mapitio hayo yamegawiwa katika sehemu kuu nne; ya kwanza, maandiko kuhusu falsafa na fasihi kwa jumla.Pili, maandiko kuhusu usihiri na mazingaombwe ndani ya kazi za fasihi. Tatu,maandiko kuhusu usihiri nje ya kazi za fasihina maandiko kuhusu riwaya za Euphrase Kezilahabi kwa jumla.

### 2.2 Kiunzi cha Nadharia ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Euprase Kezilahabi. Uliongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu[8]. Utafiti uliichagua nadharia hii kutumika katika tasnifu hii, kwa msingi kuwa, imehusiana na kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna iliyofanya yaonekane ya kawaida katika jamii husika. Aidha, nadharia ilielezea jinsi wahusika walivyotenda matendo ya usihiri yasiyo ya kawaida yaliyowatofautisha na wengine kitabia na silika zao. Kwa hivyo, ukusanyaji, uchambuzi, na uwasilishaji wa data ulifanywa kwa kuzingatia nguzo-msingi ya nadharia ya Uhalisiajabu. Msingi wa nadharia hii ndio ulioongoza na kukamilisha hatua hizo. Nadharia ya Uhalisiajabu (Uhalisiamazingaombwe) kwa mujibu wa (Wafula na Njogu,2007:113) wakimnukuu Zamora (1995) wanasema kuwa, iliasisiwa na Franz Roh[9] mnamo mwaka 1925 kutoka katika nchi ya Ujerumani. Uhalisiajabu unaelezea na kujikita katika mazingira ya kijamii,

---

[8] Istilahi hii inatumika kuelezea mkondo wa waandishi ambapo mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mtindo wa uhalisia; yaani, kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja, kana kwamba ni mambo ya kawaida. Wasanii wanaotumia mtindo huu hudhamiria kuonyesha kuwa ingawa mambo yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokea katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika. Uhalisia wa kimaajabu huhusishwa zaidi nanchi zinazoendelea kutoka bara la Afrika, Marekani ya Kusini na Asia (Wafula, 2007:113 akimnukuu Mbatiah, 2002:60).

[9]Alizaliwa katika mji wa Apolda (kwa hivi sasa ni Thuringia) tarehe 21/02/1890 na kufariki 30/12/1965. Alikuwa mwanahistoria, mpiga chapa na mchoraji wa Kijerumani (Alexander, 1990:127).

miujiza, matendo na matukio ya kifantasia ambayo hayafanani na ya kawaida iliyozoweleka kwa hadhira na jamii. Kwa sababu ya kutokea kwake sambamba na yale ya kawaida.

Aidha, Dachau (2010) anashadidia kuwa, Franz Roh ni mtu wa mwanzo kuiasisi nadharia ya Uhalisiajabu (*Magic realism*) na kujulikana zaidi mwaka 1925 kutokana na vitabu vya *Nach Expressionismus: Magischer Realismus: Probleme der neuesten europäischen Malerei.* Vilizungumzia dhana za Mazingaombwe, Uhalisiamazingaombwe na Uhalisiajabu. Roh aliitumia dhanaya Uhalisiajabu katika kazi zake alizokuwa akiziandika ili kuweza kufahamika vema istilahi hiyo. Kuelezea matendo na matukio ya uhalisi kwa kutumia picha, vielelezo na michoro kwa wakati mmoja yenye uhalisiajabu na uhalisia. Baadaye alisisitiza juu ya usihiri kama jina lipatikanalo katika kazi za fasihi. Alichunguza na kugundua kuwa, kazi za fasihi zinafungamana na falsafa ya usihiri kulingana na jamii husika. Hii ni kwa sababu mandhari, matukio na wahusika husawiriwa katika hali isiyo ya kawaida kutokea katika hali halisi. Ili kudhihirisha ufanikishwaji wake.

(Walibora, 2010:143) akimnukuu Abrams (1999) anasema: Istilahi ya ‘Uhalisiajabu’ ambayo mwanzoni ilitumika kuwahusu wachoraji katika miaka ya 1920 hadi 1925 na Roh, ilitumika kufasili kazi za bunilizi za kinathari zamuasisi mwenyewe na Jorge Luis Borges wa Argentina. Aidha, kazi za waandishi kama vile Gabriel Garcia Marquez wa Kolombia, Isabel Allende wa Chile, Gunter Grass wa Ujerumani, Italo Calvino wa Italia, na John Fowles wa Uingereza. Waandishi hawa walitumia uhalisia uliosawiriwa kwa njia maalumu katika hali inayobadilikabadilika daima, huku wakiwakilisha matukio ya kawaida na maelezo ya kina sambamba na vipengele vya kifantasia na kindoto. Na kwa kutumia mambo yaliyotokana na visasili pamoja na hekaya ili kuonesha matumizi ya

falsafa ya usihiri. Matumizi hayo huonekana kupitia Uhalisiajabu unaoyachunguza mambo ya zamani ili kupata mambo na mitindo inayozuka sasa katika kazi za watunzi mbalimbali. Maelezo ya mtaalamu hayu, yanaonekana kuwa, Wanauhalisiajabu hutumia sifa zinazobainisha kazi zao ingawa wana mitazamo na imani tofauti za kimsingi juu ya matumizi ya usihiri.

(Alexander, 1990:127) anashadidia kuwa, Uhalisiajabu ni kielelezo tosha cha kufikirisha watunzi na wasomaji, jinsi nadharia ya usasa leo inavyolazimu kufikiriwa upya juu ya riwaya za kimapokeo, kuhusu riwaya za uhalisia za karne ya kumi na nane na tisa. Roh (1925) aliutumia Uhalisiajabu katika muktadha wa ulimwengu wa sanaa kueleza aina fulani maalumu ya kudhihirisha mambo yaliyofichikana kwenye maisha ya mwanadamu kupitia uhalisia huo. Pamoja na hayo Uhalisiajabu katika kazi ya sanaa hushughulika na kazi zilizoambatana na zisizoambatana na ujumi wa uhalisia. Chanady (1985) katika Rio (1999) anasema kuwa, Uhalisiajabu unahusu matukio yasiyo ya kawaida, ya kiujiza na jambo lililo la kinyume cha uhalisia wa kawaida. Suala la kuzingatiwa ni kwamba matukio yanayotendeka katika Uhalisiajabu hayawezi kujitenga na uhalisia. Kwa msingi wa maelezo hayo matukio yasiyo ya kawaida, ya miujiza na ni kinyume cha uhalisia wa kawaida na yanayotendeka. Hayawezi kujitenga na uhalisia, kwa nia ya kubainisha matumizi ya usihiri katika jamii.

Miongoni mwa waliounga mkono nadharia ya Uhalisiajabu ni (Gromov, 2002:69) anasema kuwa Uhalisiajabu ni yale mambo yanayotokea katika mandhari na matukio ya uhalisi pamoja na yale yasiyo ya kawaida. Aidha, huelezea kawaida ya matendo na maneno yaliyomo kwenye uyakinifu wa kila siku wa maisha ya mwanadamu (Mbatiah, 2002; Wamitila, 2003).

Aidha, wananadharia hao walipendekeza kutumika kwa nadharia hii huku ikitawaliwa na msingi mmoja mkuu unaobainisha matendo, matukio na wahusika wa ajabuajabu. Msingi huo kwa mujibu wa Wamitila (2002) anafafanua kwa kusema:

> …siku za hivi karibuni, pamezuka aina ya uhalisia ambao unahusisha maajabu. Kuwako maajabu kulipingwa katika uhalisia wa zamani ambao tunaweza kuuita "uhalisia wa kirasimi" … au "uhalisia wa kirasimu"… Aina hii mpya inajulikana kama "uhalisiajabu" (*magic realism*) ... kazi ambazo zinaweza kuelezwa kama za kihalisiajabu huchanganya sifa za kihalisia na kiajabu au maajabu (uk. 117).

Nukuu hii inaelezea kwa kina kuwapo kwa kazi zenye Uhalisiajabu ambao unatokea sambamba na matukio ya uhalisia. Wamarekani ya kusini ndio waliohusishwa na nadharia hii. Wengine ni Mbatiah (2002), Copper (1998)na Wamitilla (2003). Sababu za kuzuka kwa nadharia hii ni kuonesha kuwapo matukio ya aina hii katika jamii. Kupingana na watunzi waliodai kuwa kazi zote za kifasihi zinaelezea uhalisia pekee na hazina mambo ya kimaajabu. "Kuwako maajabu kulipingwa katika uhalisia wa zamani ambao tunaweza kuuita "uhalisia wa kirasimi" (Wamitila, 2002: 117).

Kwa mujibu wa (Wamitila, 2003:274), anafafanua kuwa, sifa (msingi) mkuu wa nadharia hii ni huu ufuatao:

> i) …kuyaeleza matukio ya kifantasia au ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane ya kawaida. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonyesha kuwa matukio ya aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika.

Hapa msihiri anajulikana kwa wepesi kabisa kutokana na hali isiyo ya kawaida inayojiri katika mandhari na matukio anayoyatenda. Kutokana na sababu za kimila kidesturi, kiuchumi na kisiasa, pale anapotekeleza matumizi ya usihiri aliyoyalenga. Aidha, katika kutilia mkazo juu ya msingi wa Uhalisiajabu (Mbatiah,2001:60), anafafanua kwa:

> ii) …kuelezea… mazingira, matendo na matukio ya kifantasia husawiriwa kwa kuiga mitindo ya uhalisia, yaani, kwa kuyaeleza kwa njia ya moja kwa moja kana kwamba ni mambo ya kawaida…ingawa mambo

yanayoshughulikiwa ni ya kiajabuajabu, hutokana katika maisha ya kawaida ya jamii inayohusika.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hao, pamegundilika kuwa nadharia ya Uhalisiajabu imeundwa kwa msingi (muhimili) mmoja tu bali umefafanuliwa kwa namna tofauti. Msingi huo umekusanya mitazamo mikuu mitatu iliyosaidia kuyaelezea matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi. Yanavyosawiriwa kwa namna ya moja kwa moja inayofanya yaonekane ya kawaida kutokea katika kazi za fasihi na jamii. Kwa hiyo, mitazamo ya nadharia hii kwamujibu wa Wamitila (khj) na Mbatiah (khj) ni;

a) Matendo na matukio ya kifantasia yaliyosawiriwa na kupangiliwa kwa njia ya usihiri/ajabuajabu. Matendo hayo hufanywa na wahusika katika riwaya teule na jamii kwa kuonekana ya kawaida kutokea kwake. Kwa hivyo, nadharia ya Uhalisiajabu imesaidia utafiti kuyatafsiri matendo na matukio hayo kuwa ni ya usihiri;
b) Mazingira au mandhari yasiyo ya kawaida hubuniwa na kutokea kwa mwanadamu na katika hali halisi ya jamii. Mandhari ni nguzo muhimu katika kuimarisha matendo ya wahusika, kuwaelewa kitabia, kihisi, maudhui na dhamira walizobebeshwa. Nadharia ilisaidia kuzijua ishara, dalili na vijenzi vinavyoashiria usihiri katika mandhari au mazingira mbalimbali na;
c) Wahusika waliomo katika kazi za fasihi (za mtunzi teule) na jamii kufanya mambo ya kiajabu au kusawiriwa pamoja na tabia zao katika kuufanikisha usihiri. Kwa hivyo, nadharia ya Uhalisiajabu ilisaidia utafiti kuwapambanua wahusika wa kawaida na wa kiajabuajabu kupitia matendo na mandhari waliyosawiriwa ndani ya riwaya teule.

Kwa jumla, mitazamo hiyo ndiyo iliyohesabiwa kuwa, iliujenga msingi (muhimili) wa nadharia ya Uhalisiajabu. Pia, ilitumika kuelezea matukio, matendo na mandhari yanayoashiria usihiri kupitia wahusika na yanavyoelezewa moja kwa moja katika jamii. Ni dhahiri kuwa, matukio hayo hutambulisha na kutoa ishara kuwa wahusika wake wanatekeleza usihiri katika maisha yao. Kwa mfano, mhusika kuruka juu ya anga kwa kutumia ungo na pembe za ng'ombe pamoja na kula nyama ya kuku mweupe huku anazunguka mtaa kwa lengo la kuutakasa mji. Hivyo, nadharia ya Uhalisiajabu katika utafiti huu, imesaidia kuchunguza na kuyaelezea mandhari ya ajabuajabu kimaneno na kimatendo kupitia muhimili wake. Kwa msingi kuwa, usihiri ni kigezo kimojawapo kinachobainisha mazingira yasiyo ya kawaida kutendeka. Nadharia imesaidia kubaini matukio, aina, sababu na miktadha ya usihiri inayojitokeza katika riwaya za Euphrase Kezilahabi katika maisha ya kila siku. (Walibora, 2010:146) anasisitiza kuwa, Uhalisiamazingaombwe unapaswa kueleweka, kwa kadiri fulani, kama mkabala wa kuwakilisha uhalisia kwa kukiuka mipaka iliyopo, ingawa ni mkabala wa kifasihi unaonasibishwa zaidi na waandishi wa Amerika ya Kusini, umepenya kwingi duniani huku fasihi za mataifa mbalimbali zikizungumzwa kwa njia ya dayalojia ili kuendeleza matumizi ya falsafa ya usihiri.

Aidha, nadharia ya Uhalisiajabu imetoa mwongozo mzuri wa kuyagundua mandhari ya usihiri kupitia wahusika katika riwaya teule. Utafiti huu ulijikita katika muhimili wa nadharia kwa kutumia mtazamo wa kuyaeleza matukio ya kifantasia au kiajabu au kichawi na kisihiri kwa namna ya moja kwa moja juu ya utokeaji wake (uhalisi) katika jamii. Aidha, hali ya kushangaza na kuogofya inawasilishwa na kuwa ya kawaida.(Gromov, 2002:3-4) anasisitiza kuwa, Uhalisiajabuhutumika kuufinyanga ukweli wa maisha kwa njia tofauti na jinsi ilivyozoewa. Kwa mnasaba huo kitengo hicho kimefanikiwa kuzungumzia maswala ya kileo. Kutokana na maelezo haya, pamebainika

kuwa, wasanii hawautumii Uhalisiajabu kiajali, bali kwa lengo la kuangazia hali ya jamii wanamoishi. Mtindo huo hujadili masuala nyeti ya kimaudhui kama ya utandawazi, dini, na siasa za kimataifa. Msisitizo wa sifa za riwaya hizi ni uandishi unaokiuka kaida za kiitikadi, utathmini wa ujumi kwa ndani na uvunjaji kaida za lugha kwa namna inayompa mwandishi uhuru zaidi.

Kwa hivyo, katika uchambuzi wa data na riwaya teule mambo yasiyo ya kawaida, kuogofya na kushangaza ndio yaliyohusika na nadharia hii usihiri ukiwemo. Utafiti uliangalia jinsi usihiri ulivyotokea katika riwaya na jamii kupitia maelezo ya mwandishi, wahusika na matendo yao. Kwa kuchunguza ni kwa kiasi gani usihiri ufanywavyo na athari zake. Kubuni maana za jumla za matukio ya usihiri, kuyahusisha na historia, mila, utamaduni wa jamii kupitia wahusika. Aidha, katika kupata matumizi ya falsafa ya usihiri nguzo-msingi ya muhimili huu na mitazamo ya kuyaelezea na kuyawakilisha mambo hayo katika hali ya kawaida yalizingatiwa katika uchambuzi wa data. Kutokana na umuhimu huo, matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi yamebainika kupitia hali za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kimuktadha.

Kwa hivyo, nadharia hii ilikuwa faafu kwa utafiti huu. Kwa sababu zifuatazo: Mosi, imechangia katika kutoa jawabu mwafaka ya maswali ya utafiti na kugundua kuwa matumizi ya falsafa ya usihiri yamekwenda sambamba na jamii husika. Pili, msingi wake una uwiano na kazi za mtunzi teule, matukio na kiini cha falsafa ya usihiri. Tatu, kukamilishana, kutegemeana na kuumana kwa muhimili wa nadharia na maudhui ya maandiko pamoja na mada tafitiwa. Nne, matukio yaliyosawiriwa kisihiri yalilandana na uhalisi wa ajabuajabu kupitia riwaya na maisha ya jamii. Nadharia hii ilisaidia kuchunguza na kuona jinsi gani riwaya, jamii na mtunzi alivyotumia falsafa ya usihiri na

wasomaji walivyoathiriwa nao. Kwa kutumia nadharia hii utafiti umetoa matokeo bora na thabiti.

## 2.3 Mapitio ya Maandiko

### 2.3.1 Maandiko Kuhusu Falsafa na Fasihi kwa Jumla

Maandiko yaliyododoswa sehemu hii yanagusia dhana ya falsafa na fasihi katika nyanja za siasa, uchumi na jamii. Katika kubainisha hali hiyo wataalamu kadha wameidodosa kwa uwazi kama ifuatavyo:-

Simchimba (2012) alizungumzia falsafa ya Kiafrika katika methali za Kiswahili. Katika utafiti wake alifafanua kuwa methali zimekusanya falsafa ya hali ya juu kama zilivyo tanzu nyingine za fasihi simulizi. Aidha, alibainisha kuwa Waafrika wanayo falsafa yao waliyoirithi kwa mababu zao na siyo wageni waliowapelekea falsafa ya Kiafrika. Falsafa hiyo ndio iliyokuwa ikitumika kurithishana mila, desturi na hekima kutoka kizazi hadi kizazi. Andiko hili kwa ujumla wake limeyakinisha kuwapo kwa falsafa na ile ya Kiafrika, anasema:

> …matokeo ya utafiti huu yameonesha umuhimu wa methali katika jamii… kuwapo kwa falsafa ya Kiafrika katika methali za Kiswahili. Falsafa hiyo inaonekana katika vipengele mbalimbali vilivyotawala maisha ya Waafrika kama vile: Umoja, dini, nguvu asili, ndoa, uzazi, malezi, sanaa za jadi na maadili… methali za Kiswahili, maana na uzito wa methali upo katika vipengele vya Kiafrika… methali zinagusa maeneo mbalimbali ya maisha… na hazina wakati maalumu wa matumizi yake, zimeweza kubeba hisi za Waafrika kwa upana wake (uk. 98-99).

Kwa jumla, alizumgumzia kuwapo kwa falsafa katika methali za Kiswahili ambapo ni kipengele kimojawapo tu kinachodhihirisha falsafa kwa Waafrika. Uthibitishaji huo unatoa mwega wa kuyachunguza matumizi ya falsafa ya usihiri kwa sababu utafiti uliopitiwa umeacha mwanya wa kutododoswakwa matumizi hayo.

Mshiuna wenzake (2007) kupitia andiko lao liitwalo "*General Studies Notes*" walizungumzia dhana ya falsafa na umuhimu wake. Katika kubainisha umuhimu huo wameonesha kuwa,falsafa husaidia kudumisha na kuendeleza tabia na maadili katika jamii. Hii ni kutokana na kujifunza kanuni na maingiliano faafu ayafanyayo mwanadamu kati yake na wenzake. Maingiliano hayo hutoka katika maeneo mbalimbali kama vile ya kidini na vikudi vya ushirika ambayo ndiyo chanzo cha familia na taifa kwa jumla. Kazi hii imethibitisha kuwapo kwa falsafa na imetoa mwelekeo wa jinsi gani falsafa inavyowasaidia watu kufikiri na kuwa na tabia njema katika jamii, wanasema:

> *Philosophy enables people to generate principle and norms of conduct. Naturally man is no an isolated creature, he always interacts with other people of distant places geographically. Through such interaction a person can decide to form social groups like family, community and even nation. Within these groups of people there must be principles or norms that are formulated to guide the members of the social goup. These principles are normally based on enhancing good conduct of people in that particular sociaty. For example, there are difference norms adopted in some social institutions like churches, schools, etc which guide people to behave in an acceptable member, all these norms are under the so called normative function of philosophy* (uk. 108).
>
> Falsafa inawawezesha watu kuzidumisha mila na desturi njema. Kimaumbile mtu si kiumbe wa kujitenga pweke, kila siku anaingiliana na watu wa maeneo mengine ya kijografia. Kutokana na muingiliano kama huo mtu huamua kufanya makundi ya kijamii kama vile familia, vikundi na hata taifa. Ndani ya makundi haya ya watu lazima kuwe na kanuni au desturi ambazo zimefanywa kuwaongoza wanachama wa makundi ya kijamii. Kanuni hizi hutawaliwa na misingi ya kuziendeleza tabia njema za katika taasisi mfano wa makanisa, shule na kadhali, ambazo zinawaongoza watu kuwa wanachama wenye tabia njema zikubalikazo, taratibu zote hizo zinatokana na kile kiitwacho taratibu za falsafa katika kuendeleza maadili (Tafsiri ya Mtafiti).

Mawazo ya wataalamu hawa ni muhimu sana kwa kuuendeleza utafiti huu. Kwa sababu yamezungumzia na kudodosa juu ya umuhimu wa falsafa katika kujenga maadili na tabia njema kwa mwanadamu. Mawazo hayo yamekuwa kiungo muhimu katika kushadidia kuwapo na umuhimu wa falsafa pamoja na nafasi yake katika jamii. Lakini matatizo na mapengo kadha yaliyojitokezani; kuacha mwanya wa kuzidodosa aina, matukio, miktadha na matumizi ya falsafa ya usihiri. Hivyo, utafiti huu umeziba mianya hiyo kupitia riwaya za mtunzi teule.

Kenyatta (2004) alizungumzia nafasi ya falsafa ya usihiri katika jamii ya Wamatengo, mambo yaunganikayo na usihiri, kukamilika matendo hayo pamoja na kutokea kwake. Alibainisha imani ya kabila la Wamatengo juu ya falsafa ya Kiafrika, kwa upande wa usihiri ulivyoshika kasi katika mwambao wa Afrika Mashariki. Pia, aligusia namna ya utengenezwaji wa dawa ya Kindorobi na matumizi yake katika kabila hilo ambayo ni dawa ya kuimarisha mapenzi na hata kujikinga na usihiri. Hatimaye, alidodosa juu ya wachawi na tabia zao,pamoja na njia wazitumiazo katika kufanikisha usihirina waganga wanavyoshiriki katika uaguzi na utabiri wao ndani ya jamii. Mwandishi anasema:

> Katika jamii ya Wamatengoimani ya uchawi ilikuwepo kabla ya wewe na mimi hatujazaliwa bado. Imani hii imeendelea hadi leo ninapoandika kitabu hiki... Wachawi walikuwa wanawafanya binadamuwenzao nyama ya kula yaani mboga ama "kapili" kwa ajili ya asusa. Wachawi walikuwa wanadhulumu watu…Tena wanasadikiwa wachawi wanaweza kuruka angani kwa kutumia ungo kama ndege kwenda mbali. Kufanya matendo mabaya siku hiyo hiyo na kurudi, hata kama Ulaya, Amerika na popote duniani. Pia wachawi wakiwa katika shughuli zao wanakaa uchi wa mnyama. Asiyepitia sayansi hiyo hata kama ni kundi kubwa la wachawi wapo karibu naye hawezi kuona. Ndio maana asilimia tisini shughuli zao zilifanyika usiku wa manane. Hii ni kwa sababu waliogopa mambo yao yakifanyika mchana yataanikwa juani. Shughuli hizo zilifanyika kwenye shamba la Mungu... Wachawi wengine walikuwa na magari makubwa, wengine pikipiki… walikuwa na nguvu za ajabu lakini nguvu hizo za ajabu zilifanyika usiku tu...waganga wa kienyeji, kwa kweli chimbuko lake hasa ni wachawi(uk. 1-2).

Mawazo ya Kenyatta kuhusiana na imani ya Wamatengo yameonesha kwamba, falsafa ya usihiri ina historia ndefu, imeota mizizi katika jamii hadi watunzi na watafiti wa kazi za fasihi na zisizo za fasihi kulizungumzia suala hili. Aidha, ameonesha tabia na mienendo ya wasihiri ya kuwadhulumu wengine pasi na sababu yeyote. Hii ni kuthibitisha kuwa usihiri na wasihiri wapo miongoni mwa jamii ya Watanzania na kwengineko duniani. Hata hivyo, pameonekana pengo la kutotafitiwa kwa upande wa matumizi ya falsafa ya usihiri.Hii ni kwa sababu andiko lililododoswa limezungumzia usihiri ndani ya kabila moja tu la Wamatengo, uwepo wa usihiri na tabia za wasihiri, na jinsi gani wasihiri

wanavyoshiriki katika utendaji wa matendo ya usihiri. Hivyo, utafiti huu umezungumzia kwa kina matumizi hayo.

Husein (1976) katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ameonesha falsafa ya uchawi na ushirikina katika jamii za Kiafarika inavyofanyakazi. Ushirikina huo umefanikishwa kwa kutumia maji yaliyoaminika kuwa na nguvu na kinga dhidi ya wakoloni wanaopingana nao. Maji hayo yalitumika kuzizuia risasi zitokazo kwa wapinzani wao, kupata radhi za mizimu na kuwafufua wafu kwayo. Ubainishaji huo wa imani na matendo ya ushirikina umekwenda sambamba na jamii za Kiafrika. Viongozi wanaamini kuwa jambo lolote haliwezi kufanikiwa hadi pafanyike matendo ya ushirikina, Kinjeketile anasema:

> Haya ni maji-maji ya maisha. Hii ni silaha yetu. Huu ni usinga-usinga wa nguvu. Mwenye kunywa na kupakaa maji haya hatadhurika na chochote. Risasi itakuwa maji juu ya mwili wa mwenye kutumia dawa hii. Sasa nguvu tunazo. Hii dawa ya maji ni nguvu zetu. Radhi za mizimu tunazo…Mzee wao aliyekufa tutamfufua, tutamwita kutoka Bokero aseme nao, nao wataamini. Yote haya ni nguvu ya maji. Ni dawa ya maji… Maji tumepewa na pepo. Lakini pepo huyu nani-Hongo?... Na nikiacha anipande nitakuwa siwezi kujua. Lazima nipate wahyi kutoka kwa Mungu (uk. 15-27).

Andiko hili limethibitisha kuwapo kwa matendo ya ushirikina yanayothibitisha kuwapo kwa usihiri na falsafa ya Kiafrika kama zilivyo jamii nyingine duniani. Mtunzi ameonesha dhana ya jumla ihusuyo ushirikina na uchawi. Jambo jingine lijidhihirishalo ni udodosaji wake kuhusu dhana ya usihiri kupitia maandiko ya fasihi ya Kiswahili. Kwa kiasi fulani andiko limedodosa namna na njia za utekelezaji wa ushirikina na usihiri katika jamii ya Watanzania na nyinginezo. Andiko hili ni mwega mzuri wa kuukamilisha utafiti huu kwani umechunguza matumizi ya falsafa ya usihiri.

Wizara ya Elimu na Utamaduni (1992) imefafanua kuhusu falsafa ya elimu kwa kusema kuwa,falsafa ya elimu ni utumiaji wa mbinu za kifalsafa kwa ajili ya ufafanuzi na ufikishaji wa elimu katika jamii.  Kwa kawaida falsafa hii hutafakarisha na kuzingatia juu

ya mawandaya elimu, maana, malengo yake na kufafanua juu ya walengwa wa elimu; yaani, mwalimu na mwanafunzi.Aidha, pitio hili limefafanua nafasi ya mwanadamu katika uga wa elimu ambapo wanafalsafa wa zama zote wanaitumia kama njia ya kutafakari na kutoa maamuzi kwayo. Wizara imefafanua kwa kusema:

> …falsafa ya elimu ni utumizi wa falsafa na mbinu zake katika kufafanua masuala ya elimu; ni fikra za kifalsafa zilizoelekezwa katika masuala ya elimu. Aghalabu falsafa ya elimu hutafakari mambo mbalimbali ya kielimu kama vile; maana ya elimu. Malengo ya elimu katika jamii na namna ya kujifunza. Hali kadhalika hufafanua juu ya nafasi ya mwalimu na mwanafunzi katika medani ya elimu.Baadhi ya wanafalsafa wa kale na wengine mashuhuri wa sasa wametafakari masuala ya elimu na kutoa mawazo yao juu ya taratibu za kuendesha elimu. Mawazo haya ni falsafa za elimu za watu binafsi lakini ni mawazo muhimu ambayo watu wote wanaohusika na masuala ya elimu inafaa kuyafahamu(uk. 46).

Katika andiko hili pamefahamika kuwa, falsafa ni dhana yenye mawanda mapana ambayo yameenea katika kila nyanja kupitia maisha ya mwanadamu mwenyewe. Pia, falsafa ya elimu hujiegemeza katika maana na malengo wayahitajiayo wanajamii katika kujifunza. Wanafalsafa waliotangulia na wa sasa mawazo yao yanawiana kuhusiana na dhana na malengo ya falsafa. Kwa jumla, andiko hili limegusia falsafa ya elimu kama mbinu zitumikazo katika upatikanaji wa taaluma, malengo na mwelekeouwaongozao wanafalsafa katika kufikia malengo lengwa. Andiko hili limesaidia kuzifahamu aina za falsafa pamoja na malengo yake. Hata hivyo, pameonekana pengo la kutododoswa kwa matumizi ya falsafa ya usihiri. Kutokana na hali hiyo mtafiti ameshawishika kuyachuguza matumizi ya falsafa ya usihiri. Hivyo, kufanyika utafiti huu ni muhimu kwani ulisaidia kuchunguza na kuijua falsafa hiyo pamoja na kuziba pengo chomozi.

Thiong'o (1965) kupitia riwaya ya *River Between,* ameonesha jinsi Waafrika wanavyoiamini, kuidumisha na kuitetea falsafa yao. Mambo hayo yaiendelezayo falsafa ya Kiafrika ambayo yanabainika na kudhihirika kutokana na hatua anazozipitia

mwanadamu tangu anapozaliwa hadi utu uzima wake. Mtunzi alibainisha kuwa, kila hatua anayoipitia mwanadamu inaakisi falsafa ya jamii yenyewe Murthoni, anasema:

> *I want to be a woman. Father and Mother are circumcised, but why are they stopping me, why are they denying me? How could I be out side the tribe when all the the girls born with me at the same time have left me?* (uk. 44).
>
> Ninataka kuwa mwanamke Mama na Baba yangu wote walitahiriwa lakini ninashangaa mimi, kwa nini wananizuilia mimi kutahiriwa kama walivyofanyiwa wao? Nitaonekanaje mbele ya jamii na kabila langu ikiwa wasichana wote wa umri wangu wamekeketwa na kuniacha mimi? (Tafsiri ya Mtafiti).

Mtaalamu huyo ameonesha kuwapo kwa utamaduni, mila na falsafa ya Waafrika iwatofautishayo na bara jingine kupitia miegamo na miktadha ya matendo na maneno yao. Aidha, ametoa maoni ya jumla yaliyoashiria kuwapo tofauti za kifalsafa miongoni mwao na bara jingine. Mawazo haya yamesaidia kutoa mianya ya kukosekana kubainishwa kwa aina na njia za kuzifanikisha falsafa hizo, kutozungumzia falsafa ya usihiri pamoja na matumizi yake. Utafiti huu umeziba mapengo yaliyojitokeza.

### 2.3.2 Maandiko Kuhusu Usihiri na Mazingaombwe Ndani ya Kazi za Fasihi

Sehemu hii inazungumzia dhana ya usihiri na mazingaombwe katika maandiko ya kazi za fasihi.Kwa sababu dhana yaMazingaombwe ni aina mojawapo ya usihiri na vipengele vya falsafa ya Kiafrika. Hii ni kutokana na baadhi ya wataalamu kuyaweka katika aina za usihiri (Swanaib, 2014; Ali, 2014; Kasim, 2005).

Mohamed (2012) alizungumzia nafasi ya uhalisia mazingaombwe katika hadithi za fasihi simulizi kwa jamii ya Wazanzibar. Katika utafiti huo alibainisha kuwa uhalisia mazingaombwe una dhima kubwa katika kuifunza na kuiendeleza jamii kimaadili. Miongoni mwazo ni kuelimisha, kuadilisha, kutoa mbinu za kujenga tamthiliya, hofu, woga na kuonesha upekee wa kazi husika. Kwa jumla, andiko hilo limezungumzia dhana na istilahi za mazingaombwe. Mawazo ya mtafiti huyu ni muhimu kwa uendelezaji wa

utafiti huu. Kwa sababu umebainisha uhusiano na mapengo kadhaa, miongoni mwayo ni kuzungumzia falsafa ya mazingaombwe ambayo ni aina moja tu ya falsafa ya usihiri, kutobainisha aina, chanzo chake, pamoja na mpishano wa kiistilahi. Aidha, alidodosa falsafa ya Kiafrika zaidi na umuhimu wake kwa upande wa fasihi simulizi na kuiacha fasihi andishi. Hivyo, utafiti huu umeziba mapengo hayo kwa kutafiti matumizi ya falsafa ya usihiri kupitia riwaya za Euphrase Kezilahabi.

Mohamed (2001) alibainisha mandhari mbalimbali za umazingaombwe wazisawirizo wahusika wakuu kama ni kielelezo katika jamii. Kwa mfano, mhusika K amesawiriwa hivyo hadi mwisho wa riwaya kwa matendo ya ajabuajabu ili kuwakilisha matendo wayafanyayo viongozi au yawatokeayo. Mtunzi amelenga kugusia athari za ukoloni mamboleo kwa nchi endelevu kupitia umazingaombwe. Aidha, amebainisha kuwa misaada ipelekwayo kwa ajili ya wanyonge huishia mikononi mwa wajanja. Kugundulikana kwao nao hutafuta mbinu mpya ya unyonyaji kwayo. Pia, mtunzi amewachora Doggy na Biye wakiwa katika Kasri ya K ili kuwakilisha kundi la wasionacho na mhusika K anawakilisha kundi la walionacho, mtunzi anasema:

> Biye hakuwa na budi kwenda kuinyanyua ile sahani, mbichi au kavu, kubainishia pofu wake kwa ushahidi kamili. La, haiwezi kuwa! Lazima kuna kitu ana nini bwana huyu au wehu unamwanza au mazingaombwe? “hii hapa”, Biye alimsogezea K sahani aliyoishika mikononi mwake. K alitafakari. Hakujua hata aseme nini kuna kitu asichokifahamu kinajiri katika maisha yake ghadhabu za kutokujua nini kinatokea kati ya sahani za vyakula na jibwa lake (uk. 6).

Kwa jumla, mtunzi amezungumzia ulimwengu wa mazingira ya mazingaombwe kupitia babu Mzuka ili kuweka bayana hali iliyopo katika jamii. Na kukashifu vitendo vya ubadhirifu wa viongozi katika nchi ziendeleazo. Andiko hilo limethibitisha kuwapo kwa mazingira ya kimazingaombwe, ushirikina na uchawi. Na limeweka bayana kuhusiana na umazingaombwe unavyosawiriwa katika jamii. Utafiti huu ulichunguza matunizi ya falsafa ya usihiri kwa sababu andiko lililopitiwa halikuyadodosa.

Mung'ong'o (1997) alizungumzia athari zitokanazo na usihiri ujitokezao katika jamii ya Watanzania. Alibainisha kuwa wazazi huwarithisha vijana matendo ya usihiri wakaribiapo kufariki au hata kabla yake. Hali hiyo imeenea sana hapa Afrika kwa kuwapotezea wanadamu wengine maisha yao kupitia matendo hayo. Matokeo yake ni kupata majuto kwa wale watendao matendo ya usihiri katika jamii. Wasihiri huwakandamiza wengine ili kujinufaisha wao kutokana na kutotamani maendeleo ya wenziwao wala wao wasinufaike kwayo. Miongoni mwa athari zijitokezazona zichangiwazo na usihiri katika jamii ni ukatili, maangamizi na majuto hujitokeza kwayo. Msanii anasema:

> …sikuzaliwa duniani kuwa mkiwa hivi. Bali yote haya ni matokeo ya uovu kamili wa binadamu na ufundi mkomavu wa sihiri… vita vyetu vya sihiri vilivyopiganwa humo,… mzee alinishika mkono kwa nguvu hata nikahofu angefia mikononi mwangu! Alisema, "Mwanangu, nakuachia kazi kubwa. Ni urithi mkubwa ukiutumia vema; bali pia ni mirathi ya hatari usipojihadhari nayo. Nakuachia dawa zote na milki yangu katika mizungu ya sihiri!" "…Lakini nakuonya jambo moja: usiache upole ukutawale; hutakwenda mbali maishani" …Laiti baba angekuwa hai bado ningekubali aninyime radhi kuliko kuipokea kazi hii (uk. 2-13).

Kwa jumla, mtunzi alizungumzia maafa yaletwayo na usihiri na kuwaaidhi wanajamii wajiepushe nayo. Mawazo ya mtaalamu huyu ni muhimu kwa utafiti huu, kwa sababu ni dira muhimu katika kuthibitisha na kushadidia kuwapo kwa usihiri. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, ijapokuwa andiko hilo limetoa taswira ya kuwapo kwa usihiri kupitia maandiko mbalimbali ya kifasihi, bado limeacha mwanya wa kutafitiwa kwa upande wa istilahi zilizotumika (sihiri na usihiri) nukuu imetaja istilahi ya sihirina utafiti umezungumzia istilahi ya usihiri. Hivyo, pamebainika kuwapo kwatofauti ya kiistilahi kati yazo na vifaa vitumikavyo kufanikisha usihiri, aina, namna na mipaka ya matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya na jamii inayoandikiwa. Kwa hivyo, mapengo haya yamezibwa kupitia utafiti huu.

### 2.3.3 Maandiko Kuhusu Usihiri Nje ya Kazi za Fasihi

Sehemu hiiya mapitio imezungumzia maandiko yaliyoashiria usihiri nje ya kazi za fasihi ili kupata ithibati ya matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya kwa uwazi zaidi. Mgonja (2012) alifafanua jinsi Renatus Mungai alivyowatowa watoto wake katika kafara kwenye hekalu la mashetani. Alibainisha kuwa, katika matukio hayo ya utoaji wa kafara wa bwana huyo kwa watoto wake, ni ya kustaajabisha na yameshamiri sana huko nchini Kenya na duniani kwa jumla. Kwa upande mwingine ametaja baadhi ya ishara mbalimbali wazitumiazo wasihiri kupitia sehemu za ibada na hata nje yake. Aidha, kujibadilishabadilisha kwa wasihiri ni jambo la kawaida ili wasijulikane matendo yao. Katika kuthibitisha hayo mwandishi ametaja utaratibu wa kujiunga na viapo mbalimbali wavitumiavyo wasihiri ili kujifunga na mkataba wa giningi, anasema:

> …Master… aliniambia kuwa ndani ya siku sita napaswa niwe nimekisoma kitabu chote na kufanya kiapo cha ukamilifu ambacho kipo kwenye ukurasa wa 60 unaojumuisha majuma sita ya ukamilifu wa ibada, yaani 666x2. Katika ukurasa huu, bila kusita nilijaza watoto wangu wote watatu… unaowatoa kama dhamana ya kiapo chako unapaswa kujaza tarehe zao za kuzaliwa, mahali wanapoishi, majina yao na uwape namba ya uwakilishi isiyozidi wala kupungua tarakimu sita. Unapokamilisha kujaza hilo unapaswa kujichanja mwenyewe utoe damu na udondoshe matone sita ya damu katika sahihi yako kwenye ukurasa huo. Na ukishakamilisha taratibu zingine zilizopo kwenye kurasa zingine utapaswa kukirejesha kwa mkono wako hadi madhabahuni na hapo utaapa kukirejea mara kadhaa kiapo cha kwanza wakati unapokaribishwa hekaluni mara sita. Kisha utaapa kiapo cha pili cha kuingia kwenye *degree* ya pili ambayo inaitwa "*fellow craft*." Mwisho utaapa kiapo cha *degree* ya tatu ambacho kinaitwa *Grand Master Masons* au *Worshipful Masons*. Nilikariri kiapo hiki chanye maneno yafuatayo: "Kwa sababu yeyote ile sitatoa wala kuruhusu siri, sanaa au mfumo wowote wa siri wa kundi la masons kwa mtu yeyote au watu wowote isipokuwa mwana masons mwenzangu, au hekalu la masons. Najifunga mwenyewe katika hukumu ya kifo cha upanga au cha aina yoyote kwangu mwenyewe na kwa wadhamini wangu niliowaorodhesha." … "nitakuwa tayari koo langu likatwe kwa upanga na mwili wangu uzikwe kwenye mchanga wa bahari iwapo tu, nitavunja kiapo hiki '*solemn oath'*. Nisaidie mungu nisimame imara." Niliambiwa kiapo hicho ni kujifunga katika undani wa ibada kundini, ukikiuka hakika utakufa na kwa sababu ya matokeo ya wale wanaokiuka kiapo na adhabu wanazopata, watu wengi hudai kuwa kundi hilo linaua watu(uk. 37-38).

Andiko hili limethibitisha kuwapo kwa wakuu na viongozi wa usihiri pamoja na taratibu ziwaongozazo. Viongozi hao na waongozwao wanajiwekea mifumo maalumu ili kujikinga na maadui wao pamoja na kulidumisha kundi lao. Anayekwenda kinyume na utaratibu wa wasihiri hukabiliwa na adhabu kwa mujibu wa kosa husika. Aidha, katika kujiunga na wasihiri panatakikana mtu kuweka wadhamini wake ili iwe kikomboleo au kikoa akitoacho kwa upande wake. Kikoa hicho ndicho kinachomlinda asishambuliwe na adhabu yoyote badala yake watu aliowataja ndio wanaokuwa fidia juu yake. Hatimaye, kukamilisha kiapo cha kujifunga katika kundi la wasihiri ili kuwadhulumu wengine. Kwa jumla, andiko hili limedodosa juu ya taratibu na kiapo cha kujiunga na wasihiri. Kwa mnasaba huo linathibitisha kuwapo kwa usihiri, kiapo na taratibu zake pamoja na kuwa kichocheo chema cha kuyadodosa matumizi ya falsafa ya usihiri. Hii ni kutokana na kuonekana pengo la kutotafitiwa kwa upande wa matumizi hayo.

Haji (2011) alizungumzia tiba ya usihiri ujitokezao na ufanywao katika jamii ya Watanzania. Kupitia kitabu kiitwacho *Jitibu Nafsi Yako kwa Tiba Sahihi ya Kisharia* alichambua na kubainisha namna za kujitibu kwa kutumia dawa mbalimbali za mitishamba, aina zake na matumizi yake juu ya magonjwa sugu usihiri ukiwamo. Miongoni mwazo ni dawa ya kubatilisha usihiri. Anasema:

> Nimetaja dawa za maradhi ambayo madaktari bingwa yamewashinda kama maradhi ya … kupooza viungo, kubatilisha uchawi, …Chemsha Mwamba Mji vipande saba kwa vikombe kumi na tatu vya maji, kisio poopoo, anywe nusu kikombe cha chai mara tatu muda wa siku saba…Chemsha vipande saba vya Muuwa vikali utie vikombe kumi na tano vya maji chemsha kisha anakunywa mtu aliyerogwa au anaesumbuliwa na mashetani, au matatizo yoyote ya mambo ya uswahili, anywe na kupaka muda wa siku tisa. Kunywa nusu na kujipaka nusu kutwa mara tatu (uk. i-1).

Katika kuelezea kwake dawa hiyo anasema kuwa inawafaa hata waja wazito kwa matumizi mbalimbali. Kwa jumla, anazungumzia matumizi ya dawa na matibabu ya usihiri uwapatao wanajamii. Andiko hilo lilitoa dira ya kuwapo kwa usihiri na tiba zake.

Ibrahim (2005) alizungumzia mbinu na njia mbalimbali za kuweza kujitibu usihiri kwa kuchanganya aya za Kur-ani na Hadithi za Mtume Muhammad (s.a.w). Katika ufafanuzi wake aligusia uchanganyaji wa mitishamba mbalimbali kwa kusomewa pamoja baada ya kuchanganywa. Anasema:

> Unachukua majani saba ya mkunazi mabichi kisha unayaweka katika maji kwa kuyasomea. Baadaye unakunywa na kukogea mpaka unapoa usihiri kwa amri ya Mwenyezi-Mungu (uk. 25).

Maelezo ya wataalamu hao yalithibitisha kujitibu na kuwapo kwa usihiri. Mtafiti alishawishika kuchunguza matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule ili kupata uhakika wake kwayo.

Swabun (1976) alitoa tafsiri ya sura ya pili aya ya mia moja na mbili ya Suratul-Baqara alifafanua kuwa shetani waliwafunza watu usihiri hadi kuenea ulimwenguni. Nao baada ya kufundishwa waliwafunza wengine na kuendelea hadi sasa. Aidha, aligusia sababu ya kuzungumziwa dhana hii katika Kur-ani kwamba, mtume Muhamad (s.a.w) aliulizwa kuhusu utume wa mtume Daudi kwa sababu wafuasi wake hawakumuamini ila walisema ni msihiri tu wala siyo mtume. Andiko hili limethibitisha na kutoa dira juu ya kuwapo kwa usihiri kupitia hitoria za mitume na jinsi unavyowafanya watu kukosa imani juu ya mtuhumiwa. Kwa jumla, alizungumzia dhana ya usihiri katika jamii. Kazi hii ni mwongozo mzuri uliomsaidiamtafiti kujua ufundishwavyo usihiri, historia ya usihiri na viashiria vyake katika maandishi na jamii. Hivyo, utafiti huu ulichunguza matumizi ya falsafa ya usihiri.

Twauha (1972) alizungumzia njia na michoro mbalimbali ya kufanya ili kufanikisha usihiri. Alitaja baadhi ya majina ya majini na mashetani yanayoambatanishwa na matendo ya usihiri ili kutumika katika kuwahujumu watu na kutimia kwa usihiri, Mtunzi anasema:

> Twaurani miongoni mwa njia zake, atakaeliandika jina hili katika karatasi mara tano, pamoja na aya nne za mwisho za Suratul-Hashiri mara mia tatu na saba akaichukua atapata amani kutokana na hila za watu, majini na wanaotumia nguvu. Na atakaezisoma mara elfu moja kila siku na zitakapofika kila mia aseme; "nakuelekeeni enyi wahudumu wa jina hili tukufu mumuadhibu fulani bin fulani na muipoteze akili yake na mumpelekee juu yake maradhi yote mnayoyajua mabaya kwa haki ya jina hili, ni juu yenu kutii amri hii kwenu nyinyi baraka za Mwenyezi-Mungu na nyinyi. Hakika yake yeye hazitopita siku tatu juu yake isipokuwa atapatwa na maradhi (uk. 22).

Kwa jumla, andiko hilo limethibitisha na kushadidia kuwapo kwa usihiri, ushirikina na njia za kufanya kwazo pamoja na madhara yake. Bado limeacha mianya ya kitaaluma ihusuyo aina na matumizi ya falsafa ya usihiri ambayo ndiyo yaliyochunguzwa katika utafiti huu.

### 2.3.4Maandiko Kuhusu Riwaya za Eupharase Kezilahabi

Ponera (2014) alitafiti kuhusu ufutuhi katika nathari ya Kiswahili. Alishughulikia dhana ya ufutuhi, utokeaji wake, miktadha pamoja na aina zake. Katika utafiti huo alilinganisha baina ya riwaya za Euphrase Kezilahabi na Shaaban Robert. Alibainisha kwamba dhana ya ufutuhi hufafanuliwa kwa kutumia taaluma ya Jelatolojia. Kwa upande mwingine aligusia tofauti ijitokezayo ya kiistilahi kati ya futuhi na ufutuhi, asili na chimbuko la kila istilahi na wakati wa utumiaji wake kwazo, anasema:

> Dhana ya ufutuhi katika tasnifu hii ilitumiwa kama kisawe cha neno la Kiingereza '*comic'* ambalo linatumiwa kama nomino … Dhana hii ya ufutuhi imepatikana kutokana na upanuzi wa maana-msingi ya dhana ya ufutuhi; yaani, kijitapo cha tamthiliya ambacho hutawaliwa na unyume… Dhana ya ufutuhi imetofautishwa na ile ya futuhi kwa msingi wa kwamba, futuhi kwa kiasi kikubwa hujiegemeza zaidi katika suala la utendaji, …ilhali, ufutuhi huvuka mipaka ya jukwaa na kuchupa hadi katika mazingira mengine ya kimaisha… futuhi ni neno ambalo kisawe chake cha lugha ya Kiingereza ni *'comedy'*. Neno hili linatokana na neno 'komos' la lugha ya Kiyunani linalomaanisha sherehe za matambiko…Mwandishi anayasokota na kuyafafanua mambo yote hayo kwa kutumia mbinu mbalimbali. Miongoni mwazo ni hii ya ufutuhi. Humu, mwandishi anatweza, anatia chumvi, anakejeli, na kudhihaki masuala hayo makubwa… Zaidi ya hayo, majina yaliyomo… yana sifa za kimajazi yenye ufutuhi(uk. 1-247).

Nukuu hii imebainisha asili na chimbuko la istilahiza futuhi na ufutuhi. Futuhi ni neno litokanalo na lugha ya Kiyunani wakati ufutuhi linatokana na nomino katika lugha ya Kiingereza litumikalo katika tasnia ya tamthiliya na nje yake. Aidha, dondoo hilo limebainisha tofauti iliopo kati ya ufutuhi na futuhi. Futuhi hujiegemeza kiutendaji zaidi na ufutuhi huvuka mipaka hadi kufikia katika mazingira ya katika maisha. Kwa jumla, amegusia kuwapo kwa ufutuhi ndani ya maandiko ya Kezilahabi ambao unajengwa kwa kutumia vijenzi mbalimbali kama vile ubeuzi, kejeli, utani na vijembe.Malengo mbalimbali kama vile kukejeli na kudhihaki. Kwa upande mwingine amegusia mwelekeo wa nathari za mtunzi teule kuwa ni kigezo chema cha karne ya ishirini na moja. Ufaafu wa utafiti huo ni mkubwa kwa utafiti huu. Hii ni kwa sababu mawazo ya mtaalamu huyu yametoa mwega mzuri katika kuzifahamu istilahi na dhana za kiufutuhi katika maandiko ya mtunzi. Dhana hizo zimesaidia na kutumika katika kuzifafanua na kuzilinganisha na dhana za kifalsafa zijichomozazo katika nathari hizo usihiri ukiwemo. Aidha, utafiti huo umefungua njia ya kuzifahamu kazi za mtunzi teule na umetoa msaada na msingi mkubwa katika kufahamu historia, falsafa na mbinu za kiutunzi za mtunzi teule. Kutokana na utafiti huo pameonekana mwanya wa kutofautiana kwa upande wa dhana na istilahi za ufutuhi azizungumziazo mtafiti na zile za falsafa ya usihiri na uchawi. Hii ni kwa sababu utafiti tangulizi umezungumzia ufutuhi. Utafiti huu umeangazia falsafa ya usihiri ambapo umeziba mwanya wa dhana hizo na matumizi ya falsafa ya usihiri.

Senkoro (2011) katika uhakiki wake wa riwaya ya *Dunia Uwaja wa Fujo* alibainisha aina za falsafa ya fujo zilizojitokeza katika riwaya hiyo. Fujo hizo zilichangiwa na falsafa ya udhanaishi aliyonayo mtunzi juu ya maisha. Aidha, amebainisha kwamba aina hii ya falsafa inakatisha tamaa kwa baadhi ya watu. Kwa sababu imewapelekea kutojishughulisha na utafutaji wa maendeleo ya aina yoyote kwa kudhani kuwa haina

maana kufanya hivyo. Kwa jumla, hii ni falsafa dhaifu kwa sababu ya kutobainisha chanzo hasa cha fujo hizo. Anasema:

> ...falsafa aliyo nayo mwandishi kuhusu maisha. Falsafa hii inajitokeza hata katika jina la kitabu chenyewe: *Dunia Uwanja wa Fujo*. Falsafa hii ya kukatisha tamaa inayaona maisha kuwa ni fujo tupu; na mara nyingi fujo hizo ni za kutumia nguvu… Baadhi ya wahakiki wa kazi za E. Kezilahabi wameiona falsafa ya mwandishi huyu kuhusu maisha kuwa ni ya kukatisha tamaa…Kwa kiasi kikubwa ni falsafa dhaifu kwani haichambui mizizi hasa ya fujo hizo zinazoongelewa. Ni falsafa ambayo ijapokuwa wakati mwingine hugusia kuhusu misingi ya fujo hizo za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni, haizichukulii nguvu (uk. 89).

Kwa jumla, uhakiki huo umezungumzia falsafa ya mwandishi kuwa ni dhaifu na ya kukatisha tamaa. Hii ni kutokana na kutochimbua kiini hasa cha aina hizo za fujo. Andiko hili limetoa mwanya wa kuyatafiti matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule. Hi ni kwa sababu pameonekana upenyo wa kutoyadodosa.

Chuachua (2010) aligusia kufanana kimaudhui baina ya riwaya ya *Nagona* na *Mzingile*. Kufanana huko kunajidhihirisha kwa kuzungumzia falsafa za Kiafrika, usihiri, dhana za umazingaombwe na utumiaji wa visasili katika maandiko hayo. Aidha, amebainisha kuwa lengo la mtunzi kutumia ubunifu huo ni kuibua mbinu za upatikanaji wa suluhisho la matatizo yaikumbayo dunia. Kwa sababu ufumbuzi wa matatizo hayo ndiyo upatikanaji wa utulivu kwayo. Kwa upande mwingine, alizilinganisha kazi za Shaaban Robert na zile za Kezilahabi kiitikadi pamoja na kubainisha kuwa, Kezilahabi ni muathiriwa wa Shaaban Robert. Hii ni kutokana na kuzisoma kwanza kazi hizo kisha kutunga kwa kuiga mfumo huo wa kiutunzi. Kwa jumla, mtafiti amemuweka mtunzi huyo katika mwelekeo wa kuitetea jamii. Na mdau mkuu wa kuitafutia suluhisho migogoro inayozikumba nchi nyingi katika nyanja za kisiasa, kiuchumi na kiitikadi. Kwa hivyo, utafiti huu umejaza pengo la matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi kwa sababu mtafiti tangulizi hakulidodosa.

Khamis (2007) alihakiki riwaya ya *Nagona*, amehusisha uhalisiamazingaombwe uliosawiriwa ndani yake na dhana ya visasili vipatikanavyo katika fasihi simulizi iliyozoeleka hapa Afrika. Alibainisha kuwa mtindo huo sio mpya kutumika katika fasihi simulizi wanayoisimulia wanajamii, bali kwa upande wa fasihi andishi una upya katika kutumiwa kwake kupitia fasihi hiyo. Kupitia makala ya "Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili". Anasema:

> Njia kuu ya usimulizi wa *Nagona* kwa mfano, ni ileile ya kuyamwaga na kuyafululiza matukio, mawazo, falsafa na siasa ya mwandishi… matukio ya hadithi yanayofululiza ndio kiini cha swali.

Kwa jumla, uhakiki huu umesaidia kupata mwanya wa kiutafiti kwa upande wa matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule, kwani hakuonesha kulizungumzia suala hilo katika uhakiki wake. Hivyo, utafiti huu umedodosa matumizi hayo.

Senkoro (1996) katika makala yake iitwayo "nadharia ya fasihi na fasihi ya majaribio" ameangalia mabadiliko yaliyojitokeza katika riwaya za Kezilahabi. Amesema kuwa, majaribio hayo ni dhana ya kifalsafa ya uchotarishaji tu wa kazi za fasihi za mtunzi husika. Uchotarishaji huo unajitokeza zaidi katika riwaya ya *Rosa Mistika na Kichwamaji* kwani ni miongoni mwa riwaya zinazoshika hatamu katika usawiri wa aina hiyo. Kwa upande mwingine, anabainisha kujitokeza kwa falsafa ya udhanaishi juu ya maisha ya mwanadamu na uhalisi wa maisha ya vijiji vipatikanavyo hapa Tanzania. Kwa jumla, kazi yake imezungumzia umajaribio, umazingaombwe na falsafa ya udhanaishi, bila kugusia falsafa ya usihiri. Hata hivyo, uhakiki huo umeacha pengo lililojazwa kupitia matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi.

Mulokozi (1993) amegusia athari za kimaisha alizozipata Rosa Mistika alipokuwa shuleni. Kwa upande wa riwaya ya *Kichwamaji* amegusia falsafa ya udhanaishi juu ya maisha ya kila siku na athari za mfumo wa elimu ya kikoloni. Amebainisha kuwa, mambo hayo

ndiyo kichocheo kikuu kinachompelekea mtunzi kuzungumzia suala hilo. Kwa jumla, alizungumzia kuhusu falsafa ya maisha kwa kuilinganisha na hali halisi ya jamii za Afrika. Uhakiki huo umesaidia kupata pengo la kulitafiti lihusianalo na matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Kezilahabi kwani hakuligusia katika uhakiki wake.

## 2.4 Mapengo Yaliyojitokeza Kutokana na Mapitio ya Maandiko

Kutokana na wataalamu hao, pamegundulika mapengo yafuatayo: Mosi, wengi wamedodosa kipengele cha maudhui zaidi bila kugusia falsafa ya usihiri kimatumizi. Pili, hawakutafiti au kuhusisha usihiri uliomo katika kazi za fasihi za mtunzi teule. Tatu, dhana iliyozungumzwa kwa kina ni mazingaombwe, ambapo baadhi ya wataalamu walitofautiana kiistilahi na aina za usihiri. Nne, hawajaelezea falsafa ya usihiri kwa kina bali waliigusia tu kuwa inaingia katika vipengele vya falsafa ya Kiafrika. Tano, maandiko na tahakiki zao zimejikita zaidi katika kutoa maana bila kuielekeza jamii asili, aina na njia za kuepukana nayo. Sita, hawakuitenganisha na kuibainisha falsafa ya usihiri na kipengele cha maudhui ya fasihi ya zama hizi ila walizungumzia kwa ujumla wake. Utafiti huuumejaza mapengo yaliyojitokeza juu ya falsafa ya usihiri kutokana na watafiti waliotangulia kutoyajaza vyema mapengo hayo. Hiyo, utafiti huu ulichunguza kwa kina matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi ili kujaza mapengo yaliyojitokeza.

## 2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura hii imegusia kiunzi cha nadharia ya utafiti na mapitio ya maandiko ya aina nne; yaliyozungumzia falsafa na fasihi kwa ujumla, usihiri na mazingaombwe ndani ya kazi za fasihi na nje yake,pamoja na yaliyohusu riwaya za Euphrase Kezilahabi kwa jumla.Mapitioyote yamegusia falsafa, dhana ya falsafa ya usihiri, maana, chimbuko, vijenzi, utokeaji na utendekaji wa usihiri. Pia,maandiko yamezungumzia athari za usihiri

na vipi hutekelezwa katika mazingira ya aina mbalimbalina jinsi ya kujitibu usihiri katika jamii. Aidha, pamebainika kuwa utokeaji wa falsafaya usihiri hutokana na maneno, matendo na ishara kwa kubeba sura ya maisha ya watu ndani ya jamii. Hivyo, upo uhusiano kati ya falsafa ya Kiafrikana usihiri pamoja na falsafa za jamii nyingine duniani kwa kila moja kuwa na vijenzi vyake kulingana na jamii husika. Ingawa kumejitokeza tofauti kati ya jamii moja na nyingine katika utekelezaji wa falsafa hiyo. Falsafa ya usihiri imeonekana kwa uwazi palipoangaliwa vipengele vya falsafa ya Kiafrika kupitia maneno, matendo na vijenzi vyake katika nyanja zote za maisha ya Mwafrika.

Kwa jumla, maandiko yaliyododoswa yametoa mwanga, maarifa na taaluma kuhusu dhana ya usihiri ndani yake ambapo imemsaidia mtafiti kuyachunguza matumizi ya falsafa ya usihiri kwa uwazi.Kwa hivyo, sehemu inayofuatia itazungumzia juu yamethodolojia ya utafiti.

## SURA YA TATU

## METHODOLOJIA YA UTAFITI

### 3.1Utangulizi

Surahii inazungumzia methodolojia ya utafitiambayo imekusanya vipengele vifuatavyo: Mpango wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, jamii ya watafitiwa,usampulishajina sampuli iliyotumika,njia na zana za kukusanyia data. Aidha, mchakato wa ukusanyaji wa data, itikeli za utafiti, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, uchanganuzi wa data, mipaka ya utafitipamoja na changamoto zilizojitokeza na utatuzi wake.

### 3.2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu kwa pamoja ulifanyika maktabani na uwandani. Pia, data za maktabani zimekusanywa kupitia maandiko yaliyohusu falsafa na falsafa ya usihiri. Aidha, data zimekusanywa kutoka katika riwaya tatu teule za Euphrase Kezilahabi. Utafiti umetumia njia ya maktabani zaidi kuliko ya uwandani kutokana na asili ya utafiti wenyewe kuegemea huko. Hii ni kwa sababu kuhusisha kazi tatu za mtunzi. Data za uwandani zimekusanywa kupitia dodoso, mjadala na mahojiano. Kwa kuwa utafiti huu ulikuwa ni wa kitaamuli ukusanyaji, uchanganuzi wa data na utoaji wa matokeo umefanyika kwa njia ya maelezo na haukutumia taarifa za kitakwimu. Data zilizokusanywa kutoka maktabani na uwandani zimefanyiwa uchanganuzi na ufafanuzi pamoja na uangalifu mkubwa ili ziweze kutoa matokeo sahihi yalinganayo na malengo ya utafiti.

### 3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika miji ya Zanzibar na Dodoma kwa kiasi kikubwa.Utafiti ulizichagua sehemu hizo kwa sababu ndizo zilizosaidia kupata data kwa urahisi. Matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi ndio

yaliyochunguzwa kwa wasomaji na jamii kwa jumla. Kwa kuwa sehemu nyingine ya utafiti huu ni ya kimaktaba na ulilenga kupitia maandiko mbalimbali ndani yake, maktabazilizotumika kwa kufanyiwa udurusu ni za vyuo vikuu kama vile maktaba ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (*State University of Zanzibar Zanzibar University*),Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Abdul-Rahman Al-Sumait(*Abdul-Rahman Al-Sumait Memorial University*). Maktaba hizo zilisaidia utafiti kupata data. Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dodoma ilisaidia kupatikana kwa tasnifu mbalimbali tangulizi zilizousaidia utafiti kupata mwelekeo wa uandishi wa tasnifu. Katika vyuo hivi vilikuwapo vyanzo vilivyosaidia kupata taarifa mbalimbali zikiwemo ripoti za tasnifu, vitabu na majarida na urahisi wa kupatikana kwa wahojiwa.

### 3.4 Walengwa wa Utafiti

Walengwa wa utafiti huu wamegawanywa katika sehemu mbili kuu ambazo nijamii ya watafitiwa na sampuli iliyotumika kufanyia utafiti.

#### 3.4.1 Jamii ya Watafitiwa

Jamii hii ya watafitiwa imechaguliwa kutokana na mwelekeo, viashiria na uzoefu kuwa sehemu hizo zimekusanya matukio ya usihiri, ufahamu na weledi kwa namna moja au nyingine. Utafiti huu ulipata na kukusanya taarifa kutoka kwa makundi yafuatayo:

a) Riwaya za Euphrase Kezilahabi. Hizi zilisaidia kupata matukio, aina, sababu namiktadha inayoelekezwa matumizi ya falsafa ya usihiri;
b) Wataalamu waliozisoma au kuzihakiki riwaya za Euphrase Kezilahabi. Walithibitisha kuwapo au kutokuwapo kwa falsafa hiyo na athari ziwapatazo wasomi na jamii kiujumla;
c) Mtunzi alitoa mwelekeo na taarifa za matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya zake, na;

d) Wanafunzi wa shahada ya kwanza wa fani ya Kiswahili walichangia juu ya kuwapo kwa usihiri, aina zake, jinsi wanavyoufahamu na kupendekeza njia bora za kujifunza kwa jambo lililo zuri na kuepukana nao kwa lile ovu litokanalo na usihiri.

### 3.4.2 Usampulishaji na Sampuli Iliyotumika

Kwa mujibu wa Kothari (2008: 152) anafafanua kwamba, sampuli ni sehemu ndogo ya watu au vitu vilivyochaguliwa kwa lengo la kutoa taarifa ziwakilishazo jamii nzima. Jambo muhimu la kuzingatiwa katika ufafanuzi wake ni juu ya mtafiti kujua kiwango cha sampuli anayoitumia katika utafiti wake.Pia, Kombo na mwenzake (2006) wanashadidia kwa kusema kuwa "kusampulisha ni njia na mchakato wa kuchunguza idadi ya wawakilishi wenye sifa na tabiasawa na walengwa wa utafiti" Kwa mnasaba huo utafiti huu ulitumia mbinu ya sampuli lengwa[10] ili kupata taarifa zihusianazo na riwaya teule utafiti ulizigawa sampuli kama ifuatavyo:

a) Riwaya tatu za mtunzi teule nazo ni: *Rosa Mistika* (1971), *Kichwamaji* (1974)na *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007). Sababu za msingi zilizomsukuma mtafiti kuzichagua riwaya hizi ni kuwa, usihiri unaojitokeza ndani yake ni wa aina na matumizi tofauti kwa mujibu wa wahusika walivyosawiriwa, walivyobebeshwa na kushamiri matukio ya kiajabuajabu katika sehemu kubwa za maandiko hayo;

b) Wataalamu 10 katika uga wa fasihi waliowahi kuzisoma au kuzihakiki kazi za mtunziteule kutoka katika Vyuo Vikuu vya Dodoma, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na Chuo Kikuu cha Kumbukumbu ya Abdul-Rahman Al-Sumait

[10]Ni mbinu ya usampulishaji ambayo humruhusu mtafiti kuwachagua wawakilishi wa kutafitiwa kulingana na jinsi wanavyoweza kukidhi haja na malengo yake. Mbinu hii huwa na uwezekano hafifu wa kuwa na uwakilishi sawa kwa jimii ya watafitiwa (Said, 2015:23).

c) Wanafunzi 10 wa shahada ya kwanza wanaosoma fasihi ya Kiswahili katika Vyuo Vikuu vya Dodoma na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar;

d) Mwandishi mwenyewe, na;

e) waganga 10 wa kienyeji ambao walithibitisha matumizi ya falsafa ya usihiri.

### 3.5Ukusanyaji wa Data za Utafiti

Sehemu hii inaelezea njia na zana mbalimbali zilizotumika katika ukusanyaji wa data pamoja na mchakato wake.

#### 3.5.1 Njia na Zana za Kukusanyia Data

Utafiti huu ulitumia njia zifuatazo katika ukusanyaji wa data;udurusu wa maktabani, dodoso na mahojiano ya mtu mmoja mmoja au vikundi kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza.

##### 3.5.1.1 Udurusu wa Maktabani

Hii ilifanyika kwa kuzipitia tasnifu mbalimbali zilizoko maktabani, vitabu na majarida yanayowiana na utafiti huu. Utafiti ulikusanya taarifa zinazowiyana na matumizi ya falsafa ya usihiri kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Jambo lililokuwa nje ya malengo liliepukwa ili kwenda sambamba na utafiti wenyewe. Matini zilizopitiwa zilisaidia kupata maelezo kuhusu falsafa ya usihiri, aina na matumizi yake. Zana zilizotumia ni tasnifu zilizoko maktabani, mwongozo wa kusoma vitabu ulioandaliwa na mtafiti, tovuti, makala, majarida, tahakiki na riwaya za mtunzi teule.Hizi zimetumika kuwekea dondoo na kumbukumbu zihusianazo na utafiti**.**

##### 3.5.1.2 Dodoso

Ni orodha ya maswali ambayo yaliandikwa katika karatasi na kusambazwa kwa watafitiwa ili wayajibu. Madodoso yaligawiwa kwa wanafunzi, watalamu wa fasihi, na

mtunzi yalilandana na maudhui ya usihiri, ili kurahisisha ukusanyaji wa data na kupata mwelekeo juu ya mada tafitiwa. Mbinu hii imesaidia utafiti kupata taarifa za ziada kuhusu dhana na matumizi ya falsafa ya usihiri zilizoendeleza uchanganuzi wa data.Mtafiti alitumia njia ya kuzigawanya dodoso na watafitiwa walizijaza, kuwauliza watafitiwa kisha mtafiti kuyajaza madodoso kwa waliokuwa hawawezi kusoma au hawaoni vema. Zana zilizotumika ni maswali yaliyotayarishwa na mtafiti, daftari, kompyuta na kalamu kwa kuwekea kumbukumbu na kuandikia taarifa mbalibali alizozipata maktabani na uwandani

#### 3.5.1.3 Mahojiano

Utafiti ulitumia mbinu ya mahojiano wakati wa kukusanya data. Mbinuhii iliongozwa na mtafiti kwa watafitiwa ilifanywa ana kwa ana na kwa njia ya simu pale ilipobidi. Watafitiwa walikuwa huru kujieleza juu ya mada iliyotafitiwa kupitia maswali yaliyoandaliwa na mtafiti kwa kumhoji mtu mmoja mmoja au vikundi kwa mujibu wa maswali yalengayo falsafa ya usihiri. Katika kuifanikisha mbinu hii kundi la wanafunzi na waliowahi kuzisoma riwaya za mtuzi teule ndio waliotumika. Aidha, weledi wa falsafa ya usihiri walisaidia kutoa taarifa ya hali halisi ilivyo. Kwa hivyo, mbinu hii ilisaidia kupata taarifa za moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa. Pia, kupata data zinazozungumzia matumizi ya falsafa ya usihiri, aina na sababu kwa mitazamo chanya na hasi. Zana zilizotumika ni hojaji, dodoso kwa ajili ya wanafunzi wa shahada ya kwanza, mwongozo wa maswali ya vikundi na mtu mmoja mmoja na mwongozo wa usaili.

### 3.5.2Mchakato wa Ukusanyaji wa Data

Utafiti ulitumia njia mbalimbali ambazoni udurusu wa maktabani kwa kukusanyia data, wavuti, udurusu wa tasnifu tangulizi, majarida, makala na vitabu vilivyohusiana na utafiti huu vilitumika. Data za uwandani zilikusanywa kwa kutumia njia ya dodoso, mahojiano na hojaji ili kutumia miongozo ya maswali ya utafiti iliyotayarishwa. Dodoso lilitumika kwa kuwahoji wanafunzi na mtunzi kwa kupata taarifa zihusianazo na matumizi ya falsafa

ya usihiri. Mahojiano yalitumika kuwahoji wataalamu na wahakiki waliowahi kuzisoma kazi za mtunzi. Mtafiti aliendesha mjadala kwa kutumia mwongozo wa maswali katika makundi mbalimbali aliyoyateua katika vyuo vikuu ambavyo mada ya matumizi ya falsafa ya usihiri ilitumika kuendeshea mjadala kulingana na malengo ya utafiti.

### 3.6Uchanganuzi wa Data

Utafiti uliziunganisha, ulizichuja na kuziwasilisha data ulizozipata kwa njia ya maelezo. Nadharia iliyotumika ni uhalisiajabu. Ambapo malengo ya utafiti na muhimili wa nadharia uliongoza katika uchambuzi wa data ili kupata data zinazowiana na maswali ya utafiti huu. Data za uwandani zilikusanywa kwa kutumia miongozo ya maswali pamoja na udurusu wa maktabani. Kisha, ziliwianishwa pamoja kwa kupata usahihi wake na matokeo ya utafiti. Hatimaye, matokeo yalitolewa kwa njia ya maelezo yakisaidiwa na vielelezo, picha na michoro mbalimbali pale ilipohitajika ili kuweka bayana na kutumika katika kutolea taarifa za kitafiti.

### 3.7Itikeli za Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na misingi, maadili na kanuni za kufanyia tafiti. Mtafiti aliomba barua ya ruhusa kutoka Chuo kikuu cha Dodoma na katika taasisi nyingine zilizoko Zanzibar kama vile afisi ya makamo wa pili wa raisi wa Zanzibar na mtakwimu mkuu wa Zanzibarili kupata ridhaa ya kukusanya data kutoka katika maeneo teule kwa utafiti. Aidha, mtafiti aliwaomba watafitiwa ridhaa ya ushiriki wao na kutunza siri wasizozihitaji kutolewa. Jambo lolote linalokwenda kinyume cha maadili ya utafiti liliepukwa wakati wa kufanywa utafiti.

### 3.8 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Ili kupata matokeo thabiti na halali mtafiti alizingatia mada, malengo, maswalina mipaka ya utafiti. Aidha, alitumia nadharia ilinganayo na maudhui, walengwa wa utafiti, mbinu na zana pendekezwa za kukusanyia datakwa utafiti huu. Tathmini na upimaji wa data zilizopatikana maktabani na uwandani ilifanyika na kukamishwa kwa uchambuzi wa data.

### 3.9Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulichunguza matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi. Riwaya teule zilizotumika ni *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007), *Kichwamaji* (1974)na *Rosa Mistika* (1971).Kazi nyingine za mtunzi zilizo nje ya riwaya hazikutafitiwa. *Riwaya ya Gamba la Nyoka*(1978) ilitumika kutolea mifano na ithibati tu katika kipengele cha athari chanya za usihiri.. Aidha, ilitolewa mifano ingawa kidogo ya usihiri nje ya kazi za fasihi ili kupata vielelezo na ushahidi kwa jumla.

### 3.10Changamoto Zilizojitokeza na Utatuzi Wake

Ingawa utafiti umekuwa na mafanikio makubwa yaliyopatikana, lakini mtafiti alikumbwa na baadhi ya matatizo na changamoto wakati wa ukusanyaji wa data za maktabani na uwandani. Kwa jumla,mtafiti alikabiliwa na changamoto zifuatavyo: Mosi, uhaba wa fedha za kuendeshea na kufuatilia masuala mbalimbali yahusuyo utafiti katika maeneo ya kufanyia utafiti. Hii ni kutokana na waliotarajiwa kutoa udhamini juu ya masomo haya kwa mtafiti kujitoa katika hatua ya mwisho.Kwa madai kuwa hawadhamini fani ya fasihi ya Kiswahili kwa mwaka huu. Mtafiti alilitatua tatizo hilo kwa kukopa fedha hizo kwa ndugu, jamaa na marafiki ili kuendelea na masomo yake kwa kipindi cha miaka miwili.

Pili, ugumu wa kupata data kutoka kwa wahojiwa na wajuzi wa taaluma ya usihiri. Hii ni kutokana na taaluma yenyewe kutawaliwa na kanuni na misingi ya usiri wa kufundishwa watu.Baadhi ya watafitiwa walichelea kutoa siri za usihirikwa kukumbwa na adhabu zake na kuogopea kutumika vibaya kwa taaluma hiyo pindi wakiitoa hadharani. Mtafitialitumia busara kuwahoji kwa kuwaambia kuwa siri zote zimetunzwa na kuwaelezea kuwa fani ya usihiri na matumizi yanayochunguzwa ni kwa ajili ya kuchunguza matatizo yanayowakabili matabibu wa usihiri na jamiiili yapatiweufumbuzi.

Tatu, baadhi ya wahojiwa hawakuwa tayari kutoa taarifa kwa sharti hadi walipwe ambapo baadhi yao walitaka malipo makubwa na wengine yalikuwa ya wastani. Kwa baadhi ya wataalumu wa fani hii ilikuwa vigumu kuwapata ili kupata ithibati ya baadhi ya

mambo.Ikitokea kumpata huwezi kumaliza kuhojiananaye bila ya kukatishwa njiani kwa kuwahudumia wengine. Pia, ugumu wa jawabu iliyokusudiwa. Hata hivyo, mtafiti alitafuta njia nyingine ya kumuhoji na kumshawishi hadi kupata jawabu ilinganayo na maswali lengwa.

Nne, picha za waganga wa kienyeji hazikuambatanishwa. Hii ni kwa sababu watafitiwa haowalikubali kutoa maelezo na taarifa zote walizoulizwa bali hawakuwa tayari kupigwa picha ya aina yoyote wakiwa katika shughuli zao za tiba pamoja na wateja wao. Hali ya kuingizwa picha zao katika tasnifu walisema maadili ya kazi hiyo hayaruhusu. Kwani walisema sawa na kujidhalilisha wao pamoja na wateja wanaowahudumia. Mtafiti aliwaomba kupiga picha baadhi ya vifaa wanavyotumia katika kazi hiyo, kama vile hirizi na pembe za ng'ombe ambazo zimeambatanishwa katika tasnifu. Kwa upande wa picha za wanajamii ya Ukerewe hazikuambatanishwa. Hii ni kwa sababu ya ukata wa fedha za kujikimu na usafiri uliomkabili mtafiti hadi kufika kisiwani huko. Mtafiti alitumia picha alizozipata zenye kwenda sambamba na utafiti na kwa mujibu wa mfuko ulivyoruhusu.

### 3.11Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii imeelezea methodolojia ya utafiti iliyotumika ambapo kila moja kati yambinu za kimethodolojia zimeelezwa na kufafanuliwa kwa kadri ya hali na mazingira yanayohitajika kwa utafiti. Kwa upande wa zana za kukusanyia data zilizingatiwa zilikwenda sambamba na watafitiwa walioteuliwa. Njia ya dodoso, mahojiano na udurusu wa maktabani zilitumika kupata data kutoka kwa jamii ya watafitiwa, na kufanikisha utafiti husika ambapo ilipelekea kukamilisha na kufanikisha utafiti kwa ufanisi. Kwa hivyo, sehemu inayofuatia inazungumzia uwasilishaji na mjadala wa matokeo ya utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii inajadili kwa kina mjadala wa matokeo ya utafiti yaliyojitokeza kutokana na ukusanyaji wa data. Data hizo zilipatikana kutokana na sampuli teule ya riwaya za Euphrase Kezilahabi ambazo zilitumika kudhihirishia matumizi ya falsafa ya usihiri. Matendo, mazungumzo na mandhari ya ajabuajabu kupitia uhalisi wa maisha ya wahusika ndiyo yaliyosaidia kubaini matumizi hayo. Mjadala umefanywa ili kuthibitisha, pamoja na kutetea hoja ya kuwapo kwa usihiri na aina zake katika riwaya za mtunzi teule, ambapo mtunzi ameutumia kama mbinu mojawapo ya bunilizi zake. Mjadala huu umegawika katika sehemu kuu nne ambazo zinazingatia maswali na malengo ya utafiti. Sehemu hizo ni; mosi, aina za usihiri zinazojitokeza katika riwaya za Euphrase kezilahabi. Pili, miktadha ambayo usihiri huelekezwa katika riwaya za mtunzi teule. Tatu, sababu zichangiazo kutokea kwa falsafa ya usihiri; na hatimaye, inatathmini athari za matumizi ya falsafa ya usihiri kwa jamii na wasomaji wa riwaya teule. Mjadala huu unaongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu ambapo msingi wake mkuu umetumika kuyaeleza matukio ya usihiri.Mjadala unaanza kwa kutoa mdhihiriko wa falsafa, pamoja na muhtasari wa riwaya za mtunzi teule. Kisha, unajadili kwa kina ainaza usihiri zinazojitokeza katika riwaya za Euphrase Kezilahabi.

## 4.2Mdhihiriko wa Falsafa ya Usihiri katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi

Sehemu hii inaanza kubainisha mdhihiriko wa falsafa ya usihiri kwa kuangalia historia ya usihiri, pamoja na vijenzi vyake. Mdhihiriko huo umejitokeza kwa kuzingatia kuwapo kwa aina za usihiri kupitia maneno na matendo ya wahusika wa ajabuajabu. Pia, maudhui na mandhari zinavyosawiriwa juu ya utendekaji wa usihiri na ujumbe unaopatikana.

### 4.2.1 Historia ya Usihiri kwa Jumla

Usihiri ni miongoni mwa kipengele cha falsafa ya Kiafrika ambao unafahamika barani Afrika na duniani kwa jumla. "Kuanza kwa usihiri hakuna tarehe hasa ya lini ulianza katika dunia", (Ruickbie, 2004:4).Aidha, Kwa mujibu wa (Abdahu, 2011:35-65) katika nchi za China, Ugiriki na Rom usihiri ulishika kasi katika karne ya kumi na nne na kumi na tano. Ukifuatiwa na nchi ya Iraq, bara la Asia, miji ya India na Ulaya. Kisha, ulisambaa katika bara la Afrika kupitia nchi ya Misri na Sudani. Mnamo mwaka 119H hadi 309H wasihiri waliouliwa ni Khalidi bin Abdillah, A'twaa Al-Mukniu, Haliji Sufi na Hauliyi Al-Manki. Pia, mwaka 661 hadi 672 Abuu-Muitwi na Shaabi Rafai wote hao waliuliwa kwa matendo ya usihiri.

Pia, (Wicca, 2014:3) anasisitiza kuwa, katika nchi za Ulaya usihiri uliingizwa na wasihiri kutika karne ya 3 BC. Kijiji cha kwanza kusifikana kwa usihiri ni "*Gossip*" mnamo mwaka 1000 hadi 1022 AD. Mwaka 1498AD wasihiri waliuliwa katika nchi ya Uingereza, China, Saudi-Arabia na Misri. Mwaka 1958 kwa mujibu wa (Safari, 1993:157-158) Osale Otango (msihiri) alipasua ukuta wa Gereza la Maweni huko Tanga kwa kutumia usihiri akatoweka na hakupatikana. Pia, (Bugaywa, 2014:4) anaeleza kuwa, mwaka 2010 watu 579 waliuawa kutokana nausihiri. Mwaka 2012 waliuawa watu 642. Kuanzia mwaka 1880 hadi hivi sasa, Tanzania inaongoza barani Afrika kwa mauaji yanayotokana na usihiri. Kati ya mwaka 1970 hadi 1984 watu 3,693 waliuliwa kwa imani hizo, huku asilimia 63.5 ya mauaji hayo yalitokea katika mikoa ya Mwanza na Shinyanga. Mwaka 1991 hadi 2001 idadi ya mauaji iliongezeka na kufikia watu 23,000 nchini. Asilimia 80 ya waliouawa wakiwa wanawake wenye umri kati ya miaka 50 na 60. Kwa jumla, historia hii inabainisha matumizi mabaya ya falsafa ya usihiri. Kwa hivyo, utafiti huu umeyachunguza kwa kina matumizi ya falsafa ya usihiri ili kuongeza ufahamu wa wanajamii juu ya falsafa husika.

### 4.2.2 Vijenzi vya Usihiri

Kwa upande wa vijenzi vya usihiri ni vingi sana lakini vilivyo mashuhuri ni hivi vifuatavyo:-

#### 4.2.2.1 Jini

Kwa mujibu wa **(**Hussein, 2011:8-10) anaelezea kuwa jinini ‘kitu kilichofichwa au kisichoonekana’.Pia, (Swanaib, 2014:59) anafafanua kuwa, jini ni kiumbe aliyepewa uwezo na Mwenyezi-Mungu wa kujibadilisha na kujigeuza katika maumbile na sura tofauti bila ya kuonekana na mwanadamu hadi apendapo kufanya hivyo. Aidha, aliitwa Jini kwa sababu ya ‘kutoonekana kwake machoni mwa mwanadamu katika hali ya kawaida hadi yafanyike matendo ya usihiri ndipo ajidhihirishe’. Hali hii inathibitisha kuwa, kutoonekana huko kwa kiumbe huyo hutumiwa vibaya na wasihiri kwenda kuwadhuru wasihiriwa.

(Jazaiya, 1987:23-24) anafafanua kuwa, kutoonekana kwa majini na mashetani hakupelekei ukosekanaji wa kuwapo kwao, bali ndio kichocheo cha matumizi mabaya ya usihiri. Hii ni kwa sababu matendo ya usihiri hukamilishwa kwa njia ya kificho. Kila yanapotekelezwa kwa siri huzidi mara dufu nguvu zake katika kuufanyia kazi usihiri majini hao. Aidha, vitu vingi vipo lakini havionekani. Mathalan, roho za viumbe na mkondo wa kani ya umeme, huthibitika kuwapo kwao kutokana na athari zijitokezazo kutokana na mkondo huo, pamoja na kuishi kwa viumbe hai. Kwa hivyo, athari za jini azipatazo mwanadamu zinadhihirisha matumizi ya usihiri unaotekelezwa na msihiri kwenda kwa msihiriwa. Aidha, matumizi ya majini kwa njia za siri yanatoa ishara ya kuwapo kwao na matumizi ya usihiri katika ulimwengu. Majini hutumika kuwaficha wasihiri na kuruka nao kutoka sehemu moja hadi nyingine ili msihiri kutekeleza matendo ya usihiri. Kwa upande wa maumbile yao ni ya moto, ambayo hutumika kuwaunguzia

wasihiriwa, makazi ya wanadamu na hutumika kupigia radi za kimazingara ya usihiri katika sehemu tofauti au msihiriwa.

Maelezo ya wataalamu hao yanathibitisha kuwapo kwa majini, wanaosaidia kwa kiasi kikubwa utokeaji wa matendo ya usihiri. Inaaminika kwamba asilimia zaidi ya tisini na nane msihiri hatofanikisha matendo ya usihiri pasi na msaada wa majini. Wao humsaidia mchawi aweze kuruka angani na kujibadili apendavyo. Kwa upande wa maumbile na uwezo wa kujibadili kwao kunashadidiwa na maandiko ya Qur-an (55:15). Aidha, katika maandiko ya Blblia yameelezewa.

Mwisho, (Audhi, 2004:57) anasisitiza kuwa, majini hutumika kuufanikisha usihiri kwa kuwaingia wanadamu katika miili yao na kuingiza maradhi. Hushirikiana na msihiri kwa kupaa angani na kuwachukua wasihiriwa katika makaazi yao hadi kuwafikisha giningi. Aidha, majini hujigeuza katika sura ya mbwa, simba, bundi, chui, na mnyama mwingine yeyote ili kufanya matendo ya usihiri aliyoamriwa na msihiri. Kwa ujumla, maelezo ya wataalamu hao yanathibitisha uwezo wa viumbe hao unavyotumika katika kuufanikisha usihiri kwa wanadamu.

#### 4.2.2.2 Shetani

Ni fikra ambayo imezaliwa na binadamu kuwa kielelezo cha nguvu ambazo huwa pingamizi dhidi ya juhudi zake za kuitawala dunia na mazingira yake. Shetani anaweza kuichukua sura yoyote ile. Aghalabu, sura zote zinazochukuliwa na shetani zinatisha na kustaajabisha. Shetani anaweza kuwa kitu chochote. Pia, hutumika kwa kujikinga msihiri dhidi ya wengine ili asidhuriwe nao, (Wafula, 1999:172-176). Nalo *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010:364) linashadidia kuwa, shetani ni kiumbe anayeaminiwa kuwa yupo asiyeonekana, aliyeasi na kufukuzwa kwenye kundi la majini. Maelezo ya wataalamu yanabainisha kuwa, shetani haonekani kwa macho ya kawaida. Na hutumiwa

na mwanadamu katika nyanja za kisiasa, kwa kumtaka awafanye watu wampende msihiri; mpigiwa kura (kuwa na mvuto machoni mwa watu) ili wampe kura za ushindi. Kushika nafasi za juu katika kuwatawala viumbe wengine kimadaraka. Kiutamaduni na kijamii watu hutumia shetani ili kudumisha mila zao na kutatulia matatizo yanayowakabili. Kwa upande wa kiuchumi hutumika shetani aitwaye Chuma-ulete[11] (na wengineo) ili kukuza mapato ya msihiri na kulinda mali alizonazo.

Aiadha, (Jazaiya, 1987:130-136) anafafanua kuwa, shetani hutumika kumtia wasiwasi msihiriwa baada ya kutumwa na msihiri. Kuwafitinisha watu katika jamii kwa kuingiza bughudha na chuki katika nyoyo za wasihiriwa hadi kutengana na kugombana. Pia, shetani hutumika kuwasahaulisha na kuwafanya wasiwe na akili wasihiriwa wakati wanapochukuliwa hadi kufikishwa giningi, hatimaye kuwaua wanadamu hao. Kazi kubwa ya shetani akiwa giningi hutumika kuwaweka kizuizini wasihiriwa, kutojitambua kimawazo na kifikira katika maisha yao yote. Shetani hutumika kuwarusha juu ya anga wasihiri kutoka sehemu moja hadi nyingine nyakati zozote bila ya kuonekana na wanadamu. Maelezo hayo yametoa mwelekeo mzuri juu ya matumizi ya shetani ndani ya jamii anapotekeleza usihiri. Panaaminika kuwa bila ya kuwapo kwa shetani wasihiri wasingalifanikiwa kuruka, kujificha na kuwaficha wasihiri, pamoja na kupita ndani ya nyumba bila ya kubomoa kuta za nyumba. Kuta hizo huachana tu kisha hurejea kama

[11]Ni shetani anayetumika kuziiba pesa za wafanya biashara kwa njia ya mazingara katika maduka yao, mifuko ya suruwali na hata katika nyumba zao bila ya kujitambua.Shetani huyu hutengenezwa kwa vitu tisa (lakini alivitaja vitatu tu kutokana na miiko ya taaluma yenyewe). Navyo ni kidaka cha nazi, chungu kipya na ngozi ya mjusi. Kisha huwekwa makaburini wakati wa saa sita hadi saba za usiku kwa muda wa siku saba 7 au 21 au 27 pamoja na kufukiza uvumba. Huombwa mashetani walioko huko wampe msihiri baraka zao. Hudhihiri moshi mwingi na kiumbe mdogo kama mtoto na huchukuliwa na mchawi. Hapo kiumbe huyo humtumia katika kuibia pesa kutoka kwa watu mbalimbali. Pia,zipo njia nyingine za kumleta shetani huyo. Zipo dawa za kutembea nazo ili kuzivuta pesa za watu wanaopita barabarani pindi wakikutana na msihiri. Maelezo yaliyotolewa na Yussufu Diwani kutoka kituo cha Jamaatul-Kheir katika radio ya *Chuchu F.M 90.9* tarehe 17/04/2016. Pia, maelezo hayo yanafanana na yaliyotolewa na Dkt Salumu Omari katika radio hiyo anayeishi Fuoni-Meli-Tano,Maskani-Zanzibar. Kituo chake kinaitwa Uzima Hebalisti Cliniki, tarehe 18/03/2016.

mwanzo. Hivyo, viumbe hawa kwa kiasi kikubwa wanaaminika kuwa ndio waukamilishao usihiri kutokana na maelekezo ya msihiri katika maisha ya kila siku.

#### 4.2.2.3 Nyota

*Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010:312) linafafanua kuwa, nyota ni umbo la mviringo linaloonekana likiwa dogo angani ambalo hutoa mwangaza usiku; nujumu. (Ash-kara, 1953:349) anashadidia kuwa, nyota ni alama na maumbile maalumu yanayotoa dalili na ishara juu ya kutendeka au kutokea kwa matukio ya ulimwenguni. Zipo nyota zinazotumika kutoa ishara ya mabadiliko ya miongo kama vile kutoka kipupwe kuingia vuli au kiangazi kuingia masika. Zipo zinazoashiria juu ya hali halisi ya mwaka husika kuwa umejaliwa matukio ya shari au ya kheri. Aidha, baadhi yazo zinatumika kuwaongoza watu katika usafiri, kilimo, pamoja na kutumika katika usihiri kwa kukabidhiwa makhadimu [12] wa nyota hizo ili kuwadhuru wasihiriwa. Katika kuleta madhara hayo husaidiwa na majini na mashetani kutoka kwa wasihiri kwenda kwa wasihiriwa.

(Ali, 2014:44) anafafanua kuwa nyota hutumika kutekelezea matendo ya usihiri kwa kuhesabia na kujua nyakati za kutenda matendo ya usihiri. Kuchunguzia maradhi yanayomsumbua mwanadamu, kupigia ramli na kujua wapi yalimsibu magonjwa hayo, pamoja na ufumbuzi wake. (Al-Arabii, ht:53) anabainisha kwamba, nyota zilizo mashuhuri zinazotumika katika usihiri ni; “Shamshu, Zuhura, Atwaaridi, Kamari, Zuhali, Mush-tara na Mirihi." Maelezo hayo ya wataalamu yanabainisha kuwa, nyota hizo

[12] Ni watumishi au viumbe maalumu wanaohudhuria katika ulimwengu ambao huambatana na mawiyo pamoja na machweo (kuchomoza na kutua kwa nyota) ya nyota husika. Makhadimu hao huyatumikia maombi ya usihiri (na mengine yeyote) yanayofanywa na wanadamu/wasihiri yanayoambatanishwa na nyota husika. Kwa mfano, katika nyota ya Atwaridi wapo makhadimu wanaoitumikia hiyo, tangu wakati inapochomoza hadi inapoondoka katika uso wa dunia. Hivyo, mtu akifanya jambo lolote la shida au la raha na kuwakabidhi viumbe hao watamtumikia na kufanikiwa shida hiyo kwa wepesi.Hii ni kutokana na utukufu wa nyota hiyo. Na wasihiri huzitumia nyota hizo kupitia watumishi hao kuufanikisha usihiri wa aina yoyote wanaouhitaji. Kisha huambatanisha na majini pamoja na mashetani. Hivyo ndivyo nyota zinavyotumika katika matendo ya usihiri. (Al-Arabii; ht:12).

zinamsaada mkubwa kwa ufanikishwaji wa usihiri katika jamii. Panaaminika kuwa usihiri haukamiliki bila ya kuzitumia nyota za kuagulia. Kufanyia vitendo vya usihiri kwa kutumia nyota hizo. Hii ni kwa sababu kila nyota hufuatana namajini wanaozitumikia. Msihiri anapowapa makhadimu jukumu la kuufanikisha usihiri huutekeleza. Wasihiri huziabudia pamoja na kuyaambatanisha majini na mashetani kwazo. Huchanganya majina ya majini yapatikanayo katika nyota ili wenye majina hayo wautumikie usihiri. Wasihiri huzitumia nyota kutazamia jambo la baadaye.

(Al-Arabii, ht:55-61) anasisitiza kuwa, nyota za (shamsu, zuhura, mushtara na nyinginezo) zinapochomoza ulimwenguni zinafuatana na Khadimu wao wanaozitumikia. Pindi mwanadamu anapofanya maombi na matendo ya usihiri kwazo hufanikiwa. Khadimu hao humsikiliza mwanadamu maombi yake. Kisha humtekelezea kwa msaada na utukufu wa nyota hizo. Aidha, nyota hutumika kama dira ya kuwaongozea wanadamu na wasihiri kwa kuutengeneza usihiri mwafaka ili kumsibu msihiriwa kupitia watumishi walio katika nyota. Wakati wa usiku nyota hutumiwa na wasihiri kwenda Giningi, pamoja na kurudi katika makaazi yao ndani ya jamii. Maelezo hayo yanaweka bayana kuwa nyota hutumika kwa kupimia hali za anayesihiriwa kwa kuangalia njia za kufanya ili kumsihiri. Ash-kara (khj:30) anashadidia kuwa, nyota hutumika katika usihiri kwa kuambatanishwa na majini pamoja na mashetani ili ushihiri umpate au kumponya msihiriwa. Katika zama hizi wasihiri huzitamka nyota hizo wakati wa kupiga ramli.

Wataalamu hao wanaweka bayana kuwa, nyota hutumika kwa kutazamia mambo mbalimbali kupitia msihiri ili kujua ni usihiri gani uliompata msihiriwa au kwa namna gani anaweza kusihiriwa. Panaaminika kuwa, bila ya kuzitumia nyota hizo usihiri haufanikiwi.

#### 4.2.2.4 Ramli

Ni mizani, chombo, darubini, dira na kipimio cha kutazamia habari za siri na kutatulia matatizo yamzungukayo mwanadamu katika pande zote za dunia. Wala haiwezekani kujulikana maarifa yaliyofichikana katika mbingu na ardhi bila ya kupiga ramli, Al-Falakii (ht:4). Nalo *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010:343) linafafanua kuwa, ramli ni tendo la kutizamia kwa kutumia ubao wenye mchanga au kitabu maalumu; bao: piga ramli. Maelezo ya wataalamu hao yanabainisha kuwa, ramli hutumika kuchunguza mambo ya siri, usihiri ukiwemo ambayo kwa macho ya kwaida ya mwanadamu hayawezekani kujulikana. Kwa hivyo, ramli hutumiwa na wasihiri ili kufanyia uchunguzi wa maradhi ya aina mbalimbali. Kujua chanzo chake na usihiri wa aina gani unawiyana na nyota ya msihiriwa na kumsibu au kumtibu. Pia, Al-Falakii (khj:2-4) anafafanua kuwa, ramli hutumika kupima na kujua mambo yote yanayohusiana na viumbe ambayo yamesimama katika tabia nne; moto, hewa, maji na mchanga. Kwa sababu mwanadamu ameumbwa kwa mchanga/udongo hana budi kuitumia ramli ili kujua mambo yaliyojificha. Kama vile usihiri na matendo ya wasihiri hayaweza kujulikana ila kwa kupiga ramli na sio kwenda hospitali. Kwa upande wa hewa, maji na moto yote hayo yanapatikana katika kiwiliwili cha mwanadamu. Usihiri unapomsibu msihiriwa husababisha moto kwa kuleta homa na maumivu kwa kiumbe. Baadhi ya wakati hutengenezwa usihiri unaosarifiwa katika hewa. Mwanadamu hawezi kufahamu usihiri uliomsibu bila ya kupiga ramli. Hali zote hizo hujulikana kwa kutumia ramli. Kwani “kitu kilichotengenezwa kwa asili fulani hujulikana undani wake kwa kuichunguza asili wenyewe kwa kutumia kipimo fulani”. Hii inamaa kuwa, asili ya mwanadamu imekusanya mchanga, maji, hewa pamoja na moto. Kwa hivyo, kipimo cha kuipimia na kuijua asili hiyo inapokabiliwa na usihiri ni ramli pekee.

Kwa upande mwingine, sawa na kusema kuwa, yapo mambo manne yanayofaa kuchunguzwa kwa kutumia ramli; joto, baridi, umajimaji na uyabisi. Aidha, ramli husaidia kujua pande nne za dunia; mashariki, magharibi, kaskazini na kusini. Bila ya kupiga ramli matendo, matukio na muamala wa watu usingalijulikana kutoka pande hizo. Kwa sababu muamala huo ungalifichikana machoni mwa watu. Aidha, nyumba, mambo ya ghaibu, kuzijua nafsi za waja, yaliyowasibu, hali za mali zao, na kutolewa ushahidi, yote hujulikana kwa upigaji wa ramli. Maelezo hayo yanabainisha kuwa ramli hutumika kujua mambo yaliyofichikana. Pia, ni vigumu kuujua usihiri kwa macho ya kawaida. Kwa hivyo, ramli hutumika kujua jambo, mhusika, pahala, wakati, njia za kufanya ili kuweza kutekeleza usihiri kwa namna moja au nyingine. Inawezekana kutofanikisha usihiri na kutomtibu msihiriwa kwa baadhi ya wakati bila ya kupiga ramli.

**4.2.2.5 Mzimu**

Ni pahali kama vile chini ya mti au pangoni ambapo watu huenda kutambika. Makao ya mashetani; panga, (*Kamusi la Kiswahili Fasaha*, 2010:296). Pia, (Mberwa, 2015:11) anashadidia kuwa mizimu hutumiwa na mafundi wa uganga kufanikisha usihiri kwa kufichia vifaa vyao na kufugia mashetani na majini. Nukuu hizi zinabainisha kuwa mizimu ndizo sehemu kubwa wanazozitumia wasihiri kufanikisha usihiri kwa kuwaficha vizuu au ndondocha, kutambika na kufanikisha usihiri kwa wasihiriwa. Katika mizimu hufanywa usihiri kwa kutumia maneno na matendo ya wasihiri kwa lengo la kufanikisha usihiri au kumtibu msihiriwa. Baadhi ya wakati watu hutambika, kuomba, kuwafuga majini, kuwatuma waende kuwadhuru watu na kuwaomba. Wasihiri wanaamini kuwa, uwezo wa mizimu ni mkubwa kwa kutoa adhabu kwa wasihiriwa, pindi wachawi wanapopeleka maombi yao dhidi ya wengine. Inaaminika kuwa pasi na kuwapo kwa mizimu na mapango usihiri usingelikamilika, wala kutoa athari za kusibiwa na usihiri

kwa mlengwa. Kwa sababu mizimu hutumika kama nyumba za wasihiri, majini na mashetani pamoja na makao makuu ya giningi kwa ajili ya kutekeleza usihiri.

#### 4.2.2.6 Mitishamba

*Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010) linafafanua kuwa, mitishamba ni utumiaji kiufundi wa mimea hiyo kutoka kwa waganga wa kienyeji ili kuleta madhara kwa mtu mwengine. Aidha, *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (1981) kama ilivyonukuliwa na (Safari, 1993:154-155) inaelezea kuwa mitishamba ni mchanganiyko wa vitu na miti maalumu ya dawa wanayoitumia waganga wa kienyeji ili kuleta madhara; hutumika kumsihiri mtu, au faida kwa viumbe; hutumika kumtibu msihiriwa. (Kenyatta, 2004:28-34) anashadidia kuwa, mitishamba hutumiwa na waganga wa kienyeji kwa kurogea na kuwatibu usihiri unaowasibu wanajamii. Wakati mwingine huchanganywa mizizi ya miti hufukizwa ili kumleta jini anayetumwa kwenda kuutekeleza usihiri kwa wasihiriwa. Pia, waganga wanajua kutengeneza usihiri kwa mitishamba, dawa za kuzindika mashamba ama nyumba zao. Dawa hizo ziliwanasa watu na hawakuweza kuondoka katika mashamba au nyumba hizo. Aidha, mitishamba hutumika kutengenezea dawa za mapenzi (kindorobi [13]). Ufafanuzi huo unabainisha kuwa mitishamba ipo na inatumiwa na waganga wa kienyeji ili kufanyia usihiri au kujitibia. Hivyo, kuwapo kwa mitishamba kunafanikisha kutendeka kwa vitendo vya usihiri kwa kiasi kikubwa katika jamii ya Watanzania. Hii ni kwa sababu mitishamba inapotengenezwa na kunuwiliwa kisihiri humkaribisha jini na shetani pamoja na kugeuka kuwa kisaidizi chao kwa kuukamilisha usihiri huo. Viumbe hao wanatumika katika usihiri kwa kujibadilisha sura zao kuwa za binadamu au wanyama ili kuwadhuru wasihiriwa kwa mujibu wa manuwizi ya msihiri.

[13] Ni dawa ambayo Wamatengo walikuwa wanaitumia kwa ajili ya kuimarisha mapenzi yao. Ilitumka kuharibu mishipa ya fahamu ili mmoja wao asiwe na wivvu kwa mwenzake. Dawa hii hutengenezwa kwa mambo mengi miongoni mwayo ni; magamba ya miti, mjusi aliyekaangwa ndani ya chungu, damu ya hedhi, maziwa ya nguruwe na manuwizi ya dawa hiyo (Kenyatta, 2004:23-25).

### 4.2.3 Muhtasari wa Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi

#### 4.2.3.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Rosa Mistika*

Riwaya hii ilitungwa mwaka 1971 ikiwa ni riwaya ya kwanza ya mtunzi teule katika mfululizo wa bunilizi zake. Jina la riwaya ya *Rosa Mistika* ni la fumbo lenye maana ya 'Waridi lenye Fumbo' linalosawiri hali halisi ya maisha ya Tanzania.Riwaya hii ndiyo ya mwanzo iliyofanyiwa uchotarishaji katika bunilizi za Euphrase Kezilahabi,(Senkoro, 1996:7). Pia, riwaya inazungumzia malezi ya vijana wa kike yanayopitia hatua kwa hatua na kukabiliwa na misukosuko mbalimbali katika mazingira yao. Mtunzi ameisawiri misukosuko hiyo kuwa, huanzia ngazi ya familia, dini, elimu hadi kufikia siku ya kufa ambapo ndiyo hatima ya maisha ya wanadamu katika ulimwengu. Pia, falsafa ya udhanaishiimejumuishwa, (Wafula na Njogu, 2007:75). Hii ni kutokana na mtunzi kumsawiri Mungu kama hakimu wa kibinadamu aliyechanganyikiwa na kesi ambayo imemkabili. Mawazo kama haya hujiri kutoka katika akili ya mwandishi mwenyewe kuhusu suala la kuwapo au kutokuwapo kwa Mungu.Katika kubainisha malipo ya matendo anayoyatenda mwanadamu hapa duniani, mhusika Rosa amesimamishwa mbele ya Mungu ili kupatiwa hukumu inayostahiki. Aidha, riwaya inazungumzia matatizo ya uongozi na uchumi kwa kupitia mhusika Rosa tangu akiwa nyumbani kwao hadi kufikia elimu ya juu. Mandhari ya riwaya ni ya visiwa vya Ukerewe na kuvuka mipaka hadi kufikia mkoani Morogoro ambako ndiko Rosa alikosoma masomo ya ualimu. Hatimaye, riwaya inamalizia kwa mhusika Rosa kujiua kama ni suluhisho la migogoro inayomkabili yeye na wazee wake.

#### 4.2.3.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Kichwamaji*

Hii ni riwaya iliyotungwa mwaka 1974 ambayo inazungumzia kuhusu athari za elimu ya kimagharibi waliyoipata vijana wa Kiafrika ambayo ilizua mgogoro baina yao na wazee

waliokuwa wakipingana nayo. Wazee wanataka kuendeleza mila na desturi walizozirithi kwa wazazi wao ilihali vijana wanapigania mabadiliko na uhuru wao katika nyanja zote. Mtunzi anawawakilisha wahusika wawili katika kuujenga na kuuendeleza mgogoro huo. Nao ni Kazimoto na Manase. Riwaya hii "ndiyo ya kwanza ya kidhanaishi kuwahi kutokea katika fasihi ya Kiswahili," (Ponera, 2014b:247-248 akimnukuu Sakkos). Pia, (Wamitila, 2002:121) anashadidia kuwa, riwaya ya *Kichawamaji* inazungumzia falsafa ya udhanaishi juu ya maisha ambayo ndiyo iliyomuathiri mtunzi katika uandishi wake. Udhanaishi huo unawakilishwa na mhusika Kazimoto anapotatizika kujibu swali aliloulizwa na wazee juu ya kuwapo kwa Mungu.Majawabu aliyoyatoa kuwa, huenda kuwa hakuna Mungu ambapo wazee walikataa. Hali iliyompa ugumu kuyakinisha kuwako au kutokuwako kwake. Hii ni kwa sababu maarifa aliyonayo mwanadamu yana kikomo. Kuyatafuta maarifa hayo ni msukumo mkuu wa maisha ya binadamu. Kwa jumla, bunilizi hii inagusia nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii kwa kuisawiri hali halisi ya jamii ya Watanzania. Pia, inajadili mila na desturi kwa kuangalia wakaazi wa Ukerewe wanaowakilisha Watanzania wote. Mtunzi anadhihirisha ufanikishaji wa falsafa ya udhanaishi kwa vifo vya mama Rukia na Kazimoto. Pia, msanii anaamini kuwapo kwa falsafa ya usihiri na kutumika kwake katika jamii kama ni mojawapo ya kipengele cha falsafa ya Kiafrika, kinachowasaidia watu katika kutatua matatizo yao.

#### 4.2.3.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*

Riwaya hii imetungwa mwaka 2007 ambayo inazungumzia hali halisi ya maisha na matatizo yanayoikabili dunia kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kijamii,Senkoro (2011). Mtunzi anagusia masuala ya utawala wa busara na hekima unaothibitika badala ya kutumia nguvu katika uongozi. Pia, anagusia mpoomoko wa maadili kwa vijana, ambapo usasa na ukale unapingana; wazee wanataka kudumisha mila, desturi na malezi yaliyotawaliwa na ukale wakati vijana wanataka mabadiliko katika nyanja zote za maisha.

Halikadhalika, mtunzi anaamini kuwapo kwa usihiri katika jamii ya Watanzania si kwa watawaliwa tu, bali hata watawala wanashiriki katika matendo hayo. Aidha, mwandishi ametumia falsafa ya udhanaishi katika kuelezea nafasi ya maisha kuwa si ya kutegemewa, kwani mwanadamu hakijui kimtokezeacho kesho yake. Riwaya inajadili masuala ya malezi na athari za kijamii, (Senkoro, 2011:83-84). Aidha, Chuwa (2004) anasisitizakujadiliwa athari za matatizo ya ndoa, malezi, mvutano baina ya wazee na vijana pamoja na wakaazi wa mjini na vijijini. Pia, riwaya inayaelezea masuala ya imani na mtazamo wa mtunzi juu ya kuwapo kwa usihiri katika kiwango cha Kitaifa na Kimataifa ambayo yamejadiliwa kwa kina.Hatimaye, riwaya imekusanya matukio ya uchawi. Hii ni kuonesha kwamba, maarifa ya Wabantu hujulikana kupitia falsafa ya usihiri. Kwa sababu wahusika wa rika la wazee na vijana hushiriki shughuli za uchawi (Chuachua, 2016:277-281). Kwa hivyo riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* imeakisi matumizi ya usihiri.

### 4.2.4 Mdhihiriko wa Aina za Usihiri Zinazojitokeza katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi

Uandishi wa bunilizi za fasihi mbalimbali za watunzi hutawaliwa na mbinu mbalimbali za kifani na kimaudhui. Kama vile usihiri, taharuki na mazingaombwe kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa wepesi ndani ya jamii. Dhana ya falsafa ya usihiri na aina zake si ngeni sana katika jamii ya Watanzania na duniani kwa jumla. Usihiri uliomo na uliotumiwa na mtunzi teule kupitia riwaya zake, umejitokeza wa aina mbalimbali kwa kuzingatia vigezo vya mandhari, maneno, matendo na matukio waliyobebeshwa wahusika wa riwaya hizi. Wahusika wanaofanikisha usihiri ni wageni, wenyeji, ndugu jamaa na marafiki. Wengine ni wanyama, waganga wa kienyeji, majini na mashetani. Pia, hutumika vitu visivyokuwa binadamu wala wanyama kama vile hirizi, talasimu, mitishamba,

mitulinga na vifaa vya kuagulia. Wahusika hao wamefanya mambo yasiyo ya kawaida na ya ajabuajabu ili kuonesha athari na kuwapo kwa usihiri kulingana na matukio ya kijamii.

Utafiti ulizingatia mambo matatu katika kubaini aina za usihiri huku ukiongozwa na nadharia ya Uhalisiajabu. Kwanza, maandiko ya wataalamu kamavile Ali (2014), Label (2013), Mungwa (2013), Abdahu (2011), Tunguli (2010), Avastar (2009), Audhi (2004), na Kabalani (2004). Pili, mtazamo wa watafitiwa (wahojiwa) walioko uwandani ambapo majawabu yaliyopatikana juu ya usihiri na aina zake yalilinganishwa na yale ya wataalamu. Tatu, maelezo ya mtunzi na kuyalinganisha na sifa za wataalamu na za uwandani.Aina za usihiri zimebainika kwa kuangalia vigezo vya; matumizi ya wahusika wa ajabuajabu pamoja na matendo yao, lugha wanayoitumia katika mazungumzo, maana inayopatikana, tabia zao, mandhari na matukio yasiyo ya kawaida.Kigezo kingine ni maudhui na ujumbe unaopatikana katika riwaya jinsi yanavyolandana na yaliyoko katika jamii.Aina hizo za usihiri huweza kutendwa kwa dhahiri au kwa siri hutegemeana na msihiri husika. Kwa jumla, utafiti huu umegundua kuwapo kwa aina tano za usihiri katika riwaya za mtunzi teule kama zifuatazo:

a) Usihiri wa kufarakanisha. Kwa mfano, alifanyiwa Rosa kwa kutiliwa kwenye maji na mwanafunzi aliyesomanaye katika shule ya Rosary aliyejitambulisha kwa jina la ‘Mwalimu wa Nyakabungo’ katikariwya ya *Rosa Mistika*, Muyango alifanyiwa usihiri na wenyeji wa Ukerewe. Pia, Mugala na wajukuu zake (Leonila)waliwasihiri watu katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo;*
b) Usihiri wa sauti.Kwa mfano, bundi alitumika kutoa sauti katika *Rosa Mistika* na jogoo aliyezungumza aliyekuwa akifukizwa na wavuvi katika kisiwa cha wachawi katika *Dunia Uwanja wa Fujo;*

c) Usihiri wa mapenzi. Kwa mfano, ulifanywa na mhusika Vera katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo;*

d) Usihiri wa mazingaombwe. Kwa mfano, ulifanywa na kundi la michezo ya maonesho ya mazingaombwe la Muganga Golita na kundi la Funga Bilima, katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* na;

e) Usihiri wahirizi.Kwa mfano, hirizi walizokuwanazo wageni wa Mugala waliokaa nyumbani kwa Kasala katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo.*Mhusik*a* Pili alivaa hirizina waganga wa baba yake Kazimoto katika *Kichwamaji.*

### 4.2.5 Aina za Usihiri Zinazojitokeza katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi

#### 4.2.5.1Usihiri wa Kufarakanisha

Huu hujulikana kwa jina la usihiri wa Kutenganisha au Kugombanisha. Hufanywa kwa kutumwa jini na shetani wanaotumikakuwagombanisha na kuwafarakanisha watu wawili au zaidi. Kuwatenganisha watu hao na vitu,pamoja na ulimwengu; yaani kuuliwa. (Ali, 2014:84-86) anasisitiza kwamba “usihiri wa kufarakanisha hutumika kumtenganisha mtu na mtu au mtu na kitu.” Lizingatiwalo katika kufanikisha aina hii ya usihiri ni kuingiza uhasama na ugomvi kwa kutumia usihiri ili watu walioshikamana kwa muda mrefu watengane na wafarakane. Pia, msihiriwa kuachana na kitu alichokizoea, kimpatiacho manufaa katika maisha yake, lakini ghafla huachana nacho kwa namna ya ajabu bila kutaraji wala kutarajiwa kufanya hivyo.

Utafiti umegundua kuwa unapojiri usihiri wa aina hii huwa pamefanywa mambo matatu. Moja, jina la msihiriwa hutumika kupimia nyota zake ili kusihiriwa mhusika huyo. Pili, huokotwa nyayo, kivuli, au athari ya kitu chochote alichokitumia msihiriwa. Tatu, hukabidhiwa jini na shetani wa kuutumikia usihiri huo kwa kutumia manuizi maalumu ya kisihiri na msihiriwa husibiwa na usihiri lengwa. Katika hali hiyo kila jambo alifanyalo

msihiriwa linakuwa chini ya usimamizi wa majini na msihiriwa anakuwa hana hiyari juu ya matendo yake. Matukio hayo yamebainika kwakutumia nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa uelezeaji wa matendo ya kifantasia kwa namna ya moja kwa moja, iliyozoeleka katika jamii na kuonekana ya kawaida.

Pia,Baali (1417H) anabainisha aina za watu wanaofarakanishwa ni baina ya mtu na mama yake, rafiki, mshirika wake, mtu na mke wake, mtu na dunia; yaani kuuliwa. Kwa upande wa vitu, mtu hufarakanishwa baina ya nyumba yake; yaani kuona vitisho katika nyumba vinavyomsababisha kuhama. Aidha, huingiwa na maradhi kila anapokigusa kitu au anapoingia katika nyumba iliyosihiriwa. Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaelezeamatukio ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, inayofanya yaonekane ya kawaida katika jamii, imesaidia kugundua kuwa, mhusika mmoja anakuwa ameshikamana na mtu mwingine au jambo fulani, lakini ghafla hutokea matukio ya uchawikutoka kwa msihiri yasiyo ya kawaida machoni mwa msihiriwa.Mathalan,hudhihiri jini machoni mwa msihiriwa na humueleza bayana kuwa ametumwa ili kumfanya ahame katika sehemu hiyo. Pia, aachane na jambo analolifanya. Kutokea matukio ya kutishwa msihiriwa na mtu asiyeonekana katika macho ya kawaida isipokuwa kwa kupiga ramli na kutazamia.Maji yaliyoingizwa usihiri kufanya kichuguu. Yote hayo hujiri kwa msihiriwa. Hupelekea kuwa na bughudha moyoni mwake, kuchukiana, kugombana, kutengana na kufarakiana bila ya kujifahamu baina ya watu wanaoishi katika nyumba lengwa.

Aidha, hujiri miktadha ya matendo ya kumtenganisha mtu na dunia; kwa kuuliwa au kupelekwa Giningi au kuichukia sehemu anayoishi na kurushwa kimazingara[14]. Hata mtunzi anakiri kuwa “Mshenzi huyu ndiye aliyeniharibia maisha yangu! Sijui aliponaje.

[14]Ni hali ambayo mtu hufanyiwa usihiri unaomfanya akimbie sehemu, watu waliotenganishwa na yeye, nchi na mtaa. Kila anapotaka kurejea katika sehemu hiyo hupatwa na dharura kubwa inayomshughulisha hadi kutotekeleza jambo hilo. Au kupatwa na maradhi pamoja na ajali zisizo na sababu kutokea kwake.

Angekuwa kaburini sasa" "Alifanya nini?" (*Rosa Mistika,* uk.73-74). Hii ni dhahiri kuwa ulikuwa usihiri wa kumfarakanisha Rosa na dunia.(Makula, 2012:89) kwa upande wake anaunga mkono kuwapo kwa Giningi, matendo ya kufarakanishwa, pamoja na kuuliwa kwa wasihiriwa kwa kutumia usihiri. Kwa jumla, utafiti umebaini kuwa, usihiri wa kufarakanisha ni hatari zaidi kwa jamii za Kiafrika na unaongoza kwa kutokea kwake.

Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaeleza matukio ya uchawi kwa namna ya moja kwa moja, inayofanya yaonekane ya kawaida, imesaidia kubaini kuwa, kufarakanishwa kwa wasihiriwabila ya kujifahamu, hutokea kwa watu waliokuwa wanapendana kwa kipindi kirefu lakini kwa kufanyiwa usihiri huo hutengana ghafla. Huanza kutofautiana na kuchukiana katika hali ya ajabu. Mmoja kati yao kupitia msaada wa jini hufanya jambo dogo limchukizalo mwingine ambalo halina sababu ya kuchukiana miongoni mwao. Jini na shetani hutumika kuingiza chuki na bughudha kwa kuuchafua moyo wa kila mmoja na kununiana. Utafiti umegundua kuwa katika mikusanyiko, matukio ya shughuli za kijamii na mikabala baina ya wanajamii hufanyiana mambo mbalimbali ya kufurahisha na kuchukiza. Yanapotokea ya kuchukiza watu husameheana. Lakini wengine huweka nia na azima ya ulipizaji wa kisasi kwa matukio hayo. Inapojiri hali hiyo baadhi yao hutumia usihiri wa kufarakanisha kwa lengo la kulipiza kisasi. Hayo yamebainika kupitia mhusika Rosa alipofanyiwa usihiri wa aina hiyo katika riwaya ya *Rosa Mistika*, mtunzi anasema:

> Alichukua maji kutoka mtungini na kuweka ndani ya sufuria ili achemshe asonge ugali. Maji yalipoanza kuchemka Rosa alishangaa kuona maji yamegeuka rangi. Yalikuwa na rangi ya bluu. Alifikiri kwamba labda alichemshia kitu fulani ndani yake. Rosa aliyamwaga na kuchemsha mengine. Kabla ya kuweka maji hayo ndani ya sufuria aliyachunguza kwa makini sana. Aliyaona ni meupe na safi kama kawaida. Alipoyachemsha yaligeuka rangi tena. Rosa aliyamwaga maji hayo karibu na mlango mbele tu ya mlango wake. Aliosha sufuria na kuteka maji mengine kutoka bombani. Alipoyachemsha aliona ni sawa. Alisonga ugali wake akala akashiba. Kesho yake asubuhi Rosa alikuwa bado kitandani aliposikia watu

> nje wakishangaa: “asingepona! Asingepona! Hakika huyu mtu angalikufa mara moja. Labda amekufa. Kaite polisi! Kaite polisi!” Rosa aliamka kwenda kuangalia kulikuwa na nini nje. Alipofungua mlango alishangaa kuona kwamba mlango wote ulikuwa umezibwa na kichuguu kikubwa sana. Rosa alipitia dirishani kutoka nje. Hapo ndipo aliposimuliwa na watu waliokuwa nje kwamba sumu hiyo ilikuwa kali sana. Kama angalikunywa yale maji angalikufa mara moja, bila hata kukohoa. Watu wengi Mwanza walikuwa wamekwishakufa kutokana na sumu ya aina hiyo. Wale waliopata bahati ya kuitupa au kuimwaga, kesho yake kichuguu kiliota pale ilipotupwa. Rosa alikuwa akitetemeka alipokuwa akielezwa habari hii(uk. 73-74).

Nukuu hii inabainisha kuwa, Rosa alifanyiwa usihiri wa kufarakanisha kwa kutiliwa sumu katika maji. Kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisiajabu inayotumia msingi wakuyaelezea matukio ya usihiri kwa namna ya moja kwa moja, inayofanya yaonekane ya kawaida ndani ya jamii, imesaidia kugundua kuwa, usihiri unaweza kujulikana na kumjia msomaji kwa namna ya kumjuvya anapofikiria na kujenga taswira ya kuona sumu inavyoweza kuvimba hadi ikafanya kichuguu. Kichuguu ambacho kilimfanya Rosa asiweze kupita mlangoni. Kutajwa tukio kama hili, la sumu ya maajabu iliyobadilika rangi baada ya kuchemshwa na kufanya kichuguu ilipomwangwa mlangoni, tukio hili huzaa mawazo na fikra kuwa ni dalili za usihiri kwa wasomaji. Sumu hiyo inadhihirisha matukio ya kiajabuajabu kwa kufanya kichuguu[15], hadi zikaondoka sifa za sumu na kuwa za usihiri. zikichunguzwa sifa za maji yaliyosafi ambayo hayakuchanganywa na kitu yanapaswa kuwa meupe.

Aidha, Mhusika Rosa alipoyachota maji kutoka katika ndoo yalikuwa meupe. Lakini alipoyachemsha Rosa yalibadilika rangi ya bluu. Hili ni tukio la kiajabu kwa maji kubadilika yenyewe rangi yake bila ya kuingizwa kitu. Maji hayo yalipaswa kuwa na mapovu yenye rangi nyeupe yaliyosababishwa na kuchemka kwake. Jambo jingine la ajabu ni kuwa yalipomwagwa yalifanya kichuguu hata njia ya kupita haikupatikana.

[15]Mbinu za kisayansi nazo zina udhaifu wake… vifaa vya kukusanyia data havina uwezo wa kukusanya data zilizo njeya uwezo wake. Haviwezi kutueleza kuwapo au kutokuwapo kwa Mungu… Hii ina maana kuwa, udhaifu wa vifaa hivyo vya uchunguzi wa kisayansi haupaswi kutushawishi kuwa hakuna Mungu, uchawi, dini, maadili wala itikeli (Chuachua, 2016:212-213).

Kiuhalisi maji yaliyogeuka rangi ya bluu hayawezi kuvimba, kufanya kichuguu, au kufanya donge linalofanana na barafu. Kwani hayakuingizwa katika friji wala hayakutiwa hamira inayosababisha kuvimba. Sumu[16] haina sifa ya kufanya kichuguu. Lakini iko katika sifa ya jamii ya vitu vya majimaji, chengachenga au vidonge. Hii ni dhahiri kuwa,ulikuwa usihiri ulioambatanishwa na shetani ili kuleta athari kwa msihiriwa, baada ya kunywa maji ili avimbe tumbo na kuhama katika nyumba hiyo. Pia, kufarakana na wakazi wa humo. Ndiyo sababu aliyemtilia usihiri Rosa 'Mwalimu wa Nyakabungo' hakumsubiri Rosa atoke chooni bali aliaga na kutoweka.

Utafiti umegundua kuwa, kutokana na mtunzi kuyasawirimabadiliko ya maajabu ya sumu; kujibadili katika hali tofautini miongoni mwa tabia na dalili za usihiri. Hususan usihiri wa kufarakanisha, kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa uelelezeji wa matendo ya usihiri umesaidia kuutambua usihiri huo. Pia, tabia nyingine ya kubadilika rangi mara zote mbili kwa maji yaliyochotwa ndooni ni kusawiriwa tabia za kitu kilichosibiwa na usihiri. Hudumu katika hali iliyonuiliwa na msihiri; matakwa ya msihiri. Ikichunguzwa katika hali halisi ya maisha ya kawaida, aghalabu kitu au mtu hudumu na usihiri kama yalivyodumu nao maji.Hadi ifanyike tiba mwafaka inayolingana na usihiri.

(Ghazali, ht:19) anasisitiza kuwa, anayetaka kumtisha na kufanya kichunguu nyumbani pa adui yake na kumhamishaau kumfarakanisha, aandike talasimu ya mapambano ya katika

[16]Vipimo vya maabara vinathibitisha kuwapo kwasumu. Lakini sumu inayofanya kichuguu hadi kikaweza kuziba mlango mtu asiweze kupita haipo na haijathibitika. Bali kilichothibitika sumu kuwa na rangi tofauti. Aidha, rangi ya bluu hupatikana kwa mchanganyo wa rangi mbili; cyan na magenta. Cyan ni rangi ya kijani kibichi iliyokaribiana na bluu. Magenta ni rangi ya zambarau nyekundu iliyokoza. Rangi hizi zikichanganywa pamoja na kuwekwa katika maji hutokea rangi ya bluu. Lakini sio lazima zichemshwe ndio ijitokeze rangi hiyo, bali zinapoingizwa tu katika maji hujitokeza rangi hiyo. Pia, haziwezi kufanya kichuguu kinachomzuia mtu asiweze kupita mlangoni yalipomwagwa maji yaliyopata sumu hiyo. Aidha, zipo kemikali ambazo zikiingizwa katika maji hubadilika kutoka hali moja hadi nyingine na kuripuka, lakini hazifanyi kichuguu. Nazo ni hizi zifuatazo: Francium, Caesium, Culcium, Rubidium, Potasium na sodium. Zote huzunguka kwa kasi na huripuka zinapoingizwa katika maji. Wala hazivimbi na kufanya kichuguu. Bila shaka mandhari iliyosawiriwa katika maji hayo imeongezewa nguvu za usihiri zinaweza kufanya kichuguu. (Mahojiano baina ya Mtafiti na mkemia wa hospitali ya Mina *Dispensary*-Zanzibar, Bw. Hamid H. Jamali). Akithibitisha juu ya dhana hiyo, tarehe 19/06/2016.

vita na kuhamisha watu. Talasimu hiyo huandikwa katika karatasiau sahani. Pia, huambatanishwa na nguvu za ziada kama vile jini na shetani. Kisha, aiingize katika maji anayotumia msihiriwa au aliandike yai kisha alifukiye mlangoni au ayamwage maji katika mlango wa msihiriwa. Hutokea kichuguu kikubwa, vitisho, hofu wasiwasi na matendo ya ajabuajabu ambayo humfanya mkazi wa nyumba hiyo ahame mara moja.

Pia, njia nyingine kwa mujibu wa (Ghazal,kjh:12-13) ili pafanyike usihiri wa kufarakanisha panahitajika lipatikane jina la msihiriwa na la mama yake. Ikiwa jina la mama limekosekana hutumika jina la baba yake mzazi, likikosekana jina la baba hutumika jina la Adamu kama jina la ubini; yaani, asili ya mwanadamu yoyote ni nabii Adamu (kwa imani ya dini ya Kiislamu). Hilo ndilo hutumika kumsihiri mlengwa. Kisha, huandikwa jina la msihiriwa katika "*Twasatu"*; ni chombo maalumu (mfano wa sahani na karatasi safi) kinachotumika kuandikia talasimu. Pamoja na kukabidhiwa majini na mashetani kwa ajili ya kumfarakanisha baada ya kuingizwa katika maji. Yakinywewa maji hayo, yakikanyagwa au kuguswa na msihiriwa hupatwa na hofu, fazaa na kuchanganyikiwa hadi kufikia kuihama sehemu hiyo. Maelezo hayo yanathibitisha kuwa Rosa alifanyiwa usihiri wa kufarakanisha.Uliomhusisha mwanafunzi mwenziwe aliyejitambulisha kwa jina la'Mwalimu wa Nyakabungo' aliyesoma naye katika shule ya *Rosary*. Usihiri huo aliingiziwa ndani ya maji ya kunywa na kupikia ambapo ulijibainishabaada ya kuchemshwa maji hao. Uhalisiajabu katika msingi wa kuyaelezea matukio ya kufantasia umesaidia kubaini kuwa, usihiri huo ulikuwa na madhumuni matatu: Kwanza, kumtenganisha Rosa na dunia; kumuua ili asiwepo ulimwenguni. Pili, kumhamisha katika eneo alilokuwa anaishi kwa sababu aliyehasimiana naye alikuwapo tangu zamani karibu na eneo hilo. Tatu, kumfarakanisha Rosa na marafiki zake aliokwisha wazoeakatika nyumba aliyokuwa akiishi. Kwa hivyo, usihiri wa kufarakanisha umesibu kwa mhusika Rosa kwa sababu ya matukio ya ajabuajabu yaliyojiri katika maji na mlangoni pake.

#### 4.2.5.2 Usihiri wa Sauti

Ni usihiri ambao hutumia sauti inayosawiriwa kwa njia ya usihiri kutoka kwa msihiri kwenda kwa msihiriwa, inayotoka kinywani mwa jini na shetani katika hali ya kutisha au kinywani mwa msihiri mwenyewe. ‘Husikika sauti zimsemeshazo msihiriwa akiwa macho au amelala pia msihiriwa huporoja bila mpangilio,’ (Ash-kara,1953:79). Katika kuufanikisha usihiri huu, binadamu, wanyama, mimea, mawe, ardhi na kila kitu kiliyopo katika mandhari lengwa hutumika.(Ali, 2014:10) anasisitiza kuwa“husikika sauti zinazosema naye (msihiriwa) anapokuwa macho, lakini hamuoni mtu anayemsemesha, pamoja na kuwashuku marafiki zake.”Aidha, *Kamusi la Kiswahili Fasaha* (2010:356) linafafanua kuwa sauti ni mlio wa mtu au kitu unaotokana na kugongana kupuliza au kubonyeza kitu kama vile honi. Pia, ni mtetemeko wa mkondo wa hewa unaosababishwa na ala za matamshi. Kwa kawaida,‘sauti hutumika kufanyia usihiri unaopelekwa kwa msihiriwa lengwa’, (Ali, khj:104-105). Pia, (Makula, 2012:90) anathibitisha sauti za wahenga wa Giningi hutumika kwa malengo tofauti likiwamo la kuufanikisha usihiri. Kwa mujibu wa utafiti huu, mambo yanayozingatiwa katika kutokea kwa aina hii ya usihiri ni matatu; Kwanza, kudhihiri sauti za ajabuajabu kutoka kwa msihiri kwa namna yoyote ile inayosawiriwa kwa njia za usihiri kwenda kwa msihiriwa;iwe kwa kutumia wanyama au vinginevyo. Pili, msihiriwa huzungumza na hucheka bila ya sababu hadi kufikia kiwango cha wendawazimu; yaani sauti kutoka kinywani mwa msihiriwa. Mwisho, husikika sauti kutoka katika mazingira yaliyomzunguka msihiriwa bila ya kuonekana kwa mzungumzaji. Kwa jumla, usihiri wa sauti hutumika kuingiza hofu kwa wasihiriwa, kuifanya jamii iwe na watu wazururaji, hatimaye kuwa wapumbavu wa kudumu; wasio na akili za kuleta maendeleo kwa jamii.

Nadharia ya Uhalisiajabu inayotumia msingi wa kuyaelezea mandhari ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane ya kawaida katika jamii,

imesaidia kugundua kuwa,hali inayoweza kuzua fikra ya kuwa pametokea usihiri wa sauti kupitia sauti ya bundi[17] iliyosarifiwa kwa usihiri ni katika namna tatu. Kwanza, alitumwa jini kutoka nyumbani kwa msihiri au mapangoni hadi kwa msihiriwa. Alipofika nyumbani hapo alijigeuza sura, maumbile na sauti kutoka ya kijini na kishetani hadi kuwa ya ndege (bundi).(Jazaiya, 1987:23) anasisitiza kuwa " hali ya kuumbwa majini kwa moto inawasaidia kujibadilisha katika maumbile tofauti" Hii ni kwa sababu viumbe hao kuwa na uwezo wa kufanya hivyo kama walivyoamrishwa na wasihiri. Pili, sauti ya bundi hufanywa isikike masikioni mwa wasihiriwa ifanane na ndege huyo katika mazingira yao. Hii inaonesha kuwa katika jamii ya Ukerewe wapo bundi[18] ndiyo maana jinialiamrishwa kutoa sauti ya ndege huyo. (Kenyatta, 2004:7) akishadidia kuwa "tena mchawi aliweza kuonekana katika hali ya bundi". Tatu, sauti ya bundi hufanywa isikike masikioni mwa wakazi wa nyumba au mtaamzima ili kujenga dhana kuwa ni sauti ya ndege huyo, bali ni sauti ya jini.Lengo la sauti hiyo ni kumtia wasiwasi na kumpiga chale-tochi[19]msihiriwa kwa ajili ya kuuliwa. Kwa hivyo, dhana iliyojengeka kwa wanajamii kuwa akilia bundi ni ishara ya usihiri ni ya kweli. Wakati anapolia ndege huyo,sauti huingia katika nyoyo zawasihiriwa,pamoja na wasiokuwa hao ili kuingiza hofu.Kwani ndege hao wanaaminika kuwa ni majini na mashetani waliotumwa kufanya hivyo.

[17]Wabantu hawatasita kumhusisha mtu na uchawi ikiwa anafuga paka wengi. Paka na bundi ni viumbe wahusishwao (Chuachua, 2016:281).

[18]Ni aina ya ndege wenye sauti nzito ambao hulia usiku wa manane. Pia, ni adimu kuonekana. Sauti ya bundi ni ishara ya nuhusi inayoingia mtaani au katika kijiji alicholia. Hii ni kwa sababu bundi anatumika na anasawiriwa kisauti tu na wasihiri lakini hasa huwa jini aitwaye '*Al-Ankisi'*; yaani jini anayetumwa na wasihiri kuingiza nuhusi na mikosi katika mtaa. (Kipindi cha tiba kilichorushwa na Saidi Mketo mtaalamu anayeendesha tiba ya usihiri. katika radio *Coconut 88.9 F.M* iliopo Mnara wa Mbao-Zanzibar, tarehe 12/02/2016 saa tatu hadi nne usiku).

[19] Ni usihiri unaotumika kumjuilisha msihiri jambo lolote analofanya msihiriwa.Kama vile, kuuliwa, kuonekana alipo, hali yake ya afya ikoje, dawa anazotumia, na hata mganga anayemtibu hukatazwakumfanyia matibabu. Pia, hutumika kuwekwa msihiriwa katika orodha ya watu wanaopelekwa Giningi.Huu ni usihiri uliombaya zaidi kwa wagonjwa wa usihiri. Kwa sababu msihiriwa hawezi kujificha. Hii hufanana na darubini wanayoitumia wasihiri kuona kila jambo na tukio analolifanya aliyesihiriwa. (Maelezo yaliyotolewa na mtaalamu wa falsafa ya usihiri. Yussuf Diwani, kutoka kituo cha Jamaatul-Kheri Bububu-Zanzibar, katika redio ya *Chuchu 90.9 F.M*tarehe 10/02/2016).

Baadhi ya wakati majini hao hujigeuza umbo la ndege na mwanadamu. Hutumika kumzungumzisha msihiriwa bila ya kujua yanakotoka maneno hayo. Hali hizo zote hutumika kuwatia wasiwasi wasihiriwa na kuufanikisha usihiri. Sauti hiyo husarifiwa kwa mujibu wa matakwa ya msihiri katika hali ya kawaida,(Twauha, 1987:45-59). Kwa mfano, hutumika mnyama aliyezoeleka katika jamii husika kama vile bundi, mbwa, komba au mtu. Pia, baadhi ya vitu hutumika katika hali ya kustaajabisha na kuogofya kwa kuzungumza mfano wa sauti ya mtu bila ya kuonekana kwa mtoaji wa sauti hiyo. Msihiriwa husikia sauti inayofahamika au isiyofahamika masikioni mwake. Kwa mnasaba wa mandhari hayo, maelezo ya mtunzi teule yanathibitika kubeba sifa za usihiri wa sauti kupitia riwaya ya *Rosa Mistika*, mtunzi anasema:

> Usiku wa manane bundi walianza kusikika. Watoto walijikunja vitandani watu wa kisiwa hiki wanaamini kwamba bundi akilia karibu na mji kifo hutokea humo. Kwa hiyo bundi walipolia hofu ya watu iliongozeka (uk. 93).

Nukuu hii inabainisha mandhari ambayo usihiri husawiriwa kwa kusikika sauti ya bundi na wanyama wengine. Hali hiyo inabainisha kuwa usihiri wa sauti upo. Kwa kawaida bundi ni ndege mwenye tabia ya kuishi katika mapori yenye kiza, mizimu, mapango, na sehemu za maficho. Pia, bundi haonekani kwa urahisina aghalabu sauti yake husikika wakati wa usiku. Tabia kama hizi zinawiana na za wasihiri kwa kujificha wanapotendausihiri wakati wa usiku kama alivyo bundi. Kutokana na kuwiana kwa tabiabaina ya bundi na wasihiri, watu wamemnasibisha ndege huyo kutumika katika matendo ya usihiri. Wasihiri nao huitumia fursa hiyo kufanya matendo ya usihiri kupitiasauti ya bundi kwa kuwageuza majini na mashetani wanaowafuga wazifananishe sauti hizo ili kuwadhuru wasihiriwa.(Kenyatta, 2004:7-9) anasisitiza kuwa mchawi huweza kuonekana katika sura ya bundi (litungutu). Wamatengo waliamini bundi akifika na kutua juu ya paa la nyumba au miti iliyozunguka familia au ukoo, huwa ni ishara ya

mkosi mkubwa. Wengi walianzakuhofu walitafuta madawa ya kujikinga na adui huyo mbaya. Watu karibu asilimia tisiini na tano waliamini kuwa ni mchawi aliyeleta maradhi.

Pia, (Mbwerwa, 2015:82) anashadidiakwamba,bundi hutumika kama ni kiashirio cha kufariki kwa mtu wa mtaani na kuleta vishindo. Bundi anapolia usiku hunasibishwa na wanga na wachawi.‘katika mitaa si mara nyingi kusikilikana sauti ya bundi lakini siku inaposikika haupiti muda mrefu mtu hufariki[20]’. Maelezo hayo yanashabihiana na ya Saidi Mketoanafafanua kuwa, “jicho la bundi hutumika kutengenezea usihiri kwa kuwafukua maiti ndani ya makaburi kwa kuchanganywa na dawa nyingine[21]” Akiendelea kufafanua anasema kuwa, baadhi ya wakati sauti ya bundi hutia hofu mtaani. Aidha, mtu husikia sauti zimuitazo akiwa amelala auyuko macho lakini akitoka nje haoni mtu yoyote. Maelezo hayo yanabainisha utendekaji wa usihiri wa sauti. Lizingatiwalo hapa ni kutokea kwa sauti iliyosawiriwa kwa njia ya usihiri. Iwe anaitoa msihiri mwenyewe au anaisikia. Mandhari ya aina hiyo ya usihiri hutumika katika jamii kwa kuogofya na kutunza mila za jadi. Utafiti umegundua kuwa, jamii hutumia majini na mashetani kuigiza sauti ya bundi katika hali ya usihiri kwa njia ya ajabu. (Buhairi, 2911:43-46) anashadidia kuwa, majini hujigeuza na hugeuzwa katika maumbile na sura tofauti, pamoja na kutoa sauti zinazofanana na kiumbe huyo. Pia, hujichomozakatika umbile la mwanadamu, mbwa weusi, paka mweusi;kwa sababu wanyama weusi ndiyo wenye nguvu zaidi katika kutekeleza matendo ya usihiri.Aidha, husikikasauti za bundi, komba, mbwa, simba, chui, na wanyama wengine wa hatari katika hali ya kuogofya na kushangaza ili kumdhuru msihiriwa. Maelezo haya yanaweka ubainifu kuwapo kwa usihiri wa sauti.

[20]Mjadala uliofanyika baina ya Mtafiti na mwanafunzi Othman M. Abuu wa shahada ya kwanza katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) tarehe 17/02/2016.
[21]Maelezo yaliyotolewa katika kipindi cha tibana Saidi Mketo mtaalamu wa falsafa ya usihiri kutoka kituo cha tiba asili cha Ankabuti kiliopo Magogoni-Zanzibar. Ufafanuzi huo ulitolewa katika radio ya *Coconut 88.9 F.M* tarehe 12/02/2016).

Aidha, (Twauha, 1988:10-11) anasisitiza kuwa anayetaka kumtisha mtu kwa kutumia sauti ya ndege au mnyama wa aina yoyote, aandike mchoro na talasimu ya kutisha. Talasimu hiyo iandikwe siku ya jumatatu katika saa ya mwanzo wa mchana kwa kutumia miski, zafarani na maji. Kisha, aitundike katika hewa (juu ya mti au sehemu yoyote inayopiga upepo), baada ya kufukiziwa buhuri na kukabidhiwa mashetani na majini. Mchoro unaochorwa ndani ya talasimu hiyo unakuwa na sura ya anayesihiriwa. Mabega yake (mchoro) huandikwa; 'nakuapieni enyi watumishi wa jina (shetani) hili la kutisha, ingizeni hofu na mtisheni fulani bin fulani, asikie sauti na kelele za ndege, wanyama waliomzunguka, apige kelele na aone watu wanaomzungumzisha. Pia, ajibizane nao bila ya wengine kujua, tekelezeni hili enyi watumishi wa jina hili'. Baada ya kutundikwa talasimu hiyo, kila inapopeperushwa na upepo ndio hofu, kuzungumza na kuzungumzishwa huongezeka kwa msihiriwa.  Maelezo hayo ni ishara ya kutekeleza matumizi ya falsafa ya usihiri kupitia usihiri wa sauti.

Mandhari ya kutokea kwa usihiri wa sauti yanakuwa baina ya hali aliyonayo mgonjwa kutoa sauti na wanajamii kwa kusema kuwa ni jambo la kawaida kutokea na kuonekana kwake. (Ali, 2014:104) anafafanua dalili za usihiri wa sauti kuwa, msihiriwa hupatwa na ndoto zinazomfadhaisha, kuona ndotoni kana kwamba kuna mtu anamwita, husikia sauti zinazosema naye au zinazomwita anapokuwa macho, lakini haoni mtu anayemsemesha. Dalili nyingine ni  wasiwasi mwingi, kuwashuku sana marafiki au wendani, huona usingizi kama kwamba anataka kuanguka kutoka juuna huona wanyama wanaomfukuza usingizini. Maelezo hayo yanaweka wazi kuwa, usihiri wa sauti upo katika jamii.

#### 4.2.5.3Usihiri wa Mapenzi

Ni usihiri wa kuipendezesha na kuivutia nafsi ya mtu (msihiriwa) impende mtu mwingine (msihiri) kimapenzi. Usihiri huu hufanywa na kutengenezwa kwa kutumia mitishamba,

mizizi, viungo vya wadudu(kama vile mjusi) vinavyochanganywa na dawa za asili, majini na mashetani. Lengo hasa la aina hii ya usihiri ni mtu mmoja kumvutia, kumlainisha na kumpendezesha mwingine (iwe mapenzi ya ngono, ya urafiki, ya undugu na ya ukaribu). Linalozingatiwa katika usihiri wa aina hii ni mmoja (msihiri) kumfanyia usihiri mwingine (msihiriwa) ili apendwe wala asiwe mbali naye.(Kenyatta, 2004:23) anashadidia kuwa, usihiri wa mapenzi ni dawa inayotumika kwa ajili ya kuimarisha mapenzi katika jamii na kuingiza upole kwa wapendanao. Au hata kumvutia mtu yoyote mbele ya mwingine machoni mwake. Mwanamke anapoona penzi limeanza kupungua na anataka lirejee ili wapendane zaidi hutumia dawa hiyo. Usihiri huo huwekwa katika chakula, maji na vivywaji. Pia, upo wa kutumia dawa ya kuchanjiamwilini na kindorobi[22]. Usihiri mwingine huwekwa mfukoni au katika nguo na harufu ya dawa hiyo inapomfikia msihiriwa papo hapo huanza kumpenda msihiri bila ya kujitambua. Maelezo hayo yanabainisha njia za kufanya ili kutengeneza usihiri wa mapenzi.

Katika kufanikisha hali hiyo mmoja wa wahusika humfuata msihiri kwa lengo la kumsihiri mwingine kati ya wenye mahusiano baina ya mke na mume, mwanamke na mwanamume, baba na mtoto, mama na mtoto, au mtu mmoja na mwingine katika jamii. Maelezo ya Euphrase Kezilahabi kupitia riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* (uk.111) yanazungumzia usihiri wa mapenzi. Hii ni kutokana na matendo ya ajabuajabu aliyoyafanya mhusika Vera ya kumtilia dawa ya usihiri Dennis katika chakula na chai ili apendwe.

Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaelezea matukio ya kifantasia kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo huyafanya yaonekane ya kawaida katika

[22]Ni dawa ambayo Wamatengo walikuwa wanaitumia kwa ajili ya kuimarisha mapenzi yao. Mmoja aliweza kufanya anachotaka kwa mwenzake, hasa wasichana na kinamama. Hutengenezwa kwa kutumia magamba ya mitishamba, mjusi aliyekaangwa na damu ya hedhi. Vyote hivyo huchanganywa na huingizwa katika chakula au kinywaji (Kenyatta, 2004:23-24).

jamii,imesaidia kugundua kuwa, kutokea kwa usihiri wa mapenzi hufanyika matukio haya;msihiri anapotayarisha dawa huanza kupiga ramli ili kujua nyota za msihiriwa kwa namna gani zimewiyana na kuufanikisha usihiri huo. Huchukuliwa jina la msihiriwa na kukabidhiwa majini na mashetani ili wamdhibiti na asifanye jambo lolote la mapenzi ila analolitaka msihiri. (Kabalani, 2008:30-41) anashadidia kuwa kuchukuliwa kwa jina la msihiriwa kuna athari kubwa katika kuufanikisha usihiri wa mapenzi.Kisha,huambatanishwa na manuwizi, hufukizwa kwa uvumba na udi na hukabidhiwa shetani wa kuitumikia dawa.Wakati dawa inapoingizwa katika chakula na kinywaji hufanyika hali mbili; ya mwanzo, athari za shetani na dawa huingia katika damu ya msihiriwa kama viingiavyo virutubisho vya chakula katika mwili. Hapo matendo yake yote hutendeka na hujiri kwa athari na matakwa ya shetani pamoja na msihiri. Ya pili, shetani huiathiri dawa na hukaa katika nyumba ya msihiriwa ambapo kila jambo analolifanya aliyesihiriwa jini na shetani hulidhibiti kwa mujibu wa matakwa ya msihiri. Hatimaye, polepole msihiriwa huanza kubadilika kitabia. Pia, anakuwa mpumbavukimapenzi na hampendi mtu mwingine ila aliyemsihiri. Kwa upande mwingine, usihiri wa mapenzi hutumika kuwazuia watoto wasifanye mapenzi (zinaa) kabla ya wakati wa ndoa kufika. Kwa mfano, vijana waliokuwa wakitembelea katika mtaa wa Kasala. Vijana hao walipigwa kwa kutumia usihiri bila ya kujulikana na kuonekana mpigaji kwa nia ya kutoshiriki aina yoyote ya mapenzi, mtunzi anasema:

> Mapenzi: mapenzi ndiyo yaliyafanya mji wa Kasala ukafahamika baadaye, mapenzi hayaogopi hatari yoyote. Mapenzi ndiyo yaliyowaleta vijana nyumbani kwa Kasala: Kasala alikiwa na binti wawili wazuri kupindukia… ndani ya sanduku hilo hilo alikuta barua nyingi kutoka kwa wapenzi wa Vera. Barua zingine zilikuwa zimeandikwa kwa lugha ya Kiarabu. Barua hizi alizichukua na kuwapelekea watu waliokuwa wakifahamu Kiarabu. Dennis alishangaa barua hizo zilipofasiriwa. Barua mbili zilitaja dawa ya kuweka ndani ya chai ili kumfanya Dennis ampende sana Vera. Mbili zingine zilieleza dawa ya kuweka ndani ya chakula ili kumpumbaza D. akili asiwe na wivu. Barua hizi zote alizifunga vizuri na kumtumia Vera(uk. 3-111).

Nukuu hii inabainisha kuwa usihiri ni mojawapo ya kinga inayowasaidia wanajamii kujiepusha na mapenzi yasiyo ya halali na ya holela katika jamii. Kwa kubainika kila aliyetaka kushiriki tendo la ndoa na mke au mtoto wa mtu mwingine alipingwa. Aidha, imebainisha kuwa usihiri ni miongoni mwa njia zinazosaidia kuwafunza wanajamii kuwa na maadili na kutotoka nje ya ndoa zao kwa wasio waaminifu. (Mungwa, 2013:2) anabainisha kuwa 'ikiwa kuna mtu anamchukua mke wa mwenzake huwekewa tego; usihiri wa mapenzi na hunasa hadi kufariki'. Pia, mtunzi amebainisha matumizi mabaya ya dawa za usihiri kwa wanandoa wasio waaminifu waliowakilishwa na Vera. Mhusika Vera tabia zake zinaashiria kuwa hushiriki ngono-holela na kila mwanamume anayemtamani. Yeye alizingatia kupata pesa,uzuri wa sura wala sio tabia, pamoja na kukidhi matamanio ya ngono yasiyo ya halali. Hii ilichangia sandukuni mwake kujaa kila aina ya barua zenye lugha tofauti. Tofauti hiyo ya lugha zilizotumika kuandikia barua inaweka bayana wapenzi wa Vera walikuwa kutoka mataifa mbalimbali wazungumzao lugha hizo. Ili kumdhibiti Dennis kimapenzi, Vera alikuwa na barua nne zilizozungumzia dawa za usihiri wa mapenzi. Barua mbili zilielezea dawa za kuwekwa katika chai na mbili nyingine katika chakula. Hali hii inaweka bayana kuwa Vera aliweza kumdhibiti Dennis kwa kila hali nailimfanya kutenda lolote alipendalo mbele ya mumewe.

Dawa hizo hutumika kumpumbaza Dennis na wanaume wengine, pamoja na kutokuwa na wivu ingawa wanawake wanaibiwa kimapenzi mbele ya macho yao. Pia, (Ali, 2014:92) anabainisha matumizi mabaya ya usihiri wa mapenzi kuwa mtu anaposihiriwa anakuwa hawezi kumkataza mke au mume asiende kinyume na ndoa yao. Humpenda mapenzi yaliyozidi mipaka na kumtii kiupofu; yaani, kila analotaka msihiri kufanyiwa, msihiriwa hawezi kumkatalia (mke au mume).Mtunzi amebainisha kuwa, Vera alimsihiri Dennis

hadi akawa mpumbavu kiakili na kimawazo. Kwa hivyo, mhusika Vera alifanikiwa kudumisha penzi lake mbele ya Dennis kwa kutumia usihiri wa mapenzi.

#### 4.2.5.4Usihiri wa Mazingaombwe

Huu ni usihiri unaojiri katika hali ya kuyahadaa macho na kuyasawirisha yaone mambo yanayofanyika mbele ya hadhira yatokayo kwa msihiri ni ya kweli, bali uhakika ulivyo ni kiinimacho na ya uongo (Swanaib, 2014:26). Aidha, mazingaombwe ni kitendo cha kufanya au kumfanyia mtu udanganyifu na hila ili aamini na afuate jambo analoliona au analoelekezwa bila ya kujijua. Pia, ni ujanja wa kumdanganya mtu ili aone jambo au kitu ambacho siyo vile kilivyokuwa mwanzo.(*Kamusi la Kiswahili Fasaha*,2010:228).Kwa hivyo, usihiri wa mazingaombwe unaweza kuelezewa kuwa, ni ufundi wa kufanya mambo fulani; ya usihiri kwa kutumia matendo, maneno, ishara, na usawiri wa mandhani yasiyo ya kawaida katika kutokea kwa ghafla na haraka mambo ya ajabu katika macho ya hadhira. Yakamilishwayo kwa msaada wa shetani pamoja na jini katika utendaji wake. Maneno hayo yanashadidiwa na (Makula, 2012:1) kuwa mazingaombwe ni mambo ambayo hayafanani na kawaida yaliyozoeleka kwa hadhira kutokea sambamba na yale ya kawaida, (Wamitila, 2002:114) akishadidia dhana ya mazingaombwe anasema, ni neno la Kiingereza ambalo ni "*magic;*" yaani, uchawi au mambo ya ajabuajabu. Maelezo hayo yanabainisha kuwa usihiri wa mazingaombwe ni matendo ya hadaa, ujanja na kudanganya kwa kutumia msaada wa vijenzi vya usihiri kama vile shetani na mitishamba katika kuukamilisha kwake.

Aidha, (Swanaib,khj:87-88) anasisitiza kuwa, wasihiri 'huwatumia majini na mashetani' katika mazingaombwe, michezo ya kuigiza na maonesho. Ili kuyafanikisha mazingaombwe lazima yawepo mambo na matendo manne. Mosi, makubaliano kati ya msihiri na majini pamoja na mashetani. Hawa ndio wanaofanya matendo

wanayoamrishwa wakati wa maonesho yenyewe mbele ya hadhira. Kwa mfano, mtu anayefanya mazingaombwe kabla ya kufanya kitu chochote huzungumza na majini na mashetani ndiyo aanze kufanya. Anaweza kusema hivi '*akilikiliye'*; yaani, nitekelezeeni kazi hii ninayoifanya mbele ya hadhira enyi wahudumu wangu. Hadhira hutakiwa na msihiri waitikie '*Ye*'; yaani, wanawasisitiza shetani wamtekelezee mfanyaji mazingaombwe ikimaanisha 'ndio enyi watumishi msaidieni katika matendo mbalimbali ya mazingaombwe hayo'.

Pili, kujigeuza kwa shetani na jini katika umbile la wanadamu na kuhudhurishwa katika maonesho. Wao (majini) huonekana mfano wa watu waliohudhuria katika maonesho. Majini hufika kwa ghafla wakitakiwa watu kwenda mbele alipo muendeshaji wa mchezo wenyewe, bali wameshajuana na mfanyaji wa matendo hayo tangu mwanzoni. Watu (majini) hao huonekana kufanana na wakazi wa mahali yanapofanywa mazingaombwe. Kwa mfano, wanaweza kuhudhuria majini katika umbo la kijana au mzee wa jinsia yoyote. Tatu, kuhadaliwa macho yaone waoneshaji wa mazingaombwe wanafanya matendo mbalimbali kumbe ni ishara tu wanayoihudhurisha, bali wanaotenda hasa ni majini na mashetani waliohudhurishwa na wasihiri. Mathalan, huonekana watu wanaochimba shimo na kuingizwa mtu. Shimo hilo linakuwa siyo la uhakika bali ni la kimazingara.Pia, mhusika anayeingizwa anakuwa si mtu halisi bali ni jini na shetani waliojifananisha katika umbile la wanadamu waliohudhuria pale ili waingizwe ndani yake. Nne, kabla ya kukamilika tendo lolote la hatari jini na shetani wanaotumika hukimbia na huondoka katika hali ya ajabu na ya kimazingara, pamoja na kubakisha taswira ya vivuli vyao vinavyotumika kufanikisha mazingaombwe. Hayo yote hutokea katika hali isiyo ya kawaida.

Pia, (Qur-an,7:115-122) inashadididia kuwapo kwa hali hizo.Pia, wahusika hao wamebainika kwa kutumia nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuwaelezeawahusika wa ajabuajabu kwa namna ya moja kwa moja, iliyozoeleka katika jamii na kuonekana wa kawaida.

Utafiti umegundua kuwa, usihiri wa mazingaombwe unapatikana katika riwaya za mtunzi teule. Hii ni kutokana na matukio ya kifantasia aliyoyatumia mtunzi kwa namna ya uzugaji/hadaa wa ajabuajabu kupitia wahusika wake, anasema:

> Tumaini alianza kuwa anasumbuliwa usiku. Siku moja alikuta mlango wa nyumba yake juu ya paa. Siku nyingine alitupiwa mchanga dirishani… Kabla ya ng'ombe kutembelea mgongo maajabu yalitokea katika kijiji hiki. Yalitokea siku chache baada ya Kasala kumpiga binti yake, na siku mbili baada ya mkutano… Katika kundi la Muganga Golita jitu kubwa lilipandishwa juu. Lilikuwa na sura ya ng'ombe. Ndani ya jitu alikuwa amewekwa mtu. Mtu huyu alikuwa haonekani. Akiwa mle ndani alivuta kamba za midomo ya lile jitu kwa vile kwamba lilionekana kutafuna majani yaliyokuwa yamelijaa mdomoni… "Tazama yule mtu!" John alisema, "anatoa moto kutoka mdomoni!" Katika kundi la Funga Bilima mtu alizikwa chini udongoni, na moto ulikuwa pale pale alipozikwa. Watu wengi walingojea kuona nini kitatokea. Baada ya nusu saa walichimba kumtoa. Alikuwa mzima! Katika kundi hili hili kulikuwa na mtu aliyekuwa amechukua pipa la maji kwa mikono miwili. Kwa jumla viini-macho vingi sana vilifanywa. Labda hata mambo ya uchawi, maana mengi yalikuwa hayaaminiki(uk. 26-52)**.**

Nukuu hii inabainisha kuwa, usihiri huweza kufanywa katika sehemu na malengo tofauti. Katika kudhihirisha kuwapo kwa usihiri wa mazigaombwe ipo hali isiyo ya kawaida iliyosawiriwa na kuonekana ya kawaida. Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuwaelezea wahusika wa ajabuajabu kwa namna ya moja kwa, inayofanya waonekane wa kawaida katika jamii, imesaidia kuwachunguza wahusikawanaofanya usihiri wa mazingaombwena kuwabaini kuwa,walifanya mambo matatuya kukamilika kwa usihiri huo mbele ya hadhira. Kwanza,waoneshaji mazingaombwe katika makundi yote mawili waliyahadaa macho yaone jambo fulani linatokea au halipo kupitia msihiriwa; hadhira. Kwa mfano, mhusika Tumaini alipoukuta mlango wa nyumba yake uko juu ya paa. Hiyo

ni ishara ya hadaa iliyofanyiwa macho yake kupitia msaada wa majini na mashetani. Mlango huo ulisawazishwa na ukuta wa nyumba kimazingara. Kisha kuwekwa taswira yake juu ya paa, huku macho yanaona mshabihiano wa mlango ukiwa juu. Pia, kupitia msaada wa shetani hukuzishwa na kudogoshwa upeo wa uoni wa macho kwa kutofikiwa mipaka ya kilipo kitu chenyewe; yaani, macho hutazama lakini hayafikii kitu kilipo au hukiona kiko mbali. Kwa mfano, msihiriwa anaweza kuangalia mkono wake lakini macho huuona mrefu bila ya kufika mwisho na kinyume chake.

Pili, wasihiri hubadilisha sehemu na kuzikuzisha aukitu kutoka hali moja hadi nyingine. Kwa mfano, kubadilika nywele za vijana waliofariki hadi kuwa  na mvi ni matumizi ya mazingaombwe ya kuwabadilisha wasihiriwa kutoka hali moja hadi nyingine ili kupata urahisi wa kuwapeleka Giningi. Hata lile jitu lililoingizwa ndani yakemtu,ni taswira ya kivuli cha jini tu; yaani, jitu hilo lilikuwa ni kivuli cha jini aliyehudhurishwa machoni mwa hadhira ili waone jitu kubwa. Yule mtu aliyeingizwa ndani ya jitu ni msihri (muoneshaji wa mazingaombwe) aliyefunikwa kwa taswira ya kivuli cha jini mbele ya macho ya watazamaji. Hiyo ni dalili kuwakuonekana kwa jitu kubwa mbele ya hadira yalidanganywa machoyaone mambo yote ni makubwa bali yamekuzishwa kimazingara.

Tatu, wasihiri (waoneshaji mazingaombwe) hukipa uwezo kituna kukihudhurisha machoni mwa hadhira au kukichezesha. Hali hii husababisha kuona kitu kisicho na uhai kinacheza.Kwa mfano, jitu kubwa kufanya vitendo tofauti na wahusika wengine kufukiwa ardhini kisha kutolewa wakiwa hai ni uwezo tu waliopewa kwa njia ya usihiri.Pia, mhusika Tumaini kutupiwa mchanga katika madirisha ni miongoni mwa ajabu anazofanyiwayeye na wazee wake. Hii ni kutokana na tabia ya Tumaini ya kuwaiba watoto wa kike na kufanya nao mapenzi. Kwa hivyo, usihiri wa mazingaombwe ulitumika

kumuadhibu Tumaini na kumhamisha[23]. Aidha, wahusika waliofanya michezo ya kuigiza walifanya mambo yasiyoaminika kutokea katika mazingira halisi.Kwa sababu mwanadamu hana uwezo wa kutema moto katika hali ya kawaida.Mandhari ya kutema moto kutoka mdomoni mwa wafanyaji mazingaombwe inaashiria kuwa ni hadaa iliyofanywa mbele ya macho ya watazamaji. Mfanikishaji hasa wa mambo hayo ni shetani, bali mwanadamu anaashiria tu utendaji huo. Ng'ombe kutembelea mgongo badala ya miguu ni hali isiyo ya kawaida na ya kuhadaa pia ya mazingaombwe. Utafiti umegundua kuwa msihiri huweka kitu chochote kama vile pipa, moto, kamba na vijiti mbele ya watu wamuangaliao. Hutawaliwa na maneno, pamoja na kusema azma ambazo si mtu yoyote anayezifahamu. Vitu hivyo hucheza au huzunguka kwa haraka ya ajabu huku watu wakishuhudia.

Mtunzi ameusawiri usihiri wamazingaombwe ambao hutumika kuwahadaa, kuwadanganya na kuwastaajabisha watu katika mtindo wa kiinimacho. Hii ni kwa sababu msihiri huyasawiri mandhari ya usihiri na kuonekana ni ya kweli. Mandhari zote hizo hutumika kuwaficha wahalifu na watuhumiwa katika hali ya ajabuajabu. Hii ni kutokana na msihiri kuwa na uwezo wa kujificha machoni mwa watu ili wasimuone lakini yeye anawaona. Pia, kuwapoteza watu kwa kutumia mandhari ya kimazingara na wasionekane tena kwa kisingizio kuwa wamepotea kumbe wamefichwa na kupelekwa Giningi kwa kutumia kiinimacho.

Aidha, (Twauha, 1972:51-53) anashadidia kuwa, anayetaka kujificha na kuwazuga watu ili asionekane na adui au mtu asiyetaka kuonana naye, au kumficha mwingine asionekane, pamoja na kujificha chini ya ardhi au katika kigogo cha mti, achore duara mbili katika

[23] Kwa njia za kichawi, Wabantu wana uwezo wa kufanya miujiza mingi inayotisha. Mara nyingi mambo haya hufanywa kama onyo ili mhusika fulani aache tabia fulani au ahame mahali hapo.Aghalabu mambo haya hufanywa ikiwa watu wanakuwa wamechoshwa na tabia ya mtu huyo. Tumaini kwa kiburi chake mbele ya wazee, alianza kufanyiwa miujiza hiyo,ambayo si mambo yakustaajabisha kwa Wabantu (Chuachua, 2016:282).

karatasi au juu ya ardhi. Katikati ya duara aweke herufi za "*Baun, Dalun, Wawun*na *Haun*[24]", akae juu yake au azikanyage. Kisha asome aya ya Qur-ani ya Mwenyezi-Mungu isemayo "kauli yake ni ya kweli na yeye ni mfalme". Aandike talasimu yenye mchoro wa jini aitwaye '*Khadimu-Sihiri*; yaani, mtumishi wa usihiri aikamate mkono wa kulia, pamoja na manuwizi ya kujificha. Hakika hatoonekana mtu huyo hata wakiwa wengi. Maelezo hayo yanathibitisha kuwapo kwa usihiri wa mazingaombwe unaotumika kuwahadaa watu na kujificha. Msihiri huleta kitu kinachojulikana na watu, halafu huzungumza na azma zake ili kuukamilisha usihiri na huwaomba msaada mashetani. Anapomaliza maneno hayo watu huona mambo katika hali isiyokuwa ya kawaida, kushangaza na isiyokuwa ya hakika katika utokeaji wake. Yote hayo huwa hayafanyika katika uhalisi wake lakini macho ndiyo yanayodanganywa yaone hali hiyo bali ni kinyume chake.

Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuwaelezea wahusika wa ajabuajabu kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo inafanya waonekane wa kawaida katika jamii,imesaidia kujua kuwa, wasihirikatika kundi la Funga Bilima na Muganga Golita (waoneshaji mazingaombwe) mara baada ya kuzungumza na jini pamoja na shetaniwalitekeleza amri walizopewa. Ndiyo maana mapipa yalionekana yamechukuliwa kwa mikono na watu kufukiwa na kutolewa wako hai.Hii ni kwa sababu majini huvichezesha vitu hivyo pasi na kuonekana machoni mwa wanadamu. Kama walivyoamrishwa kufanya. Kwa jumla, kutokea kwa usihiri wa mazingaombwe macho ndiyo yaliyosihiriwa yaone kitu kinafanywa lakini ni kiinimacho kwa jambo hilo. (Ali, 2014:98) anafafanua sifa za usihiri wa mazigaombwekuwa mtu huona kitu kinachotaharaki kimetulia, na kilichotulia kinataharaki. Kidogo hukiona kikubwa, na

[24]Hizi ni herufi za Kiarabu ambazo husomwa na wanafunzi wa vyuo vya Qur-ani kwa lengo la kuifahamu Qurani. Wasihiri huzitumia katika usihiri kwa kuziambatanisha na majini na mashetani ili kufanikisha mambo yao.

kikubwa hukiona kidogo kutokana na majini na mashetani wanaovibadilisha. Huonekana vitu katika hali isiyokuwa ya hakika, kama watu walipoziona fimbo na kamba kugeuka nyoka wanaotembea wakati wa Firaun aliyeshindana na nabii Mussa (as). Nukuu hii inabainisha sifa za usihiri wa mazingaombwe unaofanywa katika jamii na riwaya za mtunzi teule. Kwa hivyo, wahusika wa kundi la Bilima na Golita wameisawiri mandhari ya ajabuajabu ili kudhihirisha ufanikishwaji wa mazingaombwe katika jamii

**4.2.5.5Usihiri waHirizi**

Huu ni usihiri unaotekelezwa na kukamilishwa kwa kutumia maandiko tofauti yahirizi yenye; naneno, picha, michoro na ishara zinazowavutia majini na mashetanikufika sehemu zilipo hirizi ili kuzitumikia kwa kila wanachoamrishwa na msihiri.Pia, (*Kamusi la Kiswahili Fasaha,* 2010:117) linasisitiza kuwahirizi ni maandishi yaliyoandikwa juu ya kitu kama vile kitambaa na karatasi kwa mfumo maalumu. Huandikwa kwa herufi za lugha yoyote au Kiarabu, iwe moja moja (huruful-mukatwaati) au zilizoungana (huruful-mutaswilati). Kwa kutumia michoro na alama zinazowakilisha maumbile ya majini na mashetani. Kisha, huvaliwa mwilini, hutundikwa juu ya nyumba, pamoja na kufukiwa ardhini na msihiri au mtu mwingine yoyote. Hirizi hutumika kama kingadhidi ya madhara, maradhi, kinga ya usihiri, majini na mashetani; azma.

Pia, (Kasimu, 2005:22-25) anafafanua kuwa, zipo hiriziza aina mbili. Kwanza, zinazovaliwa au zinazochukuliwa na wasihiri kila wanapokwenda; yaani, wanatembea nazo. Hizi hutumika kumsaidia msihiri kujikinga na kutatulia matatizo yanayomkabili popote alipo. Kwa mfano, msihiri amempenda mwanamke, kwa vile anayo hirizi huzungumza nayo na kunuilia kwa kutumia maneno ya usihiri ili kukamilisha shida yake. Papo hapo msihiriwa huyo huathirika kutokana na hirizi hiyo kwa kumpenda msihiri.Mwenye hirizi anaweza kunuilia kama hivi; ‘nakutuma mtumishi wangu muhadae

mwanamke aliye mbele yangu anipende na asijitambue.[25]’ Hirizi hizo hufanya kazi kama zilivyoagizwa huku zikisaidiwa na shetani pamoja na jini. Pili, hirizi zisizochukuliwa. Hizi ni zile zinazowekwa katika nyumba, biashara na kwengineko kwa mujibu wa lengo la msihiri. Nyingine huongezewa vipande vya mitishamba.Wakati inapong’olewa na msihiri huzungumza na majini na mashetani wanaozitumikia hirizi. Kwa jumla, maelezo ya wataalamu hao yanabainisha kuwapo kwa usihiri wa hirizi katika jamii.

Nadharia ya Uhalisiajabukupitia msingi wa kuyaelezea matukio ya usihiri kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane ya kawaida katika jamii, imesaidia kugundua kuwa, maelezo ya mtunzi teule yanazungumzia juu ya usihiri wa hirizi. Hii imebainika kwa kudhihiri matendo ya ajabuajabu aliyoyafanya mhusika Pili aliposhiriki tendo la ndoa na mhusika Kazimoto. Pili ni mhusika mwenyetabia ya kushiriki mapenzi na wanaume wengi. Lengo lake ni kustarehe nao sio kupata watoto.Kwa hivyo, alitumia usihiri wa hirizi kujikinga na ujauzito. Hirizi aliiweka kiunoni mwake na kutembea nayo kila mahali. Kabla ya kufanya tendo la ndoa huhakikisha kuwa hirizi imeambatana na mwili wake. Anapovuliwa hirizi hiyo na mwanamume anayezini naye (Kazimoto) huuliza ‘hirizi yangu iko wapi?’ (*Kichwamaji*, uk. 15). Hii ni ishara kuwa ndiyo ilikuwa kinga na tegemeo lake.

Usihiri wa hirizi hufanya kazi kwa namna mbili.Kwanza, hutumika kuzuia maji ya uzazi yasifike katika mji (mfuko) wa kubebea ujauzito. Hii ni kutokana na kujiri kizuizi cha kimazingara baina ya maji ya uzazi na mji huo. (Twauha, 1988:21) anasisitiza kuwa mwanamke hutumia hirizi inayomzuilia kutopata uzazi. Hirizi hiyo huwekwa kipande cha kucha ya mguu wa paa; (mnyama), chembe chembe za maimunal-bilkhinzil; zinafanana na habasoda. Kisha, huzungushiwa pamba, huandikwa jina la jini anayekabidhiwa

[25]Mahojiano baina ya Mtafiti na mzee Mnyanja U. Abdalla, mtaalamu wa falsafa ya usihiri na tiba za asili anayeishi Chumbuni-Zanzibar katika mkoa wa Mjini Magharibi tarehe 7/3/2016.

kuitumikiahirizi katika karatasi na kuwekwa pamoja.Mwisho, hunuiziwa kwa kuchomwa buhuri na uvumba ili kukabidhiwa jini na shetani kwa kuzisimamia. Kabla ya kufanya tendo la ndoa mwanamke ahakikishe hirizi imeambatana na mwili wake. Hakika hatopata ujauzito kwa msaada wa hirizi hiyo.

Pili, hirizi huua vichwa vya mbegu za uzazi; yaani, mbegu hai zinazotoka kwa mwanamume zinakuwa na mikia inayozisaidia kuogelea na kupita katika njia ya uzazi hadi kufikia lilipo yai linalohitajika kurutubishwa kwa mbegu hizo.Pia, vichwavya mbegu hizo vinakuwa na uwezo wa kulivunja yai na kuingia ndani ili kuweza kutungisha mimba. Lakini kwa kutumia hirizi mikia na vichwa hivyo hukatika kimazingara. Msihiri anapotumia usihiri wa hirizi husababisha kutokuwa na nguvu ya kutoka mbegu za uzazi, kukatika katika hali ya kimazingara na kutorutubisha yai la mwanamke. (Sharifu, ht:144) anasisitiza kuwa mwanamke huzuiliwa kutopata ujauzito kwa kutumia hirizi. Ndani ya hirizihuandikwa aya ya Qur-an isemayo “maa-takhadha swaahibatan wala walada”; hakufanya rafiki wala mtoto. Huandikwa jina la anayeivaa hirizi, jina la jini wa kuitumikia, hunuiliwa pamoja na kuwekwa makaburini au katika tunguli kwa muda wa siku tatu. Kisha, huvaliwa na msihiri kila anapofanya tendo la ndoa. Hakika hatopata ujauzito.Maelezo hayo ni ithibati tosha ya matumizi ya usihiri wa hirizi.

Hirizi aliyoivaa Pili iliambatanishwa na mashetani na majiniili kujikinga na ujauzito. Kwa sababu mwili wa Pili uliatharika kwa mionzi itokayo kwa shetani kupitia katika hirizi hadi mwilini mwa mhusika huyo. Kwa kisingizio kuwa hawezi kulea watoto wapatikanao katika matendo ya zinaa. Matukio hayo yanadhihirisha kuwa, sio jambo la kawaida kwa wanajamii bali la ajabu kutokea kwake, ingawa limezoeleka kwa wasihiri na waganga wa kienyeji, mtunzi anasema:

“Usinitazame!” aliniambia. Nilitazama pembeni.“Aa! Iko wapi?” Alipiga kelele.“Nini?”“Hirizi yangu!”“Hiyo hapo mezani.”“Kwa nini uliitoa?” Aliuliza kwa wasiwasi.“Kwa nini nisiitowe?”(*Kichwamaji,* uk. 15).

Maelezo hayo yanaweka bayana kuwapo kwa usihiri wa hirizi katika jamii. Aina hii ya usihiri hutumika kujikinga na ujauzito na kuingiza hofu kwa wahusika ndani ya wanajamii. Hii ni kutokana na mandhari inayojitokeza ya uvaaji wa hirizi; yaani msihiri huzibeba kila mahali. Pia, mtunzi ameibua nafasi ya waganga wa kienyejina kuonesha nafasi ya wakati katika jamii kuwa ni yenye kubadilika. Kuna wakati ambao jamii ilishika kasi katika matendo ya usihiri kwa lengo la kujikinga, kujitibu na kujipatia pesa zitokanazo na uganga. Aidha, wakati uliopita ulionesha kuwa kinga na tiba iliyoaminika katika jamii ni ile inayotumia vifaa na matendo ya usihiri iliyotolewa na waganga wa kienyeji kama ilivyoelezewa na mtunzi katika riwaya ya (*Dunia Uwanja wa Fujo,* uk. 3). Hii ni kutokana na vituo vya afya kuwapo masafa marefu hususan mnamo miaka ya sabiini na thamanini. Kwa jumla, matendo ya mhusika Pili ya kuvaa hirizi inayotumika kujikinga na ujauzito ni dalili tosha ya matumizi ya falsafa ya usihiri katika jamii.

Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaeleza matukio ya usihiri kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo inafanya yaonekane ya kawaida katika jamii,imesaidia kugundua kuwa, usihiri wa hirizi hufanywa kwa kuandikwa katika karatasi, kitambaa, au kifaa kingine chochote. Kisha, hufungwa kwa kukunjwa karatasi ambazo huwekewa kitambaa cha rangi maalumu hutegemeana na maagizo ya majini na mashetani. Aina hizo za hirizihuwekwa katika nyumba au huvaliwa mwilini kwa kufungwa kiunoni, mkononi au shingoni, nguoni na kuingizwa mifukoni mwa suruali au shati na katika ncha za nguo za jamii ya kanga na vitenge. (Buhairi, 2011:277) anafafanua kuwa, aina hii ya usihiri imehakikishwa kwa wasihiri kwa kutumia msaada wa nyota za kutazamia (kupigia ramli), na majini.Usihiri wa hirizi hutayarishwa kwa kutumia vitu mbalimbali kama vile mizizi ya mitishamba, majini na mashetani. Hutegemeana na lengo

la msihiri au huning'inizwa sehemu lengwa. Kwa jumla, usihiri wa hirizi katika jamii ya Watanzania ni wenye kuongoza kwa matumizi mbalimbali, bali hufanywa kwa siri sana.

**Miktadha ambayo Usihiri Huelekezwa katika Riwaya za Mtunzi Teule**

Suala la kubainisha miktadha ambayo usihiri huelekezwa linategemeana na mtazamo wa mtunzi na jamii iliyoandikiwa. Katika riwaya za mtunzi teuleipo miktadha kadhaa inayoelekezwa usihiri. Miongoni mwayo ni miktadha ya kifo, miktadha ya makazi, miktadha ya usafiri na miktadha ya uzazi na mapenzi.

### 4.3.1 Miktadha ya Kifo

Uhalisi wa maisha ulivyo katika dunia vitu vimeumbwa viwiliviwili. Kama vile uhai na kifo,pamoja na uzima naugonjwa. Mwanadamu anapokuwa na siha njema husahau na hafikirii kuwa kifo kinaweza kumtokezea. Itokeapo kutembelewa na ugonjwa mkubwa wa aina yoyote ile,  fikra zake zote huzielekeza katika miktadha ya kifo. Hii ni kwa sababu maradhi ndiyo chimbuko linalosababisha kutokea kwa kifo. Mtu hufanya kila mbinu kuyatibu maradhi hayo ili kifo kimuepuke. Hata kufanya matendombalimbali ya usihiri ili kujizuia na kifo.Pia, hufikiria kuwa viumbe vilivyomzunguka hutumiwa na wasihiri ili kuutekeleza usihirina mwisho apatwe na kifo. Utafiti umegundua kuwa katika riwaya ya *Rosa Mistika* na *Dunia Uwanja wa Fujo* mtunzi amezungumzia miktadha ya kifokuwandiko usihiri umeelekezwa, anasema:

> Watoto walijikunja vitandani watu wa kisiwa hiki wanaamini kwamba bundi akilia karibu na mji kifo hutokea humo. (*Rosa Mistika,* uk.93).

Nukuu hii inabainisha, kuwa usihiri huelekezwa katika miktadha ya kifo. Hii ni kutokana nakusikika kilio cha bundi watu hukitafsiri kuwa ni ishara ya kifo. Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuwaelezea wahusika wa ajabuajabu kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo huwafanya waonekane wa kawaida, imesaidia kugundua kuwa, mtunzi anakusudia kutaja athari zabundi katika kuufanikisha usihiri kwa jamii

mbalimbali za Watanzania. (Kenyatta, 2004:7) anasisitiza kuwa ‘wengi waliamini bundi ni mchawi tu aliyekuja kuleta madhara’ Hii ni kutokana na ndege huyo (bundi) kuwa na matumizi makubwa mawili katika kuufanikisha usihiri. Kwanza, hutumika kutoleaishara njema kwa wasihiri juu ya kutimia malengo yao,pamoja na kuingiza hofu kwa wasihiriwa. Pia, ishara mbaya huletwa na bundi kwa msihiriwa. Kwa sababu hufahamu kuwa amekaribia kutolewa kikoa cha giningi kutokana na sauti ya bundi. Pili, bundi hutumika katika kuufanikisha usihiri kwa kuwafukua maiti walio makaburini na kuuliwa watu kwa njia za kimazingara.

(Mungwa, 2013:2) anataja vitu vinavyotumika ili kumfukuwa maiti aliyezikwa, ni pamoja na majani yaliyokaushwa ya mti wa mfausiku, lufakale[26] na miti mingine kumi na tatu (hakuitaja).Pia, viungo vya bundi kama jicho na jiniaitwaye Munkara; anayeishi makaburini. Maelezo hayo yanabainisha kuwa vitu hivyo vikichanganywa pamoja hutumika kwa kumfukua maiti aliyezikwa au sehemu ya viungo vyake.

Aidha, Msihiri anapotekeleza matendo ya usihiri nyakatiza usiku huingia nyumbani kwa msihiriwa kwa kupasua kuta za nyumba katika hali ya ajabu kwa masada wa jini na shetani. Wakati huo msihiriwa husibiwa na usingizi mzito wa ajabu. Hata kufumbua macho hawezi. Msihiri huziziba pumzi za mlengwa na kumchukua hadi Giningi kimazingara. Kisha huweka mwili wa kubuni kwa njia ya usihiri unaofanana na wa marehemu. Yote hayo hufanyika kwa kutumia dawa za usihiri zikiwa zimechanganywa na macho ya bundi. Wanajamii wanapoamka asubuhi husikia kuwa marehemu amefariki

[26]Maana yake ni alishakufa tangu kale. Ni mti wenye nguvu za ajabu sana za kuukamilisha usihiri. Mbali ya kutumika kwenye usinga, mti huu hutumiwa na wachawi ili waishi muda mrefu duniani. Kupata dawa wanazozitengeneza wasihiri kwa mti huo na kujipaka, dawa ya kujificha ili watu wasiwaone wasihiri hao na kutengenezea fimbo ya kurukia angani inayosaidiana na ungo. Sio rahisi kuyachuma majani ya mti wa lufakale. Mtu anayechuma majani yake ahakikishe upepo hauelekei upande aliopo wala hakuna mtu anayemuona wakati anapochuma majani, pamoja na masharti mengine. Akikiuka masharti hayo hufariki (Mungwa, 2013:01).

ghafla huzikwa kimyakimya. Baada ya mazishi usiku wasihiri hukusanyika makaburini ili kuutoa mwili wa kubuni wa marehemu. Kisha huhudhurishwa msihiriwa aliyechukuliwa kimazingara na kuchinjwa. Bali wengine huchinjwa Giningi na kununuliwa nyama za marehemu aliyechinjwa; yaani, aliyedaiwa kuwa amefariki.

(Ghazali, ht:7) anafafanua kuwa, mtu anayemuua msihiriwa, 'humpelekea sauti na kumjaza hofu katika moyo wake'. Pia, bundi hutumika kumtoa maiti aliye kaburini ambapo msihiri hutafuta jicho la bundi.Kisha, hulisaga na kuchukuwa kichwa cha popo (ndege) na huandikatalasimu ya kuipasua ardhi; aya ya Qur-ani inayosema 'na tukaipasua ardhi.' Huchomwa pamoja katika sehemu ya kichwani mwa kaburi la maiti anayefukuliwa. Kisha huchukuliwa mabaki ya jivu, masinzi ya vitu hivyo na kusagwa pamoja. Anayemtoa maiti hujipaka nayo usoni, husema manuwizi ya kupasuka ardhi na kutoka maiti (hutegemea anayemtoa maiti lengo lake). Huzuka moshi kaburini alipozikwa maiti na kuchomoza nje ya kaburi.

Vilevile, (Kenyatta, 2004:9-10) anashadidia kuwa, mtu akifa mara tu baada ya kuzikwa wachawi wengi, wanakusanyika makaburini wakati wa usiku, wengine hukopa na wengi wao humnunua aliyezikwa. Yule aliyeua (mchawi) huzungumza na maiti "*Ana nugukoma ne gupita moniomo*". Maana yake; "Kama nimekuua mimi utoke humu kaburini." Ghafla yule marehemu husimama na kutoka mle kaburini. Ndipo shughuli zao za machinjo na kugawana asusa zinapoanza kwa mujibu wa idadi ya wasihiri waliohudhuria. Wasihiri wanao uwezowa kujigeuza ndege, chui, simba, mbweha na sura nyingine yoyote wanayoihitaji. Wanaporuka angani hufumba macho hadi wafike safari yao. Maelezo hayo yanathibitisha kuwa bundi akilia katika mji huleta habari mbaya ya kifo. Hii ni kutokana na matumizi yake kwa wasihiri. Kwa upande wa riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* mtunzi anathibitisha matumizi mabaya ya usihiri katika jamii, anasema:

> Watu wawili walipotea. Haikufahamika walikwenda wapi. Jamaa zao waliwatafuta sana. Wengine walifika hata Mwanza. Kwa kuwa haikuwa mara ya kwanza watu kupotea katika kijiji hiki, na kwa kuwa wenyeji walifahamu watu ambao hupotea hufanywa nini, jamaa zao walikusanyika na kufanya matanga kama kwamba walikuwa wamekufa. Katika siku hizo tu, watu wawili walikufa ghafla. Watu hawa wawili waliokufa ghafla walikuwa bado vijana, lakini walipofunuliwa kabla ya kuzikwa walikuwa na mvi. Jamaa zao walipoona mvi waliacha kulia. Walifahamu kwamba walikuwa akizika manyani au mbwa. Walifahamu wazi kwamba vijana hao walichukuliwa na kugeuzwa vuzuu. Mafundi katika kazi hii humchukua mtu yoyote na kumpumbaza bongo zake kwa dawa, halafu humkata ncha ya ulimi asiweze kuzungumza (*Dunia Uwanja wa Fujo,*uk.27).

Maelezo hayo yanabainisha kuwa muktadha wa kifo ndio unaoelekezwa usihiri kwa wingi katika jamii ya Watanzania. Hali hiyo imebainisha kuwa mtunzi ameyaeleza mazingira ya kupotea kwa watu katika hali ya kutatanisha. Kisha, husingiziwa kuwa wamefariki. Kwa kawaida mtu anapofariki nywele zake hazibadiliki kutoka nyeusi hadi kufanya mvi. Kinachobadilika ni kutoka kwa roho ya mja katika kiwiliwili na hubaki mwili usiojiweza kwa lolote. Aidha, vijana na wazee wanapofariki kabla ya kuzikwa hawabadiliki viungo vyao. Lakini kwa jamii za Kiafrika hufanyika mazingara ya usihiri na huonekana ni matukio ya kawaida. Au aliyepotea na kufariki hurudi nyumbani kwao. Hii ni kwa sababu kilipotokea kifo chake aliyezikwa sio yeye bali ni kiwiliwili kilichoshabihishwa kwa nguvu za usihiri. Hufanyiwa huduma zote za mazishi lakini jamaa wengine hukataa kumzika. Katika muktadha huo usihiri hutumika kama sehemu ya kuwaficha wasihiriwa na kujificha msihiri, kwa ajili ya kuwaangamiza wingine na kuwahadaa. Matanga ya jamaa wa maiti yanaashiria kuwa, msihiriwa aliyefariki kwa njia za usihiri ni vigumu kupatikana kwake. Kwa hivyo, ni tabia iliyozoeleka kwa wanajamii kufanya matanga ili kupeana pole.

(Twauha, ht:98) anafafanua kuwa, anayetaka kumficha mtu, kujificha na kumfumba mtu macho ili asimuone hali anamtazama, aandike jina la '*Lutwufi-Shamati'*katika vipande vitatu vya karatasi. Akifafanua maana ya Lutwufi-Shamati(Twauha, khj:96) anasema: 'ni

jina la jini anayetumika kuwaficha watu ili wasionekane wakati wote hadi wapende wenyewe (wasihiri) kufanya hivyo'. Kipande cha kwanzacha karatasi, akiweke kichwani kwake (msihiri) baada ya kukiandika. Cha pili, akifunge katika mkono wake (katika dhiraa; sehemu inayopinda). Cha tatu, akitie katika maji hadi kifutike maandishi yote. Kisha ajipake maji mwilini mwake. Anapomuona mtu siyemuhitaji kuonananaye aisome aya tukufu ya Qur-ani isemayo "Tukajaalia mbele na nyuma yao kizuizi basi tukawafunika (tukawaficha) wala wao hawaoni". Hakika hatoonekana na mtu aliyemkusudia asimuone; yaani, hapa anatia nia kama vile, "fulani bin fulani nataka asinione ikiwa anamfahamu na ikiwa hamfahamu humnyooshea kidole cha shahada tu[27]". Aidha, namna kama hiyo hufanyiwa mtu anayepotezwa ili asionekane kabisa na jamaa zake kama alivyosema mtunzi teule hapo juu.

Kwa upande mwingine (Twauha, khj:75) anafafanua kuwa, anayetaka asijione yeye mwenyewe anapojitazama kupitia kioo, na hata kumficha mtu asionekane, amchinje ndege aitwaye '*Watwawatwa* [28].' Kisha achukuwe damu yake aandikiye talasimu inayozungumzia kujificha au kumpoteza mtu, aandike katika kioo au karatasi. Atiye buhuri ya udi na kuchoma ubani katika kumfukiza ndege na talasimu aliyoiandika, huku akifanya manuwizi aliyoyakusudia. Kwa mfano, 'ewe jini na shetani fulani bin fulani (anataja majina ya majini) nendeni kwa fulani bin fulani mukamchukue na kumpoteza hadi Giningi asionekane maisha hapa ulimwengu'. Kisha vitu vyote anaviweka katika chungu na anapotaka kujificha au kumficha mtu mwingine anachukua maji hayo kidogo na kuupangusa uso wake. Ikiwa mtu mwingine anayepotezwa ili asionekane, hupakwa maji hayo akiwa usingizini bila ya kujitambua. Hii hufanyika baada ya kupelekwa jini katika nyumba yake na kufanya kazi aliyoamrishwa. Wakati mwingine hupelekwa jini ili

[27]Mahojiano baina ya Mtafiti na Bw. Hassan Kh. Alimtaalamu wa falsafa ua usihiri anayeishi Maungani-Zanzibar, tarehe 27/12/2015.
[28]Ni jamii ya ndege wanaofanana na njiwa (au kunguru) bali wao huishi mwituni kwa Zanzibar huitwa 'Pugi' au wengine huwaita njiwa uwanda. Wanaishi sana katika majangwa na miti yenye miba mikali.

wamchukue msihiriwa katika mazingira ya kutatanisha, kwa kumzunguka pande zote ili watu wasimuone anapochukuliwa. Hakika mtu huyo hupotea na haonekani milele hadi anapotafutwa kwa kutumia usihiri. Huonekana Giningi au amegeuzwa ndondocha au ameuawa. Maelezo hayo yanaweka bayana kuwa usihiri hutumika kuwaangamiza wasihiriwa kwa malengo mbalimbali.

Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaelezea matukio ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, inayofanya yaonekane ya kawaida katika jamii,imesaidia kugundua kuwa, katika miktadha ya kifo msihiriwa hufanywa kama aliyefariki au aliyepotea. Jamaa zake humzika au humtafuta. Watu wanaokufa hukutikana katika mazingira ya kutatanisha na kuwa na mvi ingawa ni vijana. Pia, hugeuzwa vizuu wanaofanyishwa kazi za kilimo nyakati za usiku bila ya kujitambua. Mara baada ya kufariki mwanadamu, watu hutafuta sababu ya kifo chake hasa ikiwa bado kijana. Aliyefariki ikiwa kifo chake kimetokea katika mazingira ya kutatanisha. Kabla ya kuzikwa watu hupandisha mashetani kwa kudai kuwa wanamuona marehemu akichukuliwa na wasihiri. Hapo hudai kuwa “tuseme tunayoyaona?” Hukatazwa na huambiwa na watu wasiseme, bali wayaache kama yalivyo. Hapo marehemu huchukuliwa na kuzikwa na watu hutawanyika.

Dhana za watu huendelea kubaki kuwa marehemu ameuliwa kwa njia ya usihiri na kupelekwa Giningi. Aidha,baadhi ya wanajamii huwafuata waganga na kutazamia kwa kupiga ramli. Kwa upande mwingine, wanapoona matukio ya usihiri yamezidi huweka mikutano na kujadiliana juu ya njia za kufanya ili kupunguza matendo ya usihiri, mtunzi anasema:

> Asubuhi ngoma ililia kwa Mwanangwa. La mgambo likilia lina jambo. Watu waliposikia walianza kwenda mmoja mmoja. Hata wazee siku hiyo walijivuta na mikongojo yao. Kabla ya jua kuchomoza watu walikuwa wamekwishakusanyika wengi. Kama kawaida walikaa katika duara wakiacha nafasi katikati ya mzungumzaji… kuna watu wengine ambao wanatenda mambo ya kusikitisha. Wanachukua wanadamu wenzao na

> kuwapumbaza akili… Kulikuwa na chupa mbili. Moja ilikuwa imejaa dawa ya uganga. Chupa ingine ilikuwa imejaa maji. Maji haya, kama ilivyokuja julikana baadaye, yalikusanywa kwa kuchoma nyama za watu. Yalikuwa mafuta ya binadamu. Kulikuwa pia na sehemu mbalimbali za binadamu ambazo zilikuwa zimekaushwa. Kulikuwa pia na kifurushi kidogo cha nywele ndani ya kitambaa. Hapakuwa na shaka tena kwamba Mugala alikuwa mchawi (*Dunia Uwanja wa Fujo,* uk. 28-30).

Nukuu inabainisha kuwapo mafuta yanayotengenezwa kwa kutumia miili ya watu waliouawa kwa njia ya usihiri katika jamii ya Watanzania. Nadharia ya Uhalisiajabu katika msingi wa kuwaelezea wahusika wanaofanyiwa matendo ya kifantasia kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya waonekane wa kawaida, imesaidia kubaini kuwa, waganga huwaambia watu kwamba maiti ameuawa kwa njia za usihiri. Amenyongwa na kukatwakatwakwa kisu cha usihiri katika tumbo au sehemu nyingine yoyote na kufanywa mafuta yanayotumika kutengenezea dawa nyingine za usihiri. Pia, huambiwa ametengenezewa unga wa ndere[29] ambao hutumika kwa matibabu ya aina mbalimbali kama vile kuchanjiwa wagonjwa katika miili, pamoja na kuchanganywa na dawa nyingine.

Mwisho, (Kenyatta, 2004:18) anabainishakuwa, siku ya pili asubuhi Wamatengo walikwenda kutazama kaburini kama kuna hitilafu yoyote. Walipogundua tatizo waliamua kuzindika (kutega) kaburi. Kama hakuna chochote kibaya kilichotokea walijua kifo hicho ni mapenzi ya Mwenyezi-Mungu. Maelezo hayo yanabainisha kuwa usihiri huelekezwa katika miktadha ya kifo kwa jamii ya Watanzania. Usihiri hutumika kama kisingizio cha kufariki kwa mtu na kuzikwa kisha wasihiri humfukua makaburi. Huchukua mabaki ya mifupa kwa ajili ya kufanyia usihiri.

---

[29]Ni unga mweupe laini unaosemekana unatokana na binadamu k.v. ubongo au mifupa unaotumiwa zaidi na wachawi kwa tiba na mazingaombwe. pia, hutumika katika kutengenezea dawa za aina mbalimbali za usihiri (*Kamusi la Kiswahili Fasaha*,2010: 310).

### 4.3.2 Miktadha ya Makazi

Hifadhi ya makazi kwa mwanadamu ni jambo liingialo katika mahitaji ya lazima. Mwanadamu hufanya kila mbinu ili kuyamiliki makazi yake. Ima kwa kujenga nyumba yake mwenywewe au kwa kukodi. Kwa vile mhusika fulani yameshajulikana makazi yake yalipo, wasihiri huitumia fursa hiyo kwa kufanya na kuelekeza matendo ya usihiri katika nyumba ya mhusika huyo. Hii ni kwa sababu ya urahisi wa kumsihiri na wepesi wa kupiga ramli ili kujua usihiri mwafaka wa kumsibu. Pia, kuwasihiri wingine. (Kenyatta, 2004:2) anasisitiza kuwa usihiri huelekezwa katika makazi kwa kufanywa matukio ya ajabuajabu "pale mlangoni pa nyumba ya mzee vijana walipanga mawe na magogo mzee alikoroma ndani. Ghafla upepo wa ajabu ulijitokeza walishangaa kumuona mzeeyupo nje. Alipitia wapi haijulikani."

Hali hii inabainisha kuwa usihiri huelekezwa katika miktadha ya makazi. Yaani, nyumbani au sehemu ya mazungumzo. Katika muktadha wa kupeana habari za matukio mbalimbali katika jamii, mtu mmoja humfuata mwingine katika makazi yake au katika sehemu ya mazungumzo (vijiweni) kwa lengo la dhahiri lakumtembelea.Au kumjunywa habari huko anakoishi. Aghalabu, msihiri huitumia fursa hiyo kutekeleza lengo lake la siri la kumroga mwingine. (Chuachua, 2016:279) akimnukuu (Tempels, 1959:67) anashadidia kuwa "aliyerogwa anapata matatizo kwa sababu mchawi anafanya kazi ya kudhoofisha kani uhai yake." Katika makazi muktadha wa kusihiriwa kwa Rosa ulitokea kwa kufarakanishwa na shoga zake pamoja na nyumba yenyewe.Matukio yote hayo yamebainika kwa kutumia nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaelezea matendo ya kifantasia kwa namna ya moja kwa moja, iliyozoeleka katika jamii na kuonekana ya kawaida.

Utekelezaji wa kumhamisha mhusika huyokatika makazi ya nyumba ya kupanga ulifanikishwa. Ndipo msihiri (mwanafunzi aliyesoma naye shule ya Rosary) alipomtilia dawa ya usihiri katika maji ili akiyatumia usihiri umpate,bila ya kujua kuwa Rosa amesihiriwa.Maji hayo anapoyagusa au yakifika tumboni, pamoja na dawa ya usihiri ichanganyike na damu kwa kuleta maradhi. Pia, usihiri huo uliambatanishwa na shetani na jini kwa lengo la kuingiza bughudha na chuki ndani ya moyo wa Rosa. Ulisababisha kutengana na wapangaji wenzake. Aidha, Rosaalipachukia mahali hapo na kutafuta sehemu nyingine kutokana na usihiri huo, mtunzi anasema:

> Rosa aliyamwaga maji hayo karibu na mlango mbele tu ya mlango wake. Aliosha sufuria na kuteka maji mengine kutoka bombani… Rosa alikuwa bado kitandani aliposikia watu nje wakishangaa: “asingepona! Asingepona! Hakika huyu mtu angalikufa mara moja. Labda amekufa. Kaite polisi! Kaite polisi!” Rosa aliamka kwenda kuangalia kulikuwa na nini nje. Alipofungua mlango alishangaa kuona kwamba mlango wote ulikuwa umezibwa na kichuguu kikubwa sana. Rosa alipitia dirishani kutoka nje (*Rosa Mistika,* uk.73).

Nukuu hii inathibitisha kuwapo kwa miktadha ya makazi ambako usihiri huelekezwa. Matendo ya usihiri hujiri iwe katika makazi, visimanina katika chemchem. Hii ni kutokana na mandhari ambayo dawa ya usihiri inapochanganyika na maji inakuwa rahisi kutumiwa na msihiriwa. Itikadi ya maji kufanya kichuguu ilitumika kumhofisha Rosa na kumtia wasiwasi ili kumrejesha nyuma katika harakati za kujiletea maendeleo. Hii ni dalili ya usihiri uliotengenezwa na kuelekezwa katika nyumba anayoishi Rosa. Ingalikuwa maji pekee yasingalifanya kichuguu hadi kumfanya Rosa kupenya kwa dirishani.

(Ghazali, ht:18-19)anasisitiza kuwa, mtu anayemfanyia usihiri mwingine kwa ajili yakumhamisha sehemu au katika makazi yake, au usihiri wa aina yoyote ile, achukuwe gao moja la mchanga alifanyie usihiri na aumwage sehemu hiyo. Au afanye usihiri na auingize katika maji anayotumia mlengwa. Ikiwa wapo watu wengi wanaosihiriwa na wanatumia maji katika chanzo kimoja huingizwa ndani yake. Hakika wanapoyatumia au

kuyagusa maji hayo usihiri huwapata, bali hutegemeana na manuizi aliyoyafanya msihiri na lengo la usihiri. Maelezo hayo yanaweka bayana kuwa, usihiri huelekezwa katika makazi kwa kuwekwa katika maji. Maji hayo hutumika kumhamisha msihiriwa na kuichukia sehemu anayoipenda kwa kuiona mbaya kama alivyofanyiwa Rosa. Hali hii husababishwa na mandhari inayosawiriwa na shetani pamoja na jini kwa kuifanya nafsi ya msihiriwa kuiona sehemu kuwa ni mbaya katika macho yake au kuyaona makazi ni mabaya na kufarakana.

Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaelezea matukio ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane ya kawaida katika jamii, imesaidia kugundua kuwa, usihiri uliotumika uliambatanishwa na dawa za usihiri zinazovimba zikipata maji. Hii ni sawa na kusema kuwa, jini aliyetumika alimsababishia Rosa aione sehemu anayoishi ni mbaya na kutengana na makazi hayo. Watu waliotiliwa usihiri ndani ya maji wanapokutanana mwingine katika sehemu iliyofanywa vitendo hivyo huchukiana.Hutoleana maneno yanayosababisha kila mmoja kumchukia mwingine. Kwa upande mwingine mtunzi anaashiria miktadhaya makazi yenye vyanzo vya maji kuwa ndiyo inayoelekezwa usihiri kwa kusema:

> Kwa kuwa wakati huu ulikuwa wakati wa kiangazi maji yalikuwa haba. Wale wenye watu wa namna hii walizoea kuwaamrisha kwenda kuoga kisimani asubuhi na mapema kabla ya wanawake kuamka kwenda kuteka maji. Siku moja kizuuu mmoja alichelewa huko kisimani. Wale wanawake ambao ni kawaida yao kwenda kisimani asubuhi walikutana naye njiani (*Dunia Uwanja wa Fujo*, uk. 27).

Mtunzi anafafanua kuwa, miktadha ya makazi yenye vyanzo vya maji ndiyo huelekezwa usihiri. Huamriwa vizuu waende wakanywe maji katika siku za kiangazi ili kuipata huduma hiyo. Katika vyanzo hivyo wao huamriwa kwenda na wale waliowageuza kuwa vizuu nyakati za usiku. (Twauha, 1972:44) anasisitiza kuwakatika miktadha ya makazi huingizwa usihiri katika maji na vyanzo vyake. Mtu hufanyiwa usihiri uliokusudiwa (kwa

mfano, usihiri wa kumfarakanisha na mwingine). Huingizwa katika maji anayotumia msihiriwa au chai. Mara baada ya kuyagusa au kuyatumia maji hayo usihiri humpata kama ulivyonuiliwa na msihiri. Pia, njia nyingine ni kuandika herufi za "*twazahaji*[30]" katika yai viza wakati inapochomoza nyota ya '*Atwaridi'* kwa manuizi ya usihiri uliokusudiwa. Msihiri huzungumza na mashetani anaowakabidhi kuukamilisha usihiri huo. Kisha yai hilo huvunjwa katika nyumba au kuingizwa katika kisima ambacho msihiriwa hutumia maji yake. Au huweka yai hilo sehemu anayopita mlengwa, basi sehemu hiyo huichukia msihiriwa. Ni dhahiri kuwa Rosa alisibiwa na usihiri katika makazi yakena ndiyo sababu iliyomfanya kuhama.

### 4.3.3 Miktadha ya Matibabu na Usafiri

Katika kutafuta matibabu mtu anapopatwa na magonjwa, watu huanza kuchunguza sababu ya maradhi. Huanza kufanya uchunguzi kwa madaktari wa hospitali kwa kufanya vipimo vya aina mbalimbali ili kujua maradhi yanayowasumbua katika miili yao. Yashindikanapo kwa kutoonekana maradhi na ugonjwa huo, huanza kufikiria kuwa ni ugonjwa wa usihiri na kurogwa. Watu huwaendea waganga wa kienyeji, waaguzi na watazamiaji wa ramli ili kuaguliwa na kuyajua maradhi yanayomsumbua mgonjwa. Baada ya kupingwa ramli au kuzungumza na majini, waganga na wasihiri huanza kusema kuwa msihiriwa amerogwa na anahitaji kufanyiwa matibabu.(Ali, 2014:63) anashadidia kuwa "matibabu ya usihiri kwa usihiri hayafai". Nukuu inabainisha matibabu ya usihiri yasiyofaa. Matukio hayo yamebainika kwa kutumia nadharia ya Uhalisiajabu katika msingi wa kuyaelezea matendo ya uchawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane ya kawaida katika jamii.

[30] Ni mjumuiko wa herufi za hijaiyat/herufi za kiarabu (Twaun, Zaun, haun na jimun) zinazotumika kutengenezea talasimu na hirizi kwa ajili ya kuwatenganisha na kuwahamisha wasihiriwa ambazo huambatanishwa na jini pamoja na shetani katika mazingira tofauti ya usihiri (Twauha, 1972:45).

Aidha, (Kenyatta, 2004:28) anasisitiza kuwa, waganga wa kuagua waliweza kutabiri chanzo cha ugonjwana kuupatia matibabu yake, kifo na matatizo yaliyowakabili wanajamii. Nukuu hii inaweka bayana kuwa usihiri huelekezwa katika miktadha ya matibabu kutokana na waganga kutabiri maradhi na matukio yajayo ndani ya jamii. Hali hii hutokea baada ya kupiga ramli na kutazamia. Mganga huweza kusema kuwa, mgonjwa amesibiwa na usihiri au maradhi mengine. Msihiriwa hupelekwa mapangoni ili kuitwa jini na shetani kwa ajili ya kuvitoa vitu alivyolishwa usiku wa manane, kama ndiyo tiba yake. Baadhi ya wakati waganga hupandisha shetani kwa kudai kuwa wanaangalia na kuwatafuta wasihiri, kuzika vitu makaburini na katika njia panda. Kuwatafuta mashetani wanaowadhuru wasihiriwa kwa kupiga mishindo na kelele.Aidha, kuwapa wasihiriwa dawa ya usihiri hadi iwakolee. Kupitia riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* mwandishi anaibainisha miktadha ya matibabu na usafiri ambayo usihiri huelekezwa kwa kusema:

> Wageni hawa hawakuwa wenyeji wa sehemu hii ya Tanzania. Lakini haikuwa mara yao ya kwanza kuwa wageni mjini kwa Kasala. Wageni hawa hawakuwa wageni wa Kasala: walikuwa wageni wa Mugala. Walikaa nyumbani kwa Kasala kwa muda wa siku tatu; kila siku wakiwa wanalala ndani ya nyumba ya Mugala. Jambo lililomtisha Misana aliporudi nyumbani hirizi zao walizokuwa wamevaa mikononi mwao; na kila siku waliweza kusikika wakikimbia kwa mishindo ‘ti! ti! ti!’ kuzunguka mji mzima wakipiga kelele: “Kamata huyo! Dawa bado haijamkolea.” Baada ya siku tatu wageni hawa walikwenda zao. Walivyokwenda, hakuna aliyefahamu isipokuwa Mugala. Watu kijijini walizoea kuwaona wakati wa mchana wakitembea. Walikuwa hawajapata kufahamu ni jambo gani lililokuwa likiwaleta nyumbani kwa Kasala karibu kila mwezi (uk. 3-4).

Nukuu hii inabainisha kuwa, wasihiri hao walikuwa wakizunguka nyumba kwa lengo la kufanya tiba kwa wakazi. Kutumia majini yaliyoambatanishwa na hirizi na waliruka angani nyakati za usiku, pamoja na kusafiri kwa kutumia mkeka na ufagio kwa kuruka angani. Hii inathibitishwa na mtunzi kwa kusema: “Baada ya siku tatu wageni hawa walikwenda zao. Walivyokwenda, hakuna aliyefahamu isipokuwa Mugala.” Yaani, katika kusafiri kwao walikuwa wakiruka angani ndiyo maana mtunzi alisema walivyoondoka hakuna aliyejua. Hii ni kutokana na mhusika Mugala kuzijua siri za usihiri. Pia, usiri wa

taaluma na njia yenyewe ya kusafiri kwa kuruka kuwa ni hatari na kukataa kujulikana walivyoondoka.(Bakize, 2014:37) anasisitiza kwa "Majaliwa alisafiri sana kwenda sehemu nyingi nchini Tanzania kwa kutumia ufagio." Aidha, vishindo na kelele walizokuwa wakizifanya waganga wa kienyeji ni kuonesha athari za kuhangaika katika kuwatafuta majini na kuwafukuza mapepo wabaya wanaowasumbua wanajamii.

Pia, (Safari, 1993:161) anasisitiza kuwa, usihiri hutumika kwa usafiri wa kuruka angani; yaani, wachawi wanaweza kuruka na kusafiri mbali kwa muda mfupi tena bila ya kuonekana. Wanaweza kupenya ndani ya nyumba bila ya kuibomoa na kuwatia watu usingizi mzito kwa muda mrefu. Maelezo haya yanaweka bayana matumizi ya usihiri katika usafiri wa anga. Kwa mnasaba wa maelezo ya mtaalamu huyo usihiri hutumika kwa usafiri kutoka sehemu moja hadi nyingine. Usafiri huo hufanyika kwa kutumia ungo. "Ungo wa wasihiri umetengenezwa na kufanana na chombo kiitwacho bajaji au pikipiki. Una urefu wa dhiraa moja lakini hurefuka ukubwa wake hadi kufikia ukubwa wa kuwabeba watu tisa katika mazingara ya ajabu ya usihiri. Katikati yake zipo gia namba moja hadi tatu. Usoni ya ungo ipo sukani ifananayo na ya pikipiki.Wanapotaka kusafiri wachawi, baada ya kuvalia nguo zao. Huchukua fimbo na kuzungumza nayo. Papo hapo ungo huo hushika moto katika mazingira ya usihiri na wao huupanda. Hupaa angani hadi wanapohitaji wafike wasihiri.[31]"

Kwa upande mwingine, (Avasttar, 2009:3-6) anashadidia kuwa, fisi ni mnyama anayetumiwa sana na wachawi wa nchi kavu katika usafiri. Usafiri huu hutumika katika maeneo ya nchi kavu tu, hauvuki bahari. Aina hiyo ya usafiri hutumiwa sana na wachawi waliopo katika mikoa ya kanda ya ziwa, Mwanza, Shinyanga na Tabora, pamoja na mikoa

[31]Maelezo yaliyotolewa na Yussufu Diwani, (kituo chake cha matibabu kinaitwa Jamaatul-Kheir). Huyu ni mtaalamu wa falsafa ya usihiri alipokuwa anafafanua dhana nzima ya ungo wa wasihiri. Kipindi kilichoendeshwa kupitia radio*Chuchu 90.9 F.M,* iliopo Mlandege-Zanzibar, katika jengo la Bombei-Bazar, tarehe 10/02/2016

ya Kigoma, Dodoma na Singida. Usafiri wa kasi sana ni wa kutumia fimbo. Kabla ya kuanza safari, msihiri anaomba dua pamoja na manuizi na kukanyanga ncha moja ya fimbo ili aweze kuruka. Roho ya uchawi na majini humuinua juu angani, kama anataka kwenda Nigeria kutoka Dar es Salaam, huoneshwa njia ya kupita yote ilivyo.Ikiwa kuna hatari yoyote huonekana. Inabidi aghairishe safari, kama njia ni nyeupe, hukanyaga incha ya pili ya fimbo. Safari huanza kwa kasi ya sauti akiwa juu ya anga. Kwa sababu safari ni ya kasi sana na upepo ni mkali sana, kiasi kuwa hawezi kufika akiwa hai, majini huchomoa roho yake ndani ya mwili wake na roho humtangulia mbele. Mwili wake huikimbiza roho yake akiwa katika hali ya umauti. Anaweza kutumia sekunde kumi kufika Nigeria, lakini ni usafiri wa hatari kuliko mwingine. Usafiri huu hujulikana kama usafiri wa kujichinja kutokana na kasi yake juu ya anga.

Pia, (Mungo'ong'o, 1977:19-20) anaonesha matumizi ya pembe ya ng'ombe kama ni mojawapo ya chombo cha kusafiria kwa kurukia angani kiusihiri. Anasema kuwa, 'baba yake Gusto aliitumia pembe hiyo kama ndege za Ulaya zinavyoruka angani akiwamo katika kazi ya usihiri.' Ndani ya pembe hili mna dawa ambayo mwenyewe alipoyasemea maneno fulani aliweza kulipanda akapaa nalo angani na kuonesha kuwa ni elimu ya pekee ikitumika vizuri mtu anaweza kuumiliki ulimwengu.Pia, (Label, 2013:3) akifafanua somo la "*electricity and air;"*umeme na hewa kuwa, ni elimu ambayo humuwezesha msihiri kuwa na uwezo wa kupaa angani kwa kujiotesha mbawa mabegani kwa msaada wa jini na shetani. Kuitiisha anga na viumbe walioko angani na uwezo wa kuwasiliana pamoja na kuvidhibiti viumbe vinavyoishi kwenye upepo na kusafiri angani. Kwa jumla, matukio hayo yanaashiria kuwa ni ya usihiri kutokana na kutoaminika kwake.

### 4.3.4 Miktadha ya Uzazi na Mapenzi

Suala la uzazi kwa jamii za Kiafrika lina mitazamo mingi. Wapo wanaolitazama kama suala linalowahusu wanawake na wanaume. Wengine hulitazama kama jambo liwahusulo wanawake peke yao. Mitazamo hiyo miwili huzingatiwa sio ule wakati wa kushiriki tendo la ndoa, bali ni wakati wa kujifungua hadi kupatikana kwa mtoto.Baadhi ya jamii za Kiafrika haziwaruhusu wanaume kuwazalisha wake zao isipokuwa kwa hali ya dharura tu. Kwa upande wa kushiriki tendo la ndoa jamii haina tatizo kuwa, lazima lifanyike kwa watu wa jinsia ya kike na ya kiume wala sio watu wa jinsia moja. Kwa sababu kimaumbile mwanamume na mwanamke wanaposhiriki tendo hilo ndio hutarajiwa kupatikana kizazi. Katika kutafuta uzazi na kujikinga kwa kutopatikana kwake, watu hutumia kinga mbalimbali ili kujizuia na ujauzito. Inapobidi hata kutumia matendo ya usihiri ili mhusika asiweze kupata watoto.

usihiri huelekezwa katika miktadha ya uzazi. Hii ni kutokana na usihiri kutumika kwa kujikinga ili kutopata mimba kwa wakati ambao mzazi na wapenzi wanaoshiriki tendo la ndoa hawako tayari kupata mtoto kwa wakati huo. Iwe kwa mtu aliyeolewa au kwa mwamnamke mwenye tabia ya kujamiiana na watu mbalimbali. Katika kulifanikisha hilo anayejikinga hutumia dawa ya usihiri, inayosaidia kujikinga na ujauzito pamoja na kuwatumia majini. Pia, hutumia hirizi kwa huwekwa kiunoni mwa mhusika ili kufanikisha malengo yake. Kupitia riwaya ya *Kichwamaji,* mtunzi anasema:

> "Aa! Iko wapi?" alipiga kelele. "Nini?" "Hirizi yangu!" … "Mimi siwezi kutunza mtoto wako."(*Kichwamaji*,uk. 15).

Nukuu hii inabainisha kuwa, usihiri huelekezwa katika miktadha ya uzazi ili kujikinga na ujauzito katika jamii. Mtunzi amemsawiri mhusika Pili akiwa amevaa hirizi kama kinga ya kuepukana na ujauzito na watoto asioweza kuwahudumia. Kwa sababu anapotumia hirizi hiyo nguvu ya manii yanayotoka wakati wa kufanya tendola ndoa hudhoofika

nahubadilika kutoka katika asili ya kupata kizazi na kuwa maji yasiyo na athari yoyote ya kubebesha ujauzito. Badala yake, huongeza hamu ya kujamiiana tu. Hali hii hutokea kwa kuwa mchupo wa mbegu hizo hudhibitiwa na jini aliyekabidhiwa kazi ya kuutumikia usihiri husika kupitia hirizi.

(Ghazali, ht:36) anashadidia kuwa, mtu anayejikinga na ujauzito au asiingiliwe na mtu asiyempenda, aandike hirizi kwa kutumia damu ya jogoo mweupe. Ndani yake huandikwa jina la jini aitwaye '*Burhatiyat*'. Mchoro wa kuyafanya maji ya uzazi (manii) yasiwe na nguvu ya kutoka hadi kuufikia mfuko wa uzazi wa mwanamke; yaani, yai linalohitaji kurutubishwa kwa mbegu za kiume.Pia, maji ya uzazi yakiingia hayatokuwa na uwezo wa kumpa ujauzito mwanamke. Aidha, panaweza kufanywa usihiri ili mtu kuganda na asiondoke au usihiri wa kumpiga bila ya kumuona anayempiga. Hutegemea aina ya talasimuna hirizi anayoitaka. Anaweza kuandika ya kuifukia mtaani ambayo humnasa yoyote anayekusudia kufanya uzinifu na wanawake wa mtaani. Au aandike yake na kuivaa kila anapokwenda na wakati anapofanya tendo la ndoa. Talasimu na hirizi hiyo hutumika kama kinga ya mtaa juu ya uasherati au kinga ya kutopata watoto. Maelezo hayo yanaungwa mkono na riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo* kuwa, usihiri hutumika na huelekezwa katika miktadha ya mapenzi. Msihiriwa hupingwa na mtu asiyemuona ili asishiriki ngono-zembe. Usihiri wa aina hii hutumika kuwazuia watu kufanya mambo machafu ndani ya jamii, mtunzi anasema:

> Mji wa Kasala ulikuwa mgumu kufahamika … ukiingia mji huu wakati wa usiku, utapigwa makofi na watu ambao huwaoni. Mapenzi: mapenzi ndiyo yaliyofanya mji wa Kasala ukafahamika baadaye. Mapenzi hayaogopi hatari yoyote. Mapenzi ndiyo yaliyowaleta vijana nyumbani kwa Kasala: Kasala alikuwa na binti wawili wazuri kupindukia. Ingawa mji wa Kasala uliwanasa vijana kama mtego wa buibui. Kasala na mke wakeMungere hawakuwa watu wa ajabu (*Dunia Uwanja wa Fujo,* uk. 3).

Kutokana na nukuu hii utafiti umejuilisha kuwa, usihiri huelekezwa katika miktadha ya mapenzi kwa wanajamii. Kwa sababu ya kufanywa matendo ya ajabuajbu mtaani pa Kasala. Kama vile kupigwa msihiriwa (vijana) na mtu wasiyemuona. Matendo hayo hudhihirisha wazi kuwa ni hali ya usihiri isiyo ya kawaida kutokea kwa wanajamii, lakini huonekana ni ya kawaida kwa wasihiri katika utokeaji wake. Hali hii inathibitisha kwamba, macho peke yake kwa baadhi ya wakati hayathibitishi kutokea kwa usihiri, bali ni wajibu uambatane na vitendo, vitisho, na mabadilikobadiliko ya matukio. Kupigwa kwa vijana katika mji wa Kasala mtunzi anakusudia kueleza kuwa, usihiri hutumika kuwakinga wanawake wa rika zote dhidi ya maradhi ya zinaa.  Pia, wasifanye tendo la ndoa na watu wasioruhusika kujamiana nao. Kwa upande mwingine uzuri wa wasichana wa Kasala ulichangia wazee kutenda usihiri katika miktadha ya uzazi na mapenzi. Hii ni kwa sababu kila mtu aliwapenda wasichana hao. Wakati mwingine hufanyiwa husda ili kudhurika na kupata ugonjwa usiopona kabisa.

(Ghazali, ht:44) anabainisha kuwa, anayehitaji kumkinga mwanamke na watoto wasijishughulishe na tendo la ndoa, kujikinga na adui, pamoja na mwizi aandike talasimu ya Riqai[32] katika karatasi nne. Kisha aziingize katika chombo kisichopitisha maji na kuweka katika sehemu nne za mtaa au nyumba. Hakika kila anayekuja kwa lengo baya hudhurika na kurudi bila ya kufanikiwa au hupotea. Katika karatasi hizo huandikwa aya za Qur-ani zisemazo “viziwi, mabubu, vipofu na wala hawatorejea”, “amewaondoshea Mwenyezi-Mungu nyoyo zao”, “tukajaalia mbele na nyuma yao kizuizi kiwafunikacho wala hawaoni” na “enyi kundi la majini na watu pindi mukitaka kupenya ngome ya mbingu na ardhi penyeni na hamtoweza ”. Mwisho, huambatanishwa na majina ya majini na shetani wazitumikiao wapatao saba miongoni mwao ni Burhatiyat na Umi-Subiani.

[32] Hizi ni talasimu na hirizi zinazoandikwa wakati maalumu wa kuvuka kwa nyota ya Atwaridi na Zuhali. Pia, hukabidhiwa Makhadimu wa nyota hizo wautekeleze usihiri. Huambatanishwa na majini na mashetani, pamoja na manuwizi wakati zinapoandikwa. Kisha hufukiwa ardhini, kutundikwa juu ya miti, juu ya nyumba au kuvaliwa mwilini (Ghazal, ht: 43-45; Twauha, 1988:69-74).

Kwa mujibu wa utafiti uliofanyika, matumizi kama haya ya usihiri ni kwa ajili ya kuondosha madhara ya kimapenzi katika maisha yao watu. Aidha, katika riwaya ya *Rosa Mistika* mtunzi anazungumzia usihiri unavyoelekezwa katika miktadha ya uzazi na mapenzi kwawanajamii hadi kuonekana kuwa ni wa kawaida, mtunzi anasema:

> Ndalo na mkewe walikuwa wakisumbuliwa na jambo moja–uzazi. Walikuwa wamekwishapoteza pesa nyingi sana kutafuta dawa ya uzazi. Mwaka mmoja walikwenda nchi za mbali kuitafuta. Walirudi na nusu debe la mizizi ya miti. Mizizi ilikwisha, na wala hapakuwa na alama yoyote ya Bigeyo kupata mimba. Mwaka uliofuata walikwenda pengine. Huko walimkuta mganga mmoja wa kienyeji aliyewaambia kwamba Bigeyo alikuwa hazai kwasababu alipokuwa bado msichana alikataa kuwabeba wadogo zake mgongoni. Dawa ya uzazi sasa ilikuwa lazima kupata mkojo wa wadogo zake ajimwagilie mgongoni. Waliporudi nyumbani, haukupita muda mrefu mdogo wake akamtembelea… Wakati wa kulala ulipofika alimpelekea mdogo wake kopo. Alimwambia kwamba katika kijiji hicho kulikuwa na wachawi wengi na ilikuwa hatari kutoka nje wakati wa usiku. Alimwambia akojoe ndani ya kopo. Asubuhi na mapema Bigeyo alichukua lile kopo na kwenda kujimwagia mgongoni. Mwaka ulipita. Bigeyo alipokuwa anashiba sasa mumewe alimwuliza kama amepata mimba. Miaka miwili ilipita: hapakuwa na alama yoyote kwamba Bigeyo alichukua mimba. Mwaka uliofuata walijaribu hospitali. Daktari alimwambia wazi kwamba hawatapata mtoto lakini wao hawakuamini. Mwishowe walikata shauri kwenda kaskazini, huko walimkuta mganga mwingine aliyewaambia wale nyama ya kuku mweupe wakikimbia kuzunguka nyumba ili kutakasa mji. Regina aliwakuta wakila nyama hii. Bigeyo alipokuwa akiambiwa kwamba wasichana wengi hutoa mimba siku hizi hakuamini. Alizoea kusema… Regina alipowakuta wanakula nyama wanakimbia alifahamu nia yao. Alisimama kwa muda kuwangoja wamalize matendo yao. Walipomaliza alibisha hodi nyumbani. Bigeyo alimueleza juu ya mganga wao mpya (uk. 17-18).

Maelezo ya Euphrase Kezilahabi yanaonesha kuwa kwa kiwango kikubwa usihiri huelekezwa katika miktadha ya uzazi (kwa watu kutafuta watoto kwa kutumia usihiri). Katika kulifanikisha hilo mhusika Bigeyo alitumia mizizi mbalimbali iliyoambatanishwa na usihiri.Hali hii ilijiri baada ya kupewa masharti mbalimbali na kuyatekeleza. Kama vile kutembea kwa mwendo wa kasi wakati anapokula nyama ya kuku. Kuchukua debe la mkojo wa mdogo wake na kujimwagia mgongoni. Matendo ya usihiri yaliofanywa na mhusika huyo yalikuwa na lengo la kuusafisha mji. Mji wanaoishi Bigeyo na Ndalo wenye tatizo la uzazi,huku wakiambiwa kula nyama ya kuku mwenye rangi maalumu na

kutumia mizizi. Yote hayo yamebainika kwa kutumia nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaelezea matukio ya ajabuajabu kwa namna ya moja kwa moja, iliyozoeleka katika jamii na kuonekana ya kawaida.

(Twauha, ht:83-84) anashadidia kuwa, ikiwa mwanamke ameshatumia dawa na hajabahatika kupata kizazi, huandikwatalasimu na hirizi. Ndani yake huwakilishwa jina la jini aitwaye "*Burhatiyat*" na wengine ambao huzihudumia. Kisha, huandikwa ndani ya sinia au mfano wake kwa kutumia herufi za '*Bitwanati*'; yaani, zilizo katikati ya mchoro wa jina la '*Burhatiyat*' kwa idadi ya mistari tisa. Mstari wa kwanza huandikwa herufi ya '*Alifun*', wa pili herufi ya '*Alifun*' na '*Baaun'*. Wa tatu unakuwa na herufi za '*Alifun'*, '*Baaun*' na '*Jiimun*' hadi kufikia herufi ya '*Thaaun*'. Hurejewarejewa vivyo hivyo hadi kufikiwa mistari tisa. Kisha husomewa Suratu Al-Imrani yote na kufutwa maandishi hayo kwa maji safi au ya mvua pamoja na kuhifadhiwa katika mitulinga ya usihiri kwa ajili ya kupata baraka za majini na mashetani. Hupewa mwanamke huyo anywe, hakika hupata ujauzito. Hivyo, usihiri hutumika katika uzazi ili kupata watoto katika jamii. Nadharia ya Uhalisiajabukupitia msingi wa kuyaeleza matukio ya ajabuajabu yanayojitokeza kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo inafanya yaonekane ya kawaida katika jamii, imesaidia kugundua kuwa,usihiri hutumika katika miktadha ya mapenzikwa malengo mbalimbali katika jamii. Miongoni mwayo ni kupata dawa ya kizazi. Kuwavutia wapenzi na wanaume ili kumpenda mwanamke. Aidha, matukio ya kuzunguka nyumba kwa mhusika Bigeyo na mume wake huku wakiwa wanakula nyama ya kuku kwa ajili ya kuutakasa mji ni matendo ya usihiri. Matukio hayo yanaonekana kuwa ni ya kawaida kutokea katika jamii hadi kuonekana kuwa si ya usihiri.

(Twauha, khj:21) anasisitiza kwa kusema mtu huzuiliwa asipate mtoto wala asizae kwa kuchukua chembechembe za ‘Maimunal-Banzihiri;’zinafanana na haba soda, kiasi ya hamsini au sitini au thalathini. Kisha, huambatanishwa nyayo za msihiriwa na kwato ya paa; sehemu ya chini ya mguu wa mnyama wa jamii ya paa. Huingizwa katika gamba la tunda la ‘Maimunal-Banzihiri’ambalo huzunguushiwa pamba juu yake.Hufanya umbile dogo mfano wa kitu kinachochukuliwa na  mwanamke katika tumbo lake. Yote hayo huhifadhiwa katika mitulinga maalumu kwa muda wa siku saba. Mwanamke huyo hatopatwa na ujauzito. Maelezo hayo yanakiri kuwapo kwa kizuizi cha usihiri kinachotumika kumkinga mtu asipate ujauzito.

## 4.4 Sababu Zichangiazo Kutokea kwa Falsafa ya Usihiri katika Riwaya za Mtunzi Teule

Utafiti umegundua kuwapo kwa sababu kadhaa zichangiazo kutokea kwa falasafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule. Nazo zimejitokeza katika mawanda yafuatayo; shughuli za kisiasa, shughuli za kiuchumi, sababu za tajiriba (mazoea ya jamii) na shughuli za kiutamaduni.

### 4.4.1 Shughuli za Kisiasa

Utafiti umegundua kuwa watu hufanyiwa usihiri kwa sababu ya madaraka waliyonayo au hata baada ya kustaafu katika nyadhifa mbalimbali za uongozi. Mazingira yanayowasukuma kufanya usihiri ni kwa ajili ya kulipa kisasi kwa mambo waliyofanyiwa na viongozi au waliokuwa madarakani. Kutokana na makosa waliyokosana nao. Mtunzi akifafanua juu ya usihiri aliofanyiwa Rosa kutokana na uongozi anasema kuwa, ‘Rosa alichaguliwa na sista John kuwa mkuu wa darasa’ (*Rosa Mistika*, uk. 22). Maelezo hayo yanaunga mkono kuwa, Rosa alikuwa kiongozi na alihusika kutaja majina ya wanafunzi waliokwenda disko, waliochoma mashuka ya Rosa na waliochana mabuku yakehadi

kufukuzwa shule. Hali hii ilichangia kujenga chuki baina yao na kufanyiana usihiri. Mtunzi anasema:

> Rosa hakuwafahamu adui zake. Rosa hakufikiri kwamba kulikuwa na watu wanaomchukia sana… "Mwalimu huyu ninamchukia, sijui kama nini tu!" "Yuko wapi?" Mwanamke mwingine alitoka nje kumchungulia. "Mshenzi huyu ndiye aliyeniharibia maisha yangu! Sijui aliponaje. Angekuwa kaburini sasa" "Alifanya nini?" "Ndiye alifanya tukafukuzwa shule huko Rosary! Alituchongea! Asingalikuwa yeye kutuchongea nisingekuwa nafanya kazi humu ndani ya *bar*" Rosa … alipofika nyumbani aliuliza zaidi juu ya huyo mwanamke aliambiwa na watu waliokuwa wakimfahamu kwamba alikuwa zamani akisoma shule ya wasichana ya Rosary (*Rosa Mistika,* uk. 72-74).

Maelezo haya yanabainisha kuwa uongozi aliokuwa nao Rosa ndio uliosababisha kutokea kwa uhasama huo hadi kufanyiwa usihiri. Hii ni kutokana na Rosa kuwataja wasichana mbele ya mwalimu mkuu. Chuki hizi zilisababishwa na matendo ya wasichana hao walipokwenda kucheza disko. Jambo la kutoka nje ya shule na kwenda muziki lilikuwa kinyume cha maadili ya shule hiyo. Hii ni kutokana na Rosa kulazimishwa kuwataja kutokana na uongozi aliokuwanao darasani. Ili kulipa kisasi cha kufukuzwa shule msichana aliyejitambulisha kama 'Mwalimu wa Nyakabungo' alikwenda kwa Rosa na kumtilia usihiri katika maji. Tukio hilo lilijulikana kwa msaada wa Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaeleza matukio ya kifantasia kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo inayafanya yaonekane ya kawaida katika jamii.

(Ghazali, ht:6) akishadidia juu ya usihiri unaoweza kufanyiwa kiongozi au mtawala anasema kuwa, mtu humfunga mdomo kiongozi, raisi, waziri, shujaa na mfalme mdogo na mkubwa, na kulipa kisasi dhidi yake, huandika talasimu ya "*Latwifu*[33]*"* akiambatanisha na "*Ayatullahi-Latwifu*[34]". Baada ya kuiandika aambatanishe na jini '*Makata'* na '*Khadimu-sihiri.'* Kisha aizike katika mlango au sehemu anayopita msihiriwa, au aiingize katika

[33]Jina la Mwenyezi-Mungu lenye maana ya mpole linaloandikwa kwa utaratibu na mfumo maalumu wa usihiri ili kumlainisha mlengwa.

[34]Aya ya Qur-ani iliyoteremshwa na Mwenyezi-Mungu yenye maana ya upole inayoandikwa kwa njia na mfumo maalumu wa talasimu. Huambatanishwa pamoja na jina lake na kuwekewa msihiriwa kwa lengo la kumlainisha.

maji anayotumia mlengwa. Hakika humtekelezea shida iliyokusudiwa bila tatizo. Pia, talasimu hiyo inaweza kutumika kumuua au kumuingiza maradhi mbalimbali yasiyoweza kutibika. Hutegemeana na manuizi ya msihiri.

Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaeleza mandhari ya kifantasia kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane ya kawaida, imesaidia kugundua kuwa, viongozi wakorofi hufanyiwa usihiri. Mandhari ya kutayarishwa usihiri huo husawiriwa katika kitu kinachofanana na sumu pindi kinapoingizwa katka maji. Huvimba hadi kufanya kichuguu kinachomzuwia msihiriwa kutoka nje ya nyumba. Pia, huandikwa talasimu inayoingizwa katika maji na hubadilika rangi. Hii ni kutokana na manuizi aliyoyafanya msihiri. Talasimu hiyo huambatanishwa na jini ili aifanyie kazi. Mandhari yanayojiri kwa msihiriwa inapofanya kazi talasimu hiyo huingiwa na hofu,hubadilika kitabia kutoka ukali hadi upole au upole kuwa ukorofi na hulainika au huritadi. Hii hufanywa kwa lengo la kulipiza kisasi, kumuua, na kumtia ugonjwa wa milele. Ugonjwa huo hautibiki kwa dawa za hospitali isipokuwa kwa tiba inayolingana na usihiri wenyewe. Pia, utafiti umegundua kuwa usihiri huo huwekwa katika sehemu ya njia panda, katika makazi yake, vinywaji na baadhi ya wakati hutundikwa juu ya miti hutegemeana na malengo ya msihiri, pamoja na maagizo ya mchawi.

### 4.4.2 Shughuli za Kiuchumi

Katika harakati za maisha, jamii hutegemea kilimo katika kukuza uchumi na kuendesha harakati zao za kila siku. Jamii ya Tanzania na Ukerewe hujishughulisha na kilimo cha migomba, minazi na michenza pamoja na kumiliki ardhi kwa ajili ya makazi. Maeneo yote ya ardhi katika visiwa vilivyomo wilayani Ukerewe vinamilikiwa na wakazi wa hapo. Itokeapo mtu mmoja kujishughulisha na harakati za kimakazi, biashara na kiuchumi kwa upande wa kilimo ndani ya eneo la mwingine husababisha migogoro ndani ya jamii

na kufanyiana usihiri. Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaelezea matukio ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane ya kawaida katika jamii, imesaidia kugundua kuwa, mmiliki wa mwanzo wa eneo husika hufanya usihiri kwa lengo la kumuogofya na kumhamisha mtu aliyehamia katika eneo lake. Mtu huyo humpelekea jini na shetani anayejibadili katika umbo la mwanadamu. Au kwenda katika umbo lake halisi. Shetani afikapo katika makazi ya mlengwa (msihiriwa) wakati wa usiku au mchana hurusha mchanga, kupitia madirisha ya nyumba, kubinya miili ya wasihiriwa, kuzitikisa nyumba, sehemu walizolala na kuwapiga mikwaju. Hali hii inadhirika katika jamii na kupitia riwaya ya *Kichwamaji,* mtunzi anasema:

> …Nilifunga safari kwenda nchi za mbali kuwaona waganga. Huko waganga wameniambia wazi kwamba ni kina Masesa na watoto wake. Hawa ndio watu ambao huwa wanakuja hapa usiku. Na sababu yenyewe nimeambiwa kwamba ni mashamba. Unafahamu kwamba sisi tuliletwa hapa na serikali, ingawa kweli tumekaa kwa muda mrefu. Sasa Bwana Masesa anataka tuhame ili achukue tena mashamba yake"(*Kichwamaji,* uk.39).

Nukuu hii inabainisha sababu za kiuchumi zilizomfanya mhusika Masesa na watoto wake kuwafanyia usihiri Kazimoto na wazazi wake. Utafiti umegundua kuwa Masesa aliwafuata wasihiri na kupewa majini na mashetani kuwapelekea wahusika Kazimoto na wazazi wake. Waliohodhi ardhi za wengine (Masesa) kama ilivyotokea katika riwaya ya *Kichawamaji*kwa lengo la kuwaogofya ili warejeshewe ardhi yao. Ardhi ambayo inawasaidia katika harakati za kiuchumi katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Katika muktadha huu usihiri umetumika kwa lengo la kuwahamisha watu katika sehemu lengwa ili kurejeshewa ardhi yao.

(Twan-datai, ht:30) anaunga mkono kuwa anayetaka kumhamisha mtu katika sehemu aliyoikaa kwa nguvu au kwa kuazimwa na hataki kuhama kwa hiyari yake, kwa maneno au mazungumzo matupu, mtu aliyechukuliwa ardhi yake achukuwe karatasi achore picha/micharo za watu wawili.  Ya kwanza, iwe ya anayetakiwa kuhamishwa (ikiwa

mmoja au zaidi wanaweza kupigwa picha). Na ya pili, ni ya muhamishaji. Picha/mchoro wa anayehamisha unaandikwa majina ya majini hawa; '*Abarikhi*' liandikwe mara mbili, '*Yurikhu'* mara moja, '*Anukhu*' mara mbili, '*Surukhu',* '*Barikhu*' mara tatu kila moja na '*Baarukhu*' mara mbili. Kisha achukue mchoro/sura ya anayehamishwa iwe chini. Kwa kuaandikwa mara moja moja mjina ya majini haya; '*Janushi*', '*Abrushi*', '*Arashi*', '*Jawashi*' na '*Haihushi'* majina hayo yote yanaandikwa katika picha ya kila mlengwa. Kisha unawekwa uso wa anayehamishwa chni ya anayehamisha; yaani, uso au picha au sura ya muhamishaji uwe juu wakati zinapoweka, na wa muhamishwaji uwe chini. Zifungwe pamoja katika kitu kisichopitisha maji. Kisha zisomewe talasimu ya kuhamisha mara arubaini na tano. Nayo ni "*Ayahu biqatw-rabili Jalishu*…" na zisomewe mara moja talasimu ya "*Al-Ahadil-Qadimi*". Msomaji wa talasimu hizo huhisi kimojawapo ya kiungo katika mwili wake ni kizito kama daliliya kufanyakazi usihiri huo.

Kisha,picha zifungwe pamoja na talasimu na zifukiwe katika sehemu anayohamishwa mlengwa. Humalizia na manuizi maalumu wakati wa kufukia sehemu hiyo. Kwa mfano, 'ewe mwenye kutumwa ukatumika, nakutuma nikiondoka hapa tu fulani bini fulani mtishe hadi ahame sehemu hii asiwe na hamu nayo milele'. Hakika msihiriwa huanza kutishwa na kuona matukio ya ajabuajabu yanayomfanya kuhama kama alivyosema mtunzi teule.

Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaelezea matukio ya kifantasia kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo inafanya yaonekane ya kawaida katika jamii, imesaidia kugundua kuwa, wasihiri huwachukuwa watu kwa njia za usihiri. Pia, kugeuzwa vizuu, ndondocha na kufanyishwa kazi za kulima mashambani nyakati za usiku bila ya kujitambua. Matendo hayo hufanywa na wenyejina wageni kwa kuwaficha wasihiriwa katika sehemu maalumu kama vile vichakani na mapangoni pamoja na kuwafanyisha kazi. Hali hii hupelekea wenye vizuu kumiliki mashamba na kupata

mavuno mengi kuliko wasiowamiliki. Pia, watu wengine hushawishika kuwapumbaza watu ili nao wafaidike na mambo hayo. Hali hii inathibitika kupitia riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*, (uk. 27-30).

(Safari, 1993:158-160) akiunga mkono kutumikishwa kwa vizuu katika mashamba, anasema kuwa ukulima wa kiserema ni wa kujitafutia mlowa siku tu, basi anayetaka kupata mazao mengi hana budi apate watu wengi wamlimie na watu hao wanataka kulipwa. Kulipwa nako kunapunguza faida. Hivyo, la kufanya ni kuweza kupata watu kwa namna nyingine. Hapa ndipo taaluma ya uchawi kama vile ndondocha, mizuka na misukule hutumika katika kazi za kilimo. Vizuu ni watu bora zaidi maana hawawezi kugoma wala kujali vitu vizuri. Ndiyo maana watu hupotea katika mazingira ya kutatanisha.Katika jitihada za kupata mifugo wachawi hutumia usihiri kuwaiba ng'ombe wa wenzao ili kupata mavuno mengi, wachawi huhitaji huduma ya watu wengi mithili ya watumwa.

Hivyo, hutumia mbinu ya kuwafanya watu waonekane wafu kumbe wazima. Kisha huwatumikisha kulima mashamba na kuyahudumia. Aina hii ya usihiri ni maarufu kote Afrika. Kwa baadhi ya wakati mtu mzima hukamatwa usiku au mchana na kukatwa viungo mbalimbali akiwa yuko hai kama vile albino. Viungo hivyo kama vile macho, mikono na maini huchanganywa na vitu vingine na hutumiwa kama dawa ya mavuno. Aidha, watu huuliwa na kukatwa sehemu za siri kwa kuamini kuwa sehemu hizo zinavutia utajiri wa biashara. Inaaminika baadhi ya viungo vya mwanadamu kama vile maini na moyo vikikatwa kwa mtu yungali hai hutumiwa kumpa ujasiri mchawi na mtu yoyote anayetaka ujasiri na uwezo huo ili kutisha ndani na nje ya jamii zao.

### 4.4.3 Shughuli za Kiutamaduni

Kwa kutumia nadharia ya Uhalisiajabu,kupitia msingi wa kuyaeleza matukio ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja,kwa namna ambayo inafanya yaonekane ya kawaida katika jamii, imesaidia kugundua kuwa, watu hufanyiana usihirikwa sababu ndio utamaduni wao.(Chuachua, 2016:288)anashadidia hoja hii kwa kusema:'Uchawi ni amali ya kitamaduni inayoaminika kuwapo miongoni mwa Wabantu, ijapokuwa hauthaminiwi. Uchawi haupendwi, na wanaoonekana kuwa na tabia hiyo huongopwa na kutengwa na pengine kuuawa. Kani hii inayodhuru; na kwamba wahenga ndio wenye uwezo wa kuidhoofisha isilete madhara yoyote'.

Kwa mfano, watu kupotea kila mwaka bila sababu, kugeuzwa vizuu, kutolewa kikoa[35] msihiriwa na kutunza mila na desturi za mababu, wahenga pamoja na waliotangulia katika jamii husika. Yote hayo husababisha watu kufanya usihiri. Mtunzi anasema:

> Kwa kuwa haikuwa mara ya kwanza watu kupotea katika kijiji hiki, na kwa kuwa wenyeji walifahamu watu ambao hupotea hufanywa nini, jamaa zao walikusanyika na kufanya matanga kama kwamba walikuwa wamekufa. Katika siku hizo tu,watu wawili walikufa ghafla. Watu hawa wawili waliokufa ghafla walikuwa bado vijana, lakini walipofunuliwa kabla ya kuzikwa walikuwa na mvi. Jamaa zao walipoona mvi waliacha kulia. Walifahamu kwamba walikuwa wakizika manyani au mbwa. Walifahamu wazi kwamba vijana hao walichukuliwa na kugeuzwa vuzuu. Mafundi katika kazi hii humchukua mtu yoyote na kumpumbaza bongo zake kwa dawa, halafu humkata ncha ya ulimi asiweze kuzungumza... maji haya, kama ilivyokuja julikana baadaye, yalikusanywa kwa kuchoma nyama za watu. Yalikuwa mafuta ya binadamu (*Dunia Uwanja wa Fujo*, uk. 27-39).

Dondoohii inabainisha kuwa, mandhari ya kupotea kwa watu katika vijiji na vijana waliofariki kuwa na mvi wakati wanapozikwa ni hali ya utekelezajiwa kutoa kikoa cha usihiri. Kinachozunguka kwa kila mwanachama ndani ya kikundi cha wasihiri kila mwaka kama ni utamaduni waliojiwekea. Watu wanaopotea hufanywa mambo matatu. Mosi,

---

[35]Ni tendo la watu (wasihiri) kushirikiana kwa kumfanyia mtu uchawi wa kumpeleka Giningi (*Kamusi la Kiswahili Fasaha*, 2010:167).

huchinjwa na kuliwa nyama huko Giningi ili kudhihirisha utamaduni wao wa kula nyama za watu. Pili, hugeuzwa vizuu ambao hutumikishwa kwa shughuli mbalimbali za usihiri na kilimo. Tatu hugeuzwa watumishi wa Giningi. Kwa upande wa matumizi ya mvi, bundi na mbwa kwa wasihiriwa ni taashira inayoashiria ukubwa na ubaya waliofanyiwa watu na hali ya kudanganywa macho ya jamaa za wasihiriwa. Hii ni kutokana na kuwakatisha tamaa kwani hawatowapata tena.  Maiti wenye mvi wanaoonekana na wanajamii inakuwa sio maiti ya mhusika aliyechukuliwa bali ni taswira za kivuli chake tu. Huwekwa miili ya kubuni inayotokana na vigogo vya mgomba kisha hulinganishwa na mwili wa msihiriwa. Msihiriwa huwako Giningi na hapo nyumbani hubakishwa gogo tu; mwili wa kubuni kwa njia za usihiri.

Mberwa (2015:45) anasisitiza kuwa mambo hayo hufanyika ikiwa msihiri anadaiwa damu katika mzimu wao wa jadi au ni deni la uchawini analodaiwa. Vile vile, uchawini uko utamaduni na utaratibu kwa  wasihiri kuwatoa kikoa watoto wao. Ikiwa mchawi ameshindwa kutoa mtoto pindi ikifika zamu yake, hutolewa kikoa yeye mwenyewe binafsi. Maelezo hayo yanashadidia mauaji ya wasihiriwa kwa njia za usihiri. Katika kutekelezwa hili hazingatiwi msihiriwa amefanya kosa au la bali huchaguliwa kwa mujibu wa mzunguko wa kila mwanachama aliyefikiwa na wakati wa kutoa. Msihiri hutoa watu aliowataja kama wadhaminiwake tangu siku ya kiapo cha kuingia katika usihiri. Akiunga mkono  (Kenyatta, 2004:1-9) anafafanua kuwa wasihiri waliitwa kuwauwa wenzao na kupata asusa au kitoweo na nyama ya kula. Yule anayedaiwa madeni ya kutoa kikoa au kafara anatakiwa kuua mtoto au mtu mwingine wa karibu yake. Kama ikishindikana yeye mwenyewe alijitoa sadaka kwa wachawi aliowakopa. Mzee wa uchawi akifa ghafla huwa ameshindwa kutoa familia yake na huwa amejitoa mwenyewe.

Pia, (Safari, 1993:159) akibainisha sababu za utamaduni zinazochangia kutokea kwa usihiri ni kuwa, wachawi hutumia taaluma hiyo kufanya ufidhuli wa kuwachezea watu usiku kama vile kuwapanda, kuoneshana miujiza, kucheza uchi na kula nyama za watu waliowaua. Aidha, wachawi hutumia taaluma ya usihiri kuwapora watu wake waliowaoa ndani ya jamii. Ikibidi hata kuwaua waume zao kwanza kwa kutumia mazingara ya usihiri. Maelezo hayo yanabainisha kuwapo kwa matumizi ya usihiri ili kutekeleza utamaduni wa wasihiri. Kwa mujibu wa utafitiuliofanywa umebaini matendo yote hayo hutumia usihiri kwa walengwa kama ni miongoni mwa utamaduni waliojiwekea.

Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaelezea matukio ya kifantasia kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo inafanya yaonekane ya kawaida katika jamii, imesaidia kugundua kuwa, msihiriwa hupelekewa jini ambaye humfuata kwa nyuma yake. (Muhando, 1989:40) anasisitiza kuwa wasihiriwa kufuatwa kwa nyuma wakati wanaposihiriwa au wanapotibiwa na wasihiri. Anasema: "vaeni hirizi upesi". Tutawafuata nyumanyuma. Kila wakiimba nasi tutaimba". Maelezo hayo yanathibitisha kuwa msihiri na jini humfuata msihiriwa. jini akifika katika nyumba ya msihiriwa hupasua pembe za nyumba na kuingia. Wakati huo wasihiri huzunguka nyumba ya msihiriwa, wakisubiri kupewa ishara kutoka kwa jini wa usihiri ili waingie katika nyumba. Mara itolewapo ishara huingia na kumchukua msihiriwa. Katika hali hiyo ndiyo watu hupotea katika mazingira ya kutatanisha. Msihiri aliye karibu na msihiriwa kiukoo ndiye huongoza katika kumtoa nje na husaidiwa na wasihiri wengine. Hupaishwa juu ya anga kwa msaada wa majini na mashetani hadi Giningi. Hapo huweka kikao na kuamua jinsi ya kufanywa msihiriwa. Wamo wanaofanywa watumishi wa Giningi, wanaochinjwa na nyama zao kutengenezewa mafuta na wengine hutengenezwa unga wa ndere kwa matumizi ya Giningi. Hali hii imezoeleka katika jamii ya Watanzania kwa kuchukuliwa watu kwa njia za usihiri na kupotea katika njia za kutatanisha. Pia, wasihiriwa hulishwa vitu vya usihiri

wakiwa usingizini, pamoja na kupotea wasijulikane walikokwenda. Mtunzi anaunga mkono suala la kulishwa usingizini kwa kusema:

> Ugonjwa huu inasemekana huletwa na dawa za kienyeji. Kwa kifupi watu walisema kwamba Muyango 'alilishwa.' … "Wale wanaofahamu wamekwisha nisikia mara nyingi nikinung'unika kwamba kumtunza mzee nyumbani ni mzigo mkubwa. Ni vigumu sana kwake kuachana na mizimu yake ya kale. Ndiyo maana watu wanapoambiwa na wanasiasa wahame kwa sababu kisiwa kimezidi, wakazi wanasema- "Babu alizikwa hapa, baba alizikwa hapa; siwezi kuacha makaburi ya babu zangu." Nilipomwambia mama yangu aache kazi hii alijibu kwamba ilikuwa kazi ya ukoo wetu na kwamba ilikuwa ni wajibu wetu kujifunnza kazi hii ili tuiendeleze baada ya kifo chake (*Dunia Uwanja wa Fujo*,uk. 14-30).

Nukuu hii inathibitisha kuwa matendo ya usihiri yanayofanywa na wasihiri ni miongoni mwa utamaduni wao katika jamii ya Watanzania. Pia, kujifurahisha ambapo hurithishana kizazi hadi kizazi kwa kuhofia kupotea mila walizoachiwa na mababu zao. Aidha, pamebainika kuwa, matendo ya kurithishana mizimu ya wazee na wahenga waliofariki, kupotea kwa wasihiriwa katika njia ya kutatanisha watu kugeuzwa vizuu yamefahamika kuwa ni ya kawaida katika jamii na kutoshughulishwa na utokeaji wake.

### 4.4.4 Sababuza Kitajiriba

Mitazamo ya kitajiriba ya wanajamii katika suala la kupata kizazi ina nyanja nyingi. Wapo wanaoona kuwa wajibu wa kila mwanandoa ni kupata kizazi, kama ni tajiriba zao na mazoea ya wanajamii. Wengine hudhani mwanamke tu ndiye mwenye matatizo ya kutobeba ujauzito. Bali wengine huona wote wawili wana haki ya kupata watoto na haifai matatizo hayo kuelekezwa kwa mhusika mmoja tu kati yao. Ili kuyaondoa matatizo hayo, jamii hufanya matendo ya usihiri kwa sababu watu wanahitaji kupata watoto.Watoto ambao huwasaidia pindi wakiwa wazee katika maisha yao ya kila siku. Aidha, watu hufanya usihiriili kujiepusha na mashambulizi ya maneno ya jamaa wa karibu wa mume (mawifi) kutokana na kutozaa kwao. Hii ni kutokana na kuzoeleka kitajiriba kuwa kila aliyeolewa ni lazima kuzaa na itokeapo kinyume chake jamii huanza kumsimbulia.

Kimbilio lake ni kufanya matendo ya usihiri ili kuwatafuta watoto. Mtu humfuata mchawi kwa kumtaka kumfanyia dawa ya kupata watoto, Mganga hutazamia kwa kupiga ramli na hutegemea aina ya ramli inayomuongoza katika kulipatia ufumbuzi suala hilo. Msihiri hutoa dawa inayoambatana na jini, kwa kuweka baadhi ya masharti anayopewamgonjwa ili kufanikiwa matakwa yake. Matendo hayo yamejulikana kwa kutumia nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa uelezeaji wa matukio ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, iliyozoeleka katika jamii na kuonekana ya kawaida. Katika kubainisha matendo hayo mtunzi anasema:

> … Regina… Alipoukaribia mji wa Ndalo alishangaa kuona matendo yaliyokuwa yakitendeka pale nyumbani. Ndalo pamoja na Bigeyo walikuwa wanakula nyama ya kuku hali wanakimbia kuzunguka nyumba. Ndalo na mkewe walikuwa wakisumbuliwa na jambo moja–uzazi. Walikuwa wamekwishapoteza pesa nyingi sana kutafuta dawa ya uzazi. Mwaka mmoja walikwenda nchi za mbali kuitafuta. Walirudi na nusu debe la mizizi ya miti … Dawa ya uzazi sasa ilikuwa lazima kupata mkojo wa wadogo zake ajimwagilie mgongoni… Wakati wa kulala ulipofika alimpelekea mdogo wake kopo. Alimwambia kwamba katika kijiji hicho kulikuwa na wachawi wengi na ilikuwa hatari kutoka nje wakati wa usiku. Alimwambia akojoe ndani ya kopo (*Rosa Mistika*,uk. 17).

Nukuu hii inabainisha kuwa, watu katika jamii hujitahidi kutafuta dawa ya uzazi ijapokuwa ya usihiri ili kuepukana na maneno ya jamaa wa karibu wa mume au hata majirani. Pia, waganga wa kienyeji wanapotoa dawa zao huambatanisha na masharti kwa kutegemeana na matakwa ya ramli, majini na mashetani. Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaelezea matukio ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo inafanya yaonekane ya kawaida katika jamii, imesaidia kugundua kuwa, Ndalo na Bigeyo katika tendo la kula nyama ya kuku huku wanazunguka mji ni ishara, dalili na sababu za kitajiriba katika kutekeleza usihiri ili kupata kizazi. Ulaji na matendo wanayoyatenda wahusika hao yanaashiria kuwa wanatekekeza maagizo ya waganga wa kienyeji, kuutimiza usihiri na kuondosha mikosi inayokwaza upatikanaji wa ujauzito. Matendo mengine ya kitajriba yaliyobainika ni kujitibu baada ya kuelekezwa na mafundi

wa usihiri. Mara nyingi mgonjwa ndiye mtekelezaji mkuu wa matendo hayo. Akithibitisha sababu za kitajriba Haji (2016) amefafanua kuwa 'fundi wa usihiri ndiye anayetenda matendo ya usihiri kwanza wakati mgonjwa akiwa nyumbani kwake ili kumfahamisha kimatendo mgonjwa ili kupata watoto. Pia, kutekeleza matakwa ya wanajamii na tajiriba zao.' Huahidiwa kuwa matatizo yote yanayomkabili yameshatatuliwa kwani wameshakabidhiwa wa kuyaondosha; majini na mashetani. Damu ya kuku hutumika kama muhanga wa kuwapa mashetani na majini ili waondoshe shida inayomkabili mgonjwa.

Nyama ya kuku iliyoliwa na Bigeyo, pamoja na Ndalo ilitumika kama kafara na dawa ya kuondoshea matatizo ya mgonjwa. Alipochinjwa kuku alikatwa kichwa mara moja tena kwa ghafla. Wasihiri wengine humkata kuku kwa kutumia mdomo na meno huku wakiifyonza damu yake hadi imalizike. Kisha, huachiwa kuku apapatike juu ya ardhi. Msihiri huzingatia upande anakoelekea kuku kuwa inaaminika ndiko aliko adui; ikiwa anatafutiwa dawa mgonjwa au anatafutwa adui. Lakini katika suala la tajiriba za wanajamii katika kupata ujauzito upande wa kusini na kaskazini huaminika kupatikana mtoto wa kiume. Mashariki na magharibi huaminika kupatikana mtoto wa kike; kuku akielekea huko baada ya kukata roho. "Pande nne za dunia zinaathari kubwa katika suala la kupata kizazi anapochinjwa kuku na kuelekea upande wa ureejua na uchwejua; yaani mashariki na magharibi inaaminika kupatikana mtoto wa kike, kwa upande wa kaskazini na kusini huaminika kupata mtoto wa kiume[36]." Utafiti umegundua kuwa wahusika Bigeyo na Ndalowalipewa masharti ya kutumia dawa, kati ya hayo ni kumchunguza kuku alipokata roho alielekea upande upi? Na wao pia waelekeekuko huko wakati wanapoanza kula nyama ya kuku. Pia, kupata mkojo wa mdogo wake kwa sharti kuwa wakati anapojimwagia aelekee upande alioelekea kuku baada ya kufariki.

---

[36] Mahojiano baina ya Mtafiti na BwHassan Kh. Ali anayeishi Maungani-Zanzibar; huyu ni mtaalamu wa falsafa ya usihiri,tarehe 13/01/2016.

Nadharia ya Uhalisiajabu katika kudhihirishamsingi wa kuyaelezea matukio ya usihiri kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo huelezewa na huonekana ya kawaida katika jamii, imesaidia kugundua kuwa, matendo ya kuzunguka nyumbahuku Bigeyo na mume wake wanakula nyama ya kukumwenye sifa maalumu ni dalili za usihiri. Hii ni kutokana na maagizo ya majini aghalabu huchagua rangi nyeupe, nyekundu na nyeusi. Pia, kufuata maagizo ya msihiri wakati alipochinjwa. Kupikwa katika chungu maalumu. Damu ya kuku wa aina hiyo hukauka ghafla kwa kuwa hunywewa na jini na shetani. Baadhi ya wakati hata alama yake haionekani. Utafiti umegundua kuwa wakati anapochinjwa kuku wa aina hii hufuatanishwa na maneno ya usihiri ndipo achinjwe. Kwa mfano, wanajamii husema "enyi wakuu tunakupeni muhanga huu ili mwanetu apate ujauzito *shelila, shelila, shelila*"; yaani, nyinyi mnao uwezo kama wa Mwenyezi-Mungu katika kufanikisha hili mbarikini mtoto wetu kizazi. (Bakize, 2014:33) anasisitiza kuwa fantasia nyingi katika kazi za fasihi huwa na motifu wa safari au msako wa utafutaji au ufumbuzi wa kitu fulani. Mambo hayo hayawezi na hayatarajiwi kutokea isipokuwa hutumiwa kwa makusudi ili kukidhi haja fulani za kifasihi. Kwa mnasaba wa tasnifu hii matendo yote yaliyofanywa na Bigeyo ni ishara ya utendekaji wa usihiri ndani ya jamii.

## 4.5 Athari za Matumizi ya Falsafa ya Usihiri katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi kwa Jamii

Utafiti umebaini kuwapo kwa athari chanya na hasi za matumizi ya falsafa ya usihiri kwa wasomaji wa riwaya teule. Ingawaje athari chanya ni kidogo ikilinganishwa na hasi.

### 4.5.1 Athari Chanya

Utafiti umebaini kuwa, matumizi ya falsafa ya usihiri yana faida zifuatayo:-

#### 4.5.1.1 Kuimarisha Mapenzi

Kwa asili mwanadamu ni kiumbe mwenye uwezo wa kufanya mambo mengi katika ulimwengu wa kihalisi na wa kidhahania; giningi. Mambo hayo anayoyatenda yapo yanayotekelezeka ndani ya uwezo wake na mengine hana uwezo wa kuyatekeleza. Kila jamii ina utamaduni wake unaoambatana na masuala ya maadili, ndoa, desturi, na kanuni za kuiendesha. Kama ni hivyo basi, katika jamii watu hutokea kuoana na kupendana kwa lengo la kuishi pamoja, kusaidiana na kuendeleza kizazi. Lakini hufika wakati wakaanza kuhitilafiana, kuchukiana na kila mmoja huwa na bughudha, chuki na uhasama miongoni mwao. Wataanza kusuluhishwa na kusuluhishana pamoja na kupeana nasaha ili kuiondoa hali ya uhasama na ugomvi iliopo. Inapoendelea kwa mmoja wao kushikilia na kuendeleza ugomvi na uhasama, fani ya usihiri na matumizi yake hutumika ili kuondosha hitilafu baina yao na hata ndani ya jamii. (Twauha, 1988:15-25) anasisitiza kuwa ‘kwa kutumia usihiri mapenzi huzidi maradufu kwa wapendanao katika jamii.’Hali hiyo imebainika kutokana na nadharia ya Uhalisiajabu inayoongozwa na msingi wa kuyaeleza matukio ya kifantasia kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo inafanya yaonekane ya kawaida katika jamii. Kupitia matumizi ya usihiri hasa katika riwaya za mtunzi teule mtu huweza kuiga kufanya usihiri kwa lengo la kumtuliza mwingine kimapenzi ili waishi kwa amani. Hali hii inayoweza kuigwa imejitokeza kwa mhusika Vera kumfanyia usihiri Dennis na waliishi kwa upendo mkubwa katika riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* (uk. 111).

Kwa vile msomaji ndiye mhusika mkuu wa kuyatambua hayo (Wamitila, 2008:28) anafafanua kuwa, usomaji ni msingi muhuimu wa uchambuzi wa kazi za fasihi. Kila msomaji ana njia zake za kuzisoma kazi za kifasihi kupitia maneno yanayopatikana katika matini hayo. Matini ya kifasihi huwa hayana maana hadi pale yanapohusishwa na msomaji anayehusisha na tajiriba zake. Pamoja na welewa au kaida azijuazo na ambazo

hudhibiti usomaji wake. Matini za kifasihi huwa hazijakamilika hadi zinapokamilishwa na wasomaji inawezekana kupiga hatua ya kifalsafa hata kudai kuwa nje ya usomaji hamna matini ya kifasihi. Uzowefu aliokuwanao msomaji unaathiri kwa kiasi kikubwa jinsi inavyoikabili kazi ya kifasihi. Usomaji unaweza kuipambanua maana kutokana na matini ya kifasihi.

Kwa mnasaba huo baada ya wasomaji na wanajamii kuzisoma kazi za mtunzi teule hupata kujua njia za mmojawapo kati ya Vera na Dennis (au mume, mke na mwingine yoyote) kutumia usihiri. Mfanyaji humfuata msihiri na kupewa dawa ili kumvutia mmoja wao kimapenzi na kuondosha uhasama, kuimarisha mashirikiano na umoja miongoni mwao. Aidha, wasomaji wamepata kujua namna ya kujikinga na kuzilinda ndoa zao. Msihiri hupendwa katika hali ya ajabu na ya kupita kiwango. Hutokea hali ya kukaa pamoja kunakotawaliwa na utulivu, upendo na umoja kati yao kwa kurogwa na kuingiziwa dawa katika chakula na kinywaji, mtunzi anasema:

> Barua mbili zilitaja dawa ya kuweka ndani ya chai ili kumfanya Dennis ampende sana Vera. Mbili zingine zilieleza dawa ya kuweka ndani ya chakula ili kumpumbaza D. akili asiwe na wivu (*Dunia Uwanja wa Fujo,* uk. 111).

Kupitia maelezo hayo msomaji hufaidika kufahamu dawa ya usihiri inayotumika kuimarisha mashirikiano katika nyanja zote kinyume na hapo mwanzo alipokuwa hajazisoma kazi za mtunzi teule. Yeye pia (msomji) huwatafuta watu na wasihiri wamfanyie dawa hiyo ili kuimarisha mapenzi kati yake na watu wengine. Hali hiyo huondoa migogoro iliyopo kwa wawili hao, katika jamii na kukuza mahusiano yaliyokuwa yakilegalega baina yao. Katika hali halisi ya mazingira ya makazi na mitaani, kwa kutumia usihiri wasihiriwa na msihiri hukuza udugu na mashirikiano zaidi na hata mazungumzo yao hutawaliwa na upendo. Utafiti umegundua kuwa utaratibu huu huendelea kwa muda mrefu hadi dawa ya usihiri aliyofanyiwa msihiriwaichakae na

imalizike muda wa kutumika kwake, ndiyo msihiriwa azindukane na aachane na mapenzi na mahusiano ya ajabuajabu kupita kiwango. Kupitia matumizi ya usihiri hasa katika riwaya za mtunzi teule mambo yote yasiyowezekana kufanywa na binadamu huwezekana kwa ufanisi na ustadi mkubwa. Matukio ya kutia dawa katika chakula na chai ili kumpumbaza Dennis kiakili hadi kutokwa na wivu huwezekana.Kwa hivyo msomaji pamoja na jamii hufaidika nayo kwa kujifunza hatua moja baada ya nyingine kiutekelezaji.

#### 4.5.1.2 Ufahari na Ulinzi

Wakati jamii ya Watanzania ikipambana na kukabiliana kwa kuyaondosha matendo ya usihiri, wahusika wengine wanayaendeleza na kuyachochea. Kiasi ambacho husababisha kushika kasi kwa lengo la kujifaharisha na kujilinda dhidi ya watu wengine. Usihiri hujidhihirisha katika jamii kama chombo cha kujifaharishia mbele ya watu. (Kenyatta, 2004:06) anasisitiza kuwa usihiri hutumika kujifaharisha kwa wazee mbele ya vijana ili kuwakataza juu ya mambo wasiyoyahitaji wazee. Kwa kusema “wewe mtoto unajivuna eti sijui kama utamaliza mwezi huu.” Hii inamaana kuwa wazee waliweza kufanya mauaji kwa kutumia usihiri kwa mtoto yoyote mwenye kudadisi siri za usihiri kupitia matendo wanayoyatenda wazee. Pia, kujifaharisha kuwa hakuna mwingine mwenye uwezo zaidi ya wao. Hali kama hiyo ya wazee ya kujifaharisha kwa kutumia usihiri huweza kumuathiri msomaji kwa kuona usihiri ni kitu kinachofaa kwa kuwakatazia watoto anaowazaa ili wasifanye jambo fulani.Pia, yeye mwenyewe hujifaharisha mbele ya wazee wenzake kwa mafanikio aliyoyapata kutokana na usihiri. (Twauha, 1972:45)anasema kuwa ni ufahari ulioje kwa mtu kuwa na nguvu za ziada zimuwezeshazo kutiiwa na waja, majini na mshetani. Ili kuyapata hayo mhusika akae riaydha; ni hali ya kujitenga na watu katika sehemu maalumu ili kuzungumza na viumbe wasioonekana. Katika kikao hichomsihiri afunge kwa ajili ya Mwenyezi-Mungu kwa muda wa siku saba kuanzia Jumapili. Kisha

afukizesehemu anayokaa kwa uvumba na udi kila siku. Aambatanishe na manuwizi ya kuwaita majini pamoja nakukaa mbali na chumvi.Pia, aandike jina la ishirini na mbili (jini aitwaye Burhatiyat) katika sahani.Kisha afute kwa maji na kuyanywa hadi zitimie siku saba.Baada hapo anakuwa na uwezo wa kujifaharihia na kuwatumia majini na mashetani apendavyo. Maelezo hao yanaweka bayana kuwa usihiri ni chombo cha kujifaharishia. Aidha, mhusika fulanianakuwa ni mwenye uwezo na nguvu katika kupambana na wengine kwa kutumia usihiri.

Pia, usihiri hutumika kwa kujifaharisha kwa jamii hiyo mbele ya wengine kwa matendo ya usihiri. Katika kulizungumzia jambo hilo, mtunzi amemsawiri mhusika "mzee mwingine" *Gamba la nyoka,* (uk. 30) kutoka katika kijiji cha Kisole,alipounganisha mazungunzo ya kujifaharisha kwa wanakijiji hao juu ya ushujaa wao wa kuwapiga askari waliopelekwa kuwahamishia katika vijiji vya ujamaa. Wanakijiji hao walikuwa wakiotamoto msituni walikojificha. Huku wakisifiana na kufaharishana kwa kila aina ya mambo waliyoyatenda. Ndipo mzee huyo alipojifaharisha mbele ya wenzake. Fahari hiyo iliyafafanua matendoya watu waliopita kabla yao. Huku akieleza wazi kuwa,laiti wangalikuwapo watu hao au wanaofanana na wao,askari wa serikali wasingaliwatambia. Hii ni kwa sababu wote wangaliuliwa kwa kutumia usihiri. Mtunzi anasema:

> Mimi nilisafiri sana kwenye maji yatembeayo. Katika safari hizo nilipata kusikia juu ya watu shujaa wa zamani. Huko pwani nilipata kusikia juu ya Fumo Liyongo, mtu mkubwa mwenye nguvu na aliyeogopwa sana vitani. Huko usukumani kulikuwa na mtu aliyeitwa Ngw'anamalundi. Kila kitu alichokinyooshea kidole kilikauka palepale. Na huku Ukerewe kulikuwa na mtu anaitwa Msomi. Huyo aliweza kusomgonyoa vichwa vya watu kama ndege na kuvitupa pembeni vizimavizima. Hao ndio walikuwa watu. Tungekuwa na watu wawili kama hao leo, hivi vijitu vya serikali visingekuwa vinatusumbua na magongo yao. Watu walicheka… nitakueleza kisa kimoja kilichotupata. Tulikuta mzee mmoja wa kike amekaa ndani ya nyumba anakula. Alipotuona hakuonyesha alama yoyote ya kushtuka. Aliendelea kula kama kwamba hatukuwapo. Tumekuja kukuhamisha! Tulimwambia kwa ukali. Mzee aliendelea kula bila kujali. Mkubwa wa kikundi chetualitoa amri ya kubeba vituvyote. Sote tulitii amri. Lakini lo! Vitu vilikuwa havibebeki. Kitanda

> hakikutingishika mtungi wa maji ulikuwa hausukumiki. Sote tulipigwa na butwaa. Mzee alicheka kwa sauti ya juu sana kama mtu aliyepagawa, na kisha akasema, “Haya bebeni! bebeni basi ninyi watoto wa serikali! Bebeni!” Tulikuwa bado hatujakata shauri nini la kufanya mara tukaona fimbo hewani zikizungushwa kutupiga. Tulipigwa sana, lakini hatukuona mikono, wala watu waliozizungusha. Tulikimbia. Tulipoingia garini zikatoweka hewani kama upinde wa mvua. Huo ni woga walionao watu wengi wanaohusisha uzee na uchawi(*Gamba la nyoka*, uk. 30-41).

Nukuu hii inathibitisha kuwa usihiri hutumika kama nyenzo ya kujifaharisha na kujilinda iwe mtu mmojamoja au jamii nzima. Ufahari unajidhihirisha pale wazee wa kijiji cha Kisole walipokuwa wakiota moto na kuelezeana uhodari wa mhusika Fumo Liyongo, Ngw’anamalundi na Msomi juu ya uwezo wao wa kishujaana wanastahiki pongezi kwa matendo ya usihiri. Hii ilijiri kwa kuwaua watu hovyo hovyo.Kutumia usihiri kwa kuvinyooshea kidole vitu na Msomi kuvisongonyoa vichwa vya watu kuwa ni vitendo vinavyostahiki. Kutokana na hali hiyo wahusika hao wangalikuwapo katika kijiji cha Kisole usihiri ungalipatikana na kufanikisha mapambano kwa vyovyote iwavyo. Pia, watendaji wa serikali wasingalikuwa na uwezo wa kuwahamisha watu. Kwa sababu wangalikuwa wanazo nguvu za ziada za usihiri dhidi ya askari wa serikali,(Uzorma, 2012:54) alijifaharisha kuwa “nilifanikiwa kupata pesa nyingi kupitia usihiri.” Aidha, (Safari, 1993:156)anasisitiza kuwa usihiri hutumika kujifaharishia kama alivyofanya Osale Otango kwa kuchana kuta za jengo la rumande mbele ya mkuu wa Gereza la Maweni huko Tanga, kwa kusema “Kwa heri tutaonana Osale Otango” na hakupatikana tena. Kauli hii inamaana kuwa ikiwa nyinyi askari mnao uwezo wa kufanya usihiri kama mimi ili kunikamata fanyeni munirejeshe gerezani, bali hamna uwezo huo.

Kwa upande mwingine, mzee wa kike aliyefuatwa na askari kwa ajili ya kuhamishiwakatika vijiji vya ujamaa, aliutumia usihiri kwa namna mbili. Kwanza, alijifaharisha kuwa yeye ni mwenye nguvu nyingi kuliko askari. Hali hiyo ilijiri alipoambiwa na askari “Tumekuja kukuhamisha.” Kwa vile anafahari ya kuwa watu

waliomwambia vile hawana uwezo huo, aliendelea na ulaji wake huku akiwamrisha majini na mashetani wawaadhibu askari kwa bakora. Kisha,kuwacheka na baadaye kuwaambia “Haya bebeni! bebeni basi ninyi watoto wa serikali! Bebeni!” Kauli hii inamaana kuwa ikiwa nyinyi ni mahodari zaidi kwa kupambana na nguvu za usihiri fanyeni mapambano nazo. Na ninahakika kuwa hamnazo nguvu za kunishinda mimi na usihiri ninaoutumia. Basi mnaweza kuvibeba vitu hivyo, lakini hamtaweza. Pili mhusika Kizee aliutumia usihiri kwa kujikinga ili asihamishwe katika kijiji alichokizoea na alifanikiwa kufanya hivyo. Hali hii humuathiri msomaji kumuiga mzee huyo kwa kujikinga dhidi ya wengine.

(Safari, khj:60) anashadidia kuwa ‘taaluma ya usihiri inaweza kutumika kwa kuleta maendeleo na hata katika ulinzi’.Hii ni kwa sababu ya uwezo walionao wasihiri wa kuingia katika sehemu bila ya kuonekana. Pia, kuvizuia vitu visichukuliwe kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa kutumia mazingara ya usihiri. Kwa jumla, jamii za Kiafrika huutumia usihiri kujifaharisha mbele ya wengine kuwa wao wanao uwezo mkubwa zaidi, pamoja na kujilinda ili wasipatwe na madhara ya aina yoyote.

### 4.5.2 Athari Hasi

#### 4.5.2.1 Kuingiza Maradhi Mwilini

Katika jamii wapo watu wanaoamini kwamba waganga, wasihiri na wapigaji ramli ni watu wenye sehemu kubwa katika ufanikishaji wa tiba kwa maradhi mbalimbali. Hali inayowafanya watu kila wapatwapo na shida kukimbilia kwa wasihiri na waganga wa tiba asili. Lakini kwa upande mwingine watu huwaendea wasihiri kwa ajili ya kutengenezewa usihiri ili kuwadhuru na kuingiza maradhi katika miili ya wengine. (Ali 2014:20) anashadidia kuwa ‘Waarabu wameiita sihiri kuwa ni sihiri; kwa sababu huondoa uzima hadi kwenye maradhi.’ Pia, (Twauha, 1988:202) anasisitiza kuwa mkia wa kondoo

husawiriwa kwa usihiri na kufukiwa makaburini, kila unapooza na mwili wa msihiriwa nao huoza na kutoka fuuza ingawa yuko hai. Maelezo hayo yanathibitisha kuwa mwili wa msihiriwa huathirika kwa usihiri. Kwa vile mtunzi ametaja baadhi ya njia na hatua za kufanya na kuwafanyia usihiri wenziwao, wasomaji na wanajamii huweza kuzijua hadi kuwafanyia wengine. Kwa mfano, mtu fulani amegombana na mwingine ikiwa mtu huyo amezisoma kazi za mtunzi teule na kuona jinsi gani mhusika Muyango alivyolishwa usihiri, huiga na huamua kwenda kwa msihiri ili amfanyie usihiri unaofanana na ule uliomo ndani ya riwaya teule, hadi mtu huyo kupata maradhi. Utafiti umegundua kuwa usihiri hutumika kwa kuingiza maradhi ndani ya miili ya wasihiriwa kwa malengo mbalimbali yaliyolengwa na msihiri.Mtunzi anasema:

> Tumaini alipokuwa darasa la kumi na mbili mama yake aliugua na kuvimba. Madaktari walikuwa hawawezi kuuponya ugonjwa huu hata kwa kisu chao cha uchawi; kwani baada ya kupasua tumbo mgonjwa hupungukiwa sana na damu; hufa ganzi upande mmoja na hazungumzi tena mpaka kufa. Ugonjwa huu inasemekana huletwa na dawa za kienyeji. Kwa kifupi watu walisema kwamba Muyango 'alilishwa.' Kwa hiyo Muyango alipougua ugonjwa huu alifahamu kwamba alilogwa na kwamba kifo chake kilikuwa kimekaribia. Alikata shauri kufia nyumbani bila kumwona daktari (*Dunia Uwanja wa Fujo*,uk. 14).

Maelezo hayo yanaweka wazi kuwa, mtu anayesihiriwa huweza kulishwa dawa za usihiri ili kufariki dunia. Hali hii huweza kuigwa na wasomaji pamoja na wanajamii kwa kuwalisha watu vyakula mbalimbali vilivyochanganywa na usihiri ndani ya jamii inayowazunguka pindi wakitokea kugombana. Akifafanua athari zichangiwazo na usihiri, Ali (2016) ameeleza kuwa 'wasihiri huwaroga watu ili wasipone. Marogo ambayo humfanya msihiriwa kuwa mgonjwa pamoja na kupata maumivu makali yasiyo ya kawaida yanayomkatisha tamaa ya kuishi'. Kuvimba tumbo kwa Muyango kumesababishwa na mambo makubwa matatu. Kwanza, alilishwa dawa za usihiri

zilizotengenezwa kwa kutumia utumbo wa guruguru[37] na kuambatanishwa na jini.Utumbo huo ulikaushwa baada ya kuchunwa mnyama huyo na kuingiziwa katika chakula na kinywaji. Pili, unga wa utumbo wa bunju[38] uliokaushwa au kukaangwa. Tatu, mmea uitwao mjomvu[39] huchukuliwa unga au magamba yake pamoja na mmea uitwao utupa; mti wenye sumu kali yenye uwezo wa kuua viumbe wenye mifupa. Mambo yote hayo huchanganywa pamoja na akilishwa msihiriwa, tumbo lake huanza kuvuja damu ndani kwa ndani, kufa ganzi kwa baadhi ya viungo. Hatimaye, kuvimba tumbo hali hiyo huendelea hadi kufariki kwa msihiriwa. Matukio hayo ya kufantasia yamethibitika kutokana na Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaelezea kwake na kuonekana ya kawaida katika jamii katika kutokea kwake.

(Ali, 2014:93-106) akifafanua maradhi yanayoingizwa kwa watu kufanya usihiri kwa wengine anasema kuwa, Mara nyingi mwanamume na mwanamke huugua kwa sababu ya usihiri.Usihiri hubadilika kinyume akawa msihiriwa anaumwa bila ya kupoa na anamchukia kila mtu. Hili hutokana na wachawi wengi kutofahamu misingi ya usihiri. Mara nyingine mke humfanyia mumewe usihiri-mchanganyiko ili awachukie wanawake wote na ampende yeye pekee. Basi ikasababisha mume kuugua na kumchukia mama yake na wanawake wote miongoni mwa jamaa zake. Wakati mwingine, usihiri-mchanganyiko hugeuka, mume akawachukia wanawake wote hata mkewe. Maumivu ya daima katika kiungo chochote kile, mshtuko wa misuli, kiungo chochote kupooza, kupooza mwili mzima, mojawapo katika hisi kutofanya kazi na mwanamke kutokwa na damu isiyokatika. Maelezo hayo yanabainisha athari za usihiri kwa wasomaji wariwaya za mtunzi teule.

---

[37]Ni mnyama muoga anayefanana na kenge anayeishi mashambani na sehemu zenye jangwa (*Kamusi la Kiswahili Fasaha*, 2010:105).
[38] Ni jamii ya samaki mwenye sumu kali inayoua= totovu (*Kamusi la KiswahiliFasaha*, 2010:35).
[39] Ni mmea ambao hutambaa juu ya miti mikuwa mfano wa gorowezi ambao hutobolewa na wadudu ukiwa uko hai. Wadudu huubovua na kutoa unga lakini haufi kwa kitendo hicho. Unga unaotoka kwenye mti huu hutumika kuwasihiri watu na hasa viungo vya miili yao kutofanya kazi, kufa ganzi pamoja na kuoza kiungo kimoja kimoja huku msihiriwa akiwa yuko hai.

Huathiriwa kwa kuiga hatua kwa hatua wanavyotenda wahusika waliomo ndani ya bunilizi teule.

Kwa mfano, mtu anaweza kushawishika kujifuza njia za kumsihiri mtu. Pia, kujifunza fani ya mazingaombwe na kuyatumia mara baada ya kusoma jinsi gani makundi ya Funga Bilima na Golita yalivyokuwa yakifanya mazingaombwe kupitia riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo,* (uk. 52). Kwa upande mwingine, matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya teule yamechangia kuiendeleza jamii kuwa na imani potofu juu ya magojwa ya aina mbalimbali kuwa hutibika bila ya kwenda hospitali. Kuamini usihiri na ushirikina kuwa ndiyo wenye nguvu. Hatimaye, husababisha kutoshiriki katika harakati za kujitafutia maendeleo kwa kuogopa kurogwa. Kwa mfano, mhusika Tumaini alipokimbia kijijini baada ya kurogwa na kuukuta mlango wake uko juu ya paa na wazazi wake kugeuzwa vizuu. Matumizi ya aina hiyo ya usihiri huwaathiri wasomaji na wanajamii kisaikolojia kwa kuona kuwa kazi kubwa ya usihiri ni kuwaangamiza watu. Jamii pia kuweza kuutumia kama walivyousoma katika bunilizi teule. Kwa hivyo, matukio haya husababishwa na matumizi mabaya ya falsafa ya usihiri kupitia riwaya za mtunzi teule kwa wanajamii.

#### 4.5.2.2 Kujenga Maadili Mabaya

Mpoomoko wa maadili huweza kurithiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine iwapo wazazi wameathiriwa na matendo pamoja na maadili mabaya ya usihiri.Pia, vijana kusoma maandishi, majarida na bunilizi mbalimbali zenye kuzungumzia na kufunza maadili hayo. Aidha, usihiri nao kama yalivyo maandiko mbalimbali na wazazi hujenga na kurithisha zaidi matendo na maadili mabaya kwa vijana. (Ali, 2014:20) anasisitiza kuwa “usihiri hujenga maadili mabaya kwa kukidhihirisha kitu katika maonesho yake mazuri ili kuvifitinisha viumbe, kuvinyima haki zao na kukirithisha kizazi amali inayopendwa na

majini na mashetani ya kuwatoa wanadamu wengine muhanga wa Giningi." Hali hiyo husababisha kurithishana na kujenga maadili mabaya miongoni mwao. Utafiti umegundua kuwa, wanajamii hurithi tabia mbaya na matendo ya usihiri kwa kusoma, kuiga na kuyafanyia mazoezi kupitia wahusika wanavyotenda matendo hayo katika riwaya teule. Kufanikiwa kwa wasihiri husababisha wengine wafanye matendo kama hayo ili nao wafanikiwe kama wenziwao.

(Uzorma, 2012:23) anashadidia kuwa "wasihiri walidhamiria kuyaondosha maisha yake kwa namna yoyote kwa sababu ya kufichua matendo na tabia mbaya ya kazi ya usihiri waliokuwa wakiifanya." Kwa hivyo, hali hiyo ilirithiwa kutoka kwa waliyowatangulia vijana hao. Katika hali halisi kwa mfano, wanaowageuza watu wawe wapumbavu na vizuu kwa lengo la kuwalimisha katika mashamba hadi kutajirika, huwachochea wengine kufanya hivyo. Wasomaji na wanajamii huzisoma riwaya za mtunzi na kuathirika nazo kwa kupata njia, mbinu na namna ya kufanya hadi kuwa wajuzi katika usihiri. Wanaposhindwa juu ya kulifahamu jambo husika kutokana na kutofafanuliwa vema katika riwaya, huanza kuuliza kwa wajuzi wa usihiri.

(Sharifu, ht:3) anasisitiza kuwa "watu waliwakimbilia wajuzi wa usihirina kuwauliza kwa shida zao zote. Pale wanapopatwa na ugumu wa mambo, ama kwa kuvisoma vitabuwasivifahamu au kwa kutokea matukio ya usihiri katika maisha yao. Wajuzi wa mambo hayo (ya usihiri) huwafafanulia hatua kwa hatua hadi nao (waulizaji) wanakuwa wataalamu." Akifafanua aliyojifunza kupiga ramli kwa kuwauliza wajuzi baada ya kupata ugumu wa kutoifahamu ramli katika maandishi aliyoyasoma Hamadi (2016) anasema: "Tumekuwa tukikimbilia kwa wajuzi wa usihiri kwa kuwauliza na kutupatia ufumbuzi wa mambo, pale inapotokezea kuyakuta katika maandishi na hayakuwekwa kwa uwazi. Wasihiri hutufahamisha na kutufundisha kwa uwazi bila ya kuficha hadi tumekuwa wajuzi

wa mambo mengi ya usihiri.Kwa sharti kwamba muulizaji ajiunge na uwanachama wa usihiri tu." Hatimaye na wao kuwa wajuzi. Yote hayo hujiri kutokana chanzo cha kusoma riwaya teulekisha kujifunza kwa wajuzi wa matendo hayo.Kwa mfano, mtunzi anasema:

> "Wananchi! Wakati sisi tunapojitahidi kuondoa hali ya kinyama katika nchi yetu, wakati tunapojaribu kuinua hali ya maisha yetu kwa kufanya kazi bila kuhimizwa, kuna watu wengine ambao wanatenda mambo ya kusikitisha. Wanachukua wanadamu wenzao na kuwapumbaza akili. Badala ya kutumia nguvu zao wanatumia nguvu za wengine katika kulima mashamba yao bila shaka mnafahamu kwamba katika kijiji chetu si mara ya kwanza jambo kama hili kutokea. Kuna mtu mmoja ambaye leo lazima tumtaje. Kati yetu kuna watu wanaomfahamu lakini wanaogopa kusema wasije wao wenyewe wakachukuliwa. Kijiji chetu kimeugua. Ugonjwa haufichwi. Afichae ugonjwa ndiye hufa (*Dunia Uwanja wa Fujo,* uk. 29).

Maelezo hayo yaliyotolewa na mhusika Mwanangwa yanabainisha kuwa, watu hugeuzwa vizuu kwa ajili ya kulima. Wasihiri wanaofanya hivyo huweza kutajirika. Hali hiyo hupelekea wanaozisoma riwaya kushawishika, kuathirika na kuiga ili nao wafaidike. Wasomaji wakiona kuwa, wananchi wanachukuliwa na wanadamu wenzao kisha hupumbazwa akili hujuiliza akili hizi hupumbazwa vipi? Na mtu gani mwenye uwezo wa kumfahamisha njia za kufanya ili naye awe na uwezo kama huo. Kwa hatua ya mwanzo huwafuata wasihiri na waganga wa kienyeji kwa kuwa wao wanazo mbinu za kujua na kufanya mambo mbalimbali ya siri. Kama vile kujigeuza kutoka sura moja hadi nyingine, kuagua chanzo cha ugonjwa, kifo na matatizo yanayoikabili jamii. Hapo wasomaji hupata ufafanuzikutoka kwa wasihiri na waganga hao kuwa, wapitie hatua tatu ili naowaumiliki uwezo kama huo. Kwanza, kujiunga na uwanachama wa wasihiri (giningi) kwa kufuata taratibu na kanuni zao.

Hapa ndipo anapoanza kupewa taratibu za kufanya pamoja na miiko ya usihiri wenyewe. Kama vile kutokuwa na huruma anapotekeleza majukumu ya giningi. Pili, kula kiapo cha kutunza siri pamoja na kuweka wadhamini wa kuweza kumkomboa ikiwa ameshindwa kutoa kafara ya uwanachama ya kila mwaka. Watu hao anaowaweka rehani ndio

huchukuliwa na kuuliwa kama ni tiketi ya kuendelea na uwanachama wake. Tatu, kufundishwa njia na taratibu za kufanya usihiri wa aina mbalimbali kama vile kuruka na kujigeuza sura na kuwa huru kufanya atakacho. Yote hayo hujiri kutokana na wasomaji kushawishika kujifunza usihiri kutokana na kuzisoma riwaya za mtunzi teule pale alipoona kuwa watu wanao uwezo wa kuwatumikisha wengine katika kilimo. Baada ya hapo anakuwa na uwezo wa kuwageuza watu vizuu na kuwatumikisha katika harakati mbalimbali za kilimo.

Akielezea athari za matumizi ya falsafa ya usihiri (Awadhi, 2016) anasema: 'zimetoa mchango wa kujenga maadili mabaya katika jamii. Kwa kuambukiza tabia mbaya kama walizonazo wahusika waliotumika katika bunilizi teule'. Mtafiti aliegemea kuifafanua jawabu hiyo kwa yale maudhui na ujumbe unaopatikana kwa msomaji na wanajamii kupitia riwaya za mtunzi teule, wasihiri na waganga. Ingawa kila msomaji, mhakiki na mwanajamii ana haki ya kuihakiki kazi anayoisoma kwa mujibu wa ufahamu wake,mandhari husika na jamii lengwa. Lakini bado wanakabiliwa na tatizo la kuzielewa kazi za fasihi na matumizi ya falsafa ya usihiri. (Sengo, 1993:104) anasisitiza kuwa kazi za fasihi zina athari nyingi kwa jamii. Hivyo, msomaji hupata na huelewa athari mbaya au nzuri katika kazi anazozipitia kwa kudhihirika matendo ya jamii, itikadi, imani, falsafa na mielekeo yao. Mawazo hayo yanaweka bayana kuwapo kwa athari za kazi za mtunzi baada ya kusomwa na wanajamii. Akitoa mfano wa athari hasi kwa matumizi ya falsafa ya usihiri (Juma, 2016) anasema: 'Jambo lolote linaweza kuiathiri jamii kwa namna ya uzuri au ubaya. Matumizi mabaya ya falsafa ya usihiri huwafanya wasomaji kuiga ubaya huo kwa watu wenye tabia mbaya. Lakini matumizi yakiwa mazuri huchochea tabia nzuri na kuiendeleza tabia hiyo kwa wanajamii.' Akiendelea kufafanuaathari hizo kuwa ni chimbuko na chanzo cha kujenga uhasama, husda na roho mbaya katika jamii na wasomaji wa riwaya teule. Utafiti umegundua kuwa maelezo ya watafitiwa juu ya

matumizi ya usihiri na wasihiri ni chanzo cha migogoro, mpoomoko wa maadili na mapenzi katika jamii.

### 4.5.2.3 Kuleta Ugomvi Ndani ya Jamii

Utafiti umegundua kuwa, usihiri unapofanywa kufanyiwa mtu mwingine huwa ndio chanzo cha kuleta ugomvi na uadui ndani ya jamii[40]. Hali hii huletwa na wanajamii kwa kutaka kulipiza kisasi kwa matendo wanayofanyiwa na wasihiri. Ama kwa kuwatupia maneno yanayosababisha mabishano na ugomvi au kwa kutaka kuwaua wasihiri. Hali hii kwa vile imo ndani ya maandiko ya riwaya za mtunzi, wasomaji nao huathirika kwa kuiga jinsi gani mtunzi alivyoandika kutokana na kosa kama hilo likitokea katika jamii, mtunzi anasema:

> Kasala aliyafahamuje mambo haya yote aliyoyasema kama yeye hashirikiani na mama yake katika kazi hii?" aliomba mji mzima wa Kasala uhamishwe. Baada ya kubishana kwa muda mrefu, Kasala na binti zake walihurumiwa, lakini majirani waliombwa kuwakazia macho. Watu walikuwa wameanza kutawanyika mwanamke mmoja alipokwenda karibu na Mugala. "Nilipokuangalia niliona kwamba uko mtu mzuri kama kwamba unajipaka sandalaiti!" "Woo!" watoto waliokuwapo walianza kuzomea. Mwanamke aliendelea kumchamba. "Mama alizaliwa na malaika nini!" "Woo! watoto waliendelea kumzomea. Lakini unapika nyama ya mbwa!" "Toboa! Watoto waliendelea. "Umepata mapengo kwa sababu ya kula nyama ya mbwa!" "Woo!" (uk. 31).

Nukuu hii inabainisha kuwa usihiri huleta ugomvi na malumbano katika jamii. Mtunzi amemsawiri mhusika Mugala na familia yake kuingia katika mgogoro na malumbano kwa sababu ya usihiri anaoutenda. Aliwafundisha wajukuu zake hadi kufichua siri za usihiri waziendeshazo. Watu wote walikuwa na hadhari kubwa juu ya kushirikiana nao katika maisha. Hatimaye, mhusika Mugala kuhamishiwa katika kisiwa cha wachawi. Watu waliofanyiwa usihiri au jamaa zao huwa hawana njia ya mkato ya kulipiza kisasi hicho ila

---

[40]Inapogundulika kuwa fulani ndiye anayehusika na uchawi uliosababisha kifo, hulaumiwa ijapokuwa si kwa wazi wakati mwingine mwanga husakamwa waziwazi na hata kuuawa. Pengine hali hii huwa ndiyo mwanzo wa uhasama, baina ya pande mbili za ndugu wa aliyetuhumiwa na wale wa marehemu (Chuachua, 2015:283).

kuwafuata wasihiri ana kwa ana ili wawashambuliye kama alivyofanya mwanamke. Yeye alikuwa akimtolea maneno mhusika Mugala kama ni msihiri mkuu kabisa, huku watoto wakimzomea kwa matendo yake machafu. Malumbano hayo huwafanya wasomaji na wanajamii kuyaiga hatua kwa hatua. Au hata kuongezeka athari ya ukubwa wa utekelezaji kwa waliozisoma riwaya teule, pindi yanapotokea ndani ya jamii wanayoishi kwa kuyakuza zaidi. Akishadidia athari hasi za matumizi ya falsafa ya usihiri, Masudi(2016) anasema: "Tumeshuhudia watu kupigana, kuhasimiana na kukata uhusiano wa ukoo kutokana na matendo ya usihiri yanayofanywa na mmoja wa wasihiri ndani ya familia." Kiasi ambacho walio wengi hushindwa kuvumilia na kuleta migogoro ndani ya jamii. Kwa hali hiyo, wasomaji wakishaona hatua zilizochukuliwa na mtunzi kupitia wahusika ndani ya riwaya teule, nao huzifuata njia walizotumia katika utatuzi wa matatizo yaletwayo na usihiri.Pia, malumbano yanayofanana ndani ya riwaya. Aidha, utafiti umeonesha jambo jingine ambalo ni kero kuwa watu kuwasogelea wasihiri na kuwashambulia kwa maneno kama alivyofanya mwanamke huku watoto wakimzomea. Jambo hili huigwa na wanajamii na kuwa ni chanzo cha uhasama unaosababishwa na usihiri.

(Kenyatta, 2004:5) anashadidia kuwa, mtoto au mwanajumuiya ama mwanaukoo anapoumwa hata kama ni homa ya kawaida lazima mwenzao walimuhisi kuwa ni mchawi ndiye aliyesababisha. Matokeo yake huleta ugomvi mkubwa na amani hutoweka. Lakini kwa upande mwingine huweza kuadhiriwa mbele ya jamii kama vile kutengwa na kuzomewa na jamii nzima kwa kutokuwa na imani naye. Maelezo haya yanawiana na ya mtunzi teule kwa kutaja athari za ugomvi ziletwazo na usihiri kwa wanajamii. Kwa upande mwingine utafiti umegundua kuwa, kila jambo baya litokealo katika jamii husingiziwa msihiri ameshalifanya kwa kuwatuma majini wake. Mathalan, kufariki kwa watoto na vijana ambao vifo vyao vimetokana na Mungu. Matokeo hayo yote kwa kiasi

kikubwa huigwa kutokana na maaandiko ya mtunzi, kwa kuwa ameyaelekezea na kufanywa kupitia wahusika wake.Kwa jumla, matumizi ya falsafa ya usihiri yameonekana kuwa ni sehemu muhimu ya kuendeleza kazi za mtunzi, huku wasomaji akiathirika nazo. Hii ni kutokana na ukweli kuwa mambo mengine hayawezekani kufafanuliwa kwa kutumia Uhalisia, bali hueleweka zaidi kwa kutumia Uhalisiajabu.

### 4.6 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii imejadili mchakato wa uchambuzi wa mjadala wa data na jinsi zilivyofafanuliwa na kutafsiriwa kupitia riwaya za mtunzi teule. Nazo ni rwaya ya *Rosa Mistika*, *Dunia Uwanja wa Fujo* na *Kichwamaji*. Nadharia ya Uhalisiajabu kupitia msingi wa kuyaeleza matukio ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna ambayo inafanya yaonekane ya kawaida katika jamii, ilitumika katika kujadili na kuchambua matumizi ya falsafa ya usihiri kupitia matendo ya ajabuajabu na maneno ya wahusika ndani ya riwaya teule. Huku ikizingatiwa na mandhari iliyosawiriwa kwa mtindo wa kifantasia.Pia, maana, ujumbe na wahusika wa ajabuajabu walivyojitokeza.  Aidha, mdhihiriko wa falsafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule  umejitokeza kwa namna mbalimbali. Wakati aina zausihiri zilizojitokeza ni; usihiri wa mapenzi, wa kufarakanisha, wa sauti,usihiri wa hirizi na usihiri wa mazingaombwe. Aidha, utafiti umegundua kuwa usihiri huelekezwa katika miktadha ya kifo, makazi, matibabu na usafiri, pamoja na uzazi na mapenzi. Kwa upande wa sababu zichangiazo kutokea kwa falsafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule ni; shughuli za kisiasa, kiuchumi, kiutamaduni na kitajiriba au mazoea. Hatimaye, tasnifu ilihitimishwa kwa kujadili athari za matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule na umebaini kuwapo kwa athari chanya na hasi. Kwa upande wa chaya ni; kuimarisha mapenzina ufahari na ulinzi katika jamii. Kwa upande wa hasi ni kuingiza maradhi na kukosekana kwa nguvumali, kujenga maadili mabaya na kuwa tegemezi katika jamii. Pia, kuleta ugomvi ndani ya jamii. Sehemu inayofuatia imezungumzia hitimisho la tasnifu, maoni pamoja na mapendekezo juu ya tasnifu zijazo.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea muhtasari wa tasnifu, hitimisho, mapendekezo,mchango mpya wa tasnifu hii, maoni yaliyopatikana kutokana na tasnifu, utoshelevu wa nadharia ya utafiti na kuhitimishwa kwa kutoa mapendekezo ya tasnifu zijazo.

### 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Tasnifu hii ilichunguza matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi. Riwaya zilizotafitiwahadi kukamilika kwa utafiti huu ni tatu. Nazi ni*Dunia Uwanja wa Fujo* (2007); *Kichwamaji* (1974) pamoja na *Rosa Mistika* (1971). Tasnifu iliongozwa na vipengele vinne  vya maswali ya utafiti. Tasnifuilianza kuchunguza aina za usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi, miktadha  ambayo usihiri huelekezwa katika riwaya za mtunzi teule, sababu zichangiazo kutokea kwa falsafa ya usihiri katika riwaya teule, na kuhitimishwa kwa kutathmini athari za matumizi ya falsafa ya usihiri kwa wasomaji wa riwaya teule. Aidha, tasnifu iligawika katika sura tano ambapo kila sura imeelezewa kwa muhtasari kama ifuatavyo:

Sura ya kwanza imeanza kwa kutoa ufafanuzi wa istilahi muhimu zilizotumika katika utafiti huu. Istilahi zenyewe ni falsafana falsafa ya Kiafrika. Nyingine niusihiri, uchawi, ushirikina na Uhalisiajabu. Zote hizo zilifafanuliwa kwa ufupi ili kumsaidia msomaji kupata mwelekeo wa ufahamu wa utafiti huu. Pia, umeelezwa usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, manufaa ya utafiti na kuhitimishwa kwa historoa ya mtunzi teule.

Sura ya pili imeanza kwa kuzungumzia kiunzi cha nadharia ya utafiti na mapitio ya maandiko mbalimbali yahusuyo tasnifu hii. Maandiko hayo ndiyo yaliyosaidia

kubainishamapengo ya utafiti huu. Maandiko mbalimbali kama vile majarida makala na tafiti tangulizi yalisaidia kuyachunguza matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za mtunzi teule. Maandiko hayo yamegawanywa katika sehemu kuu nne. Kwanza, maandiko kuhusu falsafa na fasihi kwa ujumla. Pili, maandiko kuhusu usihiri na mazingaombwe ndani ya kazi za fasihi. Tatu, maandiko kuhusu usihiri nje ya kazi za fasihi. Na maandiko kuhusu riwaya za mtunzi teule.

Sura ya tatu imeelezea methodolojia ya utafiti iliyotumika. Na vipengele vilivyojumuishwa katika kuikamilisha sura hii ni; mpango wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti, jamii ya watafitiwa, sampuli iliyotumika, jinsi data zilivyokusanywa, pamoja na vifaa mbalimbali vilivyotumika katika utafiti. Nadharia ya Uhalisiajabu ndiyo iliyotumika katika uchambuzi wa data za utafiti kwa kuzingatia msingi wake mmoja tu wa kuyachunguza na kuyaelezea matukio ya kifantasia au ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane ya kawaida katika jamii. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonesha kuwa matukio ya aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika. Nadharia hii ilihusika kuyachunguza matukio, mandhari pamoja na wahusika wa ajabuajabu katika utendaji wao, taswira iliyojitokeza, mienendo na tabia za wahusika katika ufanikishaji wa aina mbalimbali za usihiri. Kwa jumla, sura hii imejumuisha methodolojia ya utafiti pamoja na vikwazo vilivyojitokeza katika tasnifu hii na utatuzi wake.

Sura ya nne imeanza kuelezea mdhihiriko wa falsafa ya usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi. Aidha,  historia ya usihiri kwa jumla, vijenzi vyake kama vile jini, shetani, nyota ramli, mapango, na mitishamba. Kisha, imeelezea muhtasari wa riwaya za mtunzi teule. Riwaya zilizotolewa muhtasari ni pamoja na *Dunia Uwanja wa Fujo*, *Kichamaji* na *Rosa Mistika*. Kisha kujadiliwa kwa kina mdhihiriko wa aina za usihiri,  miktadha ambayo

usihiri huelekezwa, sababu zichangiazo kutokea kwa usihiri na athari za matumizi ya falsafa ya usihiri kwa jamii.Pia, sura imeonesha kwa uwazi data zilivyowasilishwa na kutafsiriwa kulingana na malengo na maswali ya utafiti ambayo yaligawika katika sehemu nne. Msingi wa nadharia ya Uhalisiajabu ulitumika kuchunguza, kuchambua na kujadili mdhihiriko wa usihiri unaofanywa na wahusika kupitia riwaya teule kwa kuzingatia mandhari, matukio, maneno na matendo yalivyojitokeza. Kwa jumla, uchambuzi wa data ulitumia nadharia ya Uhalisiajabu kupitia vigezo vitatu vya msingi vilizingatiwa; mandhari, matukio na wahusika wa ajabuajabu walivyosawiriwa katika utokeaji wa usihiri kwa namna mbalimbali.

Sura ya tano imehitimisha kwa kuelezea muhtasari wa tasnifu, utoshelevu wa nadharia ya uchambuzi wa data za utafiti, matokeo ya utafiti, mchango mpya uliobainika katika utafiti huu pamoja na mapendekezo kwa tafiti zijazo.

## 5.3 Hitimisho

Sehemu hii inaelezea utoshelevu wa nadharia, mchango mpya uliopatikana kutokana na utafiti, maoni ya mtafiti juu ya utafiti uliofanyika na mapendekezo kwa tafiti zijazo.

### 5.3.1 Utoshelevu wa Nadharia Iliyotumika

Katika kuukamilisha utafiti huu, nadharia iliyotumika ni ya Uhalisiajabu kwa kukusanya data, kuchambua na kuendeshea mjadala wa utafiti. Uchambuzi wa data ulitumia msingi wa nadharia hii. Ambao umejikita katika kuyaeleza matukio ya kifantasia au ya kiajabu au ya kichawi kwa namna ya moja kwa moja, kwa namna inayofanya yaonekane ya kawaida. Sababu hasa ya matumizi ya mtindo huu ni kuonyesha kuwa matukio ya aina hii hupatikana katika maisha ya kawaida katika jamii zinazohusika.

Msingi huu ulibeba mambo makuu matatu ambayo ni: matukio ya ajabuajabu, mandhari inayosawiriwa katika hali isiyo ya kawaida na wahusika wa ajabuajabu. Pia, msingi uliangalia wahusika wanaopatikana katika riwaya za mtunzi teule njisi walivyobebeshwa matukio ya usihiri, mandhari waliyosawiriwa nayo katika kuufanikisha na matendo wanayoyatenda yanayoashiria na kutoa taswira ya usihiri katika maisha yao ya kila siku. Msingi wa nadharia ulisaidia kuchunguza na kutathmini jinsi maisha ya wanadamu na matendo yao yanavyolandana na mazingira yanayomzunguka kwa kukabiliana nayo kwa kutumia falsafa ya usihiri katika bunilizi za kifasihi. Aidha, msingi umesaidia kugundua matumizi ya falsafa ya usihiri na kuwa ni mojawapo ya ufundi na mbinu ya kisanaa iliyotumika katika utunzi wa riwaya mnamo miaka ya sabini na thamanini katika karne ya ishirini. Hii ni kutokana na maelezo na sentensi zilizomo katika bunilizi kutumia ishara na matukio yasiyo ya kawaida kufanywa na wahusika ili kuonesha hisia na mawazo ya mtunzi juu ya utekelezaji wa usihiri ndani ya jamii au hata mambo yaliyomtokezea katika maisha yake kwa kushuhudia au kusikia yakihadithiwa. Hivyo, nadharia ya Uhalisiajabu ilikuwa mwafaka kutumika katika kuuchunguza na kuutafiti usihiri uliotumiwa na mwandishi wa riwaya teule na kubaini mazingira, matukio, mandhari, taswira, ujumbe na maana zinazopatikana kupitia wahusika na katika jamii.

### 5.3.2 Mchango Mpya Uliopatikana Kutokana na Utafiti

Utafiti umeibua michango mipya kama hii ifuatayo. Mosi,kupata njia mpya za ubunifu na mitazamo bora zaidi ya kuzitafiti na kuzishughulikia kazi za mtunzi teule; yaani, kwa kutumia nadharia ya Uhalisiajabu ikilinganishwa na hapo mwanzo watafiti wengi walizihakiki kazi hizi kwa kutumia nadharia ya uhalisia na udhanaishi. Hii ni kutokana na usihiri na ndoto kuhakikiwa katika mtazamo huo (wa udhanaishi). (Wamitila, 2002:117-127) anasisitiza kuwa:

> Katika siku za hivi karibuni pamezuka aina ya uhalisia ambao unahusisha maajabu… Aina hii mpya inajulikana kama Uhalisiajabu… kazi ambazo zinaweza kuelezwa kama za kihalisiajabu huchanganya sifa za kihalisia na kiajabu au maajabu… uelewaji wa sifa hizo ni muhimu kwa kuwa unamuwezesha msomaji na mtafiti kuzielewa sifa fulani zinazohusiana na kazi anazozisoma… suala muhimu kwa msomaji na mtafiti ni kujaribu kuelewa misingi ya kazi inayohusika kutokana na vijenzi vya kazi yenyewe… Msingi huu unaweza kuathiri sio tu jinsi mwandishi fulani anavyoishughulikia dhamira yake bali pia jinsi anavyovitumia vipengele vingine kama vile msuko, mandhari, uhusika na itikadi.

Kwa hivyo, ni vema kwa watafiti kuutumia msingi wa Uhalisiajabu ili kazi za mtunzi hayo zieleweke katika jamii.

Pili, wasomaji na wanajamii wamepata kuelewa aina za usihiri, njia zinazotumiwa na wasihiri kuingiza maradhi kwa wasihiriwa pamoja na kuyatatua matatizo yanayotokana na usihiri ndani ya jamii, pamoja na mwelekeo mpya wa kuuangalia usihiri.

Kwa hivyo, ni vema kwa wasomaji kuzisoma kazi zinazohusiana na falsafa ya usihiri kisha kulinganisha faida zipatikanazo katika fani ya usihiri na zile zilizomo katika sayansi na teknolojia ili kupata maendeleo ya kweli katika jamii. Mwisho, jamii itiliye mkazo katika kuisoma elimu ya sayansi na teknolojia ili kuelimika zaidi na kuweza kutofautisha usihiri na sayansi, kisha kuchagua ni upande gani wenye manufaa ili kuuendeleza katika jamii kinyume na hapo mwanzo.

### 5.3.3 Maoni ya Mtafiti juu ya Utafiti Uliofanyika

Kwa jumla, kukamilika kwa utafiti huu kumechangia matokeoyake kubaini kuwa,mwamko wa ufahamu wa falsafa ya usihiri na matumizi yake kwa wasomaji wa riwaya za mtunzi teule,ni wa kiwangokisichoridhisha. Hali hii imechangiwana mambo mengi; miongoni mwa hayo ni wasomaji wa kazi za mtunziteule kutozielewa aina za usihiri alizozizungumzia mtunzi na matumizi yake. Kuziita aina hizo zote kuwa ni mazingaombwe, bila ya kubagua kuwa hayo ni aina mojawapo tu ya usihiri.

Pia,kutofahamika lengola matumizi ya falsafa ya usihiri kwa wasomaji. Kwa hivyo, matumizi ya falsafa ya usihiri yasilenge kutatua haja tu ziwakabilizo Waafrika bali, yawe mithali ya mfumo wa maisha ya jamii katika ulimwengu wa nchi zinazoendelea na za Marekani ya Kusini. Pia, usihiri utumike kudumisha na kuendeleza falsafa ya Kiafrika, mila na desturi pamoja na kuiendeleza fasihi ya Kiswahili katika mtindo wa kiajabuajabu. Ipo haja kwa falsafa ya usihiri kutumiwa katika nyanjaza siasa, uchumi, na utamaduni. Ili kuimarisha utamaduni wa Mwafrika, kupata dawa mbalimbali kwa maradhi yanayowasibu wanajamii na wasomaji. Hii ni kutokana na baadhi ya wakati dawa za hospitali kushindwa kutibu ugonjwa wa usihiri kwa wanajamii. Hivyo, jamii iwe makini katika kuitumia falsafa ya usihiri pale penye faida nyingi kuliko hasara, na penye hasara zaidi isitumike.Mwisho, serikali kuweka motisha maalumu kwa wanaoendeleza fani ya usihiri, ili kuwasaidia wanajamii katika kutatua matatizo yanayowakabili. Aidha, kuweka kitengo maalumu cha wataalamu wa fani yenyewe ili kuharakisha maendeleo na ujuzi wa fani husika.

### 5.4 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Tasnifu hiiimekuwa chachu kwa wengine kufanya tafiti zinazolingana na kipengele kimojawapo cha falsafa ya usihiri, ima katika jamii au katika maandiko mbalimbali ya watunzi wa fasihi ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu utafiti huu uligusia kipengele cha matumizi ya falsafa ya usihiri kwa upande wa riwaya za mtunzi teule na kutogusia tanzu za tamthiliya,hadithi fupi na ushairi. Hivyo, utafiti umeacha mapengo kadhaa yanayohitaji kutafitiwa na watafiti wengine wajao. Mtafiti anapendekeza tafiti nyingine zifanyike katika maeneo yafuatayo:-

a) Kuchunguza matumizi ya wahusika majinina mashetani katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Hii ni kutokana na kuchukua mawanda mapana katika ufanikishaji na

utokeaji wa falsafa ya usihiri kwa jamii. Aidha, majini na mashetani wanaaminika kuwa ni viumbe wanahusika kwa kiasi kikubwa katika matendo na matukio ya usihiri kwa kushirikiana na msihiri. Kwa mfano, mtafiti anaweza kuchunguza nafasi ya majini na mashetani katika riwaya za Eupharase Kezilahabi katika kuukamilisha usihiri.

b) Kuchunguza nafasi, aina na dhima ya usihiri katika shughuli za tiba na ndoa katika kazi za waandishi wengine kwa upande wa kipengele cha ushairi na tamthiliya. Licha ya kuwa utafiti huu umegusia aina za usihiri, hata hivyoipo haja ya kutafitiwa aina moja moja za usihiri katika hali ya kujitegemea. Hii ni kutokana na kutochunguzwa kwa undani aina hizo. Ili kuondosha tatizo hilo ni vema kutafitiwa kimoja baada ya kingine.

c) Kulinganisha na kulinganua juu ya matumizi ya falsafa ya usihiri baina ya mtunzi teule na mwingine yoyote au katika jamii.

## MAREJELEO


Abdahu, S. S. A. (2011), *Usuli-Sihiri*, Daru-Ibni-Jauzii, Kairo.

Ahmad, N. S.(2008), *Muujamu Al-waswitwi*, Muasisi wa Tarehe ya Kiarabu, Beyrouth-Liban.

Alexander, M. (1990), "*Flights from Realism",* Edward Anold, London.

Al-Jibrini, A. A. (2009), "*Tahadhibi-Tas'hilil-Akidatil-Islamiya"*, Chuo Kikuu cha Saudia, Riyadhi.

Ali, U. M. (2014), *Upanga Mkali wa Kupambana na wachawi Waovu*, Maktabatul-Qaswa, Dar es Salam.

Al-Arabii, S.M. (ht), *Majmuuatu-Saatul-Khabari*, Maktabatu Ishaatul-Islamu, New-Delhi.

Al-Falakii, M. Z. (ht), *Faslu-Fii Usuli Amali Arramli*, Maktabatu Sulaimani Mur-ii,Kuwait.

Al-Fauzi, S.T. (ht), *Kitabu-Atauthiidi*, Lujnatul-Imaril-Masaajidi, Riyadhi.

Audhi, U. M. (2004), *Man-Hajil-Kur-ani Liilaji-Sihiri Walmasi Washayatiini*, Darul-Harami Liturathi, Kairo.

Amin, M. E. (2005), *"Social Science Research Conception: Methodology and Analysis,"* Makerere University Printing, Kampala.

Ash-kara, A. (1953), *Ujuzi wa Uchawi na Mazingaobwe*, Darul-Fikri, Kairo.

Avastar, M. M. (2009), *Teknolojia ya Elimu ya Giza (Uchawi)*, iliyosomwa tarehe 15/9/2015 katikahttp://2.bp.blogspot.com.

Baali, W. A. (1417H), *Swarimul-Batari-Fi-Taswadi-Lisaharatil-Ash'rari*, Kutub Khana Islamiyat-ul-Islam, New-Delhi.

Bakaani, M. P. (2001), *Kamusi ya Mwanafunzi*, Darul-Fikrat, Al-Hadiri Al- Baidhaa, Moroko.

BAKIZA, (2010), *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, Oxford University Press, East Africa Ltd.

Bakize, L. H. (2014), *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*, Moccony Printing Press, Dar es Salaam.

Bitende, F. I.(2012), "Taswira za Kidini katika Riwaya za E. Kezilahabi", Ripoiti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Bugaywa, D. (2014), Raia-Mwema, ISSN 1821-6250, Toleo Nanba 345, 'Ushirikina, Waangamiza Maisha ya Wanawake', Jumatano Aprili 2-8, 2014.

Buhairi, M. A. (2011), *Muujizatul-Ilaji-Bilkur-ani*, Darul-Taufikiya Liturathi, Kairo.

Buni, A. A. A. (ht), *Manbai Usulil-Hikmat*, Maktabat Ishaatil-Islami, New-Delhi.

Chanady, A. B. (1985), "*Magical Realism and the Fantastic"*, Garland Publishing Inc, New York.

Kezilahabi, E. (2016),"Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu",Ripoiti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Kezilahabi, E. (2010),"Suala la Itikadi katika Riwaya za Shaaban Robert",Ripoiti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Chuwa, A. R. (2004), *Kiswahili katika Karne ya 21*, TUKI, Dar-es-Salaam.

Cooper, B. (1998), "*Magical Realism in West African Fiction",* Routledge Press, New York.

Dachau, D. (2010), '*Magic Realism*' iliyosomwa tarehe 19/09/2015 katika http:///C:/www. encyclopedia.htm

D' Haen, and Theo, L. (2005), "*Magic Realism and Post modernism",* Decentering PriviledgedCenters, Zamora Lois Parkison London.

Faustine, S. (2012), "Matumizi ya Mitindo wa Uhalisia Mazingaombwe katika Riwaya Teule za E. Kezilahabi: Dhima na Athari Zake kwa Hadhira",Ripoiti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada ya Umahiri, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Fulugu, A. (2013), “Dhana ya Kujiua katika Kazi za Euphrase Kezilahabi”, Ripoiti ya Utafitikwa Ajili ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Ghazali, (ht), *Al-Aufaku*, Maktabatu Ishaatul-Islamu, New-Delhi.

Green, J.A. (2009), “*Dreams of Freedom: Magic Realism and Visionary Materialism inOkri and Blake”* Romanticism,Vol. 15, (1) p.18-32.

Gromov, M. (2002), “*Post Modernistic Elements in Recent Swahili Novels”,* Nairobi Press,Nairobi.

Haji, S. H. (2011), *Jitibu Nafsi Yako kwa Tiba Sahihi ya Kisharia,* Express Printing Service, Zanzibar.

Hountondji, P. (1977), “*African Philosophy: Myth and Reality”*, Indian University Press, New-Delhi.

Hop, D. H. (2012),*“The Witchcrft”*, iliyosomwa tarehe 23/12/2015 katika Www. Awakethewitch.com.

Husein, I. (1976), *Kinjeketile,* Oxford University Press, Nairobi.

Hussein, S.S. (2011),*Yajue Majini*, Para PrintTechnology, Dar es Salaam.

Ibrahim, Kh. A. (2005), *Jitibu Nafsi Yako kwa Mpulizo Wako,* Darul- Athari, Makatul-Mukaramat.

Ismail, H. (1968), “*The Medicine Man: Swifa ya Nguvumali”* Peter Lienhardt Oxford, Nairobi.

Jauhari, N. I. (2009), *Usahihi wa Taji la Lugha na Usahihi wa Kiarabu*, Dar-Alhadithi, Kairo.

Jazaiya I. A. (1987), *Tas-hilu Shayatwini Fi-manazilil-Insani*, Darul-Kutubi, Kairo.

Johnson, F. (1939), *“A Standard English-Swahili Dictionary,”* Oxford University Press, Dar es Salaam.

Kabalani, A.N. (2008), *Minati-Rahmani-Fi-Baadhil-Asraril-Kurani*, Daru-Saadi-Din, Saudia.

Kasim, A. M. (2005), *Muuzaji wa Dini Yake,* Maktaba ya Kueneza Kheri, Riyadhi.

Kenyatta, P. A. (2004), *Imani ya Wamatego juu ya Uchawi, Kifo, Kindorobi na Uganga wa Kienyeji,* Peramiho Printing Press, Dar-es-Salaamu.

Kezilahabi, E. (2007), *Dunia Uwanja wa Fujo,* Acme Press Kenya Ltd, Nairobi.

Kezilahabi, E. (1978), *Gamba la Nyoka,* East Afrika Publication, Arusha.

Kezilahabi, E. (1974), *Kichwamaji*, East African Publishing House, Nairobi.

Kezilahabi, E. (1971), *Rosa Mistika,* East African Literature Bureau, Nairobi.

Khamis, S.A. M. (2007), *Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili katika Kioo cha Lugha, 5,* TUKI, Dar es Salaam.

Kothari, C. R. (2008), "*Research Methodology Methods and Techniques* (2nd Revised Edt.),New age,*"* intenational publishers, New-Delhi.

Kombo, D. na Tromp, D. (2006), "*Proposal and Thesis Writing",* An Introduction, Paulines Publications Africa.

Label,G. (2013), *Ukweli Kuhusu Sayansi ya Kiafrika*, iliyosomwa tarehe 23/11/2015 katika http://www.ungoafrika.blogspot.com.

Makula, A.S. (2012), "Athari za Uhalisiamazingaombwe kwa Msomaji katika Kuzielewa Kazi za Fasihihi za Saidi Ahmed Muhamedi", Ripoiti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Malcolm, N. (1959*), "Dreaming",* Routledge and Kegan Paul Ltd, London.

Marquez, G.C. (1980), "*One Hundred Years of Solitude"* Pan Books Ltd, London.

Mbatiah, M. (2002), *Kamusi ya Fasihi,* Standard Textbooks, Nairobi.

Mbatiah, M. (2001), *Kamusi ya Fasihi,* Standard Textbooks Graphics & Publishers, Nairobi.

Mbogo, E. (1993*) Matumizi ya Dhana na Sanaa za Maonyesho za Jadi katika Tamthiliya za Leo*, Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania, Dar-es-Salaamu.

Mberwa, A. R. (2015) "*Athari ya Matumizi ya Mafumbo na Tamathali za Semi katika Nyimbo za Ngoma ya Puuo kwa Wazanzibari*", Ripoiti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Mgonja,S. E. (2012), *Ushuhuda wa Kweli wa Renatus Mungai: Nilivyowatoa Watoto Wangu Kafara Kwenye Hekalu la Shetani!,* Niim Computers and Graphics (T), Dar-es-Salaamu.

Mhilu, G. Nyangwine, N. Kanyuma, Y. (2008), *Nadharia Uhakiki na Maswali,* Nyambari Nyangwine Publishers, Dar es Salaam.

Mshiu, G. Nyangwine, N. Zombwe, G. M. (2007), "*General Studies Notes",* Nyambari Nyangwine Publishers, Dar es Salaam.

Muhando, P. (1986), *Hatia, East African* Publishing House, Dar es Salaam.

Middleton, A. (1963), *"Witchcraft and Sorcery in East Africa,"* Praegar, New York.

Mohamed, S. A. (2012), "*Nafasi ya Uhalisia Mazingaombwe Katika Hadithi za Fasihi Simulizi kwa Jamii ya Wazanzibar*", Ripoti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Mohamed, S. A. (2001), *Babu Alipofufuka,* The Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Mungwa, K. (2013) *Ulimwengu Usioonekana*, iliyosomwa tarehe 24/12/2015 katika http://www.mungwakabili.blogspot.com.htmlnahttp://mungwakabili.blogspot.com.

Mung'ong'o, C. G. (1977), *Mirathi ya Hatari*, Tanzania Publishing House, Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. na Mung'ong'o, C.G. (1993), *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji, Makala ya Semina ya Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania,* Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

Njogu, K. & Chimera, R. (1999), *Ufundishaji wa Fasihi,* Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi.

Nyangwine, N. Zombwe, G. M. Mshiu, G. (2007), "*General Studies Notes",* Nyambari Nyangwine Publishers, Dar es Salaam.

Okri, B. (1991), "*The Famished Road",* Vintage Press, London.

Olali, T. (2010), "*Structure and Anti-Structure of a Swahili New Novel: Astylistic Analysis ofBabu Alipofufuka"* University Press, Nairobi.

Ponera, A. S. (2014a) *Utangulizi wa Nadharia ya Fasihi Linganishi,* Karljamer Print Technology, Dar es Salaam.

Ponera, A. S. (2014b), *"Ufutuhi katika Nathari ya Kiswahili: Ulinganisho wa Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi",* Ripoiti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Qur-an Karim, (2013), *Suratul-Bakara, Maandiko ya Othamani, Na:2,* Maktabatul-Hatil-Abyadhi, Oman.

Rio, F. (2002), "*Margical Realism and Definitions",* Foundation Press, Nairobi.

Rogers, B. H. (2002), "*Word Work: Surviving and Thriving as a Writer"*, Invisible Cities Press, London.

Roh, F. (1968), *"German Art in the 20th Century. Greenwich Connecticut", New York Graphic Society.*

Roh, F. (1925), "Nach-Expressionismus-Magischer Realismus", Krinkhardt & Biermann Press, Leipzig.

Ruickbie, L. (2004), "*The Little Book of Whitchcraft*", Local Bookshop Press, Robert Hale-London.

Safari, A. S. (1993), *Fasihi, Uandishi na Uchapishaji*, Dar es Salaam University Press, Dar es Salaam.

Sengo, T. S. Y. (1993), *Misingi ya Uhakiki katika Fasihi ya Kiswahili*, Umoja wa Waandishi wa Vitabu, Dar es Salaam,

Senkoro, F. E. M. K. (2011), *Fasihi*, Kampuni ya Utamaduni Tafsiri na Uchapishaji (KAUTTU), Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K. (1996), *Nadharia ya Fasihi na Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio,* katika Kioo cha Lugha, Na: 2, TUKI, Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K. (2004),"Fools*, drunkerds and imbeciles Tell More Truth: Whither Satiire in Tanzania"?* katika Kiswahili, juu ya 67, Y. M. Kihore (mhariri), TUKI, Dar es Salaam.

Shaarawi, M. M. (1990), *Sihiri na Husuda*, Maktaba ya Shaarawil- Islam, Kuwait.

Sharifu, H. T. A (ht), *Kibiritul-Ah'maru,*Maktabatu-Ishaatul-Islam, Alhindi.

Simchimba, E. A. (2012), "Falsafa ya Kiafrika katika Methali za Kiswahili",Ripoiti ya Utafiti kwa Ajili ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma, (Haijachapishwa).

Strecher, M. (1999), "*Magical Realism and the Search for Identity in the Fiction of Marakami Haruki*" *Journal of Japanese Studies*, Vol. 25 (2) p.27, Okawa Press, Japan-Oklahoma.

Swabru, H.S. (2009), *Hii ni Zawadi ya Wazanzibari*, Madrasatu Omar Bin Abdul-Azizi, Zanzibar-Makadarar.

Swabun, M. A. (1976), *Swafwatu Tafsiri, Tafsiri ya Kur-an Tukufu, Jzuu1*. Maktabatul-Mukaramat Al- Azhari, Cairo.

Swanaib, GH. A. (2014), *Uchawi na Makuhani: Majini na Malaika*, Daru- Almaarifi Al-Azhari, Cairo.

Taimia, I. I. (1990), *Fur-qani Baina Auliyaai-Rahmani: Wauliyaai shayaatwini*, Daru Swahabati Liturathi, Cairo.

Thiong'o, N. (1965)*,"The River Between," Great Britain Wyman Ltd, London.*

TUKI, (2001), *Kamusi ya Kiswahili Sanifi*, Oxford University Presss, Nairobi.

Tunguli, (2010), *Uchawi*, ilyosomwa tarehe 13/06/2015 katika http:// 1.bpblogspot.com.

Twan-datai (h.t) *Risalatu-Adarul-Bahiyati*, Darul-Fikiri-Fii-Ishaatil-Islami, New-Delhi.

Twauha, A. S. (1972), *Uokozi wa Mwenye Kudhulumiwa katika Kugundua Siri za Kur-an*, Chuo cha Ufunguzi wa Elimu ya Falaki, Cairo.

Twauha, A. S. (1988), *Sihirul-Kuhanat-Fii Hudhuril-Jini*, Maktabatul-Ishaatul-Islami, New-Delhi.

Twauha, A. S. (ht), *Taskhiru-Shayatwiini-Fii-Waswalil-Ashikiina*, Darul-Fikiri, Kairo.

Ungo,A. (2007),*Falsafa ya Kiafrika*, iliyomsomwa tarehe 20/09/2015 katika http://www.ungoafrika.blogspot.com.

Uzorma, I. N. (2012), *Mkuu wa Wachawi Sasa Ampokea Kristo,* Harbinger Cristian publications, Warri-Lagos.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi,* Sai Industries Ltd, Nairobi.

Wafula, R. M. (1999), *Uhakiki wa Tamthiliya: Historian a Maendeleo Yake,* Jomo Kenyata Foundation, Nairobi.

Wamitila, K. W. (2008), *Kanzi ya Fasihi1: misingi ya uchambuzi wa fasihi*, Daisy Printers (K) Ltd, Nairobi.

Wamitila, K. W. (2003), *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia,* Focus Books, Nairobi.

Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi*, Phoenix Publication Ltd, Nairobi.

Wamitila, K. W. (2002), *Uhakiki wa Fasihi Misingi na Vipengele Vyake*, Phoenix Publication Ltd, Nairobi.

Walibora, K. (2010), *Uhalisia na Uhalisiamazingaombwe*: *Mshabaha kati ya Dunia Yao na The Tin Drum.* Swahili Forum 17(2010)p.143-157.

Walibora, K. (2001), *Kamusi ya Methali.* Longhorn Publishers, Nairobi.

Wicca (2014), "*History and Systems of* Witchcraft". iliyosomwa tarehe 17/7/2015 katika Exposing Satanism. http://history.wisc.edu/sommerville/351/351-21.htm.

Williams, R. (1999), "*Marxism and Literature*", New York University Press, New York.

Williams, R. (1995), "*The Postmodern Novel in Latin America*: *Politics, Culture, and the Crisis of Truth"*, St. Martin's Press, New York.

Wizara ya Elimu na Utamaduni, (1992), *Histiria na Falsafa ya Elimu*, National Printing Company, Dar-es-Salaam.


Yusuf, A. A. (1983), "*The Holy Quran, Translation and Commentary,"* Al-Rajhi, Maryland.

Zamora, L. P. and Faris, W. B. (1995), *"Magical Realism: Theory History Community", Duke University Press, London.*

## VIAMBATISHO

### A: Barua za Ithibati ya Kufanyia Utafiti

A.1 Barua Kutoka Chuo Kukuu cha Dodoma



THE UNIVERSITY OF DODOMA
DEPUTY VICE CHANCELLOR ACADEMIC, RESEARCH & CONSULTANCY
OFFICE OF GRADUATE STUDIES

P.O. BOX 263
DODOMA, TANZANIA
TEL: +255 23 23002 FAX: +255 23 23000 EMAIL: ahmed_ame@yahoo.com

REF/UDOM/GS-ADMS/2016/011 Wednesday, 27 January 2016

**To Whom It May Concern:**

**RE: INTRODUCING MR. MAKAME, SILIMA F.**

The above named student is enrolled at the University of Dodoma for the degree of Master of Arts in Kiswahili Literature with registration number HD/UDOM/259/T.2014

An essential requirement of the study programme is that each candidate is required to submit a dissertation report on a project undertaken within industry and supervised by a member of the University's academic staff. Where possible this project should relate to a practical situation in an organisation or firm selected by the candidate. Students are expected to use their own initiative to identify a possible project and negotiate access with a local firm or organization. The title of study is **"MATUMIZI YA FALSAFA YA USIHIRI KATIKA RIWAYA ZA EUPHRASE KEZILAHABI".**

The work may take the form of a survey, ethnography, case studies, etc. Where the report may contain confidential information and its publication could be harmful to the organization, confidentiality is assured by the University. Such reports will be seen only by the Supervisor and Examiner for examination purposes.

I would be grateful if you would provide the student with this opportunity to further his studies while at the same time gaining some useful input for your own organization through the results of the project report.

Sincerely,

Prof. Ahmed M. Ame
**Director for Graduate Studies**

## A.2 Barua Kutoka Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

**REVOLUTIONARY GOVERNMENT OF ZANZIBAR**

SECRETARY
ZANZIBAR RESEARCH COMMITTEE
P. O Box 239
Tel: 2230806
FAX: 2233788



**RESEARCH/FILMING PERMIT**
(This Permit is only Applicable in Zanzibar for a duration specified)

**SECTION**

| | |
|---|---|
| **Name:** | SILIMA FAKI MAKAME |
| **Date and Place of Birth** | 01-01-1977 |
| **Nationality:** | TANZANIAN |
| **Passport Number:** | - |
| **Date and Place of Issue** | - |
| **Date of arrival in Zanzibar** | - |
| **Duration of stay:** | TWO YEARS |
| **Research Tittles:** | "MATUMIZI YA FALSAFA YA USIHIRI KATIKA RIWAYA ZA EUPHRASE KEZILAHABI" |
| **Full address of Sponsor:** | - |

This is to endorse that I have received and duly considered applicant's request I am satisfied with the descriptions outlined above.

| | |
|---|---|
| **Name of the authorizing officer:** | MWANAISHA A. KHAMIS |
| **Signature and seal:** | |
| **Institution:** | Office of Chief Government Statistician |
| **Address:** | P. O Box 2321<br>Zanzibar. |
| **Date:** | 11/02/2016 |

S. M. Z
P.O. Box 2321
OFFICE OF THE CHIEF GOVERNMENT STATISTICIAN ZANZIBAR

## A.3 Barua Kutoka Afisi ya Makamu wa Pili wa Raisi wa Zanzibar

OMPR/M.95/C.6/VOL.XVII/

11 /02/2016

MAKAMU MKUU WA CHUO,
CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA),
<u>ZANZIBAR.</u>

MAKAMU MKUU WA CHUO,
CHUO KIKUU CHA SUMEIT,
<u>ZANZIBAR.</u>

**KUH: <u>RUHUSA YA KUFANYA UTAFITI</u>**

Kwa heshima, tunaomba uhusike na mada tulioitaja hapo juu.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imemruhusu **Ndugu Silima Faki Makame**, kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, kufanya utafiti katika mada inayohusiana na "**Mat umizi ya Falsafa ya Us ihiri katika Riwaya za Euphrase Kezilahabi**". Hivyo tunaomba mtafiti huyo asaidiwe kufanya utafiti wake. Utafiti unafanyika kuanzia 11/02/2016 hadi 14/08/2016.

Kwa nakala ya barua hii mara baada ya kumaliza utafiti, mtafiti anatakiwa kuwasilisha nakala (copy) 3 za ripoti ya utafiti huo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais- Zanzibar.

Tunaambatanisha na kivuli cha kibali cha kufanyia utafiti

Ahsante,

Wako mtiifu

**ASHRAF MOHAMMED ABDALLA**
**/KATIBU MKUU,**
**OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS,**
**<u>ZANZIBAR</u>**

**NAKALA:**

Ndugu Silima Faki Makame

**B: Miongozo ya Usaili, Mijadala na Udurusu wa Kimaktaba**

**B.1** Mwongozo wa Maswali kwa Wataalamu wa Fasihi ya Kiswahili waliowahi kuzisoma, kuzihakiki na kizitafiti pamoja na kuziandikia ripoti riwaya za Euphrase Kezilahabi katika vyuo vikuu vya; SUZA, SUMEIT na DODOMA.

Utafiti huu unahusu matumizi ya falsafa ya usihiri katika riwaya za Euphrase Kezilahabi.

Lengo la utafiti huu ni kuibua aina za usihiri zilizojitokeza katika riwaya za mtunzi teule, na kuitambua miktadha ambayo usihiri huelekezwa ndani ya riwaya hizo. Aidha, utafiti huu umekusudia kuonesha sababu zilizopelekea kutumiwa na kutokea kwa falsafa ya usihiri pamoja na kufahamu kwa kiasi gani wasomaji na wanajamii wameathirika kutokana na matumizi ya falsafa ya usihiri kutokana na riwaya hizo.

Katika utafiti huu falsafa ya usihiri imechukuliwa kama mbinu bunilizi ya kifasihi iliyotumika kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Kwa jumla, utafiti uliomgozwa na maswali yaliyoelekezwa kwa watafitiwa kama yafuatayo:

1 Tafadhali tunakuomba utuelezee maana ya falsafa?
2 Je, Waafrika tunayo falsafa?
3 Je, unaweza kutuelezea maana ya usihiri na uko wa aina ngapi?
4 Tunakuomba ututajie aina mbili kati yazo?
5 Unaweza kutuelezea maeneo gani ambayo usihiri huelekezwa zaidi katika jamii na riwaya za mtunzi?
6 Ni matukio au matendo gani yanayoashiria usihiri? Tunakuomba yataje na yaelezee matatu?
7 Kwa maoni yako, usihiri una faida au hasara zipi?
8 Ni athari gani zitokanazo na usihiri ufanywao katika jamii na kazi za mtunzi teule?

9 Baadhi ya wasomaji wa riwaya za Euphrase Kezilahabi wanapata ugumu wa kuyaelewa maudhui yazungumziyayo usihiri katika riwaya zake. Unaweza kueleza lolote juu ya jambo hilo?

10 Ni matukio gani ya usihiri yanayojitokeza katika riwaya za mwandishi huyu kama vile *Rosa Mistika* na *Kichwamaji* uyakumbukayo na je yana uhalisi katika jamii?

11 Tunakuomba tutajiye sababu tatu za kufasiriwa kuwa ni usihiri**?**

12 Ephrase Kezilahabi ni mwandishi aliyezaliwa katika mandhari ya Kitanzani, mbinu ya usihiri anyoitumia katika uwandishi wa riwaya zake inafananaje na kutofautianaje na mandhari hayo?

**B.2 Dodoso kwa Wanafunzi wa Shahada ya Kwanza wa Fasihi ya Kiswahili**

**Maelekezo**

i) Dodoso hili ni kwa ajili ya kukusanya data za utafiti wa kukamilisha shahada ya uzamili katika fasihi ya Kiswahili.

ii) Mada ya utafiti: MATUMIZI YA FALSAFA YA USIHIRI KATIKA RIWAYA ZA EUPHRASE KEZILAHABI.

iii) Ushiriki wako katika kuukamilisha utafiti huu ni muhimu sana ili kuikuza na kiiendeleza taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Hivyo, tunaomba ushirikiano wako.

**SEHEMU A: Taarifa za Mtafitiwa**

Jina (sio lazima) ……………………….. umri……………………………

Chuo……………………………………………

Uko mwaka wa ngapi? ... masomo … na fani unayosoma ... na

**SEHEMU B: Maswali Yanayohusu Utafiti**

1. Tunakuomba tuelezee maana ya usihiri?
2. Tunakuomba tutajie maeneo ambayo usihiri huelekezwa zaidi katika jamii na riwaya za mtunzi teule?
3. Ni sababu gani zipelekeazo kutokea kwa usihiri katika riwaya za mtunzi teule?
4. Euphrase Kezilahabi ni mtunzi maarufu wa kazi za kifasihi. Tunakuomba tutajie riwaya zake mbili ulizowahi kuzisoma, kuzihakiki na kuzisikia kutajwa

i) ………………………………………

ii) …………………………………………..

5. Miongoni mwa kazi ulsoma za mtunzi teule kuna ugumu upi wa kuzifahamu na maudhui yaliyojikita zaidi ni yepi?
6. Unakumbuka ni mitindo gani aipendeleayo kuitumia mtunzi huyu na je, ndiyo iletayo ugumu huo?
7. Ukirejelea kazi za mtunzi unaweza kusema lolote juu ya uandishi wake na je, kuna matukio yoyote ya kisihiri na yana ujumbe gani?
8. Matukio hayo yana umuhimu gani na athari zipi?

**B.3 Mwongozo wa Mjadala wa Vikundi kwa Wanafunzi wa Masomo ya Fasihi ya Kiswahili.**

1. Kwa maoni yenu, usihiri ni nini na una athari gani kwa jamii?
2. Je, mumewahi kusoma kazi yoyote ya Euphrase Kezilahabi inayozungumzia falsafa ya usihiri? Kama ndio, unaweza kutuelezea kwa ufupi?
3. Unafikiri kwa nini mtunzi huyu akatumia falsafa ya usihiri katika riwaya zake?
4. Usihiri na umazingaombwe unalinganaje na kutofautianaje?
5. Je, kuna mambo yoyote manne unayoyafurahiya au unayoyachukia, yahusuyo usihiri yanayozungumzwa katika kazi teule? Kama ndio tunakuomba tutajiye matatu?
6. Ni kazi zipi za Kezilahabi zimezungumzia usihiri?
7. Ni athari gani zinazopatikana kwa wasomaji wa kazi hizo?

**B.4 Mwongozo wa Udurusu wa Kimaktabani**

A) Vyanzo mbalimbali vilivyotumika katiaka udurusu wa maktabani ni kama vile tasnifu, vitabu, tovuti, makala, majarida, tahakiki na riwaya.

1. Zilitumika kupata dhana ya falsafa, usihiri na kulinganisha uhusiano kwazo na utofautiano wao.
2. Zilisaidia kupata taarifa kuhusu asili, sababu, maana, maeneo, na miktadha inayoashiria usihiri kwazo.
3. Zilisaidia upatikanaji wa taarifa kuhusiana na falsafa kwa ujumla.

B) Riwaya

Zilitumika kubaini matukio na maeneo yanayoelekezwa, aina na matumizi ya falsafa ya usihiri.

**B.5 Mwongozo wa Maswali kwa Mtunzi**

1. Katika kazi zako umegusia maudhui yahusuyo falsafa ya usihiri. Tunakuomba tuelezee nini maana ya usihiri na unalinganaje na falsafa?
2. Je, Waafrika tunayo falsafa, kama ndio au la ni kwa vipi?
3. Ni sababu zipi zilizokupelekea kutumia falsafa ya usihiri katika riwaya zako na ulikusudia matumizi hayo ni kwa Waafrika tu au duniani kote?
4. Falsafa ya usihiri imekuwa ikitumika katika mazingira tofauti kama vile katika kilimo, biashara na siasa. Je, unadhani yana athari gani kwa wasomaji na wanajamii?
5. Je, unadhani matumizi ya falsafa ya usihiri uliyoyataja katika riwaya zako yanalandana na hali halisi ya jamii ya Tanzania na nyingineyo?
6. Katika visiwa vya Ukerewe unasema kuna kisiwa cha wachawi je, kisiwa hicho hutumika vipi kiusihiri hadi kuitwa jina hilo?

## C.1 Picha Mbalimbali Zinazohusiana na Utafiti



C.1: Mtafiti akifanya mjadala na wanafunzi wa shahada ya kwanza fani ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha SUZA kampasi ya Nkuruma. Mwanafunzi wa kwanza upande wa kulia ni Bi. Wanu P.Sheha, wa Pili anayeongoza mjadala ni Mtafiti husika, wa tatu ni Bi Asha S. Ali, wa nne ni Bw. Othmani M. Abuu na wa tano ni Bw. Ame M. Haji. Wote hao ni wanafunzi wa mwaka wa kwanza. Mjadala ulifanyika katika Holi namba 1,tarehe 17/02/2016 (Utafiti, 2016).



C.2: Pembe za ng'ombe zinazotumika kurukia angani na hirizi mbalimbali zinzotumika kutibu watu, kurukia angani kwa wasihiri.Kutoka kwa mtaalamu wa falsafa ya usihiri Bw. Husein A. Ali Chunbuni-Zanzibar (Utafiti, 2016).



C.3: Ubao unaotumika kupigia ramli mara anapofika msihiriwa au anaposihiriwa. Na michoro iliyomo inaonesha kuwa mgonjwa amesibiwa na usihiri wa kufarakanisha (Hamadi A. Makame, alipohojiwa na mtafiti, tarehe 11/02/2016, anayeishi Mtoni-Kidatu, Utafiti, 2016).



C.4: Mizizi inayotumika kumsihiri mtu inapoambatanishwa na jini pamoja na shetani. Mizizi iliyopo hapo ni ya m-bono na mfausiku ikichanganywa pamoja humtibu mtu mwenye ugonjwa wa baridi (mzee Hafidhi M. Ali mtaalamu wa mitishamba anayeishi Mkwajuni Zanzibar, Mahojiano na Mtafiti ya tarehe 03/04/2016).



C.5: Hii ni picha inayoonesha wasihiri walioanguka juu ya anga huko Mwanza ambao walitoka Kigoma kwenda kumchukua msihiriwa lakini kabla ya kufika walianguka njiani (picha inashadidia matendo ya usihiri iliyosomwa katika mitandao ya kijamii (blogspot.com) kupitia simu ya Mtafiti 15/09/2015).